# SITIARI ZA KIAFYA KATIKA MATINI TEULE ZA FASIHI YA KISWAHILI YA WATOTO

**REUBEN MWILARIA**

**Tasnifu Iliyowasilishwa katika Shule ya Mafuzu kwa Minajili ya Kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamifu katika Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Chuka**

**CHUO KIKUU CHA CHUKA**

**OKTOBA 2024**

# UNGAMO NA IDHINI

**Ungamo**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada au stashahada katika Chuo Kikuu kingine chochote.

Sahihi.................................................... Tarehe 22/10/2024

Reuben Mwilaria
AD12/35380/18

**Idhini**

Tasnifu hii imetahiniwa, ikapitishwa na kuwasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu.

Sahihi.................................................... Tarehe 22/10/2024

Prof. John M. Kobia
Chuo Kikuu cha Chuka

Sahihi.................................................... Tarehe 22/10/2024.

Dr. Dorcas M. Musyimi
Chuo Kikuu cha Chuka

CHUKA UNIVERSITY
DIRECTOR BOARD OF POSTGRADUATE STUDIES AND RESEARCH
OCT 2024
P.O. Box 109-60400 CHUKA

## HATILINZI

©2024

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kurudufisha, kunakili au kuhifadhi kwa mfumo wowote ule au kutoa sehemu yoyote ya tasnifu hii bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Chuka.

# TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa mama yangu Annah Nkoroi kwa mapenzi na juhudi zake za dhati katika kunitia moyo kusoma, licha ya kuwa na umri wa miaka mingi na changamoto za kimapato.

## SHUKRANI

Kwanza namshukuru Maulana kwa siha bora na kuniwezesha kukamilisha kazi hii licha ya kuwa na changamoto nyingi za kikazi na kifamilia. Amekuwa Mungu mwaminifu na mwenye upendo usio na kipimo.

Kwa moyo mkunjufu nawashukuru mno wasimamizi wangu Profesa John Kobia na Daktari Dorcas Musyimi kwa kunipa mwongozo na mawaidha ya hali ya juu yaliyoniwezesha kuendelea na kukamilisha kazi hii. Mumekuwa katika mstari wa mbele kunielekeza, kunitia moyo na kunishauri wakati wote nilipowahitaji. Mungu awabariki sana.

Natoa shukrani za dhati kwa msimamizi wa Idara ya Fani Daktari Christine Atieno kwa kunitia moyo wa kuendelea na kumaliza masomo yangu. Ushauri wako umekuwa na manufaa si haba kwangu. Siwezi kuwasahau wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Chuka Dkt. Onesmus Ntiba na Dkt. Allan Mugambi kwa ushauri wa kufana mlionipa kila nilipowahitaji. Asanteni sana. Pia, namshukuru Dkt. Mary Kanyua tuliyesoma naye kwa kunitia moyo wa kukamilisha kazi hii. Isitoshe, natoa shukrani nyingi kwa wanafunzi wenzangu Faith Nyaga, Mutwiri Fred John na Mary Makai kwa ushirikiano mwema tuliokuwa nao masomoni.

Shukrani za dhati pia ni kwa bibi yangu Esther Mwonjiru kwa uvumilivu na kunitia moyo wa kuendelea kusoma na kukamilisha kazi hii nilipopoteza hamu ya kuendelea. Hongera sana. Zaidi nawashukuru watoto wangu Miriam Kagwiria, Josiah Mutuma, Mark Mutabari, Victoria Mwende na Rehema Kauria kwa kuvumilia na kunielewa nilipokosa kutimiza baadhi ya mahitaji yenu nilipokuwa nikiendelea kusoma. Asante kwa uvumilivu wenu kwani umezaa matunda.

## IKISIRI

Haja ya kuimarisha viwango vya afya ulimwenguni imechangia kujumuishwa kwa taaluma mbalimbali kama vile fasihi katika vita dhidi ya changamoto za kiafya. Kazi mbalimbali za kifasihi zimebuniwa zikiangazia masuala ya kiafya yanayoathiri jamii na namna ya kuyasuluhisha. Utafiti huu ulijikita katika utanzu wa fasihi ya Kiswahili ya Watoto kwa lengo la kuchanganua sitiari za kiafya katika matini teule za fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Uliongozwa na malengo yafuatayo: Kujadili aina za sitiari za kiafya katika vitabu teule vya fasihi ya Kiswahili ya Watoto, kuchunguza mtindo uliotumika kuwasilisha sitiari za kiafya katika vitabu teule na kufafanua masuala mtambuko yaliyowasilishwa na sitiari za kiafya katika vitabu teule vya fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Vitabu viteule ni: *Siku ya Ukimwi* (Kobia, 2008), *Pendo katika Shari* (Momanyi, 2008), *Sitaki Iwe Siri* (Matundura, 2008), *Madhila ya Bi. Shufaa* (Bakari, 2008), *Kosa la Marehemu* (Panja, 2010) na *Nimefufuka* (Nandwa, 2011) katika msururu wa "Afya Yangu." Vitabu hivi vilichaguliwa kimakusudi kwa sababu ya upekee wake katika kuangazia suala la afya, ambalo ni muhimu katika jamii na huchangia katika kuafikiwa kwa maendeleo endelevu. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia Changanuzi ya Sitiari ya Dhana ya Johnson na Lakoff (1980) na nadharia ya Umitindo ya Leech (1969). Nadharia Changanuzi ya Sitiari ya Dhana ilitumika kujadili aina za sitiari za kiafya na kufafanua masuala mtambuko yaliyowasilishwa na sitiari za kiafya katika vitabu teule. Nadharia ya umitindo ilitumika kuchunguza mtindo uliotumika kuwasilisha sitiari za kiafya katika vitabu teule. Utafiti huu ulifanyiwa maktabani. Data ilipatikana kwa kusoma vitabu teule kwa kina na kunakili maneno ya kisitiari, vishazi na sentensi zilizorejelea masuala ya kiafya. Data hiyo ilikusanywa na kupangwa kulingana na malengo ya utafiti. Ilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo. Matokeo ya utafiti huu ni kuwa ulibainisha aina mbalimbali za sitiari za kiafya. Pia, iligunduliwa kuwa fasihi ya Kiswahili ya Watoto ilifaa kutumiwa kama njia mbadala ya kuelimisha jamii kuhusu athari za masuala mtambuko kama vile afya, dawa za kulevya na masuala ya kijnsia yanayoathiri afya katika jamii kwa sababu iliweza kusomwa na watu wa viwango mbalimbali vya elimu. Utafiti huu pia ulibainisha na kupanua mawanda ya matumizi ya sitiari na fasihi ya Kiswahili ya Watoto katika kuboresha changamoto za kiafya na kuwa marejeleo ya tafiti za baadaye. Utafiti huu ulipendekeza kuwa, washikadau katika sekta ya afya wajumuishe fasihi ya Kiswahili ya Watoto katika kufunza masuala ya kiafya. Pia, lugha ya kisitiari itumiwe katika kuangazia masuala ya kiafya katika jamii ambazo masuala hayo hayatajwi hadharani kwa sababu ya tamaduni hasi. Pia, kulikuwa na haja ya jamii kuharamisha matumizi ya dawa za kulevya na ubagusi wa kijinsia. Waliofaidika na utafiti huu ni washikadau wanaofunza jamii kuhusu umuhimu wa afya bora, madhara ya dawa za kulevya na masuala ya kijinsia yanayosababisha afya duni.

## ABSTRACT

The need to improve health standards in the world has necessitated the involvement of various discipines like Literature in the fight againist health challenges. Various literary works have been written on health issues and how to address them. This research was based on Kiswahili Children's Literature genre that aimed on analysing the role of health metaphors in addressing health issues in selected Kiswahili Literature works. It was guided by the following objectives: To discuss the types of health metaphors used in the selected Kiswahili Children Literature books, to investigate the style used to present health metaphors in the selected books and to explain the pertinent and contemporary issues highlighted by health metaphors in the selected books. The selected books were: *Siku ya Ukimwi* (Kobia, 2008), *Pendo katika Shari* (Momanyi, 2008), *Sitaki Iwe Siri* (Matundura, 2008), *Madhila ya Bi. Shufaa* (Bakari, 2008), *Kosa la Marehemu* (Panja, 2010) *Nimefufuka* (Nandwa, 2011) in "Afya Yangu" Series. These books were selected purposively due to their uniqueness in addressing health issues, which contribute significantly in attaining sustainable development in the society. This research was guided by Conceptual Metaphor Theory by Lakoff and Johnson (1980) and Stylistic Theory by Leech (1969). Conceptual Metaphor Theory was used to discuss the types of health metaphors used in the selected texts and explain the pertinent and contemporaray issues highlighted by health metaphors in the selected books. Stylistic Theory was used to identify the style used to present health metaphors in the selected texts. This research was library based. Research data was generated after reading in depth the selected books and noting down words, phrases and sentences addressing health issues. The data was collected and organized according to research objectives. It was analysed and presented in descriptive form. The outcome of this research was that it identified various types of health metaphors. It was also found that Kiswahili children literature could be used as an alternative discipline in educating the community on the effects of emerging issues such as health and drug and substance abuse and gender issues affecting peoples health because it could be read easily by people with varied education levels.This research identified and widened the scope of Kiswahili metaphors in addressing health challenges affecting the society, as well as being reference for future research. Some of the recommendation were that the stakeholders in health sector should incorporate Kiswahili children literature in teaching health issues. Metaphoric language could also be used in addressing health issues in communities where such issues are not addressed directly due to social taboos. There was need for the community to eradicate drug abuse and genger discrimination. The beneficiaries of this research are the stakeholders with the responsibility of teaching the society about the importance of good health, dangers of substance abuse and gender issues which lead to poor health.

## YALIYOMO

**UNGAMO NA IDHINI** .......... ii

**HATILINZI** .......... iii

**TABARUKU** .......... iv

**SHUKRANI** .......... v

**IKISIRI** .......... vi

**ABSTRACT** .......... vii

**YALIYOMO** .......... viii

**ORODHA YA VIFUPISHO** .......... xv

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI** .......... 1

1.1 Usuli wa Mada .......... 1

1.2 Suala la Utafiti .......... 4

1.3 Malengo ya Utafiti .......... 5

1.4 Maswali ya Utafiti .......... 5

1.5 Umuhimu wa Utafiti huu .......... 5

1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti .......... 7

1.7 Maelezo ya Istilahi .......... 8

**SURA YA PILI: MWAUO WA MAANDISHI** .......... 9

2.1 Nafasi ya Fasihi ya Watoto katika kufafanua Sitiari za Kiafya .......... 9

2.2 Athari za Kiafya Katika Jamii .......... 11

2.4 Nafasi ya Sitiari katika Kuchanganua Kazi za Kifasihi .......... 18

2.5 Mtindo na Uchanganuzi wa Maana Katika Sitiari za Kiafya .......... 20

2.6 Misingi ya Kinadharia .......... 23

2.6.1 Nadharia Changanuzi ya Sitiari ya Dhana .......... 23

2.6.2 Nadharia ya Umitindo .......... 26

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI** .......... 29

3.1 Eneo la Utafiti .......... 29

3.2 Mpango wa Utafiti .......... 29

3.3 Kundi Lengwa .......... 29

3.4 Uteuzi wa Sampuli .......... 30

3.5 Ukusanyaji wa Data ....... 31
3.6 Uchanganuzi wa Data ....... 32
3.7 Uwasilishaji wa Data ....... 32
3.8 Maadili ya Utafiti ....... 33

**SURA YA NNE: AINA ZA SITIARI ZA KIAFYA KATIKA VITABU TEULE ....... 34**

4.1 Utangulizi ....... 34
4.2 Muhtasari wa Vitabu teule ....... 35
4.3 Sitiari Kuu za Kiafya katika Vitabu teule. ....... 36
4.3.1 Nimefufuka ....... 37
4.3.2 Sitaki Iwe Siri ....... 38
4.3.3 Ushindi ....... 39
4.3.4 Siku ya Ukimwi ....... 39
4.3.5 Pendo katika Shari ....... 40
4.3.6 Siku ya Ukimwi ....... 40
4.3.6.1 Taswira ya Kifo ....... 40
4.3.6.2 Taswira ya Utupu ....... 41
4.3.7 Kosa ....... 43
4.3.8 Mama Safi ....... 44
4.4 Sitiari za Kikaida za Kiafya katika Vitabu Teule ....... 44
4.4.1 Maisha ....... 45
4.4.2 Nyumba ya Udongo ....... 45
4.4.3 Safi Safina ....... 46
4.4.4 Matunda ....... 46
4.4.5 Gofu ....... 47
4.4.6 Mwendawazimu ....... 47
4.4.7 Meza ....... 48
4.4.8 Muhuri wa Mauti ....... 48
4.4.9 Ukuni ....... 49
4.4.10 Sare Nyeupe pe pe pe ....... 49
4.4.11 Makengeza ....... 49
4.4.12 Ndwele ....... 50
4.4.13 Uta ....... 51

4.4.14 Nyembe ........................................................................................51
4.4.15 Tambara ........................................................................................52
4.4.16 'Danger' ........................................................................................53
4.4.17 Jongoo ........................................................................................53
4.4.18 Mume Jina ........................................................................................54
4.4.19 Moto ........................................................................................55
4.4.20 Vumbi ........................................................................................55
4.4.21 Kitanzi ........................................................................................56
4.4.22 Watu wanavyotoweka ........................................................................................56
4.4.23 Safari ........................................................................................57
4.4.24 Kupalilia Mimba ........................................................................................57
4.4.25 Kombora ........................................................................................58
4.4.26 Macho ........................................................................................59
4.4.27 Kondoo ........................................................................................59
4.4.28 Pendo ........................................................................................60
4.4.29 Vita ........................................................................................60
4.4.30 Kiuno cha Nyigu ........................................................................................61
4.4.31 Nambari 8 ........................................................................................62
4.4.32 Mtoto wa Watu ........................................................................................62
4.4.33 Mtego wa Panya ........................................................................................63
4.4.34 Koo lake lilikuwa limekauka ........................................................................................63
4.4.35 Bendera ........................................................................................64
4.4.36 Nyuso zao zilitulia ........................................................................................65
4.4.37 Mbwa ........................................................................................65
4.4.38 Shamba ........................................................................................66
4.4.39 Mahindi ........................................................................................66
4.4.40 Mahindi Mabichi ........................................................................................66
4.4.41 Sumu ........................................................................................67
4.4.42 Viziwi ........................................................................................67
4.4.43 Magonjwa nyemelezi ........................................................................................68
4.4.44 Zimwi ........................................................................................68
4.4.45 Akili ikimduru ........................................................................................69
4.4.46 Tendo la Ndoa ........................................................................................70

4.4.47 Jipu....71
4.4.48 Mifupa iliyolala....71
4.4.49 Walinzi....72
4.4.50 Kuushambulia Mwili....72
4.4.51 Macho yaliyokuwa Makavu....73
4.4.52 Kiu....74
4.4.53 Tamaa mbele Mauti nyuma....74
4.4.54 Mzee....75
4.4.55 'Sweetie'....76
4.4.56 Mtu wa Miraba Minne....76
4.4.57 Kitanzi....76
4.4.58 Shetani....77
4.4.59 Mbebu Chafu....77
4.4.60 Asali....78
4.4.61 Lulu....78
4.4.62 Gofu....79
4.5 Sitiari Pana za Kiafya katika Vitabu Teule....79
4.5.1 Sokwe- Mtu- Tasa....80
4.5.2 Bomba la Dume lenye Kidari cha Duara....80
4.5.3 Kuanguka, Zimwi na Ibilisi....81
4.5.4 Utingo....82
4.5.5 Kifo cha Yuri....83
4.5.6 Ng'onda na Kiwiliwili cha Mifupa....83
4.5.7 Furaha ya Nyani imeishia Jangwani....84
4.5.8 Fukua....86
4.5.9 Afya yake ikawa inafuata Majira kama ulivyo Msimu wa Kipupwe....87
4.5.10 Baba Sukari....88
4.6 Hitimisho....88

**SURA YA TANO: MATUMIZI YA MTINDO KATIKA UWASILISHAJI WA SITIARI ZA KIAFYA KATIKA VITABU TEULE....89**

5.1 Utangulizi....89
5.2 Nyimbo....89
5.3 Ushairi....91

5.4 Barua ....................................................................................................93
5.5 Mshikamano wa Kisimulizi ...............................................................94
5.6 Majazi......................................................................................................98
5.6.1 Fukua ..................................................................................................99
5.6.2 Mama Safi........................................................................................100
5.6.3 Bi. Shufaa ........................................................................................100
5.6.4 Zuhura..............................................................................................101
5.6.5 Sikitu................................................................................................102
5.7 Tashtiti...................................................................................................102
5.7.1 Muhuri wa Mauti .............................................................................103
5.7.2 Ngamia.............................................................................................104
5.7.3 Jongoo asiyeweza kupanda Mtungi ..................................................104
5.7.4 Pendo katika Shari ...........................................................................105
5.7.5 Siku ya UKIMWI .............................................................................106
5.8 Taswira..................................................................................................107
5.8.1 Taswira za Magonjwa.......................................................................107
5.8.2 Taswira za Kifo ................................................................................110
5.8.3 Taswira za Uzinzi ............................................................................112
5.9 Chuku ....................................................................................................115
5.10 Methali ................................................................................................118
5.11 Hitimisho.............................................................................................119

**SURA YA SITA: MASUALA MTAMBUKO YALIYOWASILISHWA NA SITIARI ZA KIAFYA KATIKA VITABU TEULE.......120**

6.1 Utangulizi..............................................................................................120
6.2 UKIMWI...............................................................................................121
6.2.1 Visababishi vya Ugonjwa wa UKIMWI ............................................122
6.2.1.1 Mila na Desturi za Jamii ..............................................................122
6.2.1.2 Tamaa ya Pesa na udanganyifu katika Ndoa ................................123
6.2.1.3 Ukahaba .......................................................................................125
6.2.1.4 Kutowajibika.................................................................................128
6.2.2 Athari za Ugonjwa wa UKIMWI .....................................................129
6.2.2.1 Vifo vya Watu...............................................................................129
6.2.2.2 Kuambukizwa na Magonjwa Nyemelezi .......................................130

6.2.2.3 Kusambaratika kwa Ndoa ....... 132
6.2.2.4 Kuongezeka kwa Watoto Yatima ....... 133
6.2.2.5 Kuathirika  kwa Jmaa na Marafiki ....... 134
6.2.2.6 Ufukara ....... 136
6.2.3 Njia za kukabiliana na UKIMWI ....... 137
6.2.3.1 Kupuuza Tamaduni hasi kuhusu UKIMWI ....... 138
6.2.3.2 Uaminifu na kuepuka Ngono za kiholela ....... 139
6.2.3.3 Kuzingatia huduma bora za Kiafya ....... 140
6.2.3.4 Lishe bora ....... 141
6.2.3.5 Uwajibikaji ....... 142
6.2.3.6 Kuhamasisha Jamii ....... 143
6.3 Dhuluma za Kijinsia ....... 144
6.3.1 Visababishi vya dhuluma za kijinsia ....... 144
6.3.1.1 Utamaduni ....... 144
6.3.1.2 Ndoa ....... 147
6.3.1.3 Imani Potovu ....... 148
6.3.2 Kusuluhisha dhuluma za kijinsia ....... 149
6.3.2.1 Kusomesha Vijana wa Kike ....... 149
6.3.2.2 Sera ya Serikali ....... 150
6.4 Dawa za Kulevya ....... 150
6.4.1 Kukabiliana na Dawa za kulevya ....... 151
6.4.1.1 Taasisi za Kielimu ....... 151
6.4.1.2 Kiwango cha Jamii ....... 152
6.4.1.3 Kiwango cha Kitaifa ....... 152
6.4.2 Athari za dawa za Kulevya ....... 153
6.4.2.1 Kuongezeka kwa Uhalifu ....... 153
6.4.2.2 Mizozo katika Familia ....... 155
6.4.2.3 Kuzorota kwa Uchumi ....... 157
6.4.2.4 Kuzorota kwa Afya ....... 157
6.4.2.5 Kuathirika Kimasomo ....... 158
6.5 Hitimisho ....... 160

**SURA YA SABA: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ....... 161**

7.1 Muhtasari ....... 161

7.2 Hitimisho........................................................................................162
7.3 Mapendekezo ya tafiti za baadaye ....................................................165

**MAREJELEO ..........................................................................................167**
**VIAMBATISHO ......................................................................................173**
Kiambatisho I: Kibali cha Utafiti.............................................................173
Kiambatisho II: Idhini Ya Utafiti.............................................................174

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| **C.D.C** | : | Centre for Disease Control |
| **CMIS** | : | Continuous Malaria Indicator Survey |
| **K.I.C.D** | : | Kenya Institute of Curriculum Development |
| **NACADA** | : | National Authority for the Campaign againist Alcohol and Drug Abuse |
| **UNAIDS** | **:** | United Nations AIDS Programme |
| **USAID** | : | United States Agency for International Development |
| **WHO** | : | World Health Organisation |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Fasihi ya watoto ni dhana inayotumiwa kurejelea matini za kifasihi zilizotungwa ili zisomwe na watoto (Oberstein, 1996; Hunt, 1999; Wamitila, 2003). Watoto hufurahia kusoma fasihi hii kwa jinsi ilivyo na visa vya kufurahisha. Ingawa fasihi ya Kiswahili ya Watoto inalenga kusomwa na watoto, masuala yanayoangaziwa yana umuhimu kwa wanajamii wote. Hivyo, fasihi hii inapaswa kusomwa na watoto na watu wazima. Kuanzia mwaka wa elfu mbili, tafiti katika fasihi ya Kiswahili ya Watoto ziliongezeka na pia zikaanza kuangazia masuala mtambuko kama vile afya yanayoathiri jamii (Ngugi na Nabea, 2011). Kinachowavutia wasomaji wa fasihi ya watoto ni kuwepo na sifa bainifu zinazotambulisha na kurahisisha usomaji wa fasihi hii. Miongoni mwa sifa hizi ni matumizi bora ya mbinu za kiutunzi kama vile fantasia, lugha sahili na uchache wa visa (Matundura na wengine, 2013). Pia, matumizi ya picha, michoro na maelezo hufanikisha uelewa wa ujumbe unaowasilishwa katika fasihi ya watoto. Hivyo, watu walio katika viwango mbalimbali vya elimu wanaweza kusoma fasihi hii kwa urahisi na kuelewa yaliyomo. Umuhimu wa kuendeleza tafiti katika fasihi ya watoto pia unasisitizwa na Bakize (2013) anayesema kuwa, fasihi ya Kiswahili ya Watoto ni changa inapolinganishwa na fasihi ya watu wazima, ambayo ilishika kasi katika karne ya kumi na nane na kumi na tisa. Pia, fasihi ya watoto huibua masuala mbalimbali ya kiusomi yanayopaswa kushughulikiwa kinadharia kama fasihi ya watu wazima. Hoja hizi zinadhihirisha haja ya kuendeleza tafiti katika fasihi ya Kiswahili ya Watoto kwa sababu masuala yanayoangaziwa katika fasihi hii yana umuhimu kwa watu wote.

Senkoro (1982) anasema kuwa, mwanafasihi ana jukumu la kushughulikia masuala yanayoathiri jamii kwa jicho la kifasihi kwa sababu ana nafasi nzuri ya kuyaelewa. Baadhi ya masuala hayo ni changamoto za kiafya zinazolemaza kuafikiwa kwa maendeleo endelevu, kama ilivyoangaziwa katika matini teule za fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Kwa mujibu wa Scott na Wenziwe (2000) na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO), (2003, 2018, 2020), magonjwa na vifo ni baadhi ya changamoto za kiafya. Katika mwaka wa 2002 magonjwa mbalimbali yalisababisha vifo vya watoto milioni kumi na mia tano ulimwenguni, huku barani Afrika watoto mia tano wakiaga dunia kila baada ya saa moja (WHO, 2003, 2018). Matatizo haya yalisababisha kujumuishwa kwa

afya kama suala mtambuko katika fasihi ya Kiswahili ili kuhamasisha jamii kuhusu changamoto za kiafya (Ngugi, 2014, 2016). Baadhi ya changamoto hizi ni ukosefu wa lishe, magonjwa ya kiakili, malaria na kifua kikuu (WHO, 2018). Hata hivyo, kulingana na Mpango wa Ukimwi wa Umoja wa Mataifa (UNAIDS), (2023), UKIMWI ndio unaathiri watu zaidi. Jumla ya watu milioni thelathini na nane na laki nne wanaugua ugonjwa huu. Juhudi za Kituo cha Udhibiti wa Magonjwa (CDC), mataifa yaliyoendelea kama vile Marekani, mashirika ya kijamii kama vile Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO), Wakala wa Kimataifa wa Marekani wa Maendeleo ya Kimataifa (USAID) na Mpango wa Ukimwi wa Umoja wa Mataifa (UNAIDS) hazijafaulu kukabiliana na changamoto za kiafya.

Fasihi ya Kiswahili ya Watoto pia ina jukumu la kuangazia suala la afya ambalo ni muhimu katika kuafikiwa kwa maendeleo endelevu katika mataifa mbalimbali. Stakabadhi na ruwaza za kimataifa kama vile Malengo ya Milenia 2015 zilibuniwa ili kukabiliana na changamoto za kiafya ulimwenguni. Malengo ya Milenia 2015 yanahimiza uimarishaji wa viwango vya afya kwa kumaliza umasikini, janga la njaa na kuwepo kwa maji safi. Malengo ya maendeleo endelevu 2015 yamehimiza uimarishaji wa afya katika jamii kufikia mwaka wa 2030. Ajenda 2063 ya Afrika Tunayoitaka, imeangazia uimarishaji wa afya katika mataifa ya Kiafrika kwa kuimarisha huduma za afya, usafi, lishe bora na maji safi. Nchini Kenya, Ruwaza ya 2030 na Katiba ya Kenya 2010 pia zinatambua umuhimu wa afya katika kuimarisha uchumi wa nchi na kuafikiwa kwa maendeleo endelevu. Kifungu cha 43(1) cha Katiba ya Kenya 2010 kinahimiza haki ya kila Mkenya kupata huduma bora za kiafya. Mifumo ya kielimu nchini Kenya pia imeangazia suala la afya. Wizara ya Elimu nchini Kenya iliidhinisha kujumuishwa kwa mafunzo ya afya kupitia Fasihi ya Kiswahili ya Watoto (Wizara ya Elimu, 2002). Mtaala wa Kiumilisi nchini Kenya pia umependekeza matumizi ya hadithi, drama na nyimbo katika ufundishaji wa masuala ya afya kama vile, usafi, lishe bora na athari za magonjwa kwa binadamu. Hadithi, drama na nyimbo ni miongoni mwa vipera vyafFasihi ya Kiswahili ya Watoto vinavyotumia sitiari katika mawasiliano

Kazi za fasihi ya Kiswahili za Watoto zimetungwa kiufundi hivi kwamba zinavutia na hunasa makini ya wasomaji. Matumizi ya sitiari kama mbinu ya kiulinganishi katika kazi za kifasihi hunasa makini ya hadhira na hurahisisha uelewa wa ujumbe. Kwa

mujibu wa Johnson na Lakoff (1980), sitiari huwasilisha vitu viwili tofauti kwa njia ya ulinganifu. Sitiari hulinganisha kiumbe au vitu mbalimbali pasipo kutumia maneno ya kulinganisha kama vile, mithili ya, kama, na ja. Aidha, usemi wa kisitiari unaweza kuwa wa kinathari au kishairi unaotumia neno au maneno kurejelea maana ya dhana fulani nje ya maana yake ya kawaida. Ingawa sitiari huwa na maana tata, Lakoff (1992) anasema kuwa sitiari ni dhana kongwe na imekuwepo tangu enzi za Aristotle. Akiafikiana na maelezo haya, Mbatiah (2001) anasema kuwa sitiari hulinganisha vitu viwili vilivyotofautiana kitabia na kimaumbile, vinavyohusiana kwa njia tofauti. Ulinganishi huu huleta uwazi na kutilia mkazo maelezo yanayotolewa. Sawa na Mbatiah (keshatajwa), Wamitila (2003, 2008) na Tehseen na Khan (2015) wanafafanua sitiari kama usemi unaoeleza sifa za kitu kwa kukilinganisha na kingine bila kutumia maneno yanayolinganisha. Katika utafiti huu, sitiari ilirejelewa kama neno, kifungu cha maneno, sentensi au kisa kinachoangazia suala fulani kwa njia ya kiulinganishi bila kutumia maneno ya kulinganisha.

Fani ya sitiari ilichaguliwa katika utafiti huu kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo. Mosi, sitiari huwa na sifa ya kiulinganishi. Sifa hii humwezesha mwandishi kuwasilisha masuala mtambuko yanayochukuliwa kuwa mwiko katika jamii kwa njia inayokubalika (Kobia, 2008). Pili, sitiari ni fani pana na inaweza kubeba fani zingine kama vile tashibihi, jazanda au methali (Fadhili, 2014). Mathalan, kuna wakati ambapo jazanda au methali inaweza kutumiwa kama sitiari kulingana na muktadha wa matumizi. Tashbihi pia inaweza kuwa na kipengele cha sitiari katika muundo wake. Katika tashibihi: “Hatari kama simba,” neno simba katika tashibihi hii ni sitiari. Upekee huu umemwezesha mtafiti kuchunguza mtindo uliotumika kuwasilisha sitiari za kiafya katika matini teule za fasihi ya Kiswahili ya Watoto.

Sitiari pia hurahisisha uelewa wa dhana changamano kwa kuilinganisha na kitendo au jambo la kawaida linaloeleweka na hadhira (Wamitila, 2008). Katika kufanya hivi sitiari hutoa uwakilishi wa kuona au hisia inayosaidia ufahamu wa jambo hilo. Sitiari inapotumika kwa ufasaha katika mawasiliano, huzua taswira za mambo au jambo linalozungumziwa na kurahisisha uelewa na kukumbukika kwake. Matumizi ya sitiari katika mawasiliano huleta ulinganifu unaoeleweka kati ya dhana dhahania kwa kuilinganisha na hali halisi. Sifa nyingine zinazochochea matumizi ya sitiari ni uwezo

wake wa kuzua ubunifu, kuchochea uvumbuzi, kuibua mawazo mapya na fikra makini. Sifa hii ni muhimu katika kubuni sitiari za kiafya kama istilahi za Kiswahili zilizotumika kurejelea masuala ya kiafya. Isitoshe, matumizi ya sitiari huchochea uvumbuzi, ubunifu na kuibua mawazo mapya. Mawazo haya ni muhimu kwani yalimwezesha mtafiti kufafanua masuala mtambuko katika matini teule na kutafakari njia mwafaka za kusuluhisha changamoto za kiafya kama inavyoangaziwa katika vitabu teule.

Vitabu teule vilivyoshughulikiwa katika kazi hii ni: *Siku ya Ukimwi* (John Kobia, 2008), *Sitaki Iwe Siri* (Bitugi Matundura, 2008), *Madhila ya Bi*. *Shufaa* (Nuhu Bakari, 2008), *Pendo katika Shari* (Clara Momanyi, 2008), *Kosa la Marehemu* (Andrew Panja, 2010) na *Nimefufuka* (Rebecca Nandwa, 2011). Vitabu teule vimo katika msururu wa "Afya Yangu." Msururu huu unajumuisha vitabu vya fasihi ya Kiswahili ya Watoto vinavyoangazia masuala ya kiafya. Waandishi wa matini hizi wametumia tamathali za semi kama vile sitiari kuangazia masuala ya kiafya yanayochukuliwa kuwa mwiko katika baadhi ya tamaduni za jamii. Kwa mujibu wa Kobia (2008), ni mwiko katika baadhi ya jamii za kiafrika kuhusishwa na magonjwa kama vile UKIMWI na matumizi ya lugha ya kisitiari humwezesha mwasilishaji kupasha ujumbe unaohusu magonjwa kama hayo kwa lugha inayokubalika. Utafiti huu ukalenga kuchanganua sitiari za kiafya katika matini teule na kutathmini nafasi yake katika kusuluhisha matatizo ya kiafya.

**1.2 Suala la Utafiti**

Changamoto za kiafya kama vile ukosefu wa lishe bora, huduma duni za kiafya na magonjwa mbalimbali zimeathiri afya ya binadamu na kulemaza kuafikiwa kwa maendeleo endelevu katika mataifa mengi duniani. Licha ya taaluma za kisayansi, mashirika ya kiafya na mataifa yaliyoendelea kujitolea kukabiliana na changamoto za kiafya kwa kutoa ufadhili wa kifedha, dawa, vyakula na ushauri wa kitaaluma, suala la afya bado lingali tatizo kuu katika nchi nyingi. Katika kuchangia suluhu kwa matatizo ya kiafya, kuna haja ya kuhusisha taaluma ya fasihi ya Kiswahili ya Watoto katika kuchanganua masuala ya kiafya, kwa sababu lugha inaweza kuwa kikwazo katika usambazaji wa habari kuhusu huduma za kiafya katika jamii. Utafiti huu ulilenga

kuchanganua sitiari za kiafya katika matini teule za fasihi ya Kiswahili ya Watoto na kutathmini nafasi yake katika kusuluhisha matatizo ya kiafya.

**1.3 Malengo ya Utafiti**

Malengo yafuatayo yaliongoza utafiti huu:

i. Kujadili aina za sitiari za kiafya katika vitabu viteule vya Fasihi ya Kiswahili ya Watoto.
ii. Kuchunguza mtindo uliotumika kuwasilisha sitiari za kiafya katika vitabu viteule vya Fasihi ya Kiswahili ya Watoto.
iii. Kufafanua masuala mtambuko yanayowasilishwa na sitiari za kiafya katika vitabu viteule vya Fasihi ya Kiswahili ya Watoto.

**1.4 Maswali ya Utafiti**

Utafiti huu uliongozwa na maswali haya:

i. Ni sitiari zipi za kiafya zimetumika katika vitabu viteule vya Fasihi ya Kiswahili ya Watoto?
ii. Mtindo umetumika vipi kuwasilisha sitiari za kiafya katika vitabu viteule vya Fasihi ya Kiswahili ya Watoto?
iii. Ni masuala mtambuko yapi yaliyowasilishwa na sitiari za kiafya katika vitabu viteule vya Fasihi ya Kiswahili ya Watoto?

**1.5 Umuhimu wa Utafiti huu**

Utafiti huu umebainisha nafasi ya fasihi ya Kiswahili ya Watoto katika kufafanua matatizo ya kiafya yanayoathiri jamii kama vile magonjwa na ukosefu wa lishe bora na kuelezea njia mbalimbali za kuyasuluhisha. Jukumu hilo limesawiri fasihi ya Kiswahili ya Watoto kama taaluma mbadala ya kushughulikia masuala ya kiafya. Kulingana na stakabadhi za kitaifa na kimataifa kama vile Katiba ya Kenya 2010 na Malengo ya Milenia 2015, na malengo ya maendeleo endelevu 2015 kuna haja ya kuimarisha viwango vya afya ulimwenguni ili kuwezesha kuafikiwa kwa maendeleo endelevu. Bila afya hakuna maendeleo endelevu.

Kazi hii pia imebainisha dhima ya kutumia lugha ya kisitiari katika kuangazia masuala ya kiafya yanayochukuliwa kuwa mwiko katika jamii. Baadhi ya masuala haya ni

magonjwa kama vile UKIMWI na Saratani ambayo baadhi ya watu hawapendi kuhusishwa nayo kwa kuogopa kutengwa na jamii. Umuhimu wa kutumia lugha ya kisitiari ni kwamba, magonjwa kama hayo yameangaziwa bila kuathiri hadhi ya mwathiriwa kwa sababu lugha ya kisitiari hupunguza makali yanayosababishwa na matumizi ya lugha ya kawaida.

Kazi hii imekuza na kuendeleza matumizi ya istilahi za kisitiari katika fasihi ya Kiswahili ya Watoto kwa kupanua mawanda ya matumizi yake katika kuchanganua masuala ya kiafya na kufafanua aina na miundo ya sitiari za kiafya. Mathalan, utafiti huu umechanganua aina mbalimbali za sitiari za kiafya na maana zake jambo lililo na faida kwa walimu na wanafunzi wa lugha ya Kiswahili. Ili kufahamu ujumbe unaowasilishwa na sitiari za kiafya, msikilizaji au msomaji anapaswa kuwa na ufahamu wa matumizi ya sitiari katika miktadha mbalimbali jambo lililofafanuliwa kwa kina katika utafiti huu.

Matokeo ya utafiti huu ni muhimu kwa wakuza sera na mitaala ya Kiswahili inayohusu masuala ya kiafya kwa sababu changamoto mbalimbali za kiafya na njia za kuziboresha zimebainishwa. Fauka ya hayo, utafiti huu umechangia katika kuongezea istilahi za Kiswahili zinazorejelea masuala mtambuko hasa masuala ya kiafya. Sitiari za kiafya zilizotambuliwa zimejaza pengo la utafiti linalohusu ufahamu wa sitiari za Kiswahili zinazoangazia masuala ya kiafya. Aidha, utafiti huu umepanua mawanda ya matumizi ya kazi za fasihi ya Kiswahili ya Watoto katika kufundisha shuleni. Hatua hii itachochea Wizara ya Elimu nchini Kenya, kujumuisha vitabu vya fasihi ya Kiswahili ya Watoto katika sera ya serikali ya kupeana vitabu shuleni.

Washikadau waliotwikwa majukumu ya kushughulikia masuala ya kiafya kama vile Shirika la Afya Ulimwenguni wamefahamishwa kuhusu njia mbadala ya kukabiliana na changamoto za kiafya. Baadhi ya njia hizi ni kununua au kufadhili uandishi wa vitabu vinavyohusu masuala ya kiafya, ili wasomaji wapate maarifa mapya ya kusuluhisha changamoto za kiafya. Katika kufanya hivyo, jukumu la kuimarisha viwango vya afya katika jamii limepanuliwa kwa kuwahusisha waandishi wa fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Watoto hujumuisha idadi kubwa katika jamii na walipaswa kuhusishwa katika mpango wa kuimarisha afya. Hali kadhalika, kazi hii ni marejeleo

muhimu kwa wasomi na watafiti wa baadaye katika nyanja ya fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Imejaza pengo la uhaba wa tafiti za fasihi ya Kiswahili ya Watoto zinazoangazia sitiari za kiafya.

**1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Utafiti huu ulijikita katika fasihi Andishi ya Kiswahili ya Watoto. Mtafiti alichanganua sitiari za kiafya katika vitabu teule vya fasihi ya Kiswahili ya Watoto vinavyohusu masuala ya kiafya. Vitabu vilivyochanganuliwa ni: *Siku ya Ukimwi* (John Kobia, 2008), *Pendo katika Shari* (Clara Momanyi, 2008), *Sitaki Iwe Siri* (Bitugi Matundura, 2008), *Madhila ya Bi*. *Shufaa* (Nuhu Bakari, 2008), *Kosa la Marehemu* (Andrew Panja, 2010) na *Nimefufuka* (Rebecca Nandwa, 2011). Uchanganuzi wa matini teule ulijikita katika ubainishaji wa aina za sitiari za kiafya zilizotumika katika vitabu teule, uchunguzi wa mtindo uliotumiwa kuziwasilisha na ufafanuzi wa masuala mtambuko yaliyowasilishwa na sitiari za kiafya zilizotambuliwa. Aina za sitiari za kiafya zilizotambuliwa, mitindo ya uwasilishaji na masuala mtambuko yaliyobainishwa ndio yalikuwa data ya utafiti. Pia, maandishi muhimu yaliyohusiana na suala la utafiti yaliyopatikana katika maktaba za Vyuo Vikuu vya Nairobi, Kenyatta, Chuka na Bewa la Igembe na programu muhimu katika mtandao zilizoangazia masuala ya kiafya yalirejelewa.

## 1.7 Maelezo ya Istilahi

Yafuatayo ni maelezo ya istilahi muhimu zitakazotumiwa katika utafiti huu.

**Afya Yangu** Ni msururu wa vitabu vya fasihi ya Kiswahili ya Watoto vinavyoangazia masuala ya afya.

**Afya** mgonjwa, na wenye nguvu ya kufanya kazi katika mazingira mbalimbali.

**Nadharia Changanuzi ya Sitiari ya Dhana** Nadharia inayohusika na uchanganuzi wa matumizi ya sitiari katika kazi za kifasihi.

**Fasihi ya Watoto ya Kiswahili** Kazi ya fasihi ambayo imeandikwa kwa Kiswahili ili isomwe na watoto wa miaka sita hadi kumi na minane.

**Fasihi ya Watoto** Kazi ya kifasihi iliyoandikiwa watoto wa miaka sita hadi kumi na minane.

**Matini :** Hadithi za watoto zinazorejelea masuala ya kiafya.

**Mtambuko :** Suala la dharura linaloathiri maisha ya jamii.

**Mtoto :** Ingawa sheria ya Kenya inamrejelea mtoto kama mtu aliye na umri wa miaka chini ya kumi na minane, utafiti huu umemrejelea mtoto kama mwanafunzi wa shule ya msingi aliye na miaka chini ya kumi na sita.

**Sitiari za Kiafya** Neno, kifungu cha maneno, sentensi au kisa kinachorejelea suala la kiafya kwa njia ya kiulinganishi.

**Mtindo :** Tamathali za semi, nyimbo, barua na usimulizi uliotumika kuwasilisha sitiari za kiafya katika matini teule.

**Umitindo:** Nadharia inayochunguza mtindo uliotumika kuwasilisha kazi ya kifasihi.

# SURA YA PILI

# MWAUO WA MAANDISHI

## 2.1 Nafasi ya Fasihi ya Watoto katika kufafanua Sitiari za Kiafya

Sanaa mbalimbali za kifasihi zimetungwa zikilenga hadhira ya watoto na watu wazima. Kwa mujibu wa Nodelman (2008), sanaa ya fasihi ya watoto hutungwa ili isomwe na watoto. Baadhi ya sanaa hizi ni semi, nyimbo, ngano, ushairi na sanaa jadiya kama vile matambiko, visasili, mazimwi na zihiri (Wamitila, 2008). Sanaa hii ina sifa bainifu zinazoitambulisha kama vile kuwepo kwa visa vichache, matumizi ya fantasia, kuwepo kwa jasira, msuko mwepesi wa kazi na uchache wa wahusika. Katika uchambuzi wa kazi hizi, mhakiki huchanganua aina ya usimulizi uliotumika, wahusika na uhusika, muundo, mtindo, dhamira na maudhui (Wamitila, 2008). Yumkini, Bakize (2014) amesisitiza kuwa fasihi ya watoto inapaswa kusomwa na watoto. Hata hivyo, upungufu uliopo katika fafanuzi za wataalamu hawa umetokana na madai kwamba fasihi ya watoto imelenga kusomwa tu na watoto. Ukweli ni kwamba, fasihi hii inapaswa kusomwa na kila mtu kwa sababu masuala yaliyoangaziwa yana umuhimu kwa watu wote. Pia fasihi ya watoto huchanganuliwa kinadharia kama kazi zingine za kifasihi. Miongoni mwa masuala yanayoshughulikiwa katika fasihi ya watoto ni afya, mazingira na haki za binadamu (Ngugi, 2016). Hivyo, fasihi hii inahitaji kusomwa na wanajamii wote bila kujali mipaka ya kiumri.

Ari ya kutalii fasihi ya watoto kumechochea tafiti mbalimbali za fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Mpesha (1995) alichunguza namna fasihi ya watoto ilivyoendelea Tanzania na uwezo wake wa kukuza ubunifu baina ya watoto na kubainisha ya kwamba, watoto huathirika kitabia baada ya kutangamana na kazi za kifasihi. Hata hivyo, athari inayotokana na usomaji wa kazi za fasihi haitadhihirika ikiwa wasomaji hawana umilisi wa lugha tumizi. Bila umilisi wa lugha ni vigumu kuelewa yaliyomo. Kwa jinsi hii, fasihi ya watoto inapaswa kuchanganuliwa kwa kina ili wasomaji waweze kufahamu masuala muhimu yaliyoangaziwa na jinsi yanavyoathiri mwonoulimwengu wa mtoto. Tofauti iliopo ni kuwa utafiti huu ulihusu uchanganuzi wa sitiari za kiafya katika matini teule za fasihi ya Kiswahili ya Watoto ilhali wa Mpesha ulihusu maendeleo ya fasihi ya watoto Tanzania. Umefaidika na kazi ya Mpesha (keshatajwa) kwa kupata maarifa kuhusu dhima ya kusoma na kuelewa kazi za kifasihi kwa kina ili mchanganuzi afanikiwe katika uhakiki wa kazi anayochanganua.

Muriungi (2006) amehimiza haja ya watoto kusoma hadithi za ukweli zinazohusu watu wazima ambao wanaweza kuwaiga kwa sababu utoto ni ngazi ya kufikia utu uzima. Hoja hii ni muhimu katika uchanganuzi wa matini teule kwani wahusika wengi katika matini hizi ni watu wazima wanaoweza kuaminiwa na watoto. Isitoshe, kulingana na Muriungi (keshatajwa) hadithi za watoto hutungiwa katika mazingira tofautitofauti kama vile ya kisiasa kulingana na jinsi ulimwengu unavyobadilika. Hivyo, mazingira ya hadithi hizo huwa ya kweli na kuaminika. Tofauti na utafiti unaofanywa Muriungi (keshatajwa) hakuangazia suala la afya ilhali afya ni muhimu katika maendeleo ya jamii. Hata hivyo, utafiti huo una manufaa kwa sababu umeangazia masuala yaliyobadili mwonoulimwengu wa wanajamii kama vile uanariadha na usanii ambao unakuza ushujaa. Afya pia ni suala linalozua ushujaa kwa wanaochukulia usafi na vita dhidi ya magonjwa kama suala muhimu. Usafi wa mazingira na wa mtu binafsi ni baadhi ya masuala ya kiafya yanayoathiri jamii na yanastahili kushughulikiwa kwa jicho la kifasihi. Isitoshe, usafi wa mazingira na wa mtu binafsi ni muhimu katika kuzuia magonjwa kama vile Homa ya Matumbo na Kipindupindu.

Mwikali na Furaha (2014) walichunguza fani za fasihi zinazoibua fantasia katika ngano za watoto za Nyambura Mpesha na kutambua kuwa, fasihi huwawezesha watoto kuimarisha tabia zao na kuepuka mienendo isiyofaa. Hii ina maana kuwa, watoto wanaposoma hadithi zinazohusu masuala ya kiafya wanapata mafunzo kuhusu namna ya kuepuka mambo yanayowaathiri kiafya. Hata kama utafiti huo ulishughulikia hadithi nyingi za kifantasia, wanyama na viumbe wanaotumiwa katika hadithi za watoto ni viwakilishi vya wanajamii na uhalisia uliopo katika jamii. Uhusiano uliopo na utafiti huu ni kwamba, Mwikali (keshatajwa) alionyesha mchango wa sitiari katika kuzua fantasia jambo lililosaidia katika kuelewa maana ya sitiari za kiafya kwa undani. Tofauti iliopo ni kwamba, utafiti huo ulijikita katika mazingira ya kifantansia ilhali huu unahusu hali halisi inayojitokeza katika mazingira ya kiafya bila kutilia chuku. Utafiti huo pia ulisaidia kufafanua jinsi kipengele cha sitiari kilivyotumika kujenga maudhui ya kiafya katika matini teule za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Ufahamu huu ulimwezesha mtafiti kutambua istilahi mbalimbali za sitiari za kiafya.

Ni muhimu kutambua kuwa watoto wana tajriba mbalimbali katika kuelewa na kuipa maana kazi fulani ya kifasihi hasa wanaposoma hadithi zinazowahusu. Hata hivyo,

watoto wanapaswa kuelekezwa katika kusoma hadithi hizi ili wazihakiki ipasavyo. (Ngugi, 2016). Umuhimu wa utafiti wa Ngugi (keshatajwa) kwa huu ni kwamba, umeangazia ngazi tano za kuzingatiwa katika uchanganuzi wa kazi za kifasihi. Hizi ni ngazi ya uchambuzi, mwingiliano matini, urejelezi wa kibinafsi, uwazi na utendaji. Ngazi ya uchambuzi iliongoza katika uchanganuzi wa matini teule na kubainisha usawiri wa sitiari za kiafya zilizotumika na nafasi yake katika kuangazia masuala ya kiafya. Ngazi ya urejelezi wa kibinafsi ilimwezesha mtafiti kurejelea matukio ya hadithini yaliyoangazia changamoto za kiafya na kuyalinganisha na matukio halisi katika ulimwengu wa kawaida, ili kutoa kauli ya kweli kuhusu athari za matatizo ya kiafya na namna ya kuzisuluhisha.

Fasihi ya watoto pia ina uwezo wa kuathiri tabia ya msomaji na kumwezesha kuelewa masuala mbalimbali yaliyomo katika jamii (Mbuthia, 2018). Hivyo, kuna uwezekano wa msomaji kubadili mienendo na tabia yake kutokana na aina ya fasihi aliyoisoma. Umuhimu wa kauli hii ni kwamba imeangazia nafasi ya fasihi katika kupanua mwonoulimwengu wa msomaji. Ingawa Mbuthia (keshatajwa) alichunguza jinsi fasihi ya watoto ilivyoathiri mwonoulimwengu wa mtoto tofauti na huu unaoshughulikia sitiari za kiafya, maarifa yaliyotokana na utafiti huo yalimwezesha mtafiti kupambanua changamoto mbalimbali za kiafya katika matini teule na kubainisha njia mwafaka za kuzisuluhisha.

## 2.2 Athari za Kiafya Katika Jamii

Afya ni miongoni mwa masuala mtambuko yaliyoangaziwa katika fasihi ya watoto. Hii ni kwa sababu afya ni muhimu katika maisha ya binadamu kwa jinsi inavyoimarisha kinga dhidi ya maradhi mwilini na uwezo wa kufanya kazi. Kwa upande mwingine, afya duni husababisha majonjwa na ukosefu wa nguvu za kufanya kazi. Katika juhudi za kupunguza athari zilizotokana na matatizo kiafya, mashirika na wataalamu mbalimbali wamejitokeza kushughulikia suala la afya kwa kupeana ushauri wa kitaaluma kuhusu namna ya kuzuia matatizo ya kiafya, kupeana vyakula, fedha na mawaidha kupitia maandishi mbalimbali.

Madhara yaliyotokana na kozorota kwa afya kama vile magonjwa ya Kifua Kikuu, Malaria na Mafua ya Ndege yameathiri afya ya binadamu na kulemaza uwezo wake wa

kufanya kazi. Kwa jinsi hii, Garret (2007) alidai kuwa jamii iliyoathiriwa na matatizo ya kiafya hubaki nyuma kimaendeleo na kutatiza juhudi za kuafikiwa kwa maendeleo endelevu katika mataifa mengi. Pia, kuongezeka kwa matatizo ya kiafya kumesababishwa na uhaba wa wahudumu wa kutosha wa kiafya. Kwa mfano, kulingana na Garret (keshatajwa) kulikuwa na uhaba wa wahudumu wa kiafya takribani watu milioni nne kote ulimwenguni katika mwaka wa 2007. Utafiti huo uliangazia madhara yaliyosababishwa na huduma duni za kiafya zilizotia maisha ya binadamu hatarini. Pia, ulionyesha dhima ya afya nzuri kwa binadamu na jinsi ya kusuluhisha changamoto za kiafya. Ingawa utafiti huo si wa kifasihi, umezua suala la kiusomi kuhusu jinsi ya kushughulikia changamoto za kiafya kupitia taaluma zingine kama vile fasihi ya Kiswahili ili kushadidia juhudi za taaluma za kisayansi zinazoshughulikia masuala ya kiafya.

Aghalabu, kuzorota kwa afya kumesababisha matatizo si haba katika maisha ya binadamu. Miongoni mwa matatizo haya ni ukosefu wa lishe bora na kuzuka kwa magonjwa mbalimbali (Garret, 2013). Matatizo haya pia yamesababisha matumizi ya rasilmali nyingi za jamii ili kupata matibabu bora na lishe nzuri. Kwa mfano nchini Marekani, jumla ya dola bilioni sita zimetumika kutibu magonjwa mbalimbali nchini humo katika mwaka wa elfu mbili na moja. Kutokana na kuongezeka kwa matatizo ya kiafya, Jumuia ya Mataifa ya Ulimwengu iliibuka na malengo ya Milenia 2015 ili kushughulikia masuala ya kiafya miongoni mwa mengine. Ingawa utafiti huo uliangazia suala la afya kwa ujumla, Garret (keshatajwa) alifafanua athari za afya katika maisha ya binadamu na jinsi ya kusuluhisha matatizo ya kiafya. Matatizo ya kiafya ni miongoni mwa masuala mtambuko yaliyochunguzwa katika utafiti huu. Mtafiti alijaza pengo hili kwa kuchunguza namna sitiari za kiafya zilivyotumika kutatua matatizo ya kiafya katika matini teule za fasihi ya Kiswahili ya Watoto.

Wanjala (2015) alichunguza namna usawiri wa malezi unavyoathiri utambulisho wa vijana katika Riwaya ya Kiswahili na kubainisha majukumu muhimu yanayotekelezwa na wazazi katika kuimarisha afya ya watoto.  Baadhi ya majukumu hayo ni kuwapa watoto malezi mazuri, huduma nzuri za kiafya, makazi mema na mavazi yanayofaa. Utafiti huo ni muhimu kwa sababu uliangazia suala mtambuko la afya lililoangaziwa katika utafiti huu. Kwa mujibu wa Wanjala (keshatajwa) watoto waliolelewa vyema

wana afya nzuri inayowawezesha kujikinga na magonjwa. Utafiti huo pia unasisitiza dhima ya kuelimisha jamii kuhusu njia bora za kuimarisha afya ya binadamu kama vile kufahamu njia mwafaka za kuzuia maradhi, kula lishe bora na ufahamu wa huduma nzuri za kiafya. Maarifa haya yalimwezesha mtafiti kufahamu njia zinazotekelezwa na asasi ya elimu na familia katika kuboresha changamoto za kiafya, hivyo kubaini mbinu mwafaka za kuzingatia katika kusuluhisha matatizo ya kiafya kwa mujibu wa vitabu teule vya Fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Tofauti tu iliyopo ni kwamba, utafiti huo uliangazia nafasi ya asasi za familia na elimu kwa ujumla katika kuimarisha afya ya watoto, ilhali utafiti huu ulichunguza nafasi ya sitiari za kiafya katika kusuluhisha matatizo ya kiafya katika matini teule za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto.

Ripoti ya Shirika la Afya Ulimwenguni (2018) pia imeangazia changamoto zinazoathiri afya ya umma ulimwenguni. Miongoni mwa changamoto hizi ni ukosefu wa wahudumu wa afya, uhaba wa rasilimali za kuboresha vituo vya afya, unywaji wa pombe, matumizi ya tumbaku na ukosefu wa mazoezi ya viungo. Kwa mujibu wa ripoti hiyo, wanawake wameathiriwa zaidi na ukosefu wa mazoezi ya viungo ilhali wanaume wamejihusisha na unywaji wa pombe. Changamoto hizi zimeathiri asasi ya jamii na kuchangia katika kulemaza kuafikiwa kwa maendeleo endelevu katika mataifa mbalimbali. Hivyo, uangafu wa athari za kiafya na Shirika La Afya Ulimwenguni (keshatajwa) ulikuwa muhimu katika kuchanganua athari za kiafya zilizoshughulikiwa katika vitabu viteule. Ingawa utafiti huo si wa kifasihi, elimu kuhusu suala la afya inapaswa kuangaziwa na kufunzwa kwa kutumia mbinu mseto zikiwemo taaluma za kisayansi na kifasihi ili kunufaisha watu wengi. Ufahamu wa sitiari za kiafya katika bunilisi teule unasaidia kusambaza ujumbe wa kiafya kwa watu wengi kwa kuwajumuisha waandishi na wasomi wa fasihi.

Vilevile, upungufu wa istilahi za Kiswahili za kiafya kumeathiri maendeleo katika huduma ya afya. Odhiambo na Mars (2018) walithibitisha haya, walipochunguza jinsi watu wanavyoelewa na kutafsiri maneno ya kiafya ya Kiingereza kwa lugha ya Kiswahili. Walitambua kwamba, baadhi ya maneno ya Kiingereza yanayorejelea masuala ya afya yasingetafsiriwa kwa Kiswahili. Mathalan, maneno mengine yalikuwa na maana tatanishi baada ya kutafsiriwa. Pia, baadhi ya watu hawakuelewa maana ya maneno yaliyotafsiriwa. Ingawa utafiti huo ulifanyiwa Kaunti ya Kilifi ambako

wazungumzaji wengi ni Waswahili, wengi wao hawakufahamu istilahi mwafaka za Kiswahili zinazorejelea masuala ya kiafya. Hii ni dhihirisho kwamba, kuna tofauti kati ya lugha ya kawaida ya mawasiliano na lugha ya kitaaluma. Utafiti huo unazua pengo la kiutafiti, ambapo kuna haja ya kubuni istilahi za Kiswahili zinazorejelea taaluma ya afya ili kurahisisha mawasiliano. Utafiti huu ulishadidia katika kuongezea istilahi za Kiswahili zinazorejelea masuala ya kiafya. Baadhi ya istilahi hizi ni sitiari za kiafya zilizochanganuliwa katika matini teule za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto.

Adzo (2022), alichunguza matumizi ya Kiswahili na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika huduma za Afya nchini Kenya na kutambua umuhimu wa kuwa na istilahi maalumu za Kiswahili, zitakazotumiwa katika TEHAMA ya afya. Istilahi za Kiswahili za kiafya zitawawezesha wagonjwa kuelewa masuala ya kiafya yanayowaathiri. Alibaini kuwa, wasailiwa wengi walipendelea matumizi ya Kiswahili katika kuangazia masuala ya kiafya kwa sababu lugha ya Kiswahili ilitumika kuendeleza programu mbalimbali katika TEHAMA ya afya. Ilidhihirika kuwa, ukosefu wa istilahi mwafaka za Kiswahili za kiafya baina ya waandalizi wa programu za kiafya na wahudumu wa kiafya kulitatiza kuafikiwa kwa uamuzi huo. Ilibainika kuwa, mara nyingine wahudumu wa kiafya walitumia lugha ya Kiingereza walipokosa istilahi mwafaka za Kiswahili. Hivyo, Adzo (keshatajwa) alipendekeza kujumuishwa kwa Kiswahili katika moduli ya mafunzo ya wataalamu wa afya, ili wafahamu istilahi mwafaka za kiafya za Kiswahili. Ingawa utafiti huo unahusu mawasiliano katika TEHAMA, umefafanua dhima ya kubuniwa kwa istilahi za Kiswahili katika taaluma mbalimbali ili kurahisha mawasiliano. Hili ni pengo lililojazwa na matokeo ya utafiti huu, uliolenga kubainisha istilahi mbalimbali za sitiari za kiafya katika vitabu teule vya Fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Ubainishaji wa sitiari za kiafya katika vitabu teule unarahisisha uelewa wa masuala ya kiafya baina ya wanajamii.

### 2.3 Aina na Matumizi ya Sitiari katika Kazi za Kifasihi

Dhana ya sitiari imefafanuliwa na wasomi katika kazi mbalimbali. Simala (2000) anafafanua sitiari kama tamathali ya usemi inayolinganisha hulka ya kitu au jambo fulani na hali kamili ya kitu au jambo lingine. Ingawa anatoa ufafanuzi huu, anasema kuwa sitiari ni dhana tata na haina maana moja pekee. Sitiari moja inaweza kuwa na maana tofautitofauti kulingana na muktadha wa matumizi yake na malengo ya

mwandishi. Maana hii huangaziwa kwa njia mbili. Njia ya kwanza ni kueleza maana ya sitiari kulingana na muundo wa nje, ambapo maana huelezwa kwa kuangazia maana ya maneno yaliyounda sitiari hiyo. Katika njia ya pili, maana ya ndani inayowasilishwa na sitiari fulani huangaziwa. Mbatiah (2001) anatoa maelezo sawa na haya anaposema ya kwamba, sitiari hulinganisha vitu viwili vilivyotofautiana kitabia na kimaumbile kwa njia tofauti isiyo ya moja kwa moja. Ulinganishi wa aina hii huleta udhahiri na msisitizo katika maelezo. Fafanuzi za wataalamu hawa zinadhihirisha utata uliopo katika maana ya sitiari. Tathmini ya fafanuzi hizi ni kwamba sifa ya ulinganishi ndiyo inatawala katika fasili ya sitiari. Katika utafiti huu sitiari ilifafanuliwa kama dhana inayolinganisha hulka, vitu au watu bila kutumia maneno ya kiulinganishi. Sitiari hizi zinaweza kuwa maneno, vifungu vya maneno, sentensi, aya, ubeti au kazi nzima ya kifasihi iliyoandikwa. Utafiti huu uliangazia maana ya ndani inayowasilishwa na sitiari za kiafya katika matini teule za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto.

Wamitila (2003, 2008), amefafanua dhana ya sitiari, aina za sitiari na uainishaji wake. Anasema kuwa, ulinganifu uliopo katika sitiari ni wa kueleza uzuri au ubaya wa kitu fulani kwa kukilinganisha na kingine. Ulinganishi huu si dhahiri kwa sababu hautumii maneno ya kulinganisha: ja, kama, mithili ya, miongoni mwa mengine. Pia, anasema kwamba Sitiari huainishwa kwa kuzingatia vigezo vya kimuundo, kimawazo, na kimtindo. Katika kigezo cha kimuundo, sifa kuu inayozingatiwa ni namna sitiari imeundwa kama vile kurudia neno, virai au sentensi. Nazo sitiari za kimawazo zinahusisha fikira ilhali zile za kimtindo huangazia jinsi mtindo ulivyotumiwa katika fasihi. Kauli hizi zina manufaa kwa kazi hii kwani baadhi ya masuala yaliyochunguzwa ni aina na miundo ya sitiari za kiafya zilizotumika katika matini teule. Mawazo haya yalikuwa msingi wa kuchanganua aina za sitiari za kiafya katika matini teule kwa kuchunguza aina zake, muundo wake na maana zinazowasilisha kulingana na malengo ya utafiti huu.

Kobia (2008) alichunguza aina za sitiari zilizotumiwa na jamii ya Oluluyia kurejelea ugonjwa wa UKIMWI na kubaini kuwa, sitiari kama mbinu ya mawasiliano hueleza kitu fulani kwa kukilinganisha na kingine. Aidha, sitiari inaweza kuwasilisha ujumbe unaokisiwa kuwa mwiko katika jamii kwa mtindo tofauti unaokubalika. Alitambua kuwa ni mwiko kuhusishwa na ugonjwa wa UKIMWI katika baadhi ya jamii. Pia,

alifafanua mihimili ya nadharia Changanuzi ya Sitiari ya Dhana iliyoongoza utafiti huu. Kobia (keshatajwa) alisema kuwa, nadharia hii husaidia katika kufasiri maana ya sitiari mbalimbali katika kazi ya kifasihi. Umuhimu wa utafiti huo ni kwamba, umeangazia jinsi jamii zinavyoshughulikia masuala yaliyo mwiko katika jamii kwa kutumia maneno mbadala kuyarejelea. Kwa msingi huu, mtafiti alisoma matini teule ili afahamu sitiari zilizotumika kurejelea masuala ya kiafya. Miongoni mwa masuala haya ni UKIMWI ambao ni mwiko kuhusishwa nao baina ya wanajamii. Ingawa tafiti hizi mbili zinahusiana, utafiti huo ulichunguza sitiari zinazorejelea ugonjwa wa UKIMWI katika jamii ya Oluluyia, ilhali utafiti huu ulichanganua sitiari za kiafya katika matini teule za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto kwa kuangazia namna zilivyosawiriwa, mtindo ambao umetumiwa kuwasilisha sitiari za kiafya, na mikakati iliyozingatiwa katika kusuluhisha changamoto za kiafya.

Fauka ya hayo, sitiari ni dhana muhimu ya Isimu na ya kimsingi inayomwezesha binadamu kuelewa ulimwengu unaomzunguka. Akichanganua sitiari za mapenzi katika lugha ya Kikuyu, Gathigia (2014) anasema kuwa binadamu anatumia sitiari kwa wingi katika mawasiliano ya kila siku. Sitiari zinazotumika katika mawasiliano haya ni za aina nyingi na sitiari moja inaweza kuwasilisha maana kadhaa kulingana na mazingira ya matumizi yake, jinsia, umri na kiwango cha elimu cha watumizi wake. Kwa mfano, sitiari ya mapenzi katika utafiti huo imesawiriwa kama sehemu ya mwili au kitu kinachoonekana. Pili, mapenzi yamesawiriwa kama chanzo cha umoja na pia kama safari. Mfano huo unadhihirisha namna sitiari moja inavyoweza kuzua maana mbalimbali kulingana na mazingira na muktadha wa matumizi yake. Pia, maana hizi mbalimbali zinadhihirisha utata uliopo katika kufafanua maana ya sitiari kama ilivyoangaziwa na Simala (2000). Gathiga (keshatajwa) amechunguza matumizi ya sitiari katika muktadha wa mapenzi pekee ilhali sitari ni dhana pana na matumizi yake yanapaswa kuchunguzwa katika miktadha mbalimbali. Kwa jinsi hii utafiti huu ulichunguza matumizi ya sitiari katika muktadha wa kiafya. Wazo kwamba sitiari zinaweza kusawiriwa kwa njia tofautitofauti lina dhima katika kazi hii kwani mtafiti alichunguza usawiri wa sitiari za kiafya katika matini teule za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Hii ina maana kwamba, sitiari moja ya kiafya inaweza kusawiriwa kwa njia mbalimbali kulingana na mazingira ya matumizi yake, jinsia inayoangaziwa, mila na umri wa watumizi wa sitiari hiyo.

Gaichu (2016) alichanganua sitiari dhanifu katika methali za Kiswahili na kubaini kwamba, maana ya neno lililotumika kisitiari hutegemea muktadha wa matumizi yake na inaweza kubadilika au kubaki vilevile. Alisema ya kwamba maana kamili ya leksimu inapobadilika, maana tofauti huibuka kutokana na kaida za mawasiliano katika tambuzi na mazingira ambamo neno hilo limetokea. Vilevile, alifafanua aina za sitiari na namna ya kusimbua maana zake. Hata hivyo, pengo lililopo ni kwamba hakuangazia matumizi ya sitiari katika masuala mtambuko kama vile afya kama ilivyoshughulikiwa katika utafiti huu. Licha ya hayo, mawazo yake yalimpa mtafiti mwelekeo wa kuzingatia alipochunguza aina, maana na matumizi ya sitiari za kiafya katika matini teule kulingana na muktadha wa matumizi yake. Gaichu (keshatajwa) alichanganua sitiari dhanifu katika methali za Kiswahili, ilhali utafiti huu ulichanganua sitiari za kiafya katika matini teule za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto.

Matumizi bora ya sitiari pia hufanikisha uwasilishaji na uelewekaji wa ujumbe katika kazi ya fasihi. Mwakio (2016) alithibitisha kauli hii alipochunguza namna sitiari, tashibihi, na taashira zilivyotumika katika *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*. Alitambua kuwa ufanisi katika mawasiliano ya kisitiari utabainika tu ikiwa sitiari itatumiwa kwa ufasaha. Mawazo haya ni muhimu katika kuchunguza namna lugha ya kisitiari ilivyotumika kuwasilisha ujumbe unaohusu masuala ya kiafya katika matini teule za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Mwakio (keshatajwa) alishughulikia matumizi ya tashibihi, taashira na sitiari kwa ujumla, lakini utafiti huu ulichanganua sitiari za kiafya katika matini teule za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto.

Katika uchunguzi wao kuhusu namna maana inavyojengwa katika sitiari na tashibihi za Kiswahili, Kitundu na Malangwa (2019) walibainisha kwamba, uundaji wa maana katika sitiari huhusisha mambo matatu ambayo ni mada, kibebeo na sifabia. Mada na kibebeo huwa na uhusiano wa kisemantiki na hujengwa na nomino mbili tofauti zilizo na sifa zinazofanana. Sifa hii ya kufanana ndiyo inaibua sifabia inayokamilisha ujenzi wa maana katika sitiari husika. Licha ya hayo, utafiti huo haujafafanua kwa undani mambo yanayoathiri maana katika sitiari kama vile mazingira na muktadha wa matumizi ya sitiari hizi. Katika utafiti huu sitiari ilifafanuliwa katika muktadha wa kiafya. Hata hivyo, utafiti wao una manufaa kwa sababu unabainisha jinsi maana inavyojengwa katika sitiari. Pamoja na kufafanua aina za sitiari zinazorejelea masuala

ya kiafya, ufahamu wa jinsi maana inavyojengwa katika sitiari ni muhimu katika kuelewa masuala mtambuko yanayowasilishwa na sitiari za kiafya katika vitabu viteule. Kitundu na Malangwa (keshatajwa) walichunguza ujenzi wa maana katika sitiari kwa ujumla, ilhali upekee wa utafiti huu ni kwamba ulichanganua sitiari zinazorejelea masuala ya kiafya katika matini teule za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto.

## 2.4 Nafasi ya Sitiari katika Kuchanganua Kazi za Kifasihi

Simala (2000) alihakiki sitiari za uana katika ushairi wa Kiswahili na kutambua kuwa, matumizi yasiyofaa ya sitiari huzua dhuluma za kijinsia kama vile udhalilishwaji wa jinsia ya kike. Mathalan, jinsia ya kike imerejelewa kama chombo cha mapenzi kupitia matumizi ya sitiari kama vile ua, asali, kipusa, na dawa. Jinsia ya kiume imerejelewa kwa kutumia sitiari zinazomtukuza mwanaume kama vile fahali na simba. Tathmini ya maelezo haya ni kuwa sitiari inapotumika kwa njia isiyofaa inaweza kusababisha ubabedume na ukandamizwaji wa jinsia ya kike. Hivyo, lugha ya kisitiari inapaswa kutumiwa kwa uangalifu ili kukidhi majukumu ya lugha katika mawasiliano. Katika utafiti huu azma kuu ya matumizi ya sitiari za kiafya ni kuwasiliana kwa njia bora na inayokubalika kulingana na kaida za jamii husika. Umuhimu wa utafiti huo ni kwamba, umefafanua aina za sitiari na utendakazi wake, matumizi yasiyofaa ya sitiari ambazo zinaumbua utu wa mwanamke na kuchochea dhuluma za kijinsia kama vile ubakaji, unaoweza kusambaza maradhi ya zinaa ikiwa mbakaji ameathiriwa na magonjwa hayo. Ufahamu wa mawazo haya ulimwezesha mtafiti kuchanganua sitiari za kiafya kwa uangalifu ili kuepuka usababishaji wa mizozo ya kijinsia. Tofauti iliyopo kati ya tafiti hizi ni kwamba, Simala (keshatajwa) alihakiki sitiari zilizorejelea masuala ya kijinsia katika ushairi, lakini utafiti huu ulichanganua sitiari za kiafya katika matini teule za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto.

Sitiari kama dhana linganishi, inaweza kuwa na maana tofautitofauti kulingana na jinsi ilivyotumiwa katika kazi ya kifasihi. Kovecses (2000) alitoa hoja hii alipochunguza maana mbalimbali zinazotokana na sitiari za kihisia. Vilevile, alibaini kuwa sitiari inaweza kuwakilisha maana tofautitofauti kulingana na jinsi ilivyotumika katika miktadha mbalimbali. Alitoa mfano wa sitiari ya “mapenzi” inayoweza kutumiwa kwa maana ya moto, ushindi, lishe au mvuto. Ingawa utafiti huo ni tofauti na huu, unaangazia namna ya kutambua maana tofautitofauti za sitiari kulingana na muktadha

wa matumizi yake. Ufahamu huu ulimwezesha mtafiti kufahamu aina na maana ya sitiari za kiafya zilizotumika katika matini teule kulingana na muktadha wa matumizi yake.

Kuzmina (2013) alichunguza matumizi ya sitiari katika kiwango cha sentensi na kusema kwamba, sitiari hueleweka kwa urahisi na huweka jambo linalozungumziwa wazi inapotumika katika muundo wa sentensi. Sababu ni kwamba sentensi iliyotungwa kwa kuzingatia kaida za kisarufi huwasilisha wazo kikamilifu. Ufahamu huu ulimwezesha mtafiti kuchanganua matumizi ya sitiari za kiafya katika aina mbalimbali za sentensi. Mtafiti alibainisha sentensi za kisitiari zilizotumika katika matini teule na kufafanua jinsi zilivyotumika kuwasilisha masuala ya kiafya. Kuzmina (keshatajwa) aliangazia tu matumizi ya sitiari kwa ujumla katika kiwango cha sentensi ilhali utafiti huu ulichunguza aina za sitiari za kiafya na jinsi zilivyotumika kuwasilisha masuala ya kiafya katika matini teule za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto.

Isitoshe, Tehseen na Khan (2015) walichunguza matumizi ya sitiari katika fasihi ya watoto na kubainisha aina mbalimbali za sitiari zinazowasilisha maana kulingana na muktadha wa matumizi yake. Walifafanua namna ya kusimbua maana katika sitiari. Baadhi ya sitiari ambazo waliangazia ni sitiari dhahiri na sitiari pana. Aina hizi za sitiari pia zimetumika katika matini zilizoteuliwa kuangazia masuala ya kiafya. Dhima ya utafiti wao ni kwamba, unaelezea jinsi ya kuelewa maana inayowasilishwa na sitiari mbalimbali jambo ambalo lilitendeka katika utafiti huu. Utafiti wao uliangazia ufafanuzi wa maana ya sitiari kwa ujumla ilhali utafiti huu ulichanganua sitiari za kiafya pekee katika kuwasilisha masuala ya kiafya katika vitabu viteule vya Fasihi ya Kiswahili ya Watoto.

Imebainika pia kuwa lugha ya kisitiari hutumika kuendeleza ubagusi wa kijinsia. Anudo na Orwa (2016) walitambua haya walipochunguza aina za sitiari zinazoangazia jinsia ya kiume na kike katika nyimbo za Benga. Matokeo ya utafiti wao ni kwamba, wanawake walisawiriwa kama jinsia dhaifu kwa kutumia sitiari zilizodunisha jinsia ya kike. Wanawake walisawiriwa kama wachawi na vyombo dhaifu vinavyomtegemea mwanaume ili kupata ufanisi katika jambo lolote lile ilhali wanaume walisawiriwa kama jinsia yenye nguvu na mamlaka. Tathmini ya kauli walizotoa ni kuwa, sitiari zina

uwezo kuzua mizozo ya kijinsia kulingana na jinsi zinavyotumiwa. Hii ni tahadhari kwa watumizi wa lugha ya kisitiari katika mawasiliano, kwamba lugha hii itumiwa kwa uangalifu ili kusiwe na migawanyiko ya kijinsia katika jamii. Ingawa utafiti wao uliangazia sitiari zinazoendeleza ubagusi wa kijinsia, ni muhimu kwa sababu ulimwezesha mtafiti kufahamu aina za sitiari za kiafya zinazotumika kurejelea masuala ya kijinsia alipokuwa akichanganua sitiari za kiafya katika lengo la kwanza la utafiti huu. Ufahamu huu ulimwezesha mtafiti kuepuka matumizi ya sitiari za kiafya zilizozua migawanyiko na udhalilishwaji wa jinsia ya kike.

Uchunguzi zaidi katika matumizi ya sitiari uliendelezwa na Anudo (2018), alipochunguza sitiari za dhana katika lugha ya Kidholuo na jinsi maana dhahania inavyofasiriwa katika sitiari hizo. Alibaini kuwa, hazina ya mawasiliano ya binadamu imejawa na sitiari za dhana. Pia, sitiari za dhana ni kipengele muhimu ambacho kinaangazia ulimwengu kidhanifu na binadamu hutumia sitiari hizi kuwasiliana bila kufahamu kuwa anazitumia. Hii ni kwa sababu fikira na matendo ya binadamu yamezungukwa na ulimwengu wa kisitiari. Utafiti huo ni muhimu kwa huu kwa sababu umedhihirisha namna matumizi ya sitiari yanavyomwezesha binadamu kuelewa dhana dhahania kwa kutumia hali halisi kuzielewa. Hivyo, kuna haja ya kufahamu na kuelewa sitiari za dhana kwa sababu zinachangia katika kuelewa ujumbe. Uelewa huu utamwezesha msomaji au msikilizaji kuchanganua masuala yanayomwathiri na kupata mwelekeo wa kuyasuluhisha. Ingawa Anudo (keshatajwa) amechunguza sitiari za dhana katika Kidholuo, utafiti huo ulisaidia kubainisha aina za sitiari zinazotumiwa katika mawasiliano, suala lililochunguzwa katika lengo la utafiti huu linaloangazia aina za sitiari za kiafya katika matini zilizoteuliwa.

## 2.5 Mtindo na Uchanganuzi wa Maana Katika Sitiari za Kiafya

Fasihi huandikwa na kuwasilishwa kwa njia inayoeleweka na watumizi wake. Hivyo, kila mwandishi hutumia mbinu za kisanaa ambazo anaziona kuwa bora kwa walengwa wake. Ingawa kila mwandishi ana mtindo wake wa kujieleza, dhana ya mtindo imefafanuliwa kwa kina na wataalamu mbalimbali ili kuondoa utata na kuleta ukuruba katika fasili ya dhana hiyo. Kwa mujibu wa Leech na Short (1981), mtindo ni namna ambayo mwandishi hutumia lugha katika muktadha fulani ili kufumbata dhamira yake. Senkoro (1982) anaelezea mtindo kama namna ambavyo mwandishi anatumia fani

kuwasilisha yaliyomo katika kazi za kifasihi. Aidha, ni ujuzi unaotumiwa na mwandishi kujieleza (Njogu na Chimerah (1999). Ujuzi huu unajitokeza kupitia matumizi ya jazanda, tasfida, taswira, mbinu rejeshi na viangaza mbele. Mwandishi hutumia fani hizi kiufundi ili kuendeleza yaliyomo, dhamira na kusanifisha kazi yake. Mbatiah (2001) na Wamitila (2008), wanafafanua vipengele vingine vya kimtindo kama vile uteuzi wa maneno, miundo mbalimbali ya sentensi, aya na beti ambavyo havikutajwa hapo awali. Ingawa wataalamu hawa wameelezea maana ya mtindo katika nyakati tofautitofauti, fasili zao zina ukuruba. Wanaafikiana kwamba mtindo ni utaratibu unaotumiwa na wandishi kuwasilisha kazi kwa hadhira lengwa. Katika utafiti huu mtindo ulirejelewa kama matumizi ya tamathali za semi, usimulizi, nyimbo na barua katika kuwasilisha sitiari za kiafya katika matini teule za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Sababu ni kwamba mtindo ni dhana pana, hivyo mtafiti hangeshughulikia vipengele vyake vyote kwa wakati mmoja.

Katuku (2013) alichunguza mtindo katika Diwani ya *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine* na kufahamu kuwa fani na mbinu za kimtindo kama vile tashibihi, sitiari, kinaya, maswali ya balagha, jazanda, tasfida, methali, chuku, majazi, nyimbo, barua, takriri na usambamba huzua maana tofautitofauti kulingana na muktadha na mandhari ya matumizi yake. Pia, alibaini kuwa ukiushi katika vipengele hivyo vya fani na mbinu za kimtindo ulifanikisha uelewa wa msomaji kuhusu masuala yaliyoangaziwa. Alitambua jinsi mwandishi wa *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine* alivyofaulu kutumia tamathali na mbinu za lugha, katika kumchorea msomaji taswira ya uhalisia wa mazingira ya hadithini. Ufahamu huu ulimwezesha mtafiti kufafanua mtindo uliotumika kuwasilisha sitiari za kiafya katika muktadha na mazingira ya kiafya yanayoangazia usafi, magonjwa, lishe, huduma za kiafya na vifo. Katutu (keshatajwa) alichunguza ukiushi wa kimtindo katika vipengele vya sintaksia, semantiki na msamiati, wakati utafiti huu ulichanganua sitiari za kiafya katika matini teule za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto.

Fauka ya hayo, mtindo hutumiwa kuendeleza masuala mbalimbali yanayoangaziwa katika kazi ya kifasihi. Kwa msingi huu, Kanyua (2013) alichunguza jinsi mtindo unavyotumiwa kuwasilisha yaliyomo katika *Natala*. Vipengele alivyochunguza ni matumizi ya taswira, kinaya, jazanda, maswali ya balagha, methali, misemo, nahau, takriri, chuku, sitiari, usemaji kando na uzungumzi nafsia. Alitambua ya kwamba kuna

haja ya kutumia vipengele vya lugha kama vile sitiari kwa njia mwafaka kwa sababu vipengele hivi hujengana na kukamilishana katika kujenga ploti na kuleta muwala katika mawasiliano. Umuhimu wa utafiti huo ni kwamba, katika uchanganuzi wa sitiari za kiafya mtafiti pia aliangazia jinsi vipengele vingine vya lugha vinavyohusiana katika kuibua maana inayowasilishwa na sitiari za kiafya zinazochunguzwa. Utafiti huo pia umeonyesha jinsi vipengele vya lugha kama vile sitiari vilivyochangia pakubwa kujenga na kuendeleza yaliyomo katika katika tamthilia ya *Natala*. Utafiti wake ulihusu jinsi mtindo ulivyotumiwa kwa ujumla katika tamthilia ya *Natala*, ilhali utafiti huu ulichunguza mtindo uliotumika kuwasilisha sitiari za kiafya katika matini teule za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto.

Fadhili (2014) alichunguza matumizi ya mtindo katika tamthilia za *Kinjeketile* (1969) na *Morani* (1971) katika vipindi mbalimbali vya kihistoria na kutambua kuwa, lugha ndicho kipengele muhimu kinachotawala kazi ya kifasihi. Katika kipengele cha lugha, sitiari imejitokeza kuwa fani inayotawala uwasilishaji wa maudhui katika tamthilia hizo mbili kuliko tamathali zingine za semi. Zaidi ya hayo, sitiari pana imetumika kuwasilisha yaliyomo katika tamthilia ya *Morani* na *Kinjeketile*. Tashibihi, tashihisi, methali na takriri zimetumika kujenga sitiari pana. Sitiari imeangaziwa kama fani inayobeba fani zingine. Umuhimu wa kauli hii ni kwamba, inafafanua namna tamathali zingine za semi zinavyoungana ili kuunda sitiari pana. Hata hivyo utafiti huo haujafafanua kwa kina jinsi tashibihi pekee, methali au takriri zinaweza kuwa sitiari. Hili ni pengo lililojazwa na utafiti huu. Mojawapo ya malengo ya utafiti huu ni kuchunguza jinsi tamathali za semi, nyimbo, usimulizi na barua zilivyotumika kuwasilisha sitiari za kiafya katika matini teule za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Fadhili (keshatajwa) aliangazia kipengele pana cha lugha kilichojumuisha sitiari, tashibihi, takriri, na methali, ilhali utafiti huu ulichanganua kipengele cha sitiari pekee.

Baada ya kuchanganua namna mtindo ulivyojitokeza katika *Zinguo la Mzuka* na *Mbaya Wetu*, Nyandiwa (2015) alifahamu kwamba, fani kama vile tashibihi, sitiari, chuku, tanakuzi, kejeli na oksimora zina uhusiano wa karibu na huchangia katika kuibua maana katika kazi ya fasihi. Pia, maana inayowasilishwa na semi hizi hubadilika kulingana na muktadha. Ufahamu huu ulimwezesha mtafiti kuchunguza jinsi sitiari za kiafya zilivyotumika katika miktadha mbalimbali. Vilevile, ufahamu wa uhusiano uliopo

baina ya semi ulimwezesha mtafiti kushughulikia lengo la pili lililochunguza mtindo uliotumika kuwasilisha sitiari za kiafya katika matini teule. Mtafiti alichunguza matumizi ya vipengele vya tamathali za semi, usimulizi, barua na nyimbo na jinsi vilivyohusiana na kukamilishana kuibua taswira za kisitiari katika matini teule. Nyandiwa (keshatajwa) alichunguza namna sitiari, chuku, kejeli, oksimora na tanakuzi zilivyotumika kuwasasilisha maudhui katika tamthilia za *Zinguo la Mzuka* na *Mbaya Wetu*, wakati utafiti huu ulichanganua sitiari za kiafya katika matini teule za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto.

**2.6 Misingi ya Kinadharia**

Kila nadharia inayotumika katika uchanganuzi wa kazi za kifasihi huwa na wajibu mahsusi inaotekeleza kulingana na malengo ya msanii. Kwa jinsi hii utafiti huu ulijikita katika nadharia mbili zilizokamilishana katika viwango tofauti ili kukidhi mahitaji ya malengo ya utafiti. Nadharia hizi ni: Nadharia Changanuzi ya Sitiari ya Dhana na nadharia ya Umitindo. Nadharia Changanuzi ya Sitiari ya Dhana inahusika katika kuchanganua matumizi ya sitiari katika kazi za kifasihi. Kwa sababu utafiti huu uliangazia kipengele cha sitiari, nadharia hii ilifaa katika kuchanganua sitiari za kiafya katika matini teule na pia kutathmini ujumbe unaowasilishwa na sitiari hizi katika kusuluhisha matatizo ya kiafya kwa mujibu wa matini teule. Hata hivyo, haikufaa kubainisha mtindo uliotumika kuwasilisha sitiari za kiafya katika matini teule. Kutokana na upunguvu huu, nadharia bora iliyotumika kupambanua mtindo uliotumika kuwasilisha sitiari za kiafya katika matini teule ni umitindo. Umitindo hutumika kuchunguza mtindo uliotumiwa na wasanii kuwasilisha kazi za kifasihi.

**2.6.1 Nadharia Changanuzi ya Sitiari ya Dhana**

Nadharia Changanuzi ya Sitiari ya Dhana iliasisiwa na Lakoff na Johnson (1980). Katika nadharia hii, sitiari huangaziwa kama chombo cha utambuzi kinachotumiwa na mfumo wa binadamu wa kidhana kama ishara na dhana ya dhana dhahania. Isitoshe, Lakoff na Johnson (keshatajwa) wanasema kuwa, nadharia ya sitiari ya dhana huunganisha ufahamu wa utambuzi wa binadamu na usemi wa lugha na mambo ya kimazingira. Kwa mfano, katika usemi, "Aliwakwa na hasira," ni rahisi msikilizaji kuchukulia hasira kama moto. Kimsingi, sitiari huunda jinsi watu wanavyouona na kutazama ulimwengu kwa kuleta ulinganifu ulio wazi.

Kwa mujibu wa nadharia hii, sitiari ni dhana kongwe na ilikuwepo katika enzi za Aristotle ilipotumiwa katika lugha ya kishairi. Kulingana na Lakoff (1992), sitiari ilianza kuchanganuliwa kinadharia katika miaka ya themanini kwa kutumia Nadharia Changanuzi ya Sitari ya Dhana. Aidha, Nadharia hii imejengwa katika msingi wa dhana kwa sababu mfumo wa binadamu wa kidhana uko katika umbo la kisitiari na hudhibiti fikra za binadamu na kuunda anachokitambua na jinsi anavyowasiliana na binadamu wengine. Binadamu huunda jinsi anavyofikiria na kufanya kupitia fikra za kisitiari. Katika kufanya hivi, sitiari inakuwa operesheni ya utambuzi inayofanywa ili kupata uzoefu wa maana na kuelewa jambo kupitia jambo lingine. Kwa jinsi hii, mfumo wa kidhana hutekeleza wajibu muhimu katika kufasili hali halisi. Wazo hili ni muhimu kwa sababu matumizi ya sitiari katika mawasiliano kwa sasa ni jambo la kawaida.

Kwa mujibu wa Lakoff (1992), nadharia changanuzi ya sitiari ya dhana huangazia kwa kina jinsi sitiari inavyotumika kama njia ya kuelewa ulimwengu wa kihalisia kwa undani. Vilevile, matumizi ya sitiari katika mawasiliano husaidia kueleweka kwa dhana dhahania kwa njia rahisi. Hii ni kwa sababu maana lengwa huhusishwa na taswira ya dhana halisi katika ulimwengu wa kawaida. Hivyo, sifa za dhana lengwa hulinganishwa na za dhana ya kawaida inayofahamika na kueleweka.

Ingawa matumizi ya sitiari katika mawasiliano hurahisisha uelewa wa dhana fulani, Charteris-Black (2004) anasema kuwa, maana inayowasilishwa na sitiari fulani inaweza kutofautiana kulingana na mila na mazingira ya matumizi yake. Hivyo, inapaswa mhakiki anayetumia nadharia changanuzi ya sitiari ya dhana kuchanganua kazi za kifasihi awe makini anapofafanua maana ya sitiari mbalimbali kulingana na muktadha wa matumizi yake.

Mihimili ya nadharia changanuzi ya sitiari ya dhana kama ilivyoangaziwa na Lakoff na Johnson (1980), Lakoff (1992).

i. Sitiari ni muundo wa mfumo wa dhana unaomwezesha mtu kuelewa masuala changamano kwa njia inayoonekana na ya kiulinganishi.
ii. Sitiari hurahisisha uelewa wa dhana fulani kupitia matumizi ya taswira, ambazo huleta ukaribu wa kihalisia na ukweli unaokubalika kuhusu suala

linalozungumziwa. Nadharia ya Sitari ya Dhana hurahisisha ufasiri wa maana ya sitiari mbalimbali katika kazi ya fasihi.

iii. Sitiari huwezesha kueleweka kwa masuala changamano na mengine yaliyo mwiko katika jamii kwa njia ya kiulinganishi.
iv. Mawasiliano katika lugha ya kisitiari yana nguvu ya kunasa makini ya hadhira na kuathiri msimamo wao kuhusu suala fulani.
v. Kuna aina mbalimbali za sitiari na maana inayowasilishwa na sitiari moja inaweza kutofautiana kulingana na mila na mazingira ya matumizi yake.

Mhimili wa kwanza unaoangazia sitiari kama muundo wa dhana unaomwezesha msomaji kuelewa masuala changamano kwa njia ya kulinganisha, ulitumika kujadili aina za sitiari za kiafya na matumizi yake katika kuchanganua masuala mtambuko yanayorejelea masuala ya kiafya katika matini zilizoteuliwa. Data ya utafiti ilitokana na uchanganuzi wa maneno, vifungu vya maneno na sentensi za kisitiari ambazo zinarejelea masuala ya kiafya katika matini teule. Data hii ilichanganuliwa kwa kina ili kufahamu aina na muundo wa sitiari za kiafya zilizotumika katika matini teule za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Sitiari pia hurahisisha uelewa wa dhana fulani kupitia taswira inayoleta ukaribu wa kihalisia kuhusu yanayozungumziwa. Mhimili huu wa pili ulitumika kubainisha aina za sitiari za kiafya katika matini teule za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto na jinsi zinavyohusiana kuwasilisha masuala mtambuko katika matini teule. Sitiari hizi zinaweza kuwa maneno, au vifungu vya maneno yanayounda usemi fulani.

Mhimili wa tatu unahusu matumizi ya sitiari katika kurahisisha uelewekaji wa masuala changamano na yaliyo mwiko katika jamii. Mhimili huu ulitumika kufafanua masuala mtambuko yaliyowasilishwa na sitiari za kiafya katika vitabu viteule. Utafiti huu ulishughulikia suala la afya ambalo ni changamano kutokana na mila katika baadhi ya jamii. UKIMWI na Saratani ni miongoni mwa masuala mtambuko yaliyochunguzwa katika utafiti huu. Hivyo, matumizi ya lugha ya kiulinganishi, hasa kwa kutumia lugha ya kisitiari ilifaa zaidi kushughulikia masuala kama haya.

Mchango wa sitiari za kiafya katika kusuluhisha matatizo ya kiafya katika jamii ulijadiliwa kwa kuongozwa na mhimili wa nne. Kwa mujibu wa mhimili huu, mawasiliano ya kisitiari yana nguvu ya kunasa makini ya hadhira na kuadhiri msimamo

wao kuhusu jambo fulani. Kwa msingi huu mtafiti alijadili matumizi ya sitiari za kiafya katika kusuluhisha changamoto za kiafya katika matini teule za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Mtafiti pia alijadili jinsi aina mbalimbali za sitiari za kiafya zilivyotumika kuangazia masuala mtambuko kulingana na muktadha wa matumizi yake. Data ya utafiti ilitokana na mikakati ya kusuluhisha matatizo ya kiafya iliyopendekezwa katika matini teule za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto.

### 2.6.2 Nadharia ya Umitindo

Nadharia ya uhakiki ya Umitindo iliasisiwa na Viktor Shyklovsky mwanachama wa kundi la "The *Prague Linguistic Circle*" katika mwaka wa 1904. Wengine walioiwekea nadharia hii mizizi ni Jacobson (1960) na Murry (1976). Nadharia hii ilitumiwa na Wanaisimu katika uchambuzi wa kiisimu (Leech, 1969). Kwa mujibu wa Leech (1969) Nadharia ya Umitindo hutumika kuchambua na kufasiri mtindo uliotumiwa kuwasilisha kazi za kifasihi kwa mkabala wa kiisimu. Hii ni kwa sababu matini za kifasihi huhusisha kipengele cha semantiki ambacho ni cha kiisimu. Hivyo, nadharia hii inafaa kuhakiki vipengele vya lugha kama vile sitiari, taswira, jazanda na tamathali zingine za usemi katika kazi za kifasihi. Kimsingi nadharia hii hutumiwa kuchunguza mtindo uliotumika kuwasilisha maudhui katika matini za kifashi. Uhakiki huu ulijikita katika kipengee cha semantiki pekee, ambapo uchanganuzi wa sitiari za kiafya ulifanywa katika vitabu teule.

Indangasi (1988), anafafanua zaidi mawazo ya Leech (keshatajwa) kwa kusema kuwa, nadharia ya elimumitindo huwezesha kueleweka kwa lugha iliyotumika katika matini za kifasihi. Kwa msingi huu Bright (1992) anasema kuwa, lugha ndicho chombo muhimu kinachotumiwa na msanii kuwasilisha ujumbe kwa hadhira. Hivyo, lengo kuu la nadharia ya elimumitindo ni kuchanganua mtindo uliotumiwa na msanii katika kazi za kifasihi. Mtafiti huchunguza namna mwandishi alivyotumia lugha, muktadha wa matumizi wa lugha hiyo na malengo ya kuitumia. Maneno huchaguliwa kulingana na mazingira na muktadha wa matumizi yake, ili ujumbe unaopashwa ueleweke kulingana na kanuni zinazoongoza matumizi ya lugha katika jamii husika. Utafiti huu ulijikita katika matumizi ya sitiari za kiafya katika kuchanganua masuala ya kiafya. Yamkini, sitiari moja ya kiafya inaweza kuwasilisha maana mbalimbali kulingana na muktadha wa matumizi yake.

Nadharia ya Umitindo pia ililenga kuchunguza taratibu zinazozingatiwa katika kuchanganua sifa za kimtindo zinazodhihirika katika matini za kifasihi (Mbatiah, 2001). Miongoni mwa sifa hizi ni sintaksia, mofolojia na fonolojia. Aidha, mawazo ya Wamitila (2003, 2008) yanaoana na haya anaposema kuwa, nadharia hii hujikita katika uchanganuzi wa lugha iliyotumika katika kazi ya fasihi kwa kuzingatia misingi ya kisayansi. Mawazo ya wataalamu hawa ni kielelezo kilichozingatiwa wakati wa kufanya utafiti huu kwa jinsi yalivyofafanua namna ya kuendeleza uhakiki wa kimtindo.

Isitoshe, Mlaga (2017) anaeleza umuhimu wa kutumia nadharia ya Umitindo katika uchanganuzi wa kazi za kifasifi kwa kusema kuwa, inatumika kuchunguza mitindo iliyotumika katika kuwasilisha kazi za kifasihi. Mwanaelimumitindo huchunguza sura ya nje ya matini za kifasihi, matumizi ya aina za sentensi na jinsi matumizi ya maneno yanaweza kuzalisha sentensi zenye maana mbalimbali. Vilevile, nadharia ya Umitindo huangazia uzuri wa kiujumi uliopo katika uumbaji wa kazi za fasihi. Inamfungua mpokezi macho na kuona uzuri wa kiujumi unaotumiwa na msanii kutokana na uchaguzi wa mtindo wa mawasiliano. Katika kufanya hivi, umitindo hulenga kutoa hukumu katika kazi ya kifasihi kwa kumsaidia mhakiki kutathmini mtindo uliotumika kuwasilisha kazi husika na kutoa kauli ikiwa mtindo huo ni mzuri au la.

Leech (1969) anaangazia mihimili ifuatayo ya nadharia ya Umitindo:

i. Mtindo unaotumiwa katika kazi ya fasihi ndio nyenzo kuu inayotumiwa na mwanafasihi kupasha habari kwa hadhira.
ii. Lugha ni chombo tekelezi na ina jukumu la kufanikisha kueleweka kwa habari iliyokusudiwa na mwandishi.
iii. Matumizi mwafaka ya mbinu za kisanaa hufanikisha upashaji na uelewekaji wa ujumbe ambao mwasilishaji anakusudia kuwasilisha.
iv. Ili kuchanganua kazi ya fasihi lazima vipengele mbalimbali vya kimtindo vifanye kazi kwa pamoja. Hii huleta uwiano kati ya ujumbe na lugha ya kifasihi. Uwiano huu hutokana na muwala na mtiririko wa habari kutoka tukio moja hadi lingine.

Mhimili wa kwanza unaangazia mtindo kama nyenzo kuu inayotumiwa kuwasilisha maudhui katika kazi ya kifasihi. Mhimili huu ulimwezesha mtafiti kubainisha vipengele

vya kimtindo vilivyotumiwa na waandishi kuwasilisha sitiari za kiafya katika matini teule za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Mtafiti alisoma matini teule huku akifafanua aina na muundo wa mbinu za kimtindo zilizotumika kuwasilisha sitiari za kiafya. Umuhimu wa lugha kama chombo tekelezi umesisitizwa katika mhimili wa pili, ilhali dhima ya matumizi bora ya mbinu za kisanaa katika kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe katika kazi za kifasihi imesisitizwa katika mhimili wa tatu. Mihimili hii ilitumika kutathmini jinsi waandishi walivyofaulu kutumia mbinu za kimtindo kuwasilisha sitiari za kiafya katika matini teule.

Kuna haja ya vipengele vya kimtindo kutumika kwa pamoja ili kuwe na muwala na mtiririko unaofaa katika ujumbe unaopitishwa kama inavyoangaziwa katika mhimili wa nne. Yumkini, kuwe na uwiano kati ya ujumbe na lugha ya kifasihi. Uwiano huu hutokana na muwala na mtiririko wa habari kutoka tukio moja hadi lingine. Mbinu za kisanaa zinapotumiwa vyema hufanikisha upashaji na kueleweka kwa ujumbe unaokusudiwa kuwasilishwa. Mtafiti alichunguza jinsi vipengele vya kimtindo katika matini teule za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto vilivyotumika vinafanya kazi kwa pamoja ili kupasha ujumbe unaokusudiwa.

## SURA YA TATU

## MBINU ZA UTAFITI

### 3.1 Eneo la Utafiti

Kimsingi utafiti huu ulifanyiwa maktabani. Mtafiti alitembelea maktaba ya Chuo Kikuu cha Chuka na Bewa la Igembe ambapo alipata vitabu, majarida, tasnifu na makala yaliyohusiana na suala la utafiti. Pia alitembelea maktaba za Moi na Nairobi ambapo baadhi ya tasnifu zilipatikana. Data ya utafiti ilipatikana katika matini teule; *Siku ya Ukimwi* (John Kobia, 2008), *Sitaki iwe Siri* (Bitugi Matundura, 2008), *Madhila ya Bi. Shufaa* (Nuhu Bakari, 2008), *Pendo katika Shari* (Clara Momanyi, 2008)), *Kosa la Marehemu* (Andrew Panja, 2010) na *Nimefufuka* (Rebecca Nandwa, 2011).

### 3.2 Mpango wa Utafiti

Njia ya maelezo ilitumika kuendeleza utafiti huu. Mtafiti alisoma matini teule kwa makini na kupanga data kulingana na malengo ya utafiti. Nadharia Changanuzi ya Sitiari ya Dhana na nadharia ya Umitindo zilitumiwa kuchanganua matini zilizoteuliwa. Mtafiti aliongozwa na Nadharia Changanuzi ya Sitiari ya Dhana katika kujadili aina za sitiari za kiafya zilizotumika katika matini teule. Alisoma kila matini huku akiorodhesha na kupanga aina mbalimbali za sitiari za kiafya katika orodha ya ukaguzi. Pia mtafiti aliorodhesha masuala mtambuko yaliyowasilishwa na sitiari za kiafya katika matini teule katika orodha ya ukaguzi. Vilevile, mtafiti aliongozwa na Nadharia ya Umitindo kuchunguza mtindo uliotumika kuwasilisha sitiari za kiafya. Tathmini ya masuala mtambuko yaliyowasilishwa na sitiari za kiafya ilifanywa ili kubaini njia mwafaka zilizozingatiwa katika kusuluhisha matatizo ya kiafya.

### 3.3 Kundi Lengwa

Kundi lengwa katika utafiti huu ni matini za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto zinazoangazia masuala ya kiafya. Kwa kuzingatia uteuzi wa sampuli kimakusudi, matini sita za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto zinazohusu masuala ya kiafya katika msururu wa "Afya Yangu" zilihakikiwa. Ingawa matini teule zinalenga kusomwa na watoto, masuala yanayoangaziwa hayana mpaka wa kiusomi na yana manufaa kwa kila mtu. Hivyo, fasihi iliyopo katika vitabu teule inafaa kuchanganuliwa kwa njia ya kitaaluma kama fasihi nyingine ile.

### 3.4 Uteuzi wa Sampuli

Kombo na Tromp (2006) wanaelezea sampuli kama kundi ndogo la wahojiwa walioteuliwa na mtafiti ili kusimamia kundi kubwa la wahojiwa. Utanzu wa fasihi ya Kiswahili ya Watoto ulichaguliwa kimakusudi katika utafiti huu ili kuangazia kwa kina nafasi ya fasihi ya watoto katika kusuluhisha matatizo yanayoathiri jamii, kwani tafiti nyingi za kifasihi zinahusu fasihi ya watu wazima (Muriungi 2006, Wamitila 2008). Umuhimu wa kuendeleza tafiti katika fasihi ya watoto pia unaangaziwa na Bakize (2013) anaposema kwamba fasihi hii ingali changa ikilinganishwa na fasihi ya watu wazima ambayo ilishika kasi katika karne ya kumi na nane na kumi na tisa. Aidha, Fasihi ya Kiswahili ya Watoto pia imetungwa kiufundi hivi kwamba inavutia na hunasa makini ya wasomaji wa viwango mbalimbali vya elimu. Kwa mujibu wa Matundura, Kobia, na Mukuthuria (2013), mbinu za kiutunzi katika fasihi ya watoto kama vile kuwepo kwa visa vichache, lugha sahili na fantasia hurahisisha usomaji wa matini za fasihi ya watoto.

Suala la afya limechaguliwa katika utafiti huu kutokana na kuongezeka kwa changamoto za kiafya kama vile magonjwa ya utapia mlo, kiakili, UKIMWI na saratani yanayoathiri jamii kote ulimwenguni. Isitoshe, umuhimu wa kuimarisha afya ya binadamu umesisitizwa katika Malengo ya Milenia 2015, Ajenda 2063 ya Afrika Tunayoitaka na Katiba ya Kenya 2010. Pia, afya ni mojawapo ya nguzo muhimu zinazochangia katika kuafikiwa kwa maendeleo endelevu katika mataifa mbalimbali. Hivyo, ni muhimu kutilia maanani suala la afya kwani bila afya hakuna maendeleo endelevu. Pia, Wizara ya Elimu nchini Kenya imejumuisha suala la afya kama mojawapo ya masuala mtambuko yanayofunzwa katika shule za msingi nchini Kenya kupitia Fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Hili ni dhihirisho kuwa afya ni nguzo muhimu katika maisha ya binadamu ulimwenguni.

Kuna vitabu vingi vinavyohusu masuala ya kiafya katika fasihi ya Kiswahili. Kwa sababu hii, uteuzi wa sampuli kimakusudi ulizingatiwa katika kuchagua matini za fasihi ya Kiswahili ya Watoto zinazoangazia masuala ya kiafya katika msururu wa "Afya Yangu," vilivyochapishwa na Kampuni ya uchapishaji vitabu ya Longhorn. Vitabu vilivyoandikwa baada ya mwaka wa 2007 vilichaguliwa. Hiki ni kipindi cha baada ya vita vya kikabila vilivyotokana na uchaguzi wa mwaka wa 2007 nchini Kenya. Vita

husababisha matatizo ya kiafya kutokana na mazingira machafu ya kivita, ukosefu wa makazi, malezi bora, uhamaji na ukosefu wa huduma bora za kiafya.

Kigezo kilichozingatiwa katika uteuzi wa matini teule ni kuwepo na maudhui ya kiafya na data ya kutosha iliyohusu sitiari za kiafya. Kwa msingi huu, vitabu sita kati ya vinane katika msururu wa "Afya Yangu" vilivyochapishwa na Kampuni Longhorn katika mwaka wa 2020 vilichaguliwa. Matini teule ni: *Siku ya Ukimwi* (John Kobia, 2008), *Sitaki iwe Siri* (Bitugi Matundura, 2008), *Madhila ya Bi. Shufaa* (Nuhu Bakari, 2008), *Pendo katika Shari* (Clara Momanyi, 2008)), *Kosa la Marehemu* (Andrew Panja, 2010) na *Nimefufuka* (Rebecca Nandwa, 2011). Vitabu viwili katika msururu wa "Afya Yangu": *Masalia* (John Kobia, 2008) na *Mtu ni Afya* (Kitula King'ei, 2008) havikuchaguliwa kwa ukosefu wa istilahi za sitiari za kiafya ambazo zilikuwa data ya utafiti huu. Kitabu: *Siku ya Ukimwi* kilichaguliwa kwa sababu ya kuwepo na maudhui ya uzalendo yanayojitokeza katika vita dhidi ya magonjwa kama vile UKIMWI. Vitabu: *Madhila ya Bi. Shufaa* na *Sitaki Iwe Siri* vilichaguliwa kwa sababu ya ushujaa wa watoto katika vita dhidi ya maradhi. Zuhura na Amina katika kitabu *Madhila ya Bi. Shufaa* na Musa, Haki na Ukwa katika *Sitaki Iwe Siri* ni vielelezo vya watoto waliojitokeza kama mashujaa katika vita dhidi ya magonjwa kiwango cha kuwapiku watu wazima. *Pendo Katika Shari* ni kitabu kinachoangazia namna ambavyo utamaduni na mila za kijamii hasa katika nchi za Kiafrika zilivyokuwa na uwezo wa kuathiri asasi ya familia. Vitabu: *Kosa la Marehemu* na *Nimefufuka* vilichaguliwa kwa sababu ya kuwepo kwa maudhui ya ushindi na mwamko mpya katika vita dhidi ya magonjwa.

### 3.5 Ukusanyaji wa Data

Data humwezesha mtafiti kupata habari ya kuaminika kuhusu suala linalochunguzwa. Kwa mujibu wa Oladipo, Ikamati, Kiplang'at na Baraza (2015), data iliyokusanywa hurekodiwa katika kifaa cha utafiti. Katika utafiti huu, orodha ya ukaguzi ilitumiwa kama kifaa cha kukusanya data. Ili kupata data mtafiti alisoma vitabu teule kwa makini na kudondoa maneno, vifungu vya maneno na sentensi za kisitiari zilizorejelea masuala ya kiafya. Data hii ilikusanywa na kunakiliwa kwa ajili ya kutoa maelezo kwa kuongozwa na malengo ya utafiti. Ili kushughulikia lengo la kwanza lililojadili aina za sitiari za kiafya, mtafiti alisoma matini teule na kubainisha maneno, vifungu vya

maneno na sentensi za kisitiari zilizoangazia masuala ya kiafya na kunakili katika orodha ya ukaguzi chini ya kipengele cha sitiari. Ili kutimiza mahitaji ya lengo la pili lililochunguza mtindo uliotumiwa kuwasilisha sitiari za kiafya, data ilikusanywa kwa kuchanganua mbinu za kiutunzi zilizotumiwa kuwasilisha sitiari za kiafya katika matini teule. Data iliyokusanywa ilinakiliwa katika orodha ya ukaguzi katika kipengele cha mtindo. Data iliyotumika katika lengo la tatu lililolenga kufafanua masuala mtambuko yaliyowasilishwa na sitiari za kiafya katika matini teule ilipatikana kwa kuorodhesha masuala mtambuko yaliyoangaziwa katika matini teule. Data hii ilinakiliwa chini ya kipengele cha masuala mtambuko.

### 3.6 Uchanganuzi wa Data

Data iliyokusanywa ilinukuliwa katika kifaa cha utafiti na ilichanganuliwa kwa mtindo wa kimaelezo kwa mujibu wa malengo ya utafiti. Nadharia Changanuzi ya Sitiari ya Dhana na nadharia ya Umitindo ziliongoza katika uchanganuzi huu. Data ya utafiti ilichanganuliwa kwa kuzingatia hatua tatu kwa mujibu wa malengo ya utafiti. Hatua ya kwanza ilihusu uchanganuzi wa data iliyohusu aina ya sitiari za kiafya zilizotumika katika matini teule. Data hii ilichanganuliwa kwa njia ya maelezo. Mtafiti alipanga sitiari za kiafya katika vikundi kulingana na aina na utendakazi wake. Kila sitiari ya kiafya iliyotumika ilichanganuliwa kwa kina kwa kuzingatia vigezo hivi.

Hatua ya pili ilihusu uchunguzi wa mtindo uliotumika kuwasilisha sitiari za kiafya katika matini teule za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Data ilichanganuliwa kwa kufafanua mbinu za kisanaa zilizotumika kuwasilisha sitiari za kiafya. Mtafiti alieleza jinsi mbinu zilizotumika zilivyofanikisha kufaulu kwa sitiari za kiafya kuwasilisha yaliyomo. Hatua ya tatu ilihusu ufafanuzi wa data inayohusu masuala mtambuko yanayowasilishwa na sitiari za kiafya katika vitabu viteule. Mtafiti alijadili mchango wa masuala mtambuko katika kusuluhisha matatizo ya kiafya katika matini teule za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto.

### 3.7 Uwasilishaji wa Data

Data ambayo ilikusanywa iliwasilishwa kimaelezo. Mtafiti alijadili aina, muundo, utendakazi wa sitiari za kiafya zilizotumika katika matini teule za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Vilevile, mtafiti alichunguza mtindo uliotumiwa na waandishi wa matini

teule kuwasilisha sitiari za kiafya zilizotumika. Mtafiti alifafanua masuala mtambuko yanayowasilishwa na sitiari za kiafya katika matini teule na nafasi yake katika kusuluhisha matatizo ya kiafya. Data iliwasilishwa kwa njia ya maelezo.

### 3.8 Maadili ya Utafiti

Mtafiti alizingatia maadili yafuatayo kabla ya kuandaa utafiti. Kwanza, aliomba idhini ya kufanya utafiti katika Kitengo cha Maadili Chuka na Tume ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi (NACOSTI). Vibali hivi vilimwezesha mtafiti kutembelea maktaba mbalimbali ili kusoma maandishi yaliyohusiana na suala la utafiti. Aidha, mtafiti alitoa data ya ukweli na iliyotokana na vitabu teule, kwa kuongozwa na malengo ya utafiti, nadharia Changanuzi ya Sitiari ya Dhana na nadharia ya Umitindo. Vilevile, mtafiti alinukuu kazi zote za wataalamu waliorejelewa katika utafiti huu.

# SURA YA NNE

# AINA ZA SITIARI ZA KIAFYA KATIKA VITABU TEULE

## 4.1 Utangulizi

Sitiari za kiafya zilizojadiliwa katika utafiti huu ziliainishwa katika msingi wa usemi, kwa sababu msingi huo huangazia kazi ya kifasihi inayochanganuliwa kwa upana (Wamitila, 2008). Kwa mujibu wa Wamitila (keshatajwa) msingi wa usemi hujumuisha sitiari kuu, sitiari za kikaida na sitiari pana ambapo sitiari kuu hutawala kazi nzima ya kifasihi na huwa msingi muhimu wa kufasiri kazi hiyo. Vilevile, sitiari ya kikaida hutumiwa katika lugha ya kawaida na hushadidia kukamilika kwa sitiari kuu katika utamaduni maalum wa kijamii. Isitoshe, sitiari pana hujumuisha sitiari kadhaa zinazopanua maana ya sitiari moja. Tathmini ya sitiari hizi ni kwamba, zote zinaoana na kukamilishana katika kujenga wazo kuu lililoangaziwa katika matini teule.

Uchanganuzi wa sitiari za kiafya katika matini teule pia ulitilia maanani kauli ya Nadharia ya Sitiari ya Dhana kuwa, aina mbalimbali za sitiari hutumika kuwasilisha masuala tofautitofauti katika kazi ya kifasihi. Pia, maana iliyowasilishwa na sitiari hizi ilizimbuliwa kulingana na mila na mazingira ya matumizi yake. Katika kujadili maana iliyowasilishwa na sitiari za kiafya katika vitabu teule, mtafiti ametilia maanani kauli ya Simala (2000) kuwa, sitiari moja ina uwezo wa kuwasilisha maana tofautitofauti kulingana na muktadha wa matumizi yake. Kwa msingi huu, mtafiti amebainisha kuwa mwandishi wa matini teule ametumia aina mbalimbali za sitiari za kiafya, ambazo mtafiti amezijadili kwa kina na kutathmini maana na majukumu yake katika kupasha ujumbe wa kiafya. Pia, amegundua kuwa sitiari zilizotumika zimewasilishwa katika muundo wa neno, vifungu vya maneno, sentensi na aya.

Lengo la kwanza katika utafiti huu lilikuwa kujadili aina za sitiari za kiafya katika vitabu teule vya fasihi ya Kiswahili ya Watoto.Vitabu vilivyochanganuliwa ni *Siku ya Ukimwi* (John Kobia, 2008), *Pendo katika Shari* (Clara Momanyi, 2008), *Sitaki Iwe Siri* (Bitugi Matundura, 2008), *Madhila ya Bi*. *Shufaa* (Nuhu Bakari, 2008), *Kosa la Marehemu* (Andrew Panja, 2010) na *Nimefufuka* (Rebecca Nandwa, 2011). Sitiari za kiafya zilizotumika katika vitabu teule zimejadiliwa na kubainishwa kulingana na aina zake, utendakazi wake na maana zake. Baadhi ya sitiari zilizoangaziwa ni sitiari kuu za kiafya, sitiari pana za kiafya na sitiari za kikaida za kiafya.

### 4.2 Muhtasari wa Vitabu teule

Matini mbalimbali za fasihi ya Kiswahili ya Watoto zimeandikwa kuhusu masuala ya kiafya. Bitugi Matundura aliandika matini ya *Sitaki Iwe Siri* katika mwaka wa 2008, ambapo dhamira kuu inahusu ushindi katika vita dhidi ya UKIMWI. Mwandishi huyo ameangazia taswira ya jamii iliyofungwa na minyororo ya kitamaduni, ambapo UKIMWI ulichukuliwa kama laana katika jamii. Tamaduni hasi za kijamii zilisababisha kuepukwa na kutengwa kwa wagonjwa wa UKIMWI. Hali hii ilichochea kuibuka kwa kizazi kipya kilichoelimika, ambacho kilichangia katika kupiga vita tamaduni hasi za kijamii na janga la UKIMWI likawa si siri tena.

Masuala ya kiafya pia yameangaziwa zaidi katika matini teule ya *Pendo katika Shari* iliyoandikwa na Clara Momanyi katika mwaka wa 2008. Mhusika mkuu Pendo amesawiriwa kama mwanamke mrembo, mwenye maadili mema na anayewajibika katika shughuli zote za kifamilia. Hata hivyo, Sulubu alimtesa kwa kukosa mtoto wa kiume na akajiunga na virukanjia mtaani ambao walimwambukiza UKIMWI. Tendo hilo limechangiwa na tamaduni hasi za kijinsia na taasubi za kiume, zinazomkandamiza mwanamke na kumsawiri kama jinsia duni iliyoishi kwa kudura za mwanaume. Kwa jinsi hii, Sulubu alimhusisha mkewe na ukosefu wa mtoto wa kiume na akampa talaka.

Pia, Janga la UKIMWI limeangaziwa na John Kobia katika matini teule ya *Siku ya Ukimwi* aliyoiandika katika mwaka wa 2008. Suala kuu lililoangaziwa katika kitabu hicho ni janga la UKIMWI, ambapo ugonjwa huo umesawiriwa kama kikwazo kikuu katika maendeleo ya jamii. Waadhiriwa wa ugonjwa huo walishindwa kufanya kazi kutokana na magonjwa nyemelezi mbalimbali. Mhusika mkuu Kadogo amesawiriwa kama kurunzi ya kuangazia jamii kuhusu madhara ya UKIMWI, visababishi vyake na njia za kukabiliana na ugonjwa huo.

Katika kitabu kiteule *Kosa la Marehemu* kilichoandikwa na Andrew Panja katika mwaka wa 2010, mwandishi ameangazia janga la UKIMWI ambalo lilikuwa mwiko kuhusishwa nalo katika jamii. Tamaduni hasi za kijamii dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI zilisababisha kutengwa kwa waathiriwa wa ugonjwa huo. Kwa jinsi hii, mhusika Mshindo amejitokeza kupigania mwelekeo na mtazamo mpya wa maisha dhidi ya janga

la UKIMWI. Mshindo amesawiriwa kama kiwakilishi cha mabadiliko na mtetezi wa wanyonge dhidi ya tamaduni hasi za kijamii kuhusu janga la UKIMWI.

Kitabu kiteule *Nimefufuka* kiliandikwa na Rebecca Nandwa katika mwaka wa 2011. Mwandishi ameangazia masaibu ambayo mhusika mkuu Sikitu alipitia katika Mjibalaa, uliokumbwa na maovu kama vile matumizi ya dawa za kulevya na ufasiki. Kwa jinsi hii, Sikitu alijihisi kama mfu na aliyetamani kupata ukombozi ili asiangamie. Sikitu alianza safari ya kukomboa Mjibalaa kwa kuitisha msaada kutoka nje, hasa kwa wenyeji wa mji huo walioishi mbali kama vile shangaziye Upendo. Maudhui mbalimbali katika matini teule yamewasilishwa kwa kutumia mbinu tofautitofauti za uandishi kama vile sitiari na tamathali zingine za usemi. Yamkini, mtindo wa kibarua umetumika katika kuwasilisha masuala makuu ya kiafya yaliyoathiri Mjibalaa.

Nuhu Bakari (2016) aliandika matini teule ya *Madhila ya Bi. Shufaa* na akabainisha namna matumizi mabaya ya mamlaka na dhuluma za kijinsia zilivyochangia katika maambukizi na usambazaji wa magonjwa. Mhusika Fukua alitumia mamlaka na uwezo wa pesa kuwarai na kufanya mapenzi ya kiholela na wasichana wadogo na wanawake walioolewa, huku akiwaambukiza UKIMWI. Kupitia tabia hii, Fukua alimwambukiza Bi. Shufaa aliyekuwa mwanamke wa kutiliwa mfano ugonjwa wa UKIMWI. Baadaye wasichana wa Bi. Shufaa wamesawiriwa kama watetezi na wapiganiaji wakubwa dhidi ya UKIMWI katika familia na kote duniani.

**4.3 Sitiari Kuu za Kiafya katika Vitabu teule.**

Kwa mujibu wa Wamitila (2008) sitiari kuu huwa msingi muhimu wa kufasiri kazi ya fasihi inayoshughulikiwa. Kadhalika, sitiari kuu hudokeza maana tofautitofauti kulingana na muktadha wa matumizi yake. Gaichu (2016) anashadidia wazo hili kwa kusema kuwa, maana ya neno lililotumika kisitiari hutegemea muktadha wa matumizi yake na maana hiyo pia inaweza kubadilika au kubaki jinsi ilivyo. Aina mbalimbali za sitiari kuu za kiafya zimetumika kuangazia masuala ya kiafya katika matini teule. Baadhi ya sitiari hizi ni:

### 4.3.1 Nimefufuka

*Nimefufuka* ni aina ya sitiari kuu ya kiafya iliyotumika katika kitabu kiteule *Nimefufuka*. Kulingana na Mdee na wengine (2022) maana ya kimsingi ya dhana 'nimefufuka' ni kupata uhai baada ya kufa. Maana hiyo ndio kigezo kikuu kilichozingatiwa katika kuainisha neno hilo kama sitiari ya kiafya. Hivyo, *nimefufuka* ni aina ya sitiari kuu ya kiafya iliyobeba masuala ya kiafya yaliyoangaziwa katika kitabu kiteule. Imetumika kulinganisha matatizo ya kiafya yaliyokumba Mjibalaa na mabadiliko yaliyotekelezwa ili kuimarisha hali hiyo. Kwa mujibu wa Lakoff na Johnson (1980) ulinganishi wa kisitiari huzua taswira zinazoleta ukweli wa kihalisia na kurahisisha ufasiri wa maana katika suala linalozungumziwa. Sitiari zingine za kiafya zilizoangaziwa katika matini teule zimechangia katika kujenga maudhui yaliyoangaziwa na sitiari kuu na kukamilika kwa dhamira kuu. Kilele cha suala kuu lililoangaziwa katika matini teule kimedhihirishwa kupitia mazungumzo haya: Tazama Kielelezo 1:

> Nimemweleza yote kuhusu maisha yangu. Hana pingamizi la sisi kuishi na Shujaa kama mtoto wetu. Nitakueleza zaidi tukikutana. Mimi sasa ni mtu hai, si hoi tena: *Nimefufuka* (uk.34).

Kulingana na muktadha wa matumizi katika Kielelezo 1, sitiari kuu ya kiafya '*nimefufuka'* imetumika kuwakilisha upya ulioanza kunawiri katika Mjibalaa. Hapo awali Mjibalaa uliangaziwa kama mji wa matatizo na ukandamizwaji wa jinsia ya kike. Pia, mji huo ulikumbwa na matumizi ya dawa za kulevya, uzinzi, unywaji wa pombe haramu, taasubi za kiume na umaskini. Kulingana na mhusika Sikitu, Mjibalaa ulihitaji ukombozi wa kutoka nje ili kuepuka maangamizi zaidi. Miongoni mwa watu waliotarajiwa kukomboa Mjibalaa ni Upendo aliyependekeza mambo kadha ambayo yangechangia kuleta mabadiliko. Baadhi ya mapendekezo hayo ni kubadilishwa kwa majina kama vile Sikitu na Mjibalaa kwani yalikuwa na uwezo wa kuathari tabia ya binadamu. Kwa msingi huu, Sikitu alianza kuitwa Chaurembo kwa maana ya mwamko mpya (uk.18). Mbinu zingine za kufufua Mjibalaa zilizopendekezwa ni kupigana na tamaduni hasi zilizodunisha jinsia ya kike na kuimarisha elimu ili kuboresha maadili katika jamii. Kutokana na mabadiliko hayo, Chaurembo alijihisi kuwa mtu hai na si hoi tena kwani alikuwa *amefufuka*.

### 4.3.2 Sitaki Iwe Siri

*Sitaki Iwe Siri* pia ni sitiari kuu ya kiafya iliyoangaziwa katika matini teule ya *Sitaki Iwe Siri*. Katika matini hiyo, barua ya Musa kuhusu '*Sitaki Iwe Siri'* (uk. 45-48) imeangazia taswira ya jamii iliyofungwa na minyororo ya kitamaduni, ambapo UKIMWI ulichukuliwa kama mwiko katika jamii. Kulingana na Nadharia Changanuzi ya Sitiari ya Dhana, matumizi ya sitiari husaidia katika kuelewa masuala yaliyochukuliwa kuwa mwiko katika jamii. Kwa kuwa ilikuwa mwiko kuhusishwa na UKIMWI katika Mjibalaa, sitiari ya '*Sitaki Iwe Siri'* imefaa kurejelea ugonjwa huo. Barua hiyo ni sitiari ya kiafya iliyowakilisha mwamko mpya kuhusu vita dhidi ya UKIMWI. Imeangazia kutobolewa kwa siri iliyowekwa kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Suala kuu ambalo lililosisitizwa katika barua hiyo ni kutochukuliwa kwa maradhi ya UKIMWI kama laana kwa aliyeambukizwa bali yachukuliwe kama magonjwa mengine.

Tazama Kielelezo 2:

> Ni sadfa kwamba siri niliyoigubika kwa miaka mingi ili wajukuu wangu wasijue imefichuliwa. Wajukuu wangu hawa ni mayatima.Wazazi wao walifariki kutokana na maradhi ya UKIMWI, nao wamebaki mikononi mwangu. Walipotaka kujua ni maradhi yepi nilidinda kuwaambia. Nilitaka iwe siri. Lakini sasa Musa huyu ameandika insha ya ushindi – *Sitaki Iwe Siri*. Hii ni hatua muhimu kuhusu vita dhidi ya Ukimwi (uk.65).

Mwalonga amesawiriwa kama kiwakilishi cha tamaduni hasi za kijamii zilizochukulia UKIMWI kama kiwakilishi cha laana. Katika Kielelezo 2 Mwalonga amekiri ya kwamba, tamaduni hasi kuhusu UKIMWI zilifika kikomo na vita dhidi ya ugonjwa huo vilielekea kushinda. Musa pia amesawiriwa kama kiwakilishi cha kizazi kipya, kilichotumia elimu kama zana kuu ya kuhamasisha jamii kubadili mitazamo hasi dhidi ya waathiriwa wa UKIMWI. Alitumia sitiari mbalimbali kuelimisha jamii kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Kwa mujibu wa Simala (2000) sitiari hutekeleza majukumu muhimu kama vile kuonya, kushawishi, kujuza, kubembeleza, kukejeli na kusifu. Hivyo, uteuzi wa Musa wa kutumia sitiari katika kufunza jamii ulimwezesha kupitisha ujumbe kwa ufasaha kuhusu janga la UKIMWI.

### 4.3.3 Ushindi

*Ushindi* ambao Musa na shule ya Hekima waliopewa ni sitiari kuu ya kiafya iliyowakilisha kufaulu katika vita dhidi ya maradhi ya UKIMWI, katika viwango vya familia na jamii. Tazama Kielelezo 3:

> Ni heshima kubwa kwangu kupata fursa ya kusimama mbele yenu hivi leo ili niweze kusema mawili- matatu kuhusu *ushindi* huu. Ushindi huu si wangu pekee bali ni wetu sisi sote (uk.64).

Mazungumzo ya Musa katika Kielelezo 3, yanaonyesha jinsi ushindi katika vita dhidi ya maradhi ulivyokuwa ushindi wa kila mtu. Kutobolewa kwa *siri* ndio ulikuwa mwanzo wa ushindi. Vilevile, *tuzo* kwa Musa ni kiwakilishi cha ushindi katika kiwango cha familia. Familia ndio nguzo kuu inayojenga jamii na ikiwa jambo lolote lingefaulu lazima familia ihusishwe. Kulingana na Wanjala (2015), asasi ya familia inapaswa kuhusishwa katika ujenzi wa jamii kwani ndio huwapa watoto malezi, huduma bora za kiafya, mavazi na makazi mema. Pia, *tuzo* kwa shule ya Hekima ni sitiari ya kiafya iliyowakilisha nafasi ya elimu katika vita dhidi ya magonjwa. Kulingana na muktadha wa matumizi, taasisi ya elimu ina jukumu la kuhamasisha jamii kuhusu njia mwafaka za kuzingatiwa katika vita dhidi ya maradhi.

### 4.3.4 Siku ya Ukimwi

Katika matini teule *Sitaki Iwe Siri*, Bwana Said Selemani mwalimu mkuu wa shule ya msingi ya Uzima anawajuliza wanafunzi wajiadae ili kuadhimisha *Siku ya Ukimwi* Duniani (uk.19). Katika muktadha wa mazungumzo baina ya mwalimu mkuu na wanafunzi, *Siku ya Ukimwi* ni sitiari kuu ya kiafya inayowakilisha ushauri uliotarajiwa kupeanwa kwa watu siku iliyotengwa. Aidha, *Siku ya Ukimwi* ni sitiari kuu kwa sababu inawakilisha suala la maradhi, ambalo ni suala kuu lililoangaziwa katika matini teule. Watu walihamasishwa kuhusu janga la UKIMWI na namna ya kujikinga na kuishi na ugonjwa huo katika mkutano huo. Isitoshe, katika Mjibalaa wagonjwa wa UKIMWI na ukoma walitengwa na kuepukwa kutokana na miiko ya kijamii (uk.23). Watu waliogopa kuhusishwa na magonjwa hayo kwa sababu ya ukosefu wa elimu bora kuyahusu. Hivyo, kwa mujibu wa WHO (2003) kuna umuhimu wa kuelimisha jamii kuhusu njia za kuzuia magonjwa ili kupunguza kuambukizwa na kuenea kwa magonjwa na kuimarisha utangamano na uiano katika jamii. Shirika la Afya Ulimwenguni

liliwahusisha wanafunzi kwa kuandaa mashindano ya uandishi wa insha kuhusu suala la UKIMWI.

### 4.3.5 Pendo katika Shari

Pendo katika Shari ni sitiari kuu ya kiafya iliyoangaziwa katika jalada la matini teule *Pendo katika Shari*. Sitiari zote za kiafya katika kitabu hicho zimeshadidia kuafikiwa kwa dhamira kuu iliyoangaziwa na sitiari kuu. Jina 'Pendo' ni la kisitiari linalorejelea mapenzi ya dhati ya mhusika mkuu Pendo kwa Sulubu. Hata hivyo, matendo maovu ya mhusika kinzani Sulubu ni ya kishari. Kwa sababu ya uzinzi, Sulubu aliathiriwa na UKIMWI na akawaambukiza Pendo na mtoto aliyezaliwa. Hali hiyo ilitumbukiza upendo wao katika shari na maafa yaliyowaacha watoto wao mayatima.

### 4.3.6 Siku ya Ukimwi

*Siku ya Ukimwi* ni aina ya sitiari kuu ya kiafya inayotawala kitabu kizima cha *Siku ya Ukimwi*. Sitiari hii inadokeza maana tofautitofauti kulingana na muktadha wa matumizi yake. Gaichu (2016) anasema kuwa, maana hiyo pia inaweza kubadilika au kubaki jinsi ilivyo kulingana na muktadha wa matumizi. Kwa msingi huu, utafiti huu umetathmini fasiri mbalimbali za sitiari kuu: *Siku ya Ukimwi* katika kitabu kiteule. Katika muktadha wa matumizi, Sitiari *Siku ya Ukimwi* imetumika kuwasilisha taswira tofautitofauti za ugonjwa wa UKIMWI. Taswira hizi zimefasiriwa na kuzua picha mbalimbali kama vile taswira ya kifo na taswira ya utupu.

#### 4.3.6.1 Taswira ya Kifo

Kifo husababishwa na magonjwa, ajali au umri mrefu. Motifu ya kifo imejitokeza kutoka mwanzo hadi mwisho wa kitabu kiteule. Yamkini, ugonjwa wa UKIMWI umehusishwa na kifo hivi kwamba, kuambukizwa UKIMWI ni kama kukata tiketi ya kifo. Aidha, kupitia mazungumzo ya kiongozi wa mkutano ni wazi kuwa ugonjwa wa UKIMWI na hauna tiba na umesambaa na kuathiri watu wengi ulimwenguni. Tazama Kielelezo 4:

> Baada ya wimbo huo, kiongozi wa shughuli aliwaambia waliohudhuria, "leo ni *Siku ya Ukimwi*. Ugonjwa wa UKIMWI unaendelea kuangamiza binadamu kote duniani. Watu wengi kutoka kusini hadi kaskazini,

> kutoka magharibi hadi mashariki, wameathiriwa na UKIMWI ….”(uk.5).

Mazungumzo yaliyoangaziwa katika Kielelezo 4, yamesawiri UKIMWI kama chanzo cha vifo vya watu ulimwenguni. Kulingana na kiongozi wa mkutano ugonjwa wa UKIMWI umesababisha vifo vya watu katika kila pembe ya dunia, jambo lililozua hatari kubwa kwa maisha ya kila binadamu. Madai hayo yamedhihirishwa na ripoti ya UNAIDS (2023) kwamba UKIMWI umeathiri watu wengi ulimwenguni. Takriban watu milioni thelathini na nane na laki nne wanaugua ugonjwa huu. Kutokana na wingi wa vifo hivyo, Kadogo anakisia kuwa huenda binadamu wote wakafagiliwa na janga hili hivi kwamba dunia ingetawaliwa na miti, mabonde na milima miaka michache ijayo.Tazama Kielelezo 5:

> Ukimwi upo. Lakini dawa yake haipo. Dawa ya pekee na ya hakika ni kubadilisha tabia ya kila mmoja wetu. Tusipobadilisha mienendo yetu, kuna hatari siku sijazo. Dunia haitakuwa na watu. Dunia hii itakuwa ya miti, mabonde, mito, milima na wanyama. Watu wataangamia kabisa wasipobadilisha mienendo. Uwanja huu utakuwa mtupu. Wanyama na miti ndio watakaopamba ulimwengu (uk. 11).

Tathmini ya mazunguzo katika Kielelezo 5 ni kwamba, UKIMWI ni janga la kimataifa na hauna dawa. Ripoti ya WHO (2003) inaafikiana na kauli hii kwa kusema kuwa, UKIMWI umeathiri watu wengi ulimwenguni hasa mataifa yanayoendelea huku vifo vingi vikishuhudiwa barani Afrika. Njia ya kipekee ya kujikinga ni kuepukana na mienendo inayosababisha ugonjwa huu.

#### 4.3.6.2 Taswira ya Utupu

Dhana tupu imefafanuliwa na TUKI (2004) kama hali ya kutokuwa na kitu ndani. Katika matini teule dhana utupu inarejelea hali ya kuwa uchi, kupungukiwa kwa mawazo, afya, au uwezo wa kufanya jambo fulani. Ugonjwa wa UKIMWI umesababisha *utupu* katika jamii zilizoathiriwa na ugonjwa huu katika matini teule. Waathiriwa wa ugonjwa wa UKIMWI wamesawiriwa kama watu waliodhoofika na wasiokuwa na matumaini ya kuishi. Hali hii imedhihirishwa na wimbo ulioimbwa na waimbaji walioalikwa kutumbuiza wageni katika *Siku ya Ukimwi*.

Tazama Kielelezo 6:

> Ugonjwa umetokea,
> Unaitwa Ukimwi,
> Ukimpata mtu,
> Anamalizika kama nguo.

Mfano wa wimbo wa kisitiari ulioangazia *utupu* ulioshuhudiwa na waathiriwa wa UKIMWI umeangaziwa katika Kielelezo 6. Katika hali ya kawaida nguo hutumika kufunika uchi. Nguo inaporaruka sehemu za siri za binadabu huwekwa wazi kwa kila mtazamaji. Hali hii huleta fedheha na upungufu wa kimawazo kwa mwathiriwa. Katika muktadha wa matumizi, *nguo* ni sitiari ya kiafya iliyotumika kuwakilisha *utupu* unaomkumba mgonjwa wa UKIMWI. *Utupu* huo umejitokeza kupitia kuambukizwa na magonjwa nyemelezi, unyanyapaa na kuathirika kimawazo. Kutokana na athari hizi, wagonjwa wa UKIMWI wanajihisi kuwa watawa na watu wasiokuwa na umuhimu katika jamii. Wanapoteza matumaini na maisha kiasi kwamba wengine hujitoa uhai. Mhusika Kadogo alipong'amua jinsi wagonjwa wa UKIMWI walivyopoteza hamu ya kuishi, aliwatahadharisha dhidi ya kufa moyo kabisa kwani kulikuwa na matumaini ya kuishi maisha marefu.
Tazama Kielelezo 7.

> Hata hivyo msidhani kuwa kupatwa na Ukimwi ndio mwisho wa maisha. Ikiwa yeyote ameambukizwa, anapaswa kuishi kwa kuzingatia maadili mema, kula vyakula vyenye kujenga mwili na kukinga maradhi na pia kunywa maji safi na kufanya mazoezi.

UKIMWI hauna tiba. Hata hivyo, Kielelezo 7 kinahusu mawaidha kwa wagonjwa wa UKIMWI, ambapo Kadogo anawashauri wale lishe bora na kufanya mazoezi kila wakati, ili kupambana na makali ya ugonjwa huo. Mawaidha hayo yanashadidiwa na pendekezo la Wizara ya Elimu (2002) nchini Kenya la kujumuisha mafunzo ya kiafya kama vile usafi, lishe bora na athari za magonjwa kwa binadamu katika mtaala wa elimu, ili kuwafahamisha wanajamii njia bora za kupambana na maradhi. Pia, utekelezaji wa Ajenda 2063 ya Africa Tunayoitaka inayotilia mkazo uimarishaji wa huduma za afya, usafi, lishe bora na maji safi ni wa busara katika vita dhidi ya maradhi ya UKIMWI.

Kadhalika sitiari kuu za kiafya zimetumika kuangazia masuala mbalimbali ya kiafya katika matini teule ya *Kosa la Marehemu*. Sitiari zilizotambuliwa na mtafiti ni:

**4.3.7 Kosa**

*Kosa* ndio sitiari kuu iliyotumiwa na mwandishi kuwasilisha maudhui yake katika matini teule. Mwandishi ametumia sitiari hii kurejelea tendo la kujamiana ambalo lilisababisha mateso na kifo cha mhusika Daudi. Mwandishi pia ametumia sitiari hiyo kurejelea tendo la ngono ambalo lilikuwa mwiko kutaja hadharani katika jamii. Kwa mujibu wa Nadharia ya Sitiari ya Dhana, ni bora kutumia lugha ya kisitiari kurejelea masuala yanayochukuliwa kuwa mwiko katika jamii ili kurahisisha mawasiliano. Hivyo, masuala changamano yaliweza kuwasilishwa kwa njia ya kiulinganishi na kwa mtindo uliokubalika. Daudi alidhibitisha haya alipofafanua kosa alilolifanya na kuathiri maisha yake. Tazama Kielelezo 8;

> "Sikujua kumbe yule msichana alianza *kutembea na wanaume* akiwa bado yuko katika shule ya msingi. Alikuwa ni mwenye tamaa ya hela. Kwa hivyo wanaume aliokuwa *akitembea nao* ni wale wenye pesa. Akipata pesa alinunua vitu vidogovidogo kama chipsi na vipodosi. Maskini ya Mungu aliponzwa na hizo chipsi. *Kati ya wale wanaume aliokuwa akitembea nao* kumbe mmoja alikuwa na Virusi vya UKIMWI na baadaye alifariki. Mimi nilikuwa sijui. Watu walidai kwamba yule mwanaume alirogwa, kwa sababu ya pesa zake. Yule msichana naye aliamini hivyo. Kumbe ilikuwa ni UKIMWI. Nami bila kujua nilijamiiana naye bila kinga. Hilo ndilo *kosa* nililolifanya" (uk.51).

Mazungumzo katika Kielelezo 8 yameangazia namna Daudi alivyojuta kwa kuhusika kingono na mwanamke aliyempenda, bila kutumia kinga wala kupimwa magonjwa ya zinaa. Pia, usemi huo umethibitisha imani potovu ya kijamii dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI. Baadhi ya jamii huamini kuwa, UKIMWI ni ugonjwa uliotokana na kurogwa jambo ambalo Daudi alifutilia mbali. Kulingana na Daudi, UKIMWI ni ugonjwa uliosambazwa kupitia ngono na watu wanapaswa kujihathari kwa kupata ushauri wa daktari kabla ya ndoa ili wasifanye kosa alilofanya.

Katika kitabu kitelue *Madhila ya Bi. Shufaa,* sitiari kuu ya kiafya iliyorejelea masuala ya kiafya yaliyoangaziwa ni **Mama Safi**.

### 4.3.8 Mama Safi

Tenseen na Khan (2015) wanasema kuwa sitiari huwasilisha maana kulingana na muktadha wa matumizi yake. Kwa msingi huu, Bi. Shufaa amerejelewa kama *Mama Safi* kulingana na hali yake ya juu ya usafi katika kijiji cha Mangelepa. Hivyo, *Mama Safi* ni sitiari ya kiafya iliyotumika kuwakilisha suala la usafi katika viwango vya familia na kijamii. Katika matini teule Bi. Shufaa amesawiriwa kama kielelezo cha usafi katika asasi ya familia na jamii. Tazama Kielelezo 9.

> Mkewe mzee Iddi aliyeitwa Bi. Shufaa, alijulikana mtaani kama '*Mama Safi*.' Mama huyu alijiweka nadhifu kila wakati. Akiongea, ungedhani anayapima maneno yake kwa uzani. Nguo zake safi, msuko wake wa nywele wa matuta uliomtofautisha kabisa na wanawake wengi kijijini. Ungedhani ni mwalimu chuoni lakini wapi! Mama safi hakuwahi kuona mlango wa shule. Upande wake ulikuwa ni kama kizalia ama hata pengine ilikuwa ni talanta yake (uk. 2).

Maelezo katika Kielelezo 9, yameangazia kwa upana jinsi sitiari ya kiafya *mama safi* ilivyotumika kusawiri suala la usafi katika jamii. Mtafiti aligundua kuwa kado na usafi wa kimwili, sitiari hii pia ilirejelea adabu kama aina ya usafi. Hii ilidhihirishwa na kauli ya mwandishi kuwa Bi. Shufaa hakuwa akiongea ovyo ovyo. Alikuwa pia akiyapima maneno aliyozungumza kwa makini. Kwa ujumla, usafi ni dhana pana inayorejelea usafi wa kimwili, lugha ya adabu na mawasiliano mema na majirani.

## 4.4 Sitiari za Kikaida za Kiafya katika Vitabu Teule

Kulingana na Nadharia Changanuzi ya Sitiari ya Dhana, kuna aina mbalimbali za sitiari ambazo huwasilisha maana tofautitofauti kulingana na mila na mazingira ya matumizi yake. Sitiari za kikaida ni miongoni mwa sitiari hizi. Wamitila (2008) anasema kuwa sitiari za kikaida hutumiwa katika mawasiliano ya kawaida katika utamaduni maalumu, kwa lengo la kuipa muundo sehemu ya utamaduni wa jamii inayotumia lugha hiyo. Kobia (2008) anashadidia kauli hii kwa kusema kuwa, sitiari inaweza kutumiwa kuwasilisha ujumbe unaokisiwa kuwa mwiko katika jamii kwa njia tofauti na inayokubalika. Kauli hii inaafikiana na Nadharia ya Sitiari ya Dhana kuwa, sitiari inapotumiwa vyema katika mawasiliano hurahisisha uelewa wa masuala changamano na mengine yaliyo mwiko katika jamii kwa njia ya kiulinganishi.

Utafiti huu umebainisha kuwa, sitiari za kiafya za kikaida zilitumika kuangazia masuala ya kiafya yaliyoathiri Mjibalaa kama vile magonjwa na mihadarati katika matini teule ya *Nimefufuka*. Miongoni mwa sitiari zilizotumika ni:

### 4.4.1 Maisha

Sitiari ya *maisha* imetumika katika muundo wa sentensi ambapo Sikitu amelinganisha maisha na mnyama. Sikitu alitumia sitiari ya *maisha* kuwakilisha mnyama mkali asiyekuwa na huruma na aliyefyonza maisha ya binadamu. Kwa mujibu wa Kuzmina (2013) sitiari hueleweka kwa urahisi inapotumika katika sentensi. Hivyo, mtafiti alichunguza maana ya sitiari ya *maisha* katika muundo wa sentensi.
Tazama Kielelezo 10:

> “Dada yangu mdogo hakumaliza masomo ya shule ya upili. Alitorokea Mombasa eti kuponda *maisha*. Kumbe *maisha* yalikuwa yakimngoja, yamponde, yamfyonze, yasimbakishe hata chembe.” (uk.2).

Mwandishi ametumia sitiari ya kiafya ‘*maisha’* katika Kielelezo 10 kuwakilisha matatizo ya kiafya ambayo yalimwathiri mhusika kinzani Lena. Katika muktadha wa mazungumzo, Sikitu ametumia sitiari hiyo kuonyesha jinsi Lena alivyoponda raha na kutia afya yake katika maangamizi.

### 4.4.2 Nyumba ya Udongo

Tabia ya Lena haikumfurahisha dadake Sikitu. Lena alimkejeli Sikitu kwa kumwita mshamba. Matamshi hayo yalimhuzunisha Sikitu na alimjibu kwa kujiita *nyumba ya udongo*. Tazama Kielelezo 11.

> Akaongeza kidonda kwa kuniita sokwe-mtu-tasa. Nikajitenga kando, kwani mie *nyumba ya udongo* sihimili vishindo (uk.3).

N*yumba ya udongo* ni sitiari ya kiafya ya kikaida iliyotumika katika Kielelezo 11 kulinganisha maisha na nyumba ya udongo ambayo ingebomoka wakati wowote. Sikitu alitumia sitiari hiyo kumfahamisha Lena kuwa, afya nzuri na urembo aliokuwa nao ulikuwa wa muda na ungeweza kubomoka wakati wowote mithili ya nyumba ya udongo, ikiwa hangejihadhari na anasa za dunia.

### 4.4.3 Safi Safina

Sikitu amewaita wanaume *safi safina*. Ametumia sitiari ya kiafya *safi safina* kama kejeli kwa wanaume kutokana na jinsi walivyowanyanyasa wanawake. Anathibitisha hayo kwa kuangazia jinsi wanaume walivyotawaliwa na ubabedume na kuzingizia shida za ukosefu wa watoto kwa wanawake. Tazama Kielelezo 12.

> Mume alikataa katakata himizo la kwenda hospitalini. Alisema ukosefu wa uwezo wa kupata mtoto ni shida ya mwanamke. "Wanaume ni *safi safina* na ikiwa itatoka kasoro, hiyo ni kasoro ya mwanamke," nayakumbuka maneno haya kwa uchungu usio na mfano (uk.9).

Sikitu ametumia sitiari ya kiafya *safi safina* katika Kielelezo 12 kama kejeli kwa lengo la kuwatenganisha na matatizo ya utasa ilhali yanaweza kutokea kwa jinsia zote. Utasa ni suala la kijinsia ingawa wanaume waliwazingizia wanawake matatizo ya uzazi. Jamii zilizotawaliwa na taasubi za kiume hukumbwa na kasumba hii. Ni muhimu kufahamu kuwa utasa ni suala la kiafya na linaweza kuathiri wanaume na wanawake kwa ujumla.

### 4.4.4 Matunda

Mtoto aliyezaliwa na Lena aliugua UKIMWI na Sikitu alitumia wakati mwingi kumtafutia matibabu. Baadaye mtoto huyo alianza kupata nafuu kutokana na juhudi za Sikitu za kumtafutia matibabu na utunzi bora. Sitiari ya kiafya ya '*matunda'* imetumika katika muktadha huo kurejelea mafanikio ya matibabu ambayo Sikitu alimpa mtoto huyu. Tazama Kielelezo 13.

> Baada ya kukitazama kwa makini kitoto hicho kikipigana na vimbunga vya maisha na kuelekea kushinda, matumaini na mapenzi yameibuka. Safari za hospitali zimeanza kuzaa *matunda*. Sasa nakiita Shujaa badala ya Taabu. Pole pole anageuka mtoto badala ya kitoto. Afya yake imeanza kuimarika na uzito wa mwili kuongezeka (uk.12).

Mazungumzo ya Sikitu katika Kielelezo 13 yamedhihirisha jinsi alivyokuwa amepoteza matumaini na maisha ya mtoto Taabu. Hata hivyo, mtoto huyo alianza kupata nafuu baada ya kutibiwa kwa muda mrefu. Sikitu alirejelea ufanisi wa matibabu kama *matunda*. Anasema kuwa, safari za hospitalini zilianza kuzaa *matunda* mema na akakiita kitoto hicho Shujaa badala ya Taabu. Hili ni jambo la kutia moyo kwa wagonjwa wa UKIMWI kuwa, kuambukizwa na ugonjwa huo haukuwa mwisho wa

maisha. Kilichokuwa muhimu ni kupata matibabu ili kuzuia magonjwa nyemelezi na athari zake.

### 4.4.5 Gofu

Mdee na wengine (2022) wanaelezea dhana Gofu kama aina ya mjengo au nyumba iliyobomokabomoka na iliyohamwa. Hata wanyama hawangeishi katika nyumba ya aina hiyo kwani huhatarisha maisha. Hivyo, mhusika Sikitu anamlinganisha Jose na *gofu* kutokana na tabia yake ya ujuha. Tazama Kielelezo 14.

> Kondoo walioletwa na mjomba wametoweka. Idadi ya kuku, Sufuria, sahani, bakuli, vijiko ni simulizi tu. Uraibu wa Jose unatisha. Si ajabu amebaki *gofu* la mtu. Kuna haja gani kuwa na ndugu asiyekufaa kwa lolote? (uk.14).

Sikitu anaelezea hali ya kiafya ya nduguye kwa kumlinganisha na gofu. Kulingana na muktadha wa matumizi katika Kielelezo 14, *gofu* ni aina ya sitiari ya kiafya ya kikaida iliyotumika kumlinganisha Jose na mtu shaghalabaghala, mwenye afya duni, mwili usiokuwa na nguvu na mtu aliyeweza kuaga dunia wakati wowote. Pia ni mtu aliyekata tamaa na maisha na mgonjwa asiyejua kuwa amegonjeka. Pombe na mihadarati iliharibu afya yake. Kwa jinsi hii Sikitu anasema kuwa, Jose hakuhitaji daktari kutangaza kuwa kifo kilimkondolea macho.

Mtafiti pia amebaini aina mbalimbali za sitiari za kiafya ambazo mwandishi ametumia katika matini teule ya *Sitaki Iwe Siri* kurejelea masuala ya kiafya. Miongoni mwa sitiari alizotumia ni:

### 4.4.6 Mwendawazimu

Mwendawazimu ni mtu aliye mgonjwa kiakili (TUKI, 2004). Kutokana na upunguvu wa kiakili mwendawazimu haogi, huishi maisha ya kuhangaika na kula vyakula vichafu. Mwandishi wa matini teule ametumia '*mwendawazimu'* kama sitiari ya kiafya kuwakilisha uchafu. Tazama Kielelezo 15.

> "Hujachana nywele aisee. Zinaonekana kama za *mwendawazimu,*" Ukwa alisema na wote wakaangua kicheko. Musa aliwashukuru dada zake kwa kumkumbusha kuchana nywele zake. La sivyo angekiona cha mtema kuni shuleni (uk.5).

Haki amelinganisha tabia ya Musa ya kutochana nywele na tabia ya mwendawazimu ambaye ni mchafu na hula vyakula vichafu. Tathmini ya maana ya sitiari *mwendawazimu* katika Kielelezo 15 ni kwamba, inahimiza watu kuepukana na uchafu ili kuzuia magonjwa kama vile kipindupindu.

### 4.4.7 Meza

Kulingana na Mdee na wengine (2022), maana ya kimsingi ya neno meza ni kifaa ambacho kinatumiwa kulia, kuandikia au kuchezea. Hata hivyo, Lakoff na Johnson (1980) anasema kuwa neno linaweza kuwa na maana tofauti linapotumika kama sitiari. Hivyo, katika muktadha wa mazungumzo sitiari ya kiafya *"meza"* imetumika katika matini teule kurejelea mlo. Tazama Kielelezo 16.

> Nyanya hakuongea hadi sala ya wajukuu wake ikamilike. Alikwenda kuwaandikia *meza* ili wajipatie staftahi na baadaye waende shuleni (uk.5).

Maelezo katika Kielelezo16 yameangazia juhudi za Mwalonga katika kuwatunza wajukuu wake. *Meza* ni sitiari ya kikaida iliyotumika kurejelea chakula cha asubuhi ambacho Mwalonga alitayarishia wajukuu wake.

### 4.4.8 Muhuri wa Mauti

*Muhuri wa mauti* ni sitiari ya kiafya ambayo ilitumiwa na mwandishi kurejelea kifo. Hii imeangaziwa katika usemi ufuatao: Tazama kielelezo 17.

> Kila aliyeugua maradhi haya alianza kuepukwa kama mgonjwa wa ukoma. Akaogopwa jinsi yanavyoogopwa mauti. Akabaguliwa na jamii. Maradhi yenyewe yakachukuliwa kuwa ni *muhuri wa mauti* kwa kila aliyekumbwa na mkosi wa kuambukizwa (uk.12).

Usemi huu umetumika katika Kielelezo 17 kama sitiari ya kiafya kuangazia taswira ya kifo ambacho kilitokana na maradhi ya UKIMWI. Mtu aliyeambukizwa ugonjwa huo hakuwa na la kufanya kwani ilikuwa ni lazima afe kwani tayari amepigwa *muhuri wa mauti*.

### 4.4.9 Ukuni

Ukuni ni kibanzi kigumu cha mti kinachotumiwa kukokea moto (TUKI, 2004). Katika kitabu kiteule, mwandishi analinganisha mwili wa kondakta na ukuni. Mtafiti amebaini kuwa unywaji wa pombe na matumizi ya mihadarati huathiri afya ya mtu na kusababisha ugumu katika mwili. Matumizi ya dawa za kulevya yalidhoofisha afya ya utingo kiasi kwamba mikono yake imelinganishwa na ukuni. Tazama Kielelezo 18.

> "Haraka jamaa- tuokoe masaa- gari linataka kurudi mjini kuchukua abiria zaidi," kondakta alisema huku akiligonga gari kwa mkono wake ulioonekana kukauka kama *ukuni* (uk.31).

Katika muktadha wa matumizi, mwandishi ametumia *ukuni* katika Kielelezo 18 kama sitiari ya kiafya kuwakilisha afya duni ya utingo iliyosababishwa na athari za miraa na dawa za kulevya. Sitiari hii inatahadharisha dhidi ya matumizi ya mihadarati kwani hudhoofisha afya na kumuweka mtumizi katika hatari ya maambukizi ya maradhi.

### 4.4.10 Sare Nyeupe pe pe pe

Sare nyeupe ni vazi linalovaliwa na nesi hospitalini. Vazi hili limetumika kama sitiari ya kiafya ya kikaida kuwakilisha matumaini kwa wagonjwa. Tazama Kielelezo 19:

> Nesi waliokuwa wamevaa *sare nyeupe pe pe pe* na karatasi- umbo la sambusa mbili zilizotulia dede kichwani walifika karibu na magari yale haraka huku wanasukuma machela yenye magurudumu. Wanawake wawili waja wazito waliokuwa wakigaragara kwa maumivu makali waliondolewa kwenye ambulansi zile na kupelekwa haraka katika chumba cha kujifungua cha akina mama (uk.31-32)

Tathmini ya maelezo katika Kielelezo 19 ni kuwa, wahudumu wa kiafya wana wajibu muhimu wa kutibu wagonjwa na kuokoa maisha. Wahudumu hawa hujitoa mhanga kuokoa maisha na kutibu magonjwa. Mgonjwa anapopelekwa hospitalini hutibiwa na hupewa matumaini ya kuishi. Hivyo, matumizi ya rangi nyeupe katika hospitali ni ishara ya kuwatia wagonjwa moyo kwamba, kuna matumaini na uwezekano wa kupata afueni na kuendelea na maisha.

### 4.4.11 Makengeza

Miongoni mwa nesi waliovalia sare nyeupe kuwakilisha matumaini kwa wagonjwa, kulikuwa na nesi aliyekuwa na makengeza. Katika muktadha wa matumizi, makengeza

ni sitiari ya kiafya iliyotahadharisha kuwa si kila ugonjwa ungetibika. Tazama Kielelezo 20:

> Baada ya kuwafikisha akina mama hospitalini, ambulansi zile zilizima ving'ora vyao na kuondoka hospitalini. Musa, Haki na Ukwa nao walikwenda hadi ukumbi wa kuwapokelea wagonjwa hospitalini.Walimkuta muuguzi mmoja mfupi mnene na mwenye macho yenye *makengeza*." (uk.32).

Maelezo katika Kielelezo 20 ni ya kisitiari yanayopasha ujumbe kwamba, ingawa hospitali ni mahali pa matumaini daktari hana uwezo wa kutibu kila aina ya ugonjwa. Neno *makengeza* limetumiwa katika Kielelezo 20 kama sitiari ya kiafya kuwakilisha changamoto zinazomkumba daktari anapomtibu mgonjwa. Tathmini ya matumizi ya sitiari hiyo ni kuwa katika kutibu magonjwa pia kuna *makengeza*. Yaani ugonjwa unaweza kutibiwa au la. UKIMWI ni baadhi ya magonjwa ambayo hayana tiba ila tu dawa za kupunguza makali.

### 4.4.12 Ndwele

Kwa mujibu wa Mdee na wengine 2022), ndwele ni aina yoyote ya ugonjwa. Kulingana na muktadha wa matumizi, *ndwele* ni sitiari ya kiafya iliyotumiwa katika kitabu kiteule kurejelea ugonjwa wa UKIMWI uliosababisha vifo vya wazazi wa Musa, Ukwa na Haki na kuachwa makiwa. Ingawa Mwalonga alifahamu kuwa mwanawe aliuwawa na ugonjwa huo, alitumia sitiari '*ndwele*' kuurejelea. Mwalonga alihepa kutaja jina "UKIMWI" kutokana na miiko ya kijamii iliyochukulia UKIMWI kama laana na kuwatenga waliouugua. Katika ukurasa wa kumi na moja, tunaarifiwa kuwa Musa na dada zake walimhimiza Mwalonga kuwafahamisha aina ya ugonjwa uliowaua wazazi wao lakini alikataa katakata. Alitumia tu sitiari *ndwele.* Tazama Kielelezo 21:

> Nyanya alitumia rasilimali nyingi kugharimia matibabu yao, lakini *ndwele* hiyo haikusikia dawa. Wakakonda kama *ng'onda* na macho yao kuwaingia ndani. Mbavu zao zikaweza kuhesabika (uk.9).

Sitiari ya kiafya ya maradhi '*ndwele'* na *'ng'onda'* pia zimeangaziwa katika Kielelezo 21. Kwa mujibu wa Mdee na wengine (2022), ng'onda ni samaki aliyepasuliwa kati na kukaushwa. Sitiari ya kiafya ya maradhi *ng'onda* imetumika kuangazia taswira ya mtu dhaifu na aliyekonda. Hizo ni sifa za mgonjwa wa UKIMWI.

### 4.4.13 Uta

Kulingana na TUKI (2004) uta ni kifaa cha kufyatua kilichopinda na kufungwa na kamba na hutumiwa kuwinda. Ingawa Nyanya Mwalonga alizeeka kiasi cha kujipinda, alipitia shinda nyingi katika kulea wajukuu walioachwa mayatima. Alipitia changamoto chungu nzima ambazo zilidhoofisha afya yake na kusababisha makunyanzi katika mwili wake. Mwandishi ametumia sitiari na lugha ya taharuki kuelezea hali hiyo ya kiafya ya Mwalonga. Kwa mujibu wa Nadharia Changanuzi ya Sitiari ya Dhana, lugha ya kisitiari inapotumika kwa ufasaha huwa na nguvu ya kunasa makini ya hadhira na kuwashawishi kuzingatia mwelekeo fulani. Hivyo, lugha hiyo ilifaa katika kuangazia athari za UKIMWI katika jamii, ambapo Mwalonga aliathiriwa na vifo vya wanawe na kujitwika majukumu ya kulea watoto wao walioachwa makiwa. Katika ukurasa wa saba mwandishi anasema: Tazama Kielelezo 22:

> Nyanya Mwalongo alikuwa na umri wa miaka sitini hivi. Nywele zake kichwani zilikuwa zimebadilika na kuwa nyeupe kama theluji. Mwili wake ulikuwa umevamiwa na makunyanzi kwa sababu ya uzee. Mgongo wake ulikuwa umepinda kama 'uta' na alilazimika kutembea kwa mkongojo (uk.7).

Kielelezo 22 kimeangazia taswira ya mama mzee aliyedhoofika kiafya. Kudhoofika huku kulisababisha mgongo wake kupinda na kutembea kwa usaidizi wa mkongojo. Sitiari ya *uta* imetumika kurejelea athari za kiafya ambazo Mwalonga alipata kutokana na majukumu ya nyumbani. Ingawa alikuwa na umri wa miaka sitini, afya yake iliathiriwa na majukumu ya kulea wajukuu ilhali hakuwa na mapato. Mwalonga ni kiwakilishi cha jamaa ambazo hutwikwa majukumu ya kuwalea watoto waliofiwa na wazazi walioathiriwa na UKIMWI. Baadhi ya jamaa hizo huathirika kiuchumi na kiafya kwa sababu ya ukosefu wa mapato, jambo ambalo linatatiza kuafikiwa kwa maendeleo endelevu katika jamii.

### 4.4.14 Nyembe

Kwa mujibu wa TUKI (2004) Wembe ni kifaa cha kunyolea. Pia, hutumiwa kukata na huzua uchungu mkali kinapomkata mtu. Hivyo, Musa amefananisha maumivu ya UKIMWI na makali yanayotokana na kukatwa na wembe. Ametumia neno '*nyembe*' kama sitiari ya kiafya ya maradhi kurejelea ugonjwa wa UKIMWI. Tazama Kielelezo 23:

> Aliposhiriki katika mambo ya anasa, Yuri hakujua kuwa mambo yangemgeuka. Alikumbuka jinsi wazazi na walimu wake walivyojitahidi kwa hali na mali kumwelimisha ili ajitayarishe kwa maisha ya siku za usoni, lakini akalilia wembe**.** *Nyembe* za walimwengu zilikuwa zimemkata Yuri na kumjeruhi vibaya (uk.48).

Kielelezo 23 kimeangazia majuto ya Yuri baada ya kukaidi wasia wa wazazi wake na walimu. Ukaidi huo umemtumbukiza katika anasa za ulimwengu na kuambukizwa magonjwa ambayo yamerejelewa kama *nyembe*. *Nyembe* hizo zimemkata bila huruma. Pia, Kielelezo 23 ni sitiari ya kiafya inayochora taswira ya mhusika Yuri ambaye amekumbwa na dhiki, mahangaiko na majuto ambayo yamemchoma moyo na kuathiri afya yake. Hii ni tahadhari kwa watoto dhidi ya kukaidi mawaidha ya wazazi. Watoto wanapaswa kusikiliza na kuzingatia mashauri wanayopewa na wazazi. Wazazi wa Yuri walikuwa na ushauri ambao ungemsaidia Yuri lakini aliwadharau na kuwapuuza. Baadaye aliangulia patupu na kufunzwa na ulimwengu ambao ulimramba bila huruma. Aliugua UKIMWI na kuaga dunia.

Vilevile, sitiari za kiafya za kikaida kadhaa zimetumika kuangazia masuala ya kiafya katika kitabu kiteule *Pendo katika Shari*. Mtafiti ametambua aina zifuatazo za sitiari za kiafya:

### 4.4.15 Tambara

Pendo amejilinganisha na *tambara*. Tambara ni nguo ambayo imechanikachanika (TUKI, 2004). Hata hivyo, kama anavyosema Charteris-Black (2004), maana ya sitiari inaweza kubadilika kulingana na mila na mazingira ya matumizi yake. Kwa msingi huu, Pendo ametumia ‘*tambara* ‘kama sitiari ya kiafya kujirejelea kama mtu ambaye hakuwa na nguvu au afya nzuri kwa jinsi alivyokuwa ameteswa na Sulubu. Tazama Kielelezo 24:

> Katika keto za moyo wake alituhumu kwamba Sulubu keshapata mwanamke mwingine hasa kutokana na vile alivyokuwa akiyakwepa maswali yake. Yeye sasa alikwisha tupwa kama *tambara* (uk.2).

Aidha, kama ilivyoelezwa katika Kielelezo 24, Pendo amejilinganisha na *tambara*. Amejichukulia kama mtu hoi na asiyekuwa na maana. Ingawa Pendo alijifungua na

kuhitaji kutunzwa vyema ili apate nguvu, Sulubu alimtesa na kuhepa kutimiza wajibu wake kama mume nyumbani. Aliendelea na tabia ya hawara.

### 4.4.16 'Danger'

Mwandishi amechanganya ndimi ili kueleza kinagaubaga tabia potovu ya Sulubu. Gari lake lilipachikwa jina 'danger,' kwa sababu ya kukimbizana na wanawake mjini. Tazama Kielelezo 25:

> Kwenye mitaa hiyo, watu waliozoea kuona gari lile, walilipachika jina na kuliita '*danger*' kwani walijua mwenye gari hilo alikuwa hatari kwa kuwateka bakuja wasichana mitaani humo (uk.13).

'*Danger'* ni sitiari ya kiafya iliyoangaziwa katika Kielelezo 25 kusawiri tabia ya uzinzi ya Sulubu. Amesawiriwa kama mwanaume kahaba na hatari katika kufanya ngono za kiholela na wasichana wa mitaa bila kuogopa kuambukizwa magonjwa ya zinaa.

### 4.4.17 Jongoo

Kulingana na Mdee na wengine (2022), Jongoo ni mnyama mwenye miguu mingi na asiyekuwa na nguvu wala mifupa. Sulubu na Makelele walimwita Matano jongoo. Walitumia sitiari '*jongoo'* kumlinganisha Matano na mwanaume asiyekuwa na uwezo wa kufanya ngono. Tazama Kielelezo 26:

> Matano aliwashauri rafikize Sulubu na Makelele na kuwatahadharisha dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI uliokuwa ukiua watu kila uchao. Lakini hawa walimpuuza na kumwona kama jongoo asiyeweza kupanda mtungi. Walimsuta na kumwambia hajui maisha ni nini (uk.13).

Kielelezo 26 kimeangazia mjadala baina ya Matano, Sulubu na Makelele kuhusu hatari iliyotokana na maradhi ya UKIMWI. Baadhi ya madhara hayo ni vifo vya watu. Makelele na Sulubu wanapuuza ushauri wa Matano dhidi ya kujihusisha na ukahaba na wanamwita *jongoo*. Katika muktadha wa matumizi, j*ongoo* ni sitiari ya kiafya ambayo imetumika kurejelea upungufu wa nguvu za kiume. Wanaume wenye shinda hiyo wanahitaji kupata ushauri wa daktari. Sulubu na Makelele wametumia sitiari hiyo kumkejeli Matano kwa kususia kujiunga nao katika harakati zao za kukimbizana na wanawake.

### 4.4.18 Mume Jina

Katika matini teule imedhihirika ya kwamba, dhuluma dhidi ya jinsia ya kike zilizidi kuongezea Pendo tafrani. Kwa mujibu wa Simala (2000) jinsia ya kike imedhalilishwa na wanaume kutokana na tamaduni hasi za kijamii zilizompa mwanaume uwezo kumshinda mwanamke. Mwanamke amerejelewa kama chombo cha kutawaliwa na mwanaume. Sulubu anayetawaliwa na taasubi za kiume anaendelea kumtesa na kumnyanyasa Pendo bila huruma. Kwa jinsi hiyo, Pendo anamwita Sulubu *mume jina*. Tazama Kielelezo 27:

> Maisha kati ya Sulubu na Pendo yalizidi kuwa na tafrani nyingi, mapenzi kati yao yakaanza kutoweka mithili ya umande kwenye jua. Kwa Pendo, Sulubu alibakia kuwa *mume jina* tu. Hata hivyo, katika misukosuko hii. Pendo alizidi kuvumilia, huku akiutazamia mustakabali mwema kati yake na Sulubu (uk.7).

*Mume jina* ni sitiari ya kiafya iliyotumiwa na mhusika Pendo kurejelea utepetevu na kutowajibika kwa Sulubu kama baba katika kuikimu familia yake. Kama ilivyoangaziwa katika Kielelezo 27, Sulubu alikiuka majukumu yake ya kulisha na kutunza familia yake. Pendo alisita kumlazimisha Sulubu kuwajibika katika familia, kwa kuogopa tamaduni za kijamii zinazomtahadharisha mwanamke dhidi ya kutomdadisi au kumtia ghadhabu mumewe. Tazama Kielelezo 28:

> Lakini kwa vile utamaduni wake ulimfunza kutomdadisi mume anapochelewa kurejea nyumbani, hakutaka kwenda kinyume na ada hii. Isitoshe, alifunzwa kutomtia ghadhabu mumewe, na kila wakati kujaribu kudumisha amani katika nyumba yake (uk.2).

Mwandishi katika Kielelezo 28, ameangazia jinsi utamaduni unachangia katika kuendeleza udhalilishwaji wa jinsia ya kike. Tamaduni na mila za kijamii zimempatia mwanaume nguvu na uhuru wa kumtawala mwanamke na kumfanya anavyotaka. Tamaduni hasi za kijamii zimemchukulia mwanamke kama mali au chombo cha kutumiwa na mwanaume. Hali hii imesababisha matatizo ya kiafya kwa Pendo kama vile kusongwa na mawazo na kudhoofika kiafya kutokana na majukumu mengi ya nyumbani.

### 4.4.19 Moto

Kulingana na Lakoff (1992) Nadharia Changanuzi ya Sitiari ya Dhana inaangazia kwa undani namna sitiari imetumika katika kuelewa ulimwengu wa kihalisia. Hivyo, mwandishi ametumia sitiari ya *moto* kusawiri ukali wa maneno ambayo Sulubu alitumia kumuadhibu mkewe. Sitiari ya *moto* imetumiwa ili kuelewa hali ya Pendo kwa undani kwa kuilinganisha na hali halisi ya kuchoma. Moto ni hatari na huchoma kila kitu na kusababisha madhara makubwa. Tazama Kielelezo 29:

> "Kwa hivyo ukaona heri ujenge kibanda karibu na barabara ili kila mwanaume mpita njia aweze kukusabahi, ili nawe ufurahi huku ukipasua vicheko 'kwa, kwa, kwa,' na kuwashangaza wapita njia. Basi kawambie hao wasiri wako vicheko hivyo vimekwisha, na duka lishafungwa na mwenyewe." Sulubu alitamka kwa kejeli. *Maneno hayo yalimchoma ini Pendo mithili ya misumari ya moto* (uk.19).

Kutokana na mazungumzo katika Kielelezo 29, ni dhahiri kuwa Sulubu hakuwa na utu wala heshima kwa mkewe Pendo. Anamlinganisha na virukanjia waliotumia kila aina ya mbinu kunasa wanaume. *Moto* umetumiwa kama sitiari ya kiafya kurejelea msongo wa mawazo. Matamshi ya Sulubu yalisababisha msongo wa mawazo na kumchoma Pendo jinsi linavyochoma kaa la moto. Pendo alighadhabishwa na matamshi hayo kwa sababu alikuwa mtiifu na mwaminifu katika ndoa na alianzisha biashara tu ili ajikimu kimaisha. Tathmini ya usemi ulioangaziwa katika Kielelezo 29 ni kwamba, ukosefu wa mawasiliano bora katika ndoa husababisha kusambaratika kwake. Hivyo, kuna haja ya kuheshimiana na kukuza ushirikiano kati ya bwana na bibi ili kudumisha amani katika familia.

### 4.4.20 Vumbi

Pendo amelinganisha vumbi la rangi ya hudhurungi lililopaa angani na kutoweka kwa mapenzi kati yake na Sulubu. *Vumbi* ni sitiari ya kiafya iliyotumika kusawiri mvukizo wa mapenzi kati ya Pendo na Sulubu.Tazama Kielelezo 31:

> Pendo alilitazama *vumbi* hilo lililopaa na kutokomea kwenye anga la magharibi. Alililihusisha na kutoweka kwa mapenzi kati yake na Sulubu ambaye sasa amemtema kama mate (uk.20).

Kielelezo 31 kimeangazia namna neno 'vumbi' lilivyotumika kuelezea dhana dhahania ya kutoweka kwa mapenzi. Kulingana na Anudo (2018) sitiari za dhana huangazia

vyema ulimwengu wa kidhanifu. Hivyo, mwandishi amefaulu kuelezea dhana dhahania ya kutoweka kwa mapenzi kati ya Pendo na Sulubu kwa kuulinganisha na vumbi. Tumearifiwa kuwa baada ya Sulubu kumvuruga Pendo, aliwasha gari na kutoka mbio huku akiwacha nyuma *vumbi* la rangi ya hudhurungi lililopaa kama wingu angani. Sitiari '*vumbi'* ni ya kiafya kwa sababu inawakilisha athari za kiafya zilizotokana na mateso na msongo wa mawazo ziliosababishwa na kuvunjika kwa mapenzi kati yake na Sulubu. Ingawa Pendo alimpenda Sulubu kwa dhati, ishara ya *vumbi* ilithibisha kuvunjika kwa ndoa na mwisho wa mapenzi kati yake na Sulubu. Pendo hakuwa na lingine la kufanya ila kukubali maisha mapya yaliyomngoja.

### 4.4.21 Kitanzi

Mhusika Matano amesawiriwa kama kurunzi ya kumwangazia na kumtahadharisha Sulubu dhidi ya kujiunga na tabia ya uzinzi, ambayo ingemtumbukiza katika janga la magonjwa na maafa.Tazama Kielelezo 32:

> Leo una Amina, kesho kwa Cheupe, keshokutwa kwa Rosa. Huoni unajitia *kitanzi*? Unajua Ukimwi unaua maelfu. Tazama humu nchini, kwa mfano, jinsi watu wanavyotoweka mithili ya nyota katika nuru ya jua (uk.30).

Matano ametumia *kitanzi* kama sitiari ya kiafya kuwakilisha kifo. Kama ilivyoangaziwa katika Kielelezo 32, Matano anamtahadharisha Sulubu kuwa, kuhusika kingono na wanawake wa mitaani ni kama kujiua kwani angepatwa na ugonjwa wa UKIMWI ambao haukuwa na dawa. Hii ni tahadhari kwa wanajamii kwamba, ugonjwa wa UKIMWI haukuwa na dawa na ni baadhi ya magonjwa yanayowauwa watu kwa kiwango cha juu.

### 4.4.22 Watu wanavyotoweka

Nadharia Changanuzi ya Sitiari ya Dhana inasisitiza kuwa, matumizi ya sitiari hurahisisha uelewa wa jambo linalozungumziwa kwa kuzua taswira zinazoleta ukaribu wa kihalisia na ukweli unaokubalika (Lackoff na Johnson, 1980). Kwa msingi huu sitiari ya kiafya '*watu wanavyotoweka'* imetumika kuangazia taswira ya jinsi watu walivyoaga dunia kutokana na UKIMWI. Neno '*kutoweka*' limetumika kisitiari kuwakilisha kifo. Jambo hili limejitokeza katika Kielelezo 33:

> Unajua Ukimwi unaua maelfu ulimwenguni lakini unafikiri wewe huwezi kuwa mmoja wa hao maelfu. Tazama humu nchini, kwa mfano jinsi *watu wanavyotoweka* mithili ya nyota katika nuru ya jua (uk.30).

Usemi katika Kielelezo 33, umeangazia namna mhusika Matano alivyomsihi Sulubu kuachana na ukahaba kwa kufananisha madhara na kusambaa kwa UKIMWI na mwangaza wa jua, uliopenya kila mahali ulimwenguni na kuvyonga nuru ya nyota ingawa ni nyingi angani. Katika msingi wa Nadharia Changanuzi ya Sitiari ya Dhana, matumizi ya sitiari '*kutoweka'* yamerahisisha kuelewa dhana ya kifo katika hali ya kihalisia. Mtu anapokufa hutoweka ulimwenguni na haonekani tena. Hii ilikuwa tahadhari kwa Sulubu kwamba kuendelea na tabia ya usinzi ni kujipatia tiketi ya *kutoweka* ulimwengni.

### 4.4.23 Safari

Aidha, kifo kimesawiriwa kama safari. Kifo cha Zuhura kimethibitisha haya na Sulubu anadadua kuwa Pendo vilevile alikuwa ameanza safari hiyo. Tazama Kielelezo 34:

> Zuhura alifariki baada ya kuzidiwa na maradhi. Sulubu hakunyanyua mguu kwenda kwa mkewe wala kutuma ujumbe wowote. Alijua mtoto huyo hangeishi na *mkewe alikuwa njiani kuelekea kuko alikoenda mwanawe* (uk.32).

Usemi '*mkewe alikuwa njiani kuelekea alikoenda mwanawe'* ni sitiari ya kiafya inayowakilisha safari ya kifo. Katika Kielelezo 34 kifo kimelinganishwa na njia au safari ambayo mtu huanza anapozaliwa. Safari hiyo inatamatishwa na kifo kupitia magonjwa, ajali au hatari nyingine.

### 4.4.24 Kupalilia Mimba

Katika matini teule mwandishi amelinganisha kulea mimba na kutunza mche. Mche hunyauka haraka na huhitaji kutunzwa kikamilifu kwa kunyunyizia maji, kupalilia na kupigia dawa za kuzuia wadudu na magonjwa mengine. Vilevile, mimba huhitaji kutunzwa vivyo hivyo ili kijusi kisiathirike. Tazama Kielelezo 35:

> Sulubu na Rehema *walipalilia mimba* hiyo hadi mtoto akazaliwa. Walipata mtoto wa kike ambaye Sulubu alimwita Chema, jina la marehemu mamake (uk.41).

Sitiari ya kiafya '*kupalilia mimba'* katika Kielelezo 35 imetumiwa kulinganisha mimba na mche. Hivi ni vitu viwili vyepesi ambavyo vingeweza kudhuriwa kwa haraka bila kuzingatia utunzi wa hali ya juu. Kwa jinsi hiyo, Sulubu na Rehema walichukua muda kutunza mimba hiyo ili kuepuka matatizo ya kiafya.

Usemi wote katika Kielelezo 35 ni sitiari ya kiafya ya maradhi ambayo imeangazia taswira ya vifo vingi vya watu vinavyotokana na UKIMWI. Matano alitumia visengere mbele kumtahadharisha Sulubu dhidi ya maovu yaliyomngoja endapo angevunja ndoa yake na Pendo na kumuoa Rehema. Alimfahamisha kuwa '*uzuri wa mkakasi ndani kipande cha mti' (*uk.31). Methali hiyo ni sitiari ya kiafya ya maradhi, iliyotumiwa na Matano kama kisengere mbele katika kumuonya Sulubu dhidi ya maambukizi ya magonjwa yaliyomngoja ikiwa asingejitenga na tabia ya ukahaba. Baada ya kuugua Rehema aliathiriwa na magonjwa mbalimbali kama vile kikohozi, upele na kushindwa kula chakula. Sitiari kadhaa za kiafya zimetumika kuangazia hali hiyo. Tazama Kielelezo 36:

> Mwili wake wote sasa ulijaa vipele vingi vilivyofifisha weupe wa ngozi yake. *Kifua* kilivuma na pumzi kumpaa kila alipojaribu kuongea (uk.44).

Katika Kielelezo 36 '*kifua'* ni sitiari tashihisi ya kiafya ya maradhi iliyorejelea UKIMWI. Kwa mujibu wa Wamitila (2008) sitiari ya kitashihisi hukipa kitu kisicho na uhai sifa za uhai. Kwa msingi huo, ugonjwa wa kifua umepewa sifa za uhai kama vile kuvuma na kusawiriwa kama kiumbe. Kule kukipa kifua sifa za uhai kunasisitiza hatari inayotokana na ugonjwa wa UKIMWI unaoweza kusambaa ikiwa mbinu mwafaka za kujikinga hazizingatiwa.

### 4.4.25 Kombora

Ujumbe kuhusu ugonjwa wa UKIMWI pia umelinganishwa na kombora, ambayo ni aina ya bomu au zana za kivita zenye nguvu nyingi na zinazolipuliwa kwa kutumia mizinga. Katika muktadha wa matumizi, kuambukizwa na UKIMWI kumelinganishwa na kupigwa na *kombora*. Baada ya Daktari Hamisi kuchunguza maradhi yaliyomuathiri Sulubu, alidida kumjulisha matokeo peke yake na akawaita madaktari wengine wamsaidie. Hii ni kwa sababu Daktari Hamisi alikuwa na ujumbe wa kuogofya. Hivyo,

katika hali ya kumtayarisha Sulubu kupokea matokeo, madaktari walimhusisha katika mazungumzo mafupi. Tazama Kielelezo 37:

> Kisha Daktari Hamisi aliangusha *kombora* lililosubiriwa. Matano kimako kilimtoka akaanza kutataa mle ndani, Sulubu alifufumaa kwa huzuni kubwa (uk.50).

Kupitia mazungumzo katika Kielelezo 37, tumearifiwa kuwa Daktari Hamisi aliangusha *kombora* lililosubiriwa. *Kombora* ni sitiari ya kiafya inayorejelea ugonjwa wa UKIMWI. Kule kulinganishwa na kombora kunaangazia masaibu yaliyotokana na UKIMWI kama vile kuambukizwa na magonjwa nyemelezi, kuhangaika na kifo.

### 4.4.26 Macho

Ingawa macho hutumika kuona, Sulubu aliyachukulia kama kifaa kilichokuwa na mwangaza ulioweza kupenya ndani. Katika muktadha wa mazungumzo, Sulubu amefananisha *macho* ya Daktari Hamisi na kurunzi inayokuwa na mwangaza unaopenya hadi kumlika ndani ya viungo vya mwili. Tazama Kielelezo 38:

> Alipokuwa akimweleza hayo, Daktari hamisi alimtazama kwa *macho* ambayo Sulubu alihisi yaliangaza hadi moyoni mwake, mpaka kwa damu yake na kuona umati wa virusi vya Ukimwi ukishambulia chembechembe za damu iliyositiri uhai wake (uk.50).

Sitiari ya kiafya *macho* imetumika katika Kielelezo 38 kuwakilisha ule ujuzi wa daktari wa kutambua magonjwa kupitia taaluma ya udaktari. Aidha, sitiari hiyo imeangazia utaalamu wa Daktari katika kufahamu na kutibu magonjwa.

### 4.4.27 Kondoo

Kondoo ni myama mpole, mtiifu na anayeishi kwa kudura za mchungaji. Hata hivyo, neno hilo limetumika kisitiari kumrejelea Sulubu baada ya kuugua UKIMWI. Tazama Kielelezo 39:

> Baada ya kusimulia kisa chake, Sulubu alitulia, mfano wa *kondoo* anayesubiriwa kuchinjwa (uk.50).

Sitiari ya *kondoo* imetumika katika Kielelezo 39 kama sitiari ya kiafya kwa sababu inamwangazia Sulubu aliyekuwa kaidi na jogoo wa mjini kama mgonjwa aliyekata tamaa na maisha kutokana na makali ya magonjwa.

### 4.4.28 Pendo

Pendo amesawiriwa kama *mkombozi* aliyejitokeza kumshawishi Sulubu asijitoe uhai. Ingawa *Pendo* ni mhusika mkuu katika kazi teule, ametumika kisitiari kama *mkombozi* katika maisha ya Sulubu. Kwa mujibu wa Kovecses (2000), sitiari kama dhana linganishi inaweza kuwa na maana mbalimbali kulingana na jinsi ilivyotumiwa katika kazi ya fasihi. Kwa msingi huu Pendo kama mhusika mkuu alijitokeza akiwa mfano wa mizimu wakati Sulubu alipokuwa akijitayarisha kujitia kitanzi na kumuonya dhidi ya kujiua. Tazama Kielelezo 40:

> Kisha alichukua kamba na kuitundika darini. Aliipiga fundo sehemu ya chini, akavuta meza iliyokuwa karibu ili aweze kujitundika kwenye kamba hiyo. Huku moyo ukimwenda mbio, alipanda juu ya meza akatia lile fundo shingoni. Alipokuwa akilikaza ili ajitupe hewani na kuning'inia, alisikia mtu akijikokota nyuma yake kama mkongwe, huku akihema kwa nguvu kama mwenye kifua kikuu. Alipotazama nyuma yake, hakuamini macho yake kwa yale aliyoona. Alimwona Pendo amesimama akimtazama kwa mshtuko, mkononi kashika gongo alilotumia kujikokota (uk.54).
>
> "Su…lubu….usi…fanye hivyo. Sh…shuka chini…. upigane…kiume. Usi…we mdhaifu ka…kama mimi …hapana (uk.54)
> Kwa…heri Sulubu…lakini sifanye …hivyo tena. Usi …sijiue, wacha Mungu …Aku… chukue mwenyewe." Aliposema haya alijikokota na kuondoka pale (uk.55).

Kupitia mazungumzo katika Kielelezo 40, *Pendo* ametumika kisitiari kama *mkombozi* katika kunusuru maisha ya Sulubu. Ni mkombozi aliyejitokeza kama mizimu jambo lililomshtua Sulubu na akaghairi nia ya kujiua. Tukio hili lilimshangaza Sulubu na akaliona kama ndoto ya ajabu na ya kutisha.

### 4.4.29 Vita

Kulingana na Lakoff na Johnson (1980), sitiari hutumika katika mawasiliano ili kuwezesha kueleweka kwa masuala changamano na mengine yaliyo mwiko katika jamii. Kwa jinsi hii, Sulubu anakataa kutaja janga la UKIMWI hadharani kwani ilikuwa

mwiko kulijadili katika jamii. Hivyo, alitumia sitiari ya kiafya *vita* kurejelea mashambulizi yaliyotekelezwa na virusi vya UKIMWI mwilini mwake.

Tazama Kielelezo 41:

> "Swali lako halihitaji jibu. Unafahamu vizuri kwamba kuna *vita* vinavyoendelea ndani ya damu yangu." *Vita*? Makelele aliuliza kwa mshangao. "Naamu *vita*. *Vita* ambavyo mshindi ndiye atakayeamua hatima yangu." "Mbona sikuelewi bwana? Makelele aliuliza kwa mshangao (uk.58).

. Mazungumzo yaliyomo katika Kielelezo 41 yameangazia taswira ya vitu au viumbe vilivyokuwa vikipigana. Sitiari ya kiafya ya *vita* katika Kielelezo 41 imetumika kuwakilisha maumivu yaliyotokana na kuadhiriwa na virusi vya UKIMWI.

Isitoshe, mtafiti ametambua aina mbalimbali za sitiari za kiafya ambazo mwandishi wa kitabu kiteule *Siku ya Ukimwi* ametumia kuangazia masuala ya kiafya. Baadhi ya sitiari hizi ni:

### 4.4.30 Kiuno cha Nyigu

Mdee na wengine (2022) wanasema kuwa nyigu ni aina ya mdudu mwenye mwili mkubwa lakini kiuno chake ni chembamba. Umbo hili huonekana nzuri na hupendeza. Mwandishi ametumia *kiuno cha nyigu* kama sitiari ya kiafya kurejelea umbo nzuri na la kupendeza la Mhusika Kadogo. Kwa jicho la nje Kadogo alionekana msichana mrembo na mwenye afya nzuri. Tazama Kielelezo 42:

> Kadogo alikuwa msichana mrembo kweli. Alikuwa na *kiuno cha nyigu*. Mwili wake kwa ujumla uliandika *nambari 8*. Alikuwa nadhifu. *Mtoto wa watu*. Alikuwa ameumbwa akaumbika. Hungeamini alikuwa na Virusi vinavyosababisha ugonjwa wa Ukimwi (uk. 6).

Maelezo katika Kielelezo 42 ni ushahidi fika kuwa umbo nzuri na urembo sio dhibitisha ya kuwa na afya njema. Ingawa Kadogo alionekana mrembo na mwenye afya kwa jicho la nje, alikuwa na virusi vya UKIMWI. Hadhira haikuamini hadi alipowaambia yeye mwenyewe. Hii ilikuwa tahadhari kuwa, sura nzuri na afya ya mwili havikuwa dhibitisho kuwa mtu hakuwa na virusi vya UKIMWI na ilikuwa muhimu kutembelea vituo vya afya ili kupimwa na daktari.

### 4.4.31 Nambari 8

Hii ni sitiari ya kiafya ambayo imetumika katika kitabu kiteule kuwakilisha urembo. Kulingana na mwandishi wa kitabu hicho, mwanamke aliye na umbo la wastani na kiuno chembamba huchukuliwa kuwa mrembo. Urembo huo unatokana na kuwa safi kimwili, kuvalia mavazi mazuri na matumizi ya vipodozi. Hivyo, mwandishi ametumia nambari nane kisitiari kurejelea urembo. Mwandishi anasema: tazama Kielelezo 43:

> Mwili wake kwa ujumla uliandika *nambari 8*. Alikuwa nadhifu. Mtoto wa watu alikuwa ameumbwa akaumbika (uk.6).

Katika usemi huu mwandishi ametumia sitiari ya kiafya ya *nambari 8* kurejelea umbo nzuri la Kadogo. Hata hivyo, Kadogo hakujivunia urembo wake kwani ulikuwa na dosari. Alikuwa mgonjwa wa UKIMWI ndiposa alitahadharisha hadhira kuwa, umbo nzuri na mwili safi havikuwa dhibitisho ya kutokuwa na UKIMWI. Hivyo, anahimiza watu wawe wakitembelea vituo vya afya kila mara ili wafanyiwe uchunguzi na madaktari.

### 4.4.32 Mtoto wa Watu

Mwandishi ametumia sitiari ya kiafya '*mtoto wa watu'* katika dondoo la hapo awali kurejelea mwanamke aliyetamaniwa na wanaume kimapenzi. Kadhalika, tamaa ya wanaume kwa wanawake imesababisha mapenzi ya kiholela na kusambazwa kwa magonjwa ya zinaa kama vile UKIMWI, kaswende na kisalisali katika jamii. Magonjwa hayo yameathiri pia vijana na kuhatarisha maisha ya vizazi vya baadaye. Kwa jinsi hiyo, Kadogo anawashauri wanajamii kuepukana na raha ambayo ingewaletea karaha. Tazama Kielelezo 44:

> "Kwa kuwatahadharisha zaidi naomba kuwaeleza kwamba, mimi ni mfano wa jinsi Ukimwi unavyoweza kuathiri vijana. Nilipata Ukimwi kwa sababu ya raha. Mtahadhari sana dhidi ya marafiki zenu. Mjiepushe na raha. Raha ya siku moja huweza kuleta karaha. Vijana msilewe hadi kujisahau. Ninawaonya vijana wenzangu msijiingize katika mapenzi ya kiholelaholela. Mapenzi ya Atieno leo, Wambui kesho, Kwamboka keshokutua hayafai Hata kidogo. Jiepusheni."(uk. 14).

Mazungumzo ya Kadogo katika Kielelezo 44 yameangazia athari za kuwa *mtoto wa watu*. Mienendo kama vile unywaji wa pombe, kujiunga na marafiki waliokuwa na

hulka mbaya na mapenzi ya kiholela yangesababisha majuto baadaye. Pia, tabia hiyo husababisha magonjwa kama vile UKIMWI. Hivyo, ni jambo muhimu kwa watu kuepukana na tabia mbaya ili waishi maisha bora na kupunguza kusambaa kwa magonjwa ya zinaa na kuvunjika kwa ndoa katika jamii.

#### 4.4.33 Mtego wa Panya

Panya ni mnyama mharibifu anayekaa nyumbani. Ili kuzuia uharibifu huo mtego hutumiwa kunasa na kuua panya. Mtego wa panya umetumiwa kisitiari katika matini teule kuwakilisha hofu. Hofu hiyo imetokana na athari zilizotokana na ugonjwa wa UKIMWI. Tathmini ya maelezo haya ni kuwa, ni vigumu kutambua waathiriwa wa UKIMWI kwani athari zake hazithihiriki hadharani. Tazama Kielelezo 45:

> Hata huyu mrembo hivi, kweli anaugua Ukimwi? Sauti yake nyororo kama ya chiriku ilikuwa ya kuvutia. Kadogo aliposimama kuhutubu watu walinyamaza jii. Wakatega masikio *mfano wa mtego* wa panya ili kuyanasa yote yatakayonenwa (uk.6).

Kutokana na mazungumzo katika Kielelezo 45, wasikilizaji walikuwa na hofu kuhusu ugonjwa wa UKIMWI ambao haukuonyesha dalili zozote kwa Kadogo. Ingawa mhusika Kadogo aliambukizwa ugonjwa huo hakuonyesha dalili zozote za maumivu. Hivyo, kila aliyehudhuria hafla hiyo alitega masikio ili anase kila lililozungumziwa. Wazo muhimu linalopashwa na mazungumzo katika Kielelezo 45 ni kwamba, UKIMWI ni ugonjwa hatari na ambao athari zake hazitabiriki. Kila mtu anahitaji kujihathari na maambukizi yake.

#### 4.4.34 Koo lake lilikuwa limekauka

Sitiari hii imetumika kulinganisha koo na jani lililokauka. Jani ambalo limekauka ni kavu na halina uhai. Majani yakikauka yakiwa mtini huanguka na hutumiwa kama kuni au huozea mahali ambapo limeanguka. Mwandishi ametumia sitiari hiyo kuangazia ukavu unaotokana na UKIMWI kama vile kupungukiwa na damu na maji mwilini.tazama Kielelezo 46:

> Baada ya kutoa kauli hii, Kadogo akanyamaza. Akaashiria mmoja wa Watu waliokuwa kwenye jukwaa amsaidie kwa maji. *Koo lake lilikuwa limekauka*. Watu walikuwa na wasiwasi. Hawakujua ni nini kilichokuwa kikiendelea. Akaletewa maji. Akapiga funda la kwanza, la pili, la tatu. Akashusha pumzi (uk.7).

Tathmini ya maelezo ya mwandishi katika Kielelezo 46 ni kuwa, *sitiari koo lake lilikuwa limekauka* imetumika kuonyesha baadhi ya athari za UKIMWI. Pia, mwathiriwa anapaswa kuelewa hali yake ya kiafya ili ajitunze ipasavyo. Isitoshe, watu wanashauriwa ya kwamba unywaji wa maji kwa wingi ni muhimu kwa mgonjwa wa UKIMWI. Imefahamika kuwa mwili wa binadamu unahitaji maji kwa wingi ili uweze kufanya kazi. Hii ni kwa sababu damu na maji hupungua mwilini kutokana na vita baina ya virusi vya UKIMWI na chembechembe nyeupe za damu mwilini na kuathiri afya ya mtu. Athari hizo ndizo zilisababisha koo la Kadogo kukauka na kuhitaji maji ya kunywa. Katika ukurasa wa kumi na nne, Kadogo amethibitisha hayo mwenyewe kwa kuwashauri wagonjwa wa UKIMWI kuzingatia maadili mema kama vile kufanya mazoezi, kunyua maji safi na kula vyakula vinavyojenga mwili na kuzuia maradhi.

### 4.4.35 Bendera

Mhusika Kadogo alitumia sitiari ya kiafya ‘*bendera’* kuelezea tabia yake. Ameilinganisha na bendera ambayo haina msimamo na inayofuata upepo. Katika muktadha wa matumizi, bendera imetumiwa kama sitiari ya kiafya kurejelea tabia ya Kadogo ya ukahaba. Tabia hiyo ilimtumbukiza katika maambukizi ya maradhi ya UKIMWI. Kadogo ametumia sitiari ‘*bendera’* kuonyesha kiwango chake cha upotovu na tabia ya kukimbizana na wanaume wa kila aina bila kujali maambukizi ya magonjwa ya zinaa. Jinsi bendera inavyofuata upepo ndivyo Kadogo alivyowababamba wanaume mbalimbali bila kujali hali yao ya kiafya. Tazama Kielelezo 47:

> “Baada ya kunywa pombe iliyokuwa kali sana, nililewa chakari. Tulipiga maji hadi usiku wa manane. Mimi nilikuwa *bendera* ya kufuata upepo. Nilipolewa nililala fofofo. Nikajisahau. Sikujua nilikuwa wapi.”(uk.13).

Kinachoangaziwa katika Kielelezo 47 ni kuwa matumizi ya pombe na dawa za kulevya huathiri tabia na kusababisha maovu kama vile ubakaji, uzinzi na utukutu. Pia mazungumzo hayo yanabainisha jinsi wanarika wanavyokuwa na ushawishi mkubwa kwa wenzao. Hii imedhibitishwa na marafiki wa Kadogo waliomshawishi kunywa pombe na mwishowe kuangukia katika mikono ya wabakaji waliomwambukiza UKIMWI. Hii pia ni tahadhari kwa vijana dhidi ya kujiunga na watu walio na mienendo miovu na matumizi ya pombe kwani ni rahisi kuwaiga.

### 4.4.36 Nyuso zao zilitulia

Mhusika Kadogo aliposimama kuhutubia watu kuhusu janga la UKIMWI, watu hawakuamini kuwa aliugua ugonjwa huo kwa jinsi alivyoonekana buheri wa afya na mrembo kweli. Mwandishi wa *Siku ya Ukimwi* ametumia sitiari *nyuso zao zilitulia* kurejelea utulivu wa mawazo ambao ni muhimu katika kuimarisha afya ya binadamu. Tazama Kielelezo 49:

> Kadogo aliposimama kuhutubu, watu walinyamaza ji. Wakatega masikio mfano wa mtego wa panya ili kuyanasa yote yatakayonenwa. Watu walishangaa na wengine wakaduwaa, lakini hawakuonyesha uoga wowote. *Nyuso zao zilitulia* na kuonyesha imani na matumaini ya maisha, kwao na kwa mwenzao Kadogo (uk.6-7).

Utulivu wa watu ulioangaziwa katika Kielelezo 49 ni ishara kuwa watu walikuwa na hamu ya kufahamu ukweli kuhusu janga la UKIMWI. Hivyo, ni muhimu kuendeleza mafunzo kwa watu wote kuhusu janga hili hasa visababishi vyake ili waweze kujilinda. Aidha, ni muhimu kwa serikali na mashirika ya kijamii kuendeleza mafunzo hayo katika tahasisi za elimu na katika warsha mbalimbali.

### 4.4.37 Mbwa

Mbwa ni mnyama mkali anayetumiwa na binadamu kulinda na huwa na tabia ya kurandaranda. Mnyama huyu hatosheki hata akilishwa. Pia ni mchafu na mwenye tamaa. Anakula mizoga, vyakula vilivyooza na kulala mahali popote. Mhusika mkuu Kadogo ametumia sitiari ya *mbwa* kurejelea wanaume waliokuwa na tabia ya uzinzi. Wanaume wa aina hii huwa na tabia ya kurandaranda kila mahali wakitafuta wanawake. Ingawa magonjwa ya zinaa yameathiri watu wengi, wanaume walio na tabia ya kurandaranda hawabagui wala kujihathari na maambukizi ya magonjwa. Kama vile mbwa hula mizoga na vitu vilivyooza, wanume wa aina hiyo hufanya ngono na kila mwanamke aliyeangukia mikononi mwao. Tazama Kielelezo 50:

> "Nitawatolea hadithi. Hadithi hii itatufundisha mengi na kutufaa zote. Kulikuwa na mtu aliyekuwa *mkulima*. Alikuwa na *shamba* lake la *mahindi*. Jirani yake alikuwa na *mbwa*. Hakuwafunga *umbwa* wake. *Mbwa* hawa Walikuwa wakiharibu *mahindi* ya yule *mkulima* (uk.8).

Kielelezo 50 kinaangazia mifano ya wanaume ambao wanafanya ngono na wake za majirani bila kujali imeangaziwa.Wanaume hawa wamesawiriwa kama mbwa kutokana

na tabia ya ukahaba. Kielelezo hiki pia kimesheheni sitiari kadhaa za kiafya kama vile *shamba* na *mahindi* ambazo pia zimejadiliwa. Tazama maelezo katika 4.4.39 na 4.4.40.

### 4.4.38 Shamba

Kwa mujibu wa TUKI (2004), shamba ni sehemu kubwa ya ardhi iliyolimwa kwa minajili ya kukuza mimea. Baada ya kulima, mkulima hupanda mimea kama vile mahindi, konde, ndizi miongoni mwa mingine. *Shamba* limetumiwa kama sitiari ya kiafya katika Kielelzo 50 kilichoangaziwa hapo awali kurejelea mwanamke. Kama shamba, mwanamke ana kipawa cha kuzaa na kuendeleza jamii. Hivyo, kule kulima shamba kunarejelea tendo la kufanya ngono na wanawake. Kulingana na Kadogo, Magonjwa ya UKIMWI na zinaa husambazwa kupitia mapenzi ya kiholela, jambo linalopaswa kuepukwa na jinsia zote. Hivyo, inapaswa kila mmoja afunge *umbwa* wake na kuacha kuharibu *mashamba* ya majirani. Kutokana na sitiari hiyo, imebainika kuwa mwanamke ndiye mpokezi wa tendo la ngono na mwanaume ndiye mtendaji.

### 4.4.39 Mahindi

Kwa mujibu wa TUKI (2004), mahindi ni mimea inayopandwa kama chakula cha wanyama au watu. Mimea hii inapokua pia huzaa mbegu za mahindi ambazo husagwa na kuliwa kama chakula. Tazama Kielelezo 50 cha hapo awali. Katika muktadha wa matumizi katika kitabu kiteule, *mahindi* yametumiwa kurejelea tendo la ngono. Kule kula *mahindi* kulikoangaziwa na mhusika Kadogo ni kujamiana. Kwa mujibu wa Kadogo tendo hilo lilichangia kueneza maradhi ya zinaa.

### 4.4.40 Mahindi Mabichi

Sitiari hii imetumika kurejelea kujamiana bila kuzingatia njia za kuzuia ugonjwa wa UKIMWI. Imebainika kuwa ukahaba umekithiri katika jamii hivi kwamba, wanaume wanafanya mapenzi kiholela bila kutumia kinga. Jambo hilo limesababisha vifo vya watu na kuongezeka kwa maradhi ya UKIMWI. Tazama Kielelezo 51:

> Walivamia *shamba* na kula *Mahindi mabichi*. Mkulima hakufurahia kuona *shamba* lake la *mahindi* ikiharibiwa na *mbwa*." (uk. 8).

Katika kielelezo 51 mwanaume amesawiriwa kama mnyama mweye pupa na aliyekula chochote anachokipata bila kujali afya yake. Aidha mwanaume analinganishwa na

mbwa. Tathmini ya usemi huu ni kuwa jamii haikufurahia mapenzi ya kiholela. Hivyo, kuna haja ya kutumia njia za kuzuia maambukizi ya magonjwa ya zinaa.

### 4.4.41 Sumu

Sumu ni kemikali au kitu kilichokuwa na uwezo wa kuua. Mifano ya sumu ni kama vile dawa za kuua wadudu. Sitiari ya kiafya ya *sumu* imetumiwa katika matini teule kurejelea ugonjwa wa UKIMWI. Kadogo ametumia sitiari ya *sumu* kusawiri matokeo ya kuendelea kufanya ngono kiholela. Tazama Kielelezo 52:

> Mkulima hakufurahia kuona shamba lake la mahindi likiharibiwa na mbwa. Siku moja alitia *sumu* kwenye mahindi. Kila mbwa aliyekula mahindi yaliyotiwa *sumu* alifariki. Kila mbwa alikufa kifo kichungu. Baadhi ya majirani waliogundua mahindi yametiwa *sumu* waliwafunga mbwa zao. Hivi leo duniani kote, mahindi yametiwa *sumu*. Kila mtu afunge mbwa wake (uk.8).

Kulingana na mjadala ulioendelezwa katika Kielelezo 52, UKIMWI umeenea kote ulimwenguni na kuwa janga la kimataifa. Mazungumzo haya pia yameangazia athari za ugonjwa wa UKIMWI ambao umerejelewa kama *sumu*. Umesawiriwa kama janga la kimataifa ambao umeangamiza watu wengi. Kila aliyejiungiza na ukahaba na kuambukizwa ugonjwa huo alikufa kifo kichungu. Hali hiyo ilisababisha hofu na kila mtu alianza kujitunza.

### 4.4.42 Viziwi

Mwandishi wa matini teule ametumia sitiari '*kiziwi'* kuwakilisha upotovu wa nidhamu. Sitiari hii ni ya kiafya kwa sababu upotovu wa nidhamu ulisababisha unywaji wa pombe na ngono za kiholela zilizokuwa na kiwango cha juu cha usambazaji wa magonjwa ya zinaa. Tazama Kielelezo 53:

> "Sasa hakuna asiyejua kuna Ukimwi. Watu wameamua kujifanya *viziwi* hata wakiambiwa vipi na nani hawasikii wala kujali. Wengine husema, 'Hata kama kuna Ukimwi, huyu siachi! Tabia ya kutojali italeta ajali Na sharti kila mmoja wetu aitupilie mbali." (uk.11).

Mazungumzo katika Kielelezo 53 yameangazia uovu uliokithiri katika jamii. Watu wameamua kutojali maisha yao ya baadaye na kujiingiza katika mapenzi ya kiholela.

Hii ni tahadhari kuwa, ingawa mashirika ya kiafya kama vile Shirika la Afya Ulimwenguni yamejitolea kuhamasisha watu kuhusu ya magonjwa mbambali, bado kuna kundi katili lisilokuwa tayari kushauriwa.

#### 4.4.43 Magonjwa nyemelezi

Hii ni sitiari ya kiafya inayorejelea magonjwa mbalimbali yanayohusishwa na UKIMWI. Kulingana na Gathigia (2014), sitiari nyingi hutumika katika mawasiliano ya kila siku na sitiari moja inaweza kuwa na maana kadhaa kulingana na mazingira ya matumizi yake. Katika muktadha wa matumizi sitiari ya *magonjwa nyemelezi* imetumika kuwakilisha magonjwa ambayo huathiri mgonjwa wa UKIMWI. Ingawa ugonjwa hauna uhai, mwandishi ameyapa *magonjwa nyemelezi* sifa ya uhai na kuyalinganisha na jinsi msasi aliyejihami na silaha anavyomsaka mnyama mawindoni. Kisitiari, magonjwa nyemelezi yamelinganishwa na msasi kwa sababu yalikuwa na bakteria au virusi vinavyosababisha maradhi. Virusi hivyo vinashambulia chembechembe nyeupe za damu zinazopigana na vijidudu vinavyosababisha maradhi. Vivyo hivyo, ndivyo mgonjwa wa UKIMWI huchambuliwa na *magonjwa nyemelezi*. Kwa kuwa UKIMWI hauna tiba, athari za *magonjwa nyemelezi* ni hatari na mara nyingine husababisha vifo. Kadogo ameangazia athari za *magonjwa nyemelezi* kwa kusema: Tazama Kielelezo 54:

> “Kwa wale walio na UKIMWI, kama mimi msife moyo. Nendeni Hospitalini mpate matibabu ya *magonjwa nyemelezi*. Hospitalini mtapata dawa za kupunguza makali. Tafadhali msiwaambukize watu wengine (uk. 16).

Mazungumzo katika Kielelezo 54 yanaonyesha jinsi Kadogo alivyowarai watu walioambukizwa na ugonjwa wa UKIMWI kutembelea vituo vya afya kuhudumiwa ili wasiathiriwe zaidi na maumivu. Ingawa anawatahadharisha kuwa UKIMWI hauna tiba, anawajulisha kwamba kulikuwa na dawa za kupunguza makali ya magonjwa.

#### 4.4.44 Zimwi

Zimwi ni kiumbe hatari kinachodhaniwa kuishi na kinachofanana na binadamu. Inakisiwa kuwa kiumbe hiki kina uwezo wa kujibadilibadili na hudhuru watu. *Zimwi* limetumika kisitiari ili kunasa makini ya hadhira na kupasha ujumbe kuhusu hatari

inayotokana na kuambukizwa na UKIMWI. Kwa mujibu wa Nadharia Changanuzi ya Sitiari ya Dhana, mawasiliano ya kisitiari yana nguvu ya kunasa makini ya hadhira na kuathiri msimamo wao kuhusu suala fulani. Mhusika Kadogo analinganisha UKIMWI na *Zimwi*. Tazama Kielelezo 55:

> "Tukumbuke jitihada za kupambana na *Zimwi* la Ukimwi ni jukumu langu Na lako. Asanteni." (uk. 17).

Usemi katika Kielelezo 55 umeangazia UKIMWI kama kiumbe hatari kwa maisha ya binadamu. Jinsi *Zimwi* linavyokuwa na uwezo wa kujibadilibadili, ndivyo virusi vya UKIMWI vilivyo na uwezo wa kubadilikabadilika kwa kujitokeza kama aina mbalimbali za magonjwa nyemelezi. Hali hii imeangazia taswira ya ugonjwa hatari ulio na uwezo wa kujitokeza kupitia nyuso mbalimbali. Nyuso hizi ndizo zimerejelewa kama magonjwa nyemelezi katika utafiti huu. Aidha, Kadogo ametoa onyo kuwa ingawa *Zimwi* hilo ni hatari, linahitaji kukabiliwa na mwathiriwa mwenyewe na wala si juhudi za mtu mwingine. Katika ukurasa wa kumi na nne, Kadogo amearifu kuwa, baadhi ya mbinu za kukabiliana na *Zimwi* la UKIMWI ni kuzingatia maadili mema, kula vyakula vinavyojenga mwili na kunywa maji maenge.

Kadhalika, mtafiti amechunguza na kubainisha aina zifuatazo za sitiari za kiafya za kikaida, zilizotumiwa kuangazia masuala ya kiafya katika matini teule ya *Kosa la Marehemu.*

### 4.4.45 Akili ikimduru

Sitiari hii ni ya kiafya na imetokana na neno 'duru' linalomaaninisha kuzunguka duara. Limetumiwa kuangazia msonge wa mawazo ambayo Mshindo alipata baada ya kupokea habari kuhusu ugonjwa aliougua nduguye. Tazama Kielelezo 56:

> "Ati wanasema anaugua Ukimwi." Mshindo hakuamini masikio yake. Alitazama juu angani huku *akili ikimduru*. Ilikuwa ni jioni na jua lilikuwa likielekea magharibi kulala. Ndege walikuwa wakipita angani kuelekea viotani huku wakiimba nyimbo zao (uk.4).

Kama ilivyoelezwa na mwandishi katika Kielelezo 56, Mshindo hakuridhika na habari za kuugua kwa nduguye. Alitatizika kimawazo na kuchukua muda kuamini habari hizo.

Ingawa Mshindo alimpenda nduguye kwa dhati, ilikuwa hatari kwake kuathirika kimawazo kwa sababu matatizo ya mawazo husababisha magonjwa ya kiakili. Njanga alimtahadharisha dhidi ya kuwa na fikra nyingi ili kuepukana na shinda kama hizo.

#### 4.4.46 Tendo la Ndoa

Kwa mujibu wa TUKI (2004) Ndoa ni makubaliano halali kati ya mwanamke na mwanaume ya kuishi pamoja kama mume na mke. Ni halali kwa bibi na bwana kushiriki ngono. Pia, ni muhimu kwa hao kuwa waaminifu katika ndoa ili kuepukana na magonjwa ya zinaa. Vijana vilevile hutahadharishwa dhidi ya kujihusisha katika mapenzi kabla ya ndoa. *Tendo la ndoa* limetumiwa katika kitabu kiteule kama sitiari ya kiafya kurejelea kujamiana. Mtaalamu kutoka Wizara ya Afya aliwahutubia vijana kwa kutumia lugha ya kisitiari kurejelea masuala ya kimapenzi, ili kuwajumuisha katika kujadili masuala ambayo hayakujadiliwa hadharani kwa sababu ya mila na itikadi za kijamii zilizoharamisha mijadala ya aina hiyo. Kwa mujibu wa Kobia (2008) matumizi bora ya sitiari hurahisisha uwasilishaji wa ujumbe unaokisiwa kuwa mwiko kwa njia mbadala na inayokubalika katika jamii. Kwa jinsi hii Mtaalamu wa Wizara alifaulu kujadili masuala muhimu kuhusu ugonjwa wa UKIMWI, ambao kila mtu aliogopa kuhusishwa nao katika jamii. Mshindo na wanafunzi wenzake walijumuishwa katika kuuliza maswali bila kuogopa. Mtaalamu anasema: Tazama Kielelezo 57:

> Kufanya tendo la ngono ni kule mwanamke na mwanaume wanapokutana kimwili na kufanya *tendo la ndoa*. Katika tendo hilo ikiwa mmoja wao ana Virusi vya Ukimwi, basi atamwambukiza mwenzake. Vilevile mwanamume mwenye Ukimwi akikutana na mwanamume mwingine kwa njia ya kulawiti, atamwambukiza mwenzake (uk.15).

Mtaalamu wa Wizara ametumia sitiari kadhaa kuelezea *tendo la ndoa* ili wanafunzi waelewe. Baadhi ya sitiari alizotumia kama ilivyoangaziwa katika Kielelezo 57 ni '*kukutana'* na '*ngono'*. Hii ni kwa sababu baadhi ya wanafunzi walikuwa wachanga na walihitaji kuelewa ujumbe aliokuwa akipitisha kwa urahisi. Hivyo, mtaalamu huyo alitumia visawe kadhaa vya *tendo la ndoa*. Hii ina maana kuwa sitiari moja ya kiafya inaweza kuwa na visawe mbalimbali jambo linalokuza lugha ya Kiswahili. Kiswahili ni lugha inayokua na kuna haja ya kubuni misamiati mbalimbali kulingana na maendeleo na mabadiliko ya kiteknolojia na kijamii.

### 4.4.47 Jipu

Jipu ni uvimbe wenye maumivu makali na ndani mwake huwa na uzaha. Uvimbe huu hutibiwa kwa kupasuliwa. Mwandishi wa kitabu kiteule ametumia *jipu* kama sitiari ya kiafya kurejelea maumivu yanayotokana na maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI. Ingawa Daudi aliambukizwa UKIMWI kwa muda mrefu, wazazi wake hawakujulisha mtu yeyote. Pia, hawakumuarifu Mshindo habari za ugonjwa wa UKIMWI uliomwathiri nduguye kwa sababu zilikuwa chungu na za kukera. Hivyo, Mshindo alichunguza na akafahamu maradhi yaliyompata nduguye na akaamua kupasua mbarika. Tazama Kielelezo 58:

> "Mshindo mwanangu, umekuwa mjeuri siku hizi? Kwa nini hutaki Kunijibu?" Baba yake aliuliza kwa sauti ya juu baada ya kuona mwanawe hamjibu. Mshindo aliamua kupasua *jipu*. "Nimesikia jambo." "Jambo gani?" "Ati kaka Daudi huko mjini ni mgonjwa. Anaugua Ukimwi," alisema kwa Kusitasita huku machozi yakimlengalenga. Baba Mshindo alipigwa na butwaa (uk. 6).

Katika Kielelezo 58, uchungu wa habari hizo umelinganishwa na uchungu unaotokana na kupasuliwa kwa jipu. UKIMWI hauna dawa na waathiriwa huwa na uchungu mwingi wanapogundua kuwa maisha yao yamo hatarini. Uchungu huu hutokana na maumivu ya kimwili na kimawazo, matumizi mengi ya rasilimali na kutengwa na jamii.

### 4.4.48 Mifupa iliyolala

Mifupa hushikilia mwili wa binadamu au mnyama na baada ya kufa nyama za mwili huoza na mifupa hubaki. Katika muktadha wa matumizi, mwandishi ametumia msemo '*mifupa iliyolala'* kama sitiari ya kiafya kulinganisha mgonjwa aliyekuwa hospitalini na mfu. Tazama Kielelezo 59:

> Waliendelea mbele na kupita vitanda kadhaa vya wagonjwa waliolala. Kitanda cha mwisho kabisa karibu na mlango wa kutokea wakasimama. Hapo palikuwa na mgonjwa aliyekonda sana. Alikuwa kama *mifupa iliyolala*. (uk.28).

Msemo *Mifupa iliyolala* ulioangaziwa katika Kielelezo 59 ni sitiari ya kiafya iliyotumika kuwakilisha mtu aliyekufa. Ingawa mgonjwa huyo alikuwa hai, hakuwa na matumaini ya kuishi. Alikonda kiasi kwamba hangetambuliwa kuwa ni binadamu. Alikuwa kama maiti iliyongoja wakati wake.

### 4.4.49 Walinzi

Mlinzi ni mtu aliyetwikwa jukumu la kulinda mahali fulani, watu au mali kwa kutumia silaha au zana fulani za vita. Katika hafla ya kulinda, kuna uwezekano wa mlinzi kuumizana au kuumizwa kulingana na nguvu za adui. Katika matini teule, mtaalamu wa Wizara ametumia *walinzi* kama sitiari ya kiafya kurejelea chembechembe nyeupe za damu mwilini. Amelinganisha chembechembe nyeupe za damu na askari au mlinzi anayepigana ili kulinda mali au vitu fulani. Jinsi mlinzi anavyopigana kwa minajili ya kulinda, ndivyo chembechembe nyeupe za damu mwilini zinavyopigana na vijidudu vinavyoathiri afya ya binadamu. Katika vita hivyo, vijidudu huuwawa au kuua chembechembe za damu. Chembechembe nyeupe za damu zinapokufa afya ya mtu huzorota na kusababisha magonjwa. Mtaalamu wa Wizara ameangazia suala hili kwa kusema: Tazama Kielelezo 60:

> Sasa tuangalie mgonjwa wa Ukimwi anakuwa na dalili gani. Baada ya virusi vya Ukimwi kuangamiza *walinzi* mwilini, yaani chembechembe nyeupe za damu, uwezo wa mwili wa kupambana na magonjwa unapungua (uk.16).

Jambo muhimu ambalo limedhihirishwa katika Kielelezo 60 ni kuwa, chembechembe nyeupe za damu hutekeleza wajibu muhimu wa kulinda mwili dhidi ya maambukizi. Hata hivyo, virusi vya UKIMWI vina uwezo wa kuangamiza *walinzi* wa mwili na kuhatarisha afya ya binadamu na kufungua milango ya maambukizi ya magonjwa nyemelezi mwilini.

### 4.4.50 Kuushambulia Mwili

Kushambulia ni kutumia silaha kupigana katika vita au kuvamia kwa nguvu. Mwandishi ametumia neno *kushambulia* kama sitiari ya kiafya kulinganisha magonjwa na adui katika vita. Katika vita adui hutumia silaha anazodhania kuwa na nguvu ya kupigana. Vivyo hivyo, ndivyo vijidudu vinavyosababisha magonjwa hupigana na chembechembe nyeupe za damu mwilini. Ikiwa vijidudu vitashinda vita mtu huambukizwa ugonjwa. Tazama Kielelezo 61:

> Baada ya virusi vya Ukimwi kuangamiza walinzi mwilini, yaani chembechembe nyeupe za damu, uwezo wa mwili wa kupambana na magonjwa huanza kupungua. Ina maana kwamba, magonjwa mengi yanaweza *kuushambulia* mwili na mwili kutoweza kujilinda (uk.16).

Taswira ya vita kati ya vijidudu vinavyosababisha magonjwa na chembechembe nyeupe za damu mwilini imeangaziwa katika kielelezo 61. Magonjwa yamepewa sifa ya uhai na uwezo wa kushambulia. Hivyo, *kuushambulia* ni sitiari ya kiafya inayoangazia athari inayotokana na vita kati ya vijidudu na chembechembe nyeupe za damu. Vita hivyo huathiri afya ya binadamu kupitia maumivu au majeruhi. Ikiwa chembechembe za damu mwilini zitalemewa na vita, mwili utaambukizwa magonjwa.

Mwandishi wa *Kosa la Marehemu* pia ametumia sitiari ya kiafya kulinganisha afya ya Daudi wakati alipokuwa na siha nzuri na wakati alipogonjeka. Tazama Kielelezo 62:

> "Sawa lakini akija amekonda sana na vidonda na mapele nitahisi uchungu sana. Kwani kaka yangu alikuwa *mnene na mweye ngozi nyororo*. Muda wote alikuwa ni mwenye afya na mchangamfu," alisikitika Mshindo (uk.20).

Mshindo ametumia sitiari ya kiafya '*mnene na mwenye ngozi nyororo'* kuelezea afya nzuri ya nduguye kabla ya kuelekea mjini. Kabla Daudi aende mjini alikuwa na siha nzuri. Ingawa Mshindo hakumwona kwa muda mrefu, anakisia kuwa huenda alikuwa amekonda na mgonjwa kutokana na UKIMWI. Mawazo hayo yanatuchorea picha ya sura mbili za Daudi: mtu mnene na mwenye ngozi nyororo na mtu mgonjwa na aliyekonda.

#### 4.4.51 Macho yaliyokuwa Makavu

Sitiari hii pia ni ya kiafya na imetokana na neno ukavu. Kisawe cha ukavu ni ukame ambao hutokea wakati ambapo mvua umekosekana. Wakati wa ukame mimea hukauka na wanyama hufa kwa sababu ya ukosefu wa maji na chakula. Mwandishi wa kitabu kiteule ametumia '*macho yaliyokuwa makavu'* kama sitiari ya kiafya kurejelea hali mahututi ya mgonjwa aliyelazwa hospitalini. Hali yake ya kiafya imelinganishwa na ukavu wa arthi ambapo mimea hukauka na wanyama kuaga dunia. Tazama Kielelezo 63:

> Yule mgonjwa aliwaangalia bila kupepesa macho. Jinsi alivyokonda na *macho yake yaliyokuwa makavu* alionekana kama mfu. Njanga aliogopa sana na kuanza kutetemeka. Lakini Mshindo baada ya kuona mgonjwa katulia bila kusema lolote, akajua kwamba alikuwa amezidiwa sana (uk.28).

Kielelezo 63 kinaangazia taswira ya kifo. Mgonjwa huyo amesawiriwa kama mtu aliyekata tamaa ya kuishi na aliyechungulia kaburi. Ingawa ako hai amelinganishwa na mfu. Vilevile, dondoo hili linadhibitisha madai ya WHO (2018) kuwa, UKIMWI umesababisha maumivu na vifo vya watu wengi ulimwenguni na mikakati kabambe ya kuuzuia inapaswa kutekelezwa. Baadhi ya mikakati hii ni kuhamasisha jamii kuhusu changamoto za kiafya na jinsi ya kukabiliana nazo.

### 4.4.52 Kiu

Mwandishi wa matini teule ametumia '*kiu'* kama sitiari ya kiafya kuwakilishaa shauku ya elimu kuhusu UKIMWI. Amelinganisha shauku ya elimu kuhusu UKIMWI na *Kiu* cha maji. Jinsi binadamu au mnyama anavyokuwa na kiu cha maji, ndivyo wanafunzi walivyokuwa na kiu cha kutaka kufahamishwa kuhusu kilichosababisha UKIMWI, namna ya kutunza wagonjwa wa UKIMWI na njia za kuzuia maambukizi yake. Hamu hiyo ilidhihirishwa na maswali mbalimbali yaliyoulizwa na wanafunzi. Tazama Kielelezo 64:

> Siku iliyofuata asubuhi, Njanga alimpitia Mshindo na wakaenda shuleni. Walikuwa wameshasahau pilkapilka za usiku uliopita. Kilichokuwa vichwani mwao ni kipindi cha maswali na majibu kuhusu Ukimwi ambacho yule mtaalamu aliwaahidi. Walipofika shuleni waliendelea na ratiba za vipindi kama kawaida. Na ilipofika saa tano na nusu *kiu* yao ikatimizwa kwani mtaalamu aliingia darasani (uk.32).

Maelezo katika Kielelezo 64 yamethihirisha kuwa wanafunzi walikuwa na hamu ya mafunzo kuhusu UKIMWI kiasi kwamba, walirauka shuleni asubuhi na mapema kumngoja mtaalamu. Hivyo, jukumu la mtaalamu wa Wizara la kuendeleza elimu kuhusu UKIMWI lilikuwa muhimu kwani liliambatana na Ajenda 2063 ya Afrika Tunayoitaka, inayohimiza uimarishaji wa afya ya binadamu kwa kuendeleza elimu kuhusu usafi, lishe bora na kuboresha huduma za afya.

### 4.4.53 Tamaa mbele Mauti nyuma

Hii ni methali ya kisitiari inayohusisha *tamaa* na *mauti*. Kwa mujibu wa methali hii, *tamaa* ya vitu au jambo fulani inaweza kusababisha madhara na hata kifo. Sitiari hii inaonya watu dhidi ya kutamani kuishi zaidi ya uwezo wao. Katika muktadha wa matumizi, methali hii ni sitiari ya kiafya kwa sababu imetumika kuangazia madhara ya

kiafya kama vile mauti ambayo yalitokana na tamaa. Mtaalamu wa Wizara ametumia muda kuwaonya wanafunzi dhidi ya kuingiwa na tamaa ya mapenzi mapema, kwani tabia hiyo ingewatumbukiza katika janga la UKIMWI. Mtaalamu anasema: Tazama Kielelezo 65

> "Kwa wasichana epukeni *tamaa* ndogondogo ambazo zinaweza kusababisha kufanya ngono. Kumbuka: *tamaa mbele mauti nyuma*. Kwa wavulana nyinyi ndiyo chanzo cha mabadiliko. Endeleeni na Masomo tutaonana wiki ijayo." (uk.39).

Mwandishi ametumia methali katika Kielelezo 65 kama kiangaza mbele kuwaonya wanafunzi dhidi ya changamoto zilizowangoja ikiwa watajihusisha na ngono. Miongoni mwa matatizo yaliyowangoja ni maambukizi ya UKIMWI ambayo yangewasababishia vifo vya mapema.

**4.4.54 Mzee**

Baba Mshindo alihuzunishwa sana na hali ya kiafya ya Daudi baada ya kumtembelea hospitalini. Alionekana amebadilika kisura na kiafya. Kutokana na mabadiliko hayo mwandishi anamlinganisha na mzee. Tazama Kielelezo 66:

> Baba yake alikuwa sebuleni. Alimsalimia na kumuuliza hali ya kaka yake. Baba yake alisita kujibu. Alionyesha kama alikuwa akitafuta la kumjibu. Mshindo alimuuliza tena huku amemkazia macho. Sura ya baba yake ilikuwa imekunjamana na alionekana mchovu sana. Macho yalionekana mekundu na Mshindo alihisi kama baba yake amekuwa *mzee* zaidi muda ule (uk.45).

Mzee ni mtu mkongwe. Mwandishi ametumia sitiari '*mzee'* katika Kielelezo66 kurejelea kuvunjika moyo na kudhoofika kiafya kwa baba Mshindo. Kugonjeka kwa Daudi kuliumiza babake kiafya na kimawazo. Hii ni tahadhari kwa kila mtu kwamba, maambukizi na kuenea kwa ugonjwa wa UKIMWI kunapaswa kuzuiliwa kwani athari zake huumiza mgonjwa, familia yake na marafiki.

Pia, mtafiti ametambua aina mbalimbali za sitiari za kiafya katika matini teule *ya Madhila ya Bi. Shufaa.* Miongoni mwa sitiari hizi ni:

### 4.4.55 'Sweetie'

'Sweetee' ni neno la Kiingereza linalomaanisha utamu. Kulingana na muktadha wa matumizi, mwandishi ametumia neno hili kama sitiari ya kiafya ya uzinzi. Sule ametumia sitiari hiyo katika barua aliyomwandikia Amina kurejelea mapenzi aliyokuwa nayo kwake (uk.3). Mtafiti amebainisha sitiari hiyo katika kitengo cha uzinzi kwa sababu mapenzi hayo yalihusisha wanafunzi wa shule ya msingi, ambao walikuwa wachanja na mapenzi ya mapema yangewatumbukiza katika ngono za kiholela ambazo zingewaambukiza magonjwa ya zinaa.

### 4.4.56 Mtu wa Miraba Minne

Mwandishi ametumia sitiari hii kurejelea hali ya kiafya ya Bw. Majanja. Kulingana na maelezo yaliyotolewa, Majanja alikuwa mtu mnene na alilinganishwa na nguruwe. Tazama Kielelezo 67 :

> Bwana Fukua, kama alivyofahamika mtaani, alikuwa ndiye diwani wa eneo lile. Alikuwa *mtu wa miraba minne.* Ilikuwa vigumu kuona shingo yake. Alijazana minyama kila mahali. Alikuwa kanona kama nguruwe (uk.8).

Kinachoangaziwa katika kielelezo 67 ni kwamba, ingawa '*mtu wa miraba minne'* ni sitiari ya kiafya ya siha, unene wa Fukua ulikuwa wa kutilia shaka. Hii ni kwa sababu Fukua aliugua ugonjwa wa UKIMWI. Kulingana na UNAIDS (2023) UKIMWI umeathiri watu wengi ulimwenguni. Hivyo, unene wa Fukua haukuwa ushahidi kuwa alikuwa buheri wa afya.Tathmini ya maelezo hayo ni kwamba, sura ya nje ya mtu au ukubwa wa kimwili sio dhibitisho ya kuwa na afya nzuri. Uchunguzi wa daktari unapaswa kutekelezwa ili kufahamu hali ya mtu.

Vilevile, sitiari mbalimbali za kiafya zimetumika kurejelea ugonjwa wa UKIMWI. Sitiari hizo ni:

### 4.4.57 Kitanzi

Katika lugha ya kawaida neno *kitanzi* hurejelea tendo la mtu la kujinyonga kwa kutumia kamba. Mwandishi ametumia sitiari hii kurejelea ugonjwa wa UKIMWI uliomwathiri

Fukua. Hivyo, hatua ya Bi. Shufaa ya kumkaribisha Fukua aliyeugua UKIMWI katika maisha yake ni kukaribisha kifo. Tazama Kielelezo 68:

> "Kwanza ingia ndani. Si vyema kuzungumzia kwenye upenu wa milango. Kwani kuna tatizo lolote?" Mama alisaili asijue kwamba yuko karibu kujitia *kitanzi* bila kujua (uk.10).

Mazungumzo katika Kielelezo 68, yanaonyesha jinsi Bi. Shufaa alivyomkaribisha Fukua kwa moyo mkujufu bila kujua ya kuwa, Fukua alikuwa na hila katika matembezi yake. Nia yake ilikuwa ni kufanya ngono na Bi. Shufaa na hatimaye kumwambukiza UKIMWI. Hivyo, katika mazingira ya mazungumzo hayo, *kujitia kitanzi* ni kuambukizwa ugonjwa wa UKIMWI.

### 4.4.58 Shetani

Pia, ugonjwa wa UKIMWI umelinganishwa na *shetani* ambaye anahusishwa na maovu kama vile kuua, kusababisha magonjwa, ajali na maovu mengine mbalimbali. Tazama Kielelezo 69:

> "Je, kulikoni? Imekuwaje leo ukafika huku kwetu?" Kwa hamasa, mama aliuliza. Hajui tu, kumbe, Bi. Shufaa ndio mwanzo anamwalika *shetani* maishani mwake. Fukua alijibabatiza kwa maneno yasiyokuwa na mwanzo wala mwisho (uk.11).

Kulingana na mazungumzo katika kielelezo 69, *shetani* ni sitiari ya kiafya ya maradhi iliyotumika kurejelea ugonjwa wa UKIMWI ambao haukuwa na dawa na hatima ya mwathiriwa ni kifo.

### 4.4.59 Mbebu Chafu

Katika kitabu kiteule, mhusika Fukua amelinganishwa na mpanzi ambaye hutayarisha mbegu kwa makini kwa lengo la kuzipanda katika shamba. Mbegu inapopandwa huchipuka na kuwa mmea. Pia mwanaume na mwanamke huwa na mbegu za uzazi ambazo zinapokutana wakati wa kujamiiana huungana na kuwa kiinitete. Mwandishi ametumia '*mbegu chafu'* kama sitiari ya kiafya kurejelea virusi vya UKIMWI. Tazama Kielelezo 70:

> Bwana Fukua alikuwa na kiu cha wanawake. Kinyua chake kilikuwa na makali kama ya nyembe. Pale mtaani tayari alikuwa na jamii kama sio

> jamaa. Kila nyumba alipanda *mbegu*, tena *mbegu chafu*. Wasichana wengi walimpenda kwa sababu ya pesa zake (uk.11).

Katika Kielelezo 70, mwandishi amelinganisha virusi vinavyosababisha UKIMWI na mbegu iliyochipuka baada ya kupandwa. Fukua alipanda *mbegu chafu* ya UKIMWI kwa wanawake aliofanya nao mapenzi bila kinga. *Mbegu* hiyo ilipochipuka iliathiri afya ya wanawake hao kama vile Bi. Shufaa na kusababisha vifo. Hii ni tahadhari kwa wanaojihusisha na ukahaba kwamba, madhara mbalimbali ya kiafya yanawangoja ikiwa hawatabadili tabia hiyo.

### 4.4.60 Asali

Asali ni tamu na hutengenezwa na nyuki kama chakula chake na wala si kwa minajili ya kutumiwa na binadamu. Binadamu huinyemelea na kuirina kama mwizi. Katika kitabu kiteule, magora ya leso yamelinganishwa na asali. Fukua alitumia magora hayo kama mtego wa kunasa Bi. Shufaa na kumhusisha katika ukahaba.
Tazama Kielelezo 71:

> Bwana Fukua huja na kumwachia Bi. Shufaa magora ya khanga zenye maandishi yanayovutia. Magora hayo ya leso yakawa ndio asali ya moyo wa ‘Mama safi.’ Ama kwa kweli, mcheza chuma huchuma, kama hakuchuma tumbo hunguruma (uk.13).

Tathimini ya usemi katika Kielelezo 71 ni kwamba, mwandishi ametumia *asali* kama sitiari ya kiafya kuwakilisha mapenzi kati ya Fukua na Bi. Shufaa. Ingawa Bi. Shufaa alijaribu kuihepa mienendo ya Fukua ya kumnyemelea, tamaa ya pesa na mali ya bure ilimtumbukiza katika mapenzi nje ya ndoa yaliyomwambukiza ugonjwa wa UKIMWI. Tendo hili limedhihirisha jinsi tamaa ya pesa na mali ilivyokuwa na uwezo wa kuangamiza asasi ya ndoa.

### 4.4.61 Lulu

Mdee na wengine (2022) wanaelezea kuwa Lulu ni kito cha thamani kinachong’ara na kutumiwa kama pambo. Bi. Shufaa amelinganishwa na *lulu* kwa sababu ya usafi na uwajibikaji wake katika jamii. Alitekeleza majukumu yake kwa ustadi na alikuwa mfano wa kuigwa katika jamii. Tazama Kielelezo 72:

> Yule yakhe Bw. Fukua hakuwahi kuonekana tena. Alitimiza wajibu wake; kazi ya kuimaliza nafsi ya mwanamke aliyekuwa *lulu* ya jamii yake. 'Mama Safi,' usafi ukatoweka na uchafu kuchukua hatamu (uk.23).

Katika Kielelezo 72, *lulu* ni sitiari ya kiafya ya usafi iliyotumiwa na mwandishi kurejelea usafi na uwajibikaji wa hali ya juu wa Bi. Shufaa. Baadaye hali hiyo iliathiriwa na matatizo ya kiafya kiasi kwamba, uchafu ulichukua nafasi ya kwanza katika maisha yake. Tathmini ya maelezo hayo ni kwamba, maradhi ya UKIMWI ni kikwazo kikuu katika maendeleo ya jamii kwa jinsi yanavyoathiri nguvu na utendakazi wa mtu. Kwa mujibu wa Wanjala (2015) kuna umuhimu wa kuzuia maradhi kama hayo, kwa kuelimisha jamii kuhusu njia za kuzuia magonjwa kama vile kula lishe bora, kufahamu huduma mwafaka za kiafya na kuepuka njia zinazosababisha maradhi.

#### 4.4.62 Gofu

Bi. Shufaa aliathiriwa kiafya kiasi kwamba amelinganishwa na *gofu*, ambalo ni jumba kuu na hame lililobomokabomoka. Ingawa *gofu* ni aina ya nyumba, pia neno hilo limetumika kama sitiari inayoangazia athari za kiafya zilizompata Bi. Shufaa. Kulingana na Kovecses (2000) sitiari moja inaweza kuwa na maana mbalimbali kulingana na namna ilivyotumiwa katika kazi ya fasihi. Hivyo, sitiari *gofu* imetumika kurejelea hali ya kiafya ya Bi. Shufaa. Afya yake ilidhoofika hivi kwamba hangetambuliwa. Tazama Kielelezo 73:

> Bi. Shufaa hana pa kushika, amekonda kama ng'onda. Mabintize Walijitahidi kumliwaza na kuhakikisha mama yao anatumia ARVs. Wakamlisha kila aina ya matunda anayonunua baba yao. Jirimu lake nzuri limekuwa *gofu*. Kwa Mzee Iddi na wanawe, maisha yakawa yenye dhiki kabisa (uk.23).

Kielelezo 73 ni mfano wa aya ya kisitiari inayoangazia taswira ya mtu hoi na aliyekonda kiasi kwamba hangeshikika. Bi. shufaa amesawiriwa kama *gofu* tu la mtu.

### 4.5 Sitiari Pana za Kiafya katika Vitabu Teule

Utafiti huu umebainisha aina zifuatazo za sitiari pana za kiafya, ambazo wandishi wa vitabu viteule wametumia kuangazia masuala mbalimbali ya kiafya. Katika matini teule *Nimefufuka* mwandishi ametumia aina zifuatazo za sitiari pana za kiafya:

### 4.5.1 Sokwe- Mtu- Tasa

Sitiari ya kiafya *'Sokwe- mtu- tasa'* imetumika katika kitabu kiteule kulinganisha Sikitu na *Sokwe*. Katika lugha ya kawaida, Sokwe ni mnyama mkubwa jamii ya nyani na anayeweza kutembea kama binadamu. Naye tasa ni kiumbe au mtu asiyeweza kuzaa. Sitiari hii ni ya kiafya kwa sababu inawakilisha ule uwezo wa binadamu wa kuzaa. Utaza husababishwa na matatizo ya kiafya kama vile magonjwa. Lena alitumia sitiari hiyo kumlinganisha dadake na *Sokwe*. Tazama Kielelezo 74:

> Nakumbuka alipotutembelea, nilimwonya kupunguza kukurukakara zake. Alinikejeli na kuniita 'mshamba.' Akaongeza sumu kwa kidonda kwa kuniita *sokwe- mtu- tasa*. Nikajitenga kando, kwani mie *nyumba ya udongo* sihimili vishindo (uk.3).

Katika Kielelezo 74 Lena anamlinganisha Sikitu na Sokwe tasa. Pia, ametumia sitiari *Sokwe* kurejelea Sikitu kama sura mbaya ambayo haingependeka na binadamu. Vilevile, Sitiari ya *utasa* imetumika kumsawiri mhusika Sikitu kama mtu aliyekumbwa na matatizo ya uzazi.

### 4.5.2 Bomba la Dume lenye Kidari cha Duara

Mwandishi ametumia sitiari ya kiafya '*bomba'* kurejelea mwanaume Mwarabu aliyeishi na Lena. Maana ya kimsingi ya '*bomba*' ni kifaa chenye uwazi ndani kinachotumiwa kusafirisha vioweo kama vile maji (TUKI, 2004). Kumrejejea Mwarabu huyo kama *bomba la dume* kulitilia unene na afya yake shaka. Ingawa alikuwa mwanaume mnene, afya yake ilikuwa na dosari ndiposa alimwambukiza Lena UKIMWI. Tazama Kielelezo 75:

> Muda si muda, Lena alitokeza akiwa nusu uchi. Sidiria na chupi tu ndiyo mavazi yake. Anapania kuutangaza uchi wa kuku. Mwarabu wake vilevile, *bomba la dume lenye kidari cha duara na manyoya meupe yaliyofanya msitu kifuani pake* (uk.5).

Sentensi *bomba la dume lenye kidari cha duara na manyoya meupe yaliyofanya msitu kifuani pake* katika Kielelezo 75 pia ni sitiari ya kiafya inayoangazia taswira ya jitu la mwanaume lililokuwa na dosari katika afya yake. Sitiari ya *bomba* katika sentensi hiyo inaashiria utupu au kasoro ya kiafya.

Sitiari pana ya kiafya, pia imetumika katika muundo wa sentensi kusawiri mimba kama kiumbe hai na kilichokuwa na uwezo wa kuamua hatima yake. Tazama Kielelezo 76:

> "Inadaiwa mimba hiyo ilimkataa. Iliasi kukaa chupani mwake. Ikaomba itoke lakini akaiomba kughairi tarehe ya kutoka." (uk.7).

Usemi katika Kielelezo 76 ni wa kisitiari unaoangazia taswira ya mimba ambayo ni kiumbe hai, kinachosikia na chenye uwezo wa kuamua kingeishi wapi. Hii ndio sababu kilikataa kuishi katika chumba cha uzazi na ikabidi Lena akisihi kighairi nia ya kutoka. Sitiari hiyo imewakilisha magonjwa na maumivu ambayo Lena alipitia katika harakati za kubeba mimba. Baadhi ya magonjwa ambayo yalimwandama ni kifua kikuu, malaria ukosefu wa damu, kuhara na kutapika.

Aina mbalimbali za sitiari pana za kiafya pia zimetumika kuangazia masuala ya kiafya katika matin teule ya *Sitaki- Iwe- Siri*. Miongoni mwa sitiari hizi ni:

### 4.5.3 Kuanguka, Zimwi na Ibilisi

Sitiari hizi zimetumiwa kwa mfululizo kuunda sitiari pana ya kiafya kuwakilisha ugonjwa wa UKIMWI. Katika matini teule, Yuri amesawiriwa kama msichana kaidi na kahaba asiyesikia la mkuu wala mteka maji msikitini. Ukaidi huo unamtumbukiza katika ukahaba na akaambukizwa UKIMWI. Baada ya kuugua, watu walianza kumtoroka ili asiwaambukize ugonjwa huo. Tazama Kielelezo 77:

> Walijua bayana kuwa Yuri alikuwa ameanza *kuanguka*. Tetesi zilikuwa zimeanza kusambaa mithili ya moto kwenye biwi la nyasi kavu wakati wa kiangazi katika mji wa Mwembe Tayari kwamba Yuri alikuwa amekwaruzana mabega na *ibilisi*. Ingawa wahenga walisema kuwa *zimwi* likujualo halikuli ukakwisha, hili lililompata Yuri katika pilkapilka zake kwenye majumba ya starehe liliapa kumumaliza (uk.45).

Tathmini ya mazungumzo katika Kielelezo 77 ni kwamba, Musa ametumia sitiari za kiafya za maradhi *kuanguka*, *Ibilisi* na *Zimwi* kurejelea ugonjwa wa UKIMWI. *Kuanguka* ni Sitiari ya kiafya ambayo imetumika kurejelea ugonjwa wa UKIMWI. Musa ametumia neno '*kuanguka*' kutuchorea taswira ya ugonjwa *unaongusha* au kuua. Pia, Musa amefananisha UKIMWI na *Zimwi* na *shetani*. *Shetani* anaogopwa na

binadamu kote ulimwenguni kwa sababu ya matendo yake maovu kama vile kuua. Vilevile, UKIMWI ni ugonjwa unaoua na umesambaa kote ulimwenguni. Pia ugonjwa huo hauna dawa.

Hali kadhalika, Musa ametumia usemi wa kisitiari kuelezea tabia ya Yuri baada ya kuambukizwa ugonjwa wa UKIMWI kama inavyoangaziwa katika Kielelezo 78:

> Leo hii Yuri alikuwa akirandaranda kwenye chumba kidogo cha takriban mita kumi na sita mraba mithili ya kuku aliyetaka kutaga mayai. Aliwaza jinsi maisha yalivyomgeuka. Watu walikuwa wamenong'ona kuwa maumbile ya Yuri yalikuwa yamebadilika si haba. Kioo kilimwambia ukweli. Mwili wake ulikuwa umekondeana. Macho yalikuwa yamemwingia ndani. Mitulunga ilikuwa inaonekana huku mwili wake mzima ukiny'ong'onyea kama mkufu kwa sababu ya kuishiwa nguvu (uk.47).

Kielelezo 78 ni aya ya sitiari pana ya kiafya ya maradhi, inayochora taswira ya Yuri aliyeambukizwa UKIMWI na kuwa mnyonge, mwenye afya duni na asiyeweza kutembea. Kifo kimemtazama kwa macho. Hapo awali Yuri alikuwa msichana mrembo, mwenye siha na kipenzi cha wanaume mitaani. Sitiari hii imesawiri UKIMWI kama ugonjwa hatari kwa kuharibu sura na mwili wa mtu na unapaswa kuepukwa vyovyote vile.

**4.5.4 Utingo**

Utingo ni kiwakilishi cha uchafu. Amesawiriwa kama mnywaji wa pombe na dawa za kulevya ambazo huathiri hulka za watu. Hali hii imedhihirishwa na mwandishi. Tazama Kielelezo 79:

> "Mwisho wa gari," Utingo, mwamamme mwenye umri wa makamo hivi na mwenye macho mekundu kama damu alisema. Kinywani alikuwa na miraa ambayo alikuwa anatafuna mithili ya mbuzi anayecheua nyasi. Katika mkono wake wa kulia, alikuwa amebeba bunda la noti alizokuwa amekusanya kama nauli. Katika mkono huo huo alifumbata furushi la miraa ambalo alikuwa anachovya na kutia kinywani na kusaga kwa meno kama kinu cha mahindi (uk.30).

Kielelezo 79 ni aya ya kisitiari ya kiafya inayoangazia taswira ya uchafu na matumizi ya dawa za kulevya. *Utingo* amesawiriwa kama mtu mchafu na mlevi mwenye macho mekundu na asiyezingatia kanuni za usafi. Alichanganya pesa na miraa aliyoikula ilhali

pesa huwa na uchafu mwingi. Ulaji wake wa miraa haukuzingatia kanuni za kiafya kama vile kunawa mikono ili kudumisha usafi na umelinganishwa na mbuzi anayecheua nyasi au jinsi kinu kinavyosaga mahindi. *Utingo* ni kiwakilishi cha uozo wa afya uliosambaa katika jamii. Hili limedhihirishwa katika ukurasa wa thelathini na moja ambapo tumearifiwa kuwa, watu wengi waliobebwa katika gari hilo walikuwa wagonjwa au waliokuwa wakienda kuwatembelea wagonjwa wao hospitalini.

### 4.5.5 Kifo cha Yuri

Kilele cha vita dhidi ya UKIMWI kimeangaziwa na kifo cha Yuri. Kifo cha mhusika mkuu Yuri ni sitiari ya kiafya inayowakilisha mwamko mpya katika vita dhidi ya UKIMWI (uk. 61). Ujumbe mkuu unaopashwa kwa hadhira kupitia barua ya Musa ni kwamba, maambukizi na vifo vinavyotokana na UKIMWI visiwekwe kama siri tena.

Mwandishi wa *Pendo katika Shari* pia ametumia aina mbalimbali za sitiari za kiafya kufafanua masuala ya kiafya. Baadhi ya sitiari ambazo alitumia ni:

### 4.5.6 Ng'onda na Kiwiliwili cha Mifupa

Kwa mujibu wa TUKI (2004) ng'onda ni aina ya samaki ambaye amepasuliwa sehemu mbili zilizofanana na kukaushwa juani. Pendo amejilinganisha na *ng'onda* kwa jinsi alivyokonda kutokana na kuteswa na Sulubu. Aliendelea kudhoofika na kuachwa *kiwiliwili cha mifupa*. Haya yamedhihirishwa na matamshi ya Pendo. Tazama Kielelezo 80:

> "Maskini Pendo mie…nimesalia *ng'onda, kiwiliwili cha mifupa tu*," alijisemea huku machozi yakilengalenga machoni. Juma lilipita na hali ya Zuhura ikazidi kuzorota. *Mafua, homa na Kikohozi vilimwandama vikakazana kuukamua uhai ndani yake* (uk.20)

*Ng'onda* na *kiwiliwili cha mifupa* katika Kielelezo 80 ni sitiari za kiafya zilizotumika kusawiri matatizo ya kiafya kama vile kudhoofika, kuteseka kimawazo na kukosa malezi bora, ambayo Pendo alipata baada ya kutengwa na bwanake. Isitoshe, usemi huo wote ni sitiari pana ya kiafya inayotuchorea taswira ya mwanamke dhaifu, aliyekonda na kukondeana na aliyepoteza matumaini katika maisha. Kadhalika, magonjwa yaliyomwathiri Zuhura kama vile mafua, homa na kikohozi yamelinganishwa na

mnyama aliyeamua kumuua. Usemi huo ni sitiari ya kiafya ya kitashihisi. Kwa mujibu wa Wamitila (2003) sitiari ya kitashihisi hulinganisha vitu visivyokuwa hai kwa kuvipa sifa ya uhai. Kwa msingi huu, magonjwa kama vile mafua, homa na kikohozi yalipewa sifa ya uhai. Kwa mujibu wa Nadharia Changanuzi ya Sitiari ya Dhana ulinganifu wa aina hii unaleta uhalisi unaokubalika katika jamii (Lakoff, 1992).

### 4.5.7 Furaha ya Nyani imeishia Jangwani

Katika matini teule Pendo amemrejelea Sulubu kama *nyani* kutokana na tabia yake potovu. *Nyani* ni mnyama mkubwa jamii ya tumbili na aliyekuwa na bato jekundu sehemu za matako. Mnyama huyo ni mjanja na hufurahia kuishi mitini. Ana ujuzi wa kuruka kwenye mti mmoja hadi mwingine na ni vigumu kumshika. Hata hivyo, akifika jangwani ujaja huu hufika kikomo na ni rahisi kumshika. Pendo alimlinganisha Sulubu na *nyani* kutokana na madharau na maringo kwamba, hangeweza kuambukizwa UKIMWI. Ulinganifu huu unaweka wazi tabia ya Sulubu na kuafikiana na kauli ya Nadharia Changanuzi ya Sitiari ya Dhana kuwa, matumizi mwafaka ya sitiari huleta ulinganifu wa kihalisia na kurahisisha uelewa wa suala linaloangaziwa (Johnson 1980, Lakoff 1992). Mafikira ya Pendo yanashadidiwa na methali kwamba: “nyani haoni kudule, huliona la mwenziwe.” Tazama Kielelezo 81:

> Pendo alizipokea habari za tanzia hiyo kwa moyo mzito. Alikumbuka Jinsi mumewe alivyomsuta juu ya maradhi yake. Alishusha pumzi na kutamka, “Mnh, *furaha ya nyani imeishia jangwani. Sasa mwenye ndwele atajulikana hivi karibuni* (uk. 46).

Katika maelezo yaliyotolewa katika Kielelezo 81, Pendo ametumia lugha ya kisitiari kurejelea ugonjwa wa UKIMWI. Ingawa Pendo alimhurumia mumewe, pia alitaka ukweli ujulikane kuhusu kiini cha ugonjwa uliowapata. Hivyo, sitiari ya kiafya kuwa *furaha ya nyani imeishia jangwani* imetumika kurejelea ugonjwa wa UKIMWI uliompata Sulubu. Yamkini, Pendo anatuarifu kuwa Sulubu aliyeringa kuwa asingeweza kugonjeka, wakati huo alikuwa mgonjwa wa UKIMWI.

Matumizi zaidi ya sitiari za kiafya yalijitokeza wakati ambapo Sulubu alitembelea kituo cha afya ili kutibiwa maradhi yaliyokuwa yakimsumbua. Tazama Kielelezo 82:

> Daktari Hamisi alimtazama kwa macho ambayo Sulubu alihisi yaliangaza hadi moyoni mwake, mpaka kwa damu yake na kuona umati wa virusi vya Ukimwi ukishambulia chembechembe za damu iliyositiri uhai wake. Kila alipozidi kuyatazama macho hayo, ndivyo Sulubu alivyohisi yeye ni muwele mbele yake. Baada ya kusimulia kisa chake, Sulubu alitulia mfano wa kondoo anayesubiri kuchijwa (uk.50).

Usemi ulioangaziwa katika Kielelezo 82 ni mfano wa sitiari pana ya kiafya ya maradhi iliyotumika katika kitabu kiteule kusawiri makali ya ugonjwa wa UKIMWI. Kama anavyosema Wamitila (2008) kuwa sitiari pana ni sitiari iliyopanuliwa kimaana na kuwepo kwa sitiari zingine, dondoo hili limeundwa na mkufu wa sitiari ili kuelezea kwa kina na kurahisisha uelewa wa suala linalozungumziwa. Kuzmina (2013) anashadidia wazo hili kwa kusema kuwa, sititiari hueleweka vyema inapotumika katika muundo wa sentensi, kwa sababu sentensi hutungwa kwa kuzingatia kaida za kisarufi na huwazilisha wazo kikamilifu. Hivyo, aya iliyotumika katika Kielelezo 82 imechora taswira ya mtu aliyepoteza matumaini na maisha kutokana na athari za magonjwa yaliyomwathiri.

Sitiari pana za kiafya pia zimetumika kusawiri masuala ya kiafya katika matini teule ya *Madhila ya Bi. Shufaa*. Mwandishi ametumia sitiari zifuatazo kufafanua masuala ya kiafya: Tazama Kielelezo 83:

> Kipenzi Amina, macho yako ya kikombe, shingo ya upanga, kiuno cha nyigu, Meno ya theluji yamenifanya niuone ulimwengu kama tambara bovu. Uzungumzi wako hauna mpinzani. Usheshi wako unamithilishwa na viumbe waliotukuka peke yake (uk.4).

Kielelezo 83 ni mfano wa sitiari pana ya kiafya iliyotumika katika kitabu kiteule. Sitiari hii imeundwa na sitiari zingine zilizokuwa katika muundo wa sentensi ili kuelezea kwa ukamilifu sura ya Amina. Kulingana na Wamitila (2008), sitiari pana hujumuisha sitiari mbalimbali zinazofanya kazi kwa pamoja ili kuelezea wazo fulani. Mkufu huo wa sitiari mara nyingine huwa vifungu vya maneno au sentensi na huelezea wazo kuu kwa kina. Ni muhimu pia kufahamu kuwa, sitiari zinapotumika katika muundo wa sentensi hueleza suala linalozungumziwa kwa urahisi (Kuzmina, 2013). Katika msingi huu, dondoo lililoangaziwa hapo awali ni aya ya kisitiari iliyosheheni mkufu wa sitiari zilizoelezea umbo nzuri la Amina. Tathmini ya sitiari hizi ni kwamba zimetumika kuerejea mapenzi kama sehemu ya mwili au kitu kilichoonekana.

### 4.5.8 Fukua

Mwandishi wa *Madhila ya Bi. Shufaa* ametumia sitiari pana ya kiafya '*Fukua'* kumsawiri Bw. Juma Majanja kama kahaba, aliyehusika kingono na wanawake mbalimbali bila kujali umri wao, ndoa zao au hali yao ya kiafya. Hii ni sitiari pana kwa sababu mhusika kinzani Majanja ametumika kama kurunzi ya kuangazia visababishi vya UKIMWI, njia za usambazaji na kuzuia janga la UKIMWI ambayo ni masuala makuu ya kiafya yaliyoangaziwa katika matini teule. Majanja ameitwa jina la kimajazi '*Fukua'* kwa sababu ya ujasiri wake wa kutembea kila mahali na kutaka kupeleleza kila kitu. Tazama Kielelezo 84:

> Alikuwa kanona kama nguruwe. Jina lake kamili lilikuwa Bw. Juma Majanja. Jina lake hilo la msimbo- Bwana *Fukua*, alipewa na wanakijiji kwa sifa yake ya ujasiri. Angeweza kuingia kila mahali bila woga na hata kusema kile anachotaka kwa yeyote yule. Kwa ufupi, alikuwa *njemba la mtu*! (uk.8).
>
> Kwa bahati mbaya, mtu huyu alipenda usherati. *Alifukua* hata *visivyofukuliwa*. Kwa upande mwingine, aliwanyemelea wake za wenyewe na hata mabanati tumbitumbi! Kwa Bi. Shufaa alianza kujenga hema (uk.12).

Tathmini ya muktadha wa matumizi ni kwamba katika Kielelezo 84 ni kuwa, *Fukua* ni sitiari ya kiafya iliyotumiwa kurejelea tabia ya Majanja ya kufanya ngono na wasichana na wanawake walioolewa. Hivyo, *Fukua* ni sitiari ya kiafya ya uzinzi. Mhusika huyo alikuwa kahaba na mgonjwa wa UKIMWI. Alitumia fedha na cheo chake cha udiwani kukimbizana na wasichana na wanawake walioolewa katika kijiji cha Mangelepa. Kutokana na tabia ya kufanya ngono na kila mwanamke aliyempata, watu walimwita *Fukua*. *Alifukua* kila mwanamke aliyemkubali. Aidha, wanakijiji walitumia lugha hiyo ya kisitiari ili kuepuka makali ya lugha ya kawaida ambayo ingeeleweka na hata watoto na kumkosea heshima. Uamuzi wa kutumia lugha ya kisitiari uliafikiana na kauli ya Kobia (2008) kwamba, sitiari ilipotumiwa katika mawasiliano ingeweza kuwasilisha ujumbe kinzani kwa njia iliyokubalika. Kwa jinsi hii wanakijiji walitumia jina *Fukua* kurejelea mtindo wa Bw. Majanja wa kufanya ngono kiholela. Cheo cha Majanja cha udiwani pia kilichangia katika kutumia lugha ya kisitiari ili kuepuka kumzusha hadhi katika jamii.

### 4.5.9 Afya yake ikawa inafuata Majira kama ulivyo Msimu wa Kipupwe

Hii ni sitiari pana ya kiafya ambayo imelinganisha afya duni ya Bi. Shufaa na upepo mkali uliokuwa na baridi. Sitiari hiyo imeangazia taswira ya mwanamke aliyekabiliwa na maradhi kali yaliyodhoofisha afya yake hivi kwamba asingeweza kujimudu. Tazama Kielelezo 85:

> Ikawa wiki hii ina heri na wiki inayofuatia ni shari moja kwa moja. *Afya yake ikawa inafuata majira kama ulivyo msimu wa kipupwe*. Hata marafiki za akina Amina na Zuhura wakawa wanawafariji kwa pamoja (uk.22).

Katika mfano uliotolewa katika Kielelezo 85, sitiari hii ni ya maradhi inayosawiri ukali wa ugonjwa wa UKIMWI uliomwathiri Bi. Shufaa. Umelinganishwa na kipupwe ambao ni upepo mkali na baridi.

Katika matini teule ya *Madhila ya Bi. Shufaa* mwandishi ametumia mkufu wa sitiari za kiafya kusawiri hali ya kiafya ya Bi. Shufaa. Kulingana na Wamitila (2008) sitiari pana huhusisha mkufu wa sitiari ulioangazia suala kuu katika kazi ya kifasihi. Suala kuu lililoangaziwa katika matini teule ni ugonjwa wa UKIMWI na Bi. Shufaa ndiye mhusika mkuu aliyeendeleza suala hilo. Kwa jinsi hii, mwandishi alitumia mfululizo wa sitiari za kiafya kuangazia hali yake ya kiafya: Tazama Kielelezo 86:

> Mama akapewa kila aina ya tiba na wala hakuna dawa iliyokubali mwili.ARVs zilijaribu lakini wapi! Akawa wa kuingizwa na kutolewa. Kila anachopewa kikawa sumu. Ikafika wakati ambapo Bi. Shufaa anakuangalia lakini hakuoni! *Amekonda na kukondeana. Si sindano si ng'onda, si mtu si kifyefye. Kivuli cha mtu lingekuwa jina bora zaidi* (uk.23).

Katika Kielelezo 86 vifungu vya maneno: *Amekonda na kukondeana, si sindano si ng'onda, si mtu si kifyefye.* na *kivuli cha mtu lingekuwa jina bora zaidi*, ni sitiari za kiafya za maradhi zinazoeleza athari za ugonjwa wa UKIMWI kwa ujumla kwa mwathiriwa. Baadhi ya athari hizi kama ilivyoelezwa katika Kielelezo 86 ni kudhoofika kiafya, kushindwa na kula chakula, kutopona kwa magonjwa nyemelezi na kushindwa kuona vitu vizuri. Bi. Shufaa amelinganishwa na *ng'onda*, *kifyefye* na *kivuli*. Ingawa sitiari hizo ni tofauti, zimetumika kutoa ujumbe wa pamoja kwamba UKIMWI ni ugonjwa hatari unaoathiri afya, sura, na utendakazi wa mtu.

### 4.5.10 Baba Sukari

*Baba sukari* ni sitiari pana ya kiafya ya uzinzi ambayo imetumika kurejelea wanaume wanaowanyemelea wasichana kwa lengo la kufanya mapenzi. *Baba sukari* kama vile Fukua, walitumia fedha kuwarai wasichana na wake za watu kufanya ngono za kiholela. Katika harakati za kufanya ngono, wanaume hao walisambaza magonjwa ya zinaa na kuhatarisha maisha yao. Ili kujihadhari na *mababa sukari,* wanawake wa kijiji cha Mangelepa waliunda kikundi cha kutahadharisha jamii dhidi ya kujihusisha na mababa hao kupitia nyimbo. Tazama Kielelezo 87:

> Ogopa *Baba- sukari*, huwa wana nyingi ndumba, Huyanunua magari, machoni wakafumba Kumbe wanakuathiri, kukumwagia kasumba. Tumalizeni kasumba, tujikinge na Ukimwi (uk.29).

Wimbo ulioangaziwa katika Kielelezo 87 umetumiwa kama onyo kwa wanawake kwamba, Baba- sukari ni hatari katika kuwashawishi wanawake katika kufanya mapenzi ya kiholela. Pesa na mali zao ni kama dawa za kienyeji za kuvutia wanawake. Waimbaji wanawarai wanawake wajihadhari na wazee hao kama njia mojawapo ya kujikinga na maambukizi ya UKIMWI.

## 4.6 Hitimisho

Kwa ujumla, sura hii imejadili aina mbalimbali za sitiari za kiafya kama vile sitiari kuu, sitiari pana na sitiari za kikaida. Imebainika kuwa, sitiari hizi zimetumika kwa ufasaha kuwasilisha masuala ya kiafya kwa njia ya kiulingaishi iliyozua taswira mbalimbali zinazoelimisha na kuonya jamii dhidi ya kujihusisha na mienendo inayohatarisha maisha. Pia imebainika kuwa, sitiari hizi zote zimejengana na kukamilishana ili kujenga dhamira ya mwandishi.

# SURA YA TANO

# MATUMIZI YA MTINDO KATIKA UWASILISHAJI WA SITIARI ZA KIAFYA KATIKA VITABU TEULE

## 5.1 Utangulizi

Sura imeshughulikia lengo la pili la utafiti ambalo ni kuchunguza mtindo uliotumika kuwasilisha sitiari za kiafya katika vitabu viteule vya fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Data ya utafiti ilichanganuliwa kwa kurejelea matini teule: *Siku ya Ukimwi* (Kobia, 2008), *Pendo katika Shari* (Momanyi, 2008), *Sitaki Iwe Siri* (Matundura, 2008), *Madhila ya Bi. Shufaa* (Bakari, 2008), *Kosa la Marehemu* (Panja, 2010) na *Nimefufuka* (Nandwa, 2011). Kwa mujibu wa Senkoro (1982) mtindo ni jinsi mwandishi anavyotumia fani za lugha kuwasilisha masuala mbalimbali katika kazi ya kifasihi. Miongoni mwa fani na mbinu za mawasiliano ambazo mwandishi hutumia ni tamathali za semi kama vile tashbihi, taswira na methali, miundo mbalimbali ya sentensi, nyimbo, ushairi, usimulizi, uteuzi wa maneno, majazi, takriri, barua miongoni mwa mbinu zingine za uandishi. Kwa ujumla, kila mwandishi wa kazi ya kifasihi huwa na mtindo wa kipekee wa kujieleza unaomtofautisha na wandishi wengine. Mbinu za uandishi zilizojitokeza katika vitabu teule ni pamoja na usimulizi, barua, nyimbo, majazi, ushairi, tashtiti na tamathali za usemi kama vile methali, tashbihi, taswira, chuku na kinaya.

## 5.2 Nyimbo

Arege na Chacha (2023) wanasema kuwa wimbo ni maneno yanayotamkwa kwa sauti ya mziki au utungo unaotumia mahadhi na mapigo yenye mpangilio maalum. Nyimbo zimeanishwa katika aina mbalimbali kama vile nyimbo za watoto, dini, kisiasa, wasifu, harusi na nyimbo za huzuni  (Finnegan 1970, Nandwa na Rukenya 1983) . Akivaga na Odaga (1982) na Kabira na Mutahi (1988) wanaeleza kuwa nyimbo hizi hutekeleza majukumu muhimu katika jamii husika yakiwemo burudani, kushawishi, kufunza maadili, kuonya na kuendeleza tamaduni za kijamii. Zaidi ya hayo Timmamy (2002) anasema kuwa nyimbo ni sehemu ya fasihi simulizi na baadhi yake hutumia sitiari kuangazia masuala yanayochukuliwa kuwa mwiko katika jamii. Kwa msingi huu mtafiti amechunguza na kubaini kuwa utanzu wa nyimbo umetumika kama mbinu muhimu katika kuwasilisha sitiari za kiafya katika baadhi ya vitabu teule.

Katika kitabu kiteule cha *Siku ya Ukimwi* mwandishi ametumia wimbo kama mtindo wa kuwasilisha sitiari ya kiafya *nguo* inayoangazia taswira ya mgonjwa wa UKIMWI. Tazama Kielelezo 1:

Ugonjwa umetokea,
Unaitwa ukimwi,
Ukimpata mtu,
Anamalizika kama nguo (uk.5).

Nadharia ya Umitindo ilitumika kuchanganua suala linalowasilishwa na wimbo huu kwa sababu inarahisisha uelewekaji wa ujumbe. Kwa mujibu wa Indangasi (1988), nadharia ya Umitindo huwezesha kueleweka kwa lugha ambayo imetumika katika kazi ya fasihi. Bright (1992) anaafikiana na kauli hii kwa kusema kuwa lugha ndicho chombo muhimu kinachotumiwa na mwanafasihi kupasha ujumbe kwa hadhira. Kwa msingi huu mbinu ya wimbo ilimwezesha msikilizaji kuelewa kuwepo kwa janga la UKIMWI na changamoto zake kupitia matumizi ya msamiati wa kawaida unaotumika katika jamii na unaoeleweka na hadhira. Wimbo wa Kielelezo 1 ndio uliotumiwa na waimbaji kama mbinu ya kuangazia athari zinazotokana na janga la UKIMWI. Kupitia wimbo huo, wanajamii wanafahamishwa kuhusu kuwepo kwa ugonjwa wa UKIMWI unaoathiri afya ya binadamu na kusababisha kudhoofika kiafya kiasi cha kulinganishwa na *nguo*. Sitiari ya kiafya *nguo* imetumika katika matini teule kuangazia madhara ya UKIMWI. Madhara hayo yanalinganishwa na nguo kuukuu iliyochanikachanika. Mtindo wa kuwasilisha sitiari za kiafya kupitia nyimbo umetumika ili kuvutia hadhira kusikiliza ujumbe unaowasilishwa. Wamitila (2008) anasema kuwa sitiari hutumiwa kunasa makini ya hadhira. Hivyo, matumizi ya nyimbo katika kuwasilisha sitiari za kiafya huvutia wasikilizaji kwa jinsi zinavyokuwa na midudo inayovutia na kunasa makini ya hadhira. Katika kusikiliza mahadhi na midundo ya nyimbo, wasikilizaji pia hung’amua maana ya ujumbe unaowasilishwa.

Wimbo wa kisitiari pia umetumika katika matini teule ya *Madhila ya Bi. Shufaa* kusawiri baadhi ya visababishi vya UKIMWI. Baadhi ya visababishi hivi ni tamaa ya pesa na ufukara. Tazama Kielelezo 2:

Duniani kuna watu, waliopita kiwango
Wamekamilisha utu, ni wangwana kwenye bongo

Wanakupa kila kitu, tena bila masimango
Bando nasubiri mbongo, uwapi bwana Fukua?
Tayari'mepika chai, usichelewe muhibu
Ndio yako matilai, penzi letu lingaswibu
Bado nasubiri mbongo, uwapi bwana Fukua?

Wewe si goi goi, kama walivyo wengine
Unajua masilahi, mwepesi kama mashine
Hima fika asubuhi, unione nikuone
Bado nasubiri mbongo, uwapi bwana Fukua?
(uk.15).

Wimbo huu unaangazia jinsi tamaa ya pesa ilivyomwingia Bi. Shufaa na kuangukia mikononi mwa Bwana Fukua ambaye alimwambukiza ugonjwa wa UKIMWI. Fukua alitumia pesa na magora ya leso kumnasa Bi. Shufaa, mama aliyekuwa na tabia nzuri na kielelezo cha kupigiwa mfano katika jamii. Baadhi ya sitiari ambazo Bi. Shufaa alitumia kumrejelea bwana Fukua ni *Mbongo* na *habibu*. Ingawa Bi. Shufaa anamrejelea Fukua kama rafiki kupitia sitiari hizo, hii ni kejeli kwa sababu rafiki wa kweli ni bwanake. Ujumbe muhimu unaopashwa kwa jamii ya sasa ni kwamba, tamaa ya pesa na mapenzi ya kiholela yanapaswa kuepukwa kwani ni miongoni mwa visababishi vya ugonjwa wa UKIMWI. Maswali ya kibalagha yametumika kama mtindo wa kuendeleza wimbo na ujumbe unaopashwa na mwimbaji katika wimbo huu. Jambo hili limejitokea baada ya kila mshororo wa mwisho wa kila ubeti ambapo mwimbaji anamalizia kila kipande kwa kusema: *Bado nasubiri mbongo, uwapi Bwana Fukua?* Katika swali hili sitiari *mbongo* imetumiwa kuangazia utajiri wa Fukua ulionyemelewa na Bi. Shufaa.

### 5.3 Ushairi

Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999) ushairi ni sanaa ya lugha ambayo inaeleza wazo au jambo fulani kwa njia ya mkato na kwa namna inayonasa hisia za msikilizaji au msomaji. Wamitila (2008) anasema kuwa, utungo huo una mpangilio maalumu wa mbinu za lugha zinazomwezesha mtunzi wa ushauri kuwasilisha ujumbe kwa ufasaha na kwa ufupi. Arege na Chacha (2023) wanaafikiana na fafanuzi hizi na kuongezea kuwa ushairi ni jumla ya maarifa ambayo yanahusiana na mashairi na yanayohusu utunzi, usomaji au uchambuzi wa ushairi. Wanainisha aina za mashairi kama vile ushairi arudhi, ushairi huru na ushairi maumbo. Kwa msingi huu baadhi ya waandishi

wa vitabu teule wametumia ushairi kama mbinu ya kuwasilisha sitiari za kiafya ili kupasha ujumbe kwa njia ya mkato na inayonasa makini ya hadhira.

Kulingana na Leech (1969) mtindo unaotumiwa katika kazi ya kifasihi ndiyo njia kuu inayotumiwa na mwanasanaa kupasha ujumbe kwa hadhira. Kwa jinsi hii mtindo wa kishairi umetumika kuwasilisha suala la kiafya katika kitabu kiteule cha *Madhila ya Bi. Shufaa*, ambapo Bi. Kipungu alitunga shairi lililoangazia janga la UKIMWI. Shairi hilo lilitumika kuwasilisha sitiari za kiafya mbalimbali kama vile *kachumbari* na *sahani ya pamba*. Tazama Kielelezo 3:

> Cheleeni kujibari, kudanganyiza wachumba
> Kama wewe ni hodari, tafuta wako unyumba
> Usimwage *kachumbari*, kwenye *sahani ya pumba*
> Tumalizeni kasumba, tujikinge na UKIMWI
>
> Ogopa *Baba- sukari*, huwa wana nyingi ndumba
> Huyanunua magari, machoni wakakufumba
> Kumbe wanakuathiri, kukumwagia kasumba
> Tumalizeni kasumba, tujikinge na UKIMWI (uk.28).

Kielelezo 3 ni aina ya shairi la kiarudhi ambalo lina mizani '*ri'* ya kati na '*mba*' ya mwisho katika kila mshororo. Mizani hizi zinazua midundo inayonasa makini ya hadhira. Sitiari za kiafya *kachumbari* na *sahani ya pumba* zimebeba mizani hizi katika silabi zake. Shairi hilo limetumika kuwasilisha sitiari za kiafya *kachumbari* na *sahani ya pumba*. Kachumbari hutengenezwa na nyanya, vitunguu, pilipili au limau na huongezea ladha katika chakula. Kadhalika, pumba ni uchafu ulioko kwenye ume usiotahiriwa. Katika muktadha wa matumizi *kasumbari* ni sitiari ya kiafya inayowakilisha afya nzuri ilhali sitiari ya kiafya *sahani ya pumba* imetumika kuwakilisha UKIMWI. Mwandishi ametumia sitiari hizi kuwaonya vijana dhidi ya kujiunga na uzinzi ambao ungeathiri afya yao nzuri (*kasumbari*) na kuambukizwa UKIMWI unaolinganishwa na *sahani ya pumba*. Mwandishi ametumia lugha ya kisitiari kuangazia suala la UKIMWI ili kuepuka makali ya lugha ya moja kwa moja. Wazo hili linaafikiana na kauli ya Kobia (2008) kuwa sitiari inaweza kuwasilisha ujumbe uliokisiwa kuwa mwiko katika jamii kwa mtindo unaokubalika. Kwa msingi huu mtindo wa kishairi la kiarudhi umetumika kuwasilisha sitiari za kiafya *kasumbari* na *sahani ya pumba* kuangazia janga la UKIMWI kwa njia inayokubalika.

Isitoshe, katika shairi la Kielelezo cha 3 kilichoangaziwa hapo awali, sitiari ya kiafya *Baba- sukari* imetumika kusawiri tabia ya ukahaba ya Bwana Fukua. Hata hivyo maneno *baba* na *sukari* yaliyotumika katika ushairi huo yana ukinzani kimaana. *Baba* ni neno la heshima linalorejelea mwanaume mzazi na limetumika kurejelea Bwana Fukua ilhali neno *sukari* limetumika kuwakilisha matendo ya kikahaba ya Bwana Fukua ambayo hayaambatani na tabia ya baba mzazi. Hata hivyo kulingana na muktadha wa matumizi, uteuzi wa sitiari hiyo una mantiki kwa sababu inaakisi kwa uyakinifu matendo ya ukahaba ya Bwana Fukua. Ingawa alikuwa na umri mkubwa na diwani, alitumia maneno matamu kama sukari kuendeleza ukahaba kwa wasichana wachanga na mabibi za watu. Sitiari hiyo pia imetumika kuangazia uozo uliopo katika jamii, ambapo desturi na mila za kijamii zinazohimiza kudumishwa kwa heshima na mipaka ya mahusiano ya kimapenzi kati ya wazazi na watoto zimekiukwa. Kwa mujibu wa mtafiti, mtindo wa kishairi la kitarbia umetumika kwa ufasaha kuwasilisha sitiari ya kiafya *Baba- sukari* katika kuangazia tabia ya Bwana Fukua.

### 5.4 Barua

Arege na Chacha (2023) wanaelezea barua kama utungo ulio na muundo wenye anwani na tarehe ambao mtu humwandikia mwingine kuhusu suala fulani. Barua hutumika kama mtindo wa mawasiliano baina ya binadamu. Kulingana na nadharia ya Umitindo, matumizi bora ya mbinu za sanaa hufanikisha uwasilishaji wa habari kwa njia inayoeleweka (Leech, 1969). Kwa jinsi hii mtindo wa barua ya kirafiki umetumika bora katika kuwasilisha baadhi ya sitiari za kiafya katika vitabu teule vya fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Kupitia matumizi ya barua ya kirafiki, wandishi wa barua zilizomo katika matini teule walipitisha ujumbe kuhusu masuala ya kiafya kwa njia ya kiurafiki iliyokuwa na uwezo wa kunasa makini ya hadhira. Aidha, barua ya kirafiki humpa mwandishi uhuru wa kuwasilisha mawazo yake kwa mtindo unaomrusu kuangazia masuala kama vile kujuliana hali na maudhui mbalimbali kulingana na dhamira yake. Aidha, Arege na Chacha (keshatajwa) wanaelezea kuwa mtindo wa kutumia barua rasmi humfunga mwandishi katika mada fulani rasmi, huwa na toni rasmi na huzingatia sifa ya ufupi. Kwa kuzingatia mawazo ya Mlaga (2017) kuwa nadharia ya Umitindo humwezesha mchanganuzi kuchunguza mitindo ya uwasilizaji wa kazi fulani ya kifasihi, mtafiti alisoma kwa kina barua katika matini teule huku akitathmini na kufafanua maneno na sentensi za kisitiari zilizotumika kusawiri masuala ya kiafya.

Mwandishi ametumia mtindo wa barua za kirafiki kuanzia mwanzo hadi mwisho wa matini teule *Nimefufuka* kuwasilisha sitiari za kiafya. Tathmini ya matumizi ya mtindo wa barua katika matini teule ni kwamba, barua ya kirafiki kama mbinu ya mawasiliano ina uwezo wa kuwasilisha masuala mbalimbali kama zifanyazo mbinu zingine za mawasiliano kama vile hadithi na ushairi. Pia, imebainika kuwa kwa kutumia mtindo wa kibarua mwandishi amefaulu kuwasilisha maudhui na dhamira yake kuhusu suala la afya kwa ufanisi, jambo linalopanua mawanda ya matumizi ya barua katika mawasiliano ya kinathari. Katika barua zilizotumika mwandishi ametumia aina mbili za sitiari za kiafya. Kundi la kwanza linahusu sitiari za kiafya zilizoangazia matatizo yaliyotokana na afya duni. Baadhi ya sitari hizo ni: *maisha* (sitiari inayowakilisha matatizo ya kiafya), *nyumba ya udongo* (sitiari inayowakilisha utupu wa maisha), *gofu* (taswira ya mtu mwenye afya duni), *jehanamu* na *safari* (sitiari zinazowakilisha matatizo ya kiafya) na *wapita njia* ( sitiari inayowakilisha dhana ya kifo). Mhusika Sikitu na Upendo walitumia sitiari hizo katika barua zao ili kusisitiza uzito wa matatizo yaliyotokana na changamoto za kiafya. Kundi la pili la sitiari za kiafya zinaangazia mafanikio yaliyotokana na uimarishaji wa viwango vya afya katika jamii. Mifano ya sitiari hizo ni kama vile *Nimefufuka,* ambayo pia imetumika katika jalanda la kitabu kiteule. Sitiari *nimefufuka* pia imetumika kuwakilisha ufufuo na mwamko mpya katika kukabiliana na matatizo ya kiafya. Vilevile, sitiari ya kiafya ya *matunda:* imetumika kuwakilisha uponyaji. Sitiari hizo zimetumika kuwapa moyo waathiriwa wa kiafya kwamba, kulikuwa na matumaini ya kuishi ikiwa mbinu mwafaka za kuimarisha viwango vya afya zingezingatiwa.

### 5.5 Mshikamano wa Kisimulizi

Kwa mujibu wa Wamitila (keshatajwa) mshikamano wa kisimulizi ni jambo la kimsingi katika kazi ya fasihi na hudhihirika wakati ambapo matukio hufuata kaida ya usababishi. Matukio hayo hufuatana kimantiki na huwa na muwala. Kimsingi, Wamitila (keshatajwa) anasema kuwa kazi ya fasihi inastahili kuwa na mshikamano wa matukio ili kuwe na umoja katika kazi moja. Kwa kuongozwa na nadharia ya Umitindo, mtafiti amedhihirisha ya kwamba waandishi wa vitabu teule wamezingatia mtindo wa mshikamano wa kisimulizi katika utunzi wa matini teule na uwasilishaji wa sitiari za kiafya. Hii ni kulingana na Ingangasi (1988) kuwa, matumizi ya nadharia ya Umitindo katika kuchanganua kazi za kifasihi humwezesha mchanganuzi kuelewa lugha

iliyotumika katika kazi za kifasihi. Mlaga (2017) anachangia kwa kusema kuwa, katika uchanganuzi wa matini za kifasihi mchambuzi anachunguza mitindo iliyotumika katika uwasilishaji wa kazi kwa kutathmini sura ya nje ya matini, aina za sentensi na lugha iliyotumika na namna maneno yanavyoweza kuzalisha sentensi zenye maana mbalimbali.

Katika kitabu kiteule *Siku ya Ukimwi* sitiari za kiafya *kiuno cha nyigu*, *nambari 8*, na *mtoto wa watu* zimewasilishwa kwa kuzingatia mtindo wa mshikamano wa kisimulizi. Ili kuwasilisha sitiari ya kiafya *kiuno cha nyigu*, *nambari nane* na *mtoto wa watu,* mwandishi ameanza kwa kueleza maandalizi yaliyofanywa kabla ya siku ya Ukimwi kuwadia. Matukio hayo yalifuatana kiusababishi hadi pale ambapo mhusika mkuu Kadogo alipoalikwa kuhutubia hadhira. Baada ya Kadogo kujitokeza ndipo mwandishi alipotumia sitiari za kiafya kueleza maumbile wake. Tazama Kielelezo 4:

> Kadogo alipoalikwa kuhutubia watu, alichomoka kutoka kwa umati wa watu. Alitembea kwa mwendo wa taratibu na kwa ukakamavu wa hali ya juu. Watu walimpigia makofi na vigelegele vya kumshangilia. Akapanda jukuani huku ameivaa tabasamu usoni. Kadogo alikuwa msichana mrembo kweli.
>
> Alikuwa na *kiuno cha nyigu*. Mwili wake kwa ujumla uliandika *nambari 8*. Alikuwa nadhifu. *Mtoto wa watu* alikuwa ameumbwa akaumbika. Haungeamini alikuwa na virusi vinavyosababisha ugonjwa wa UKIMWI. Baadhi ya watu walisikika wakiulizana kwa mshangao; ………(uk.6).

Tathmini ya maelezo ya Kielelezo 4 ni kwamba, mwandishi amezingatia kaida ya usababishi na mtindo wa mshikamano wa kisimulizi katika matumizi ya sitiari za kiafya zilizoangaziwa katika dondoo hili. Kabla ya kutumia sitiari za kiafya *kiuno cha nyigu*, *nambari 8* na *mtoto wa watu*, mwandishi alitumia mtindo wa maelezo kuangazia jinsi Kadogo alivyoanza kuamka, kutembea na jinsi halaiki ya watu ilivyompokea. Matukio hayo yanafuatana kimantiki na kiusabishi kabla ya kuamwangazia kwa kutumia sitiari za kiafya.

Mtindo wa mshikamano wa kisimulizi pia umetumika kuwasilisha sitiari za kiafya katika matini teule *Pendo katika Shari*. Mwandishi ametumia mtindo huo kuwasilisha sitiari za kiafya mbalimbali. Baadhi ya sitiari zilizowasilishwa kwa kuzingatia mtindo huo ni: *Tambara* (uk.2), ‘*Danger*’ (uk.13), *Jongoo* (uk.13), *Safari* (uk.32) na *kombora*

(uk.50). Kwa mfano, kabla ya mwandishi kutumia sitiari ya kiafya *kombora*, aliangazia kimantiki mfuatano ya matukio yaliyotangulia na kusababisha tukio lililoangaziwa kama *kombora*. Kulingana na muktadha wa matumizi *kombora* ni sitiari ya kiafya iliyotumika kuwakilisha ugonjwa wa UKIMWI. Sulubu aliambukizwa ugonjwa huo na viruka njia aliojiunga nao mitaani. Kabla ya Sulubu kuambikizwa UKIMWI matukio yafuatayo yalitokea: Sulubu alianza tabia ya kujivinjari na wasichana wa mitaani na kuwasili nyumbani usiku, Sulubu kujiunga na marafiki walevi kama vile Makelele, Sulubu kuvunja ndoa yake na kumuoa Rehema, Pendo kugundua kuwa aliambukizwa UKIMWI na Sulubu na kuanza kuugua, Sulubu kuugua na kutafuta ushauri wa daktari, ujumbe kutoka kwa daktari kuwa Sulubu aliugua UKIMWI (*kombora*). Kwa msingi huu, sitiari ya kiafya *kombora* inayowakilisha UKIMWI imewasilishwa kwa kutumia mtindo wa mshikamano wa kisimulizi. Vilevile, Pendo anajilinganisha na *tambara* kwa sababu ya kuachwa na kuteswa na Sulubu. Katika muktadha wa matumizi tambara ni sitiari ya kiafya inayowakilisha afya duni. Tendo la Sulubu la kumuacha Pendo lilisababisha Pendo kujichukulia kama kiumbe dhaifu kilichokaribia hatima ya maisha yake. Pia, Sulubu na Makele walimwita Matano *jongoo* kwa sababu ya tendo lake la kukataa kujiunga nao katika uzinzi. Walitumia sitiari ya kiafya *jongoo* kumsawiri kama kapera, ilhali Matano alikuwa akiheshimu utu wake. Tathmini ya matukio haya ni kwamba, yametokea kimantiki na kwa kuzingatia kanuni ya kiusababishi na sitiari za kiafya zilizotumika zimewasilishwa kwa mtindo wa mshikamano wa kisimulizi.

Mwandishi wa matini teule *Kosa la Marehemu* pia amewasilisha sitiari za kiafya kwa kutumia mtindo wa mshikamano wa kisimulizi. Katika ukurasa wa 6, mwandishi ametumia sitiari ya kiafya *jipu* kuwakilisha uchungu uliotokana na habari kuhusu maambukizi ya UKIMWI. Tendo la wazazi wa Mshindo la kumficha habari kuhusu ugonjwa aliougua nduguye lilisababisha Mshindo kupeleleza na hatimaye kufahamu ugonjwa huo. Hivyo, Mshindo aliamua kufichua ugonjwa huo kama njia ya kuwaadhibu wazazi wake. Vilevile, sitiari ya kiafya *mifupa iliyolala* imetokana na matendo kadhaa yaliyoangaziwa katika matini teule. Kwanza, sitiari hii ina mantiki kwa sababu ilitokea katika mazingira ya hospitalini. Baada ya Mshindo kutembelea wagonjwa hospitalini, walikutana na mazingira ya kuogofya ambapo wagonjwa wengi wa UKIMWI walionekana kuzindiwa na kuonekana kama wafu. Kutokana na

mazingira hayo, mwandishi alitumia sitiari ya kiafya *mifupa iliyolala* kurejelea wagonjwa wa UKIMWI.

Mtindo wa mshikamano wa kisimulizi pia umetumika katika matini teule *Nimefufuka,* na *Sitaki iwe Siri* kuwasilisha sitiari za kiafya kama vile *gofu* na *mwendawazimu*. Mwandishi wa matini teule *Nimefufuka* ametumia mtindo wa mshikamano kisimulizi kuwasilisha sitiari ya kiafya *gofu* kumsawiri Jose kama mtu ovyo, mwizi na mlevi. Tazama Kielelezo 5:

> Hakuna kileo ambacho Jose hajakitumia; sigara kubwa, sindano, miraa, muratina, chang'aa, kumi kumi, chibuku- vyote amevitumia. Ameingilia uhalifu wa kila aina; uporaji, ulaghai, ukahaba, ilimradi apate fedha za kununua vileo na kupumbaza akili zake.Vitu vya maana nyumbani vimeuzwa. Ameuza ile radio kubwa aina ya *Sony*. Ameuza runinga ya LG iliyokuwa ikituletea malimwengu ulimwenguni. Ameuza saraka na mitoto ya meza na kisha meza nzima. Zulia lilipapa bei tulipokuwa kondeni tunaisaka tija. Kondoo walioletwa na mjomba wametoweka. Idadi ya kuku, sufuria, sahani, bakuli, vijiko ni simulizi tu. Uraibu wa Jose unatisha. Si ajabu amebaki *gofu* la mtu (uk.14).

Mtindo wa mshikamano wa kisimulizi umedhihirika pale ambapo Sikitu ameangazia matendo kadhaa yanayofuatana kimantiki kusawiri tabia ya Jose. Kwanza ni mlevi shupavu aliyeathiriwa kiafya na mihadarati na pili ni mhalifu na mporaji wa mifugo na vifaa vya nyumbani. Kutokana na tabia hiyo Jose amedhoofika kiafya na mwandishi anamrejelea kama *gofu*.

Katika kitabu kiteule *Sitaki iwe Siri,* sitiari ya kiafya *mwendawazimu* imewasilishwa kwa kutumia mtindo wa kisimulizi kuangazia uchafu na uozo uliopo katika jamii. Kabla ya kutumia sitiari hii mwandishi amesimulia tabia ya wanafunzi ya kujitayarisha kwa kupiga meno mswaki, kuvalia sare na kujinadhifisha ili waende shule. Hata hivyo, Haki na Ukwa hawakufurahishwa na tabia ya Musa ya kutochana nywele na wakamhimiza azichane. Tazama Kielelezo 6:

> "Hujachana nywele aisee. Zinaonekana kama za *mwendawazimu*,"
> Ukwa alisema na wote wakaangua kicheko (uk.5)

Sitiari ya *mwendawazimu* iliyotumika katika Kielelezo 6 inawakilisha uchafu wa kiafya katika kiwango cha familia. Aidha, sitiari hiyo pia inawakilisha uchafu wa kiakili. Kwa mujibu wa Bi. Mwalonga chafu huo ungeondolewa tu kupitia elimu.
Tazama Kielelezo 7:

> Haya wajukuu wangu. Jitahidini na mhakikishe kwamba mmevisoma vitabu vyote ulimwenguni. Juhudi hizo zitakuja kuwasaidia siku za usoni. Mimi sitokuwepo siku hizo (uk. 6).

Tathmini ya matumizi ya mtindo wa mshikamano wa kisimulizi katika kuwasilisha sitiari za kiafya katika Kielelezo 7 ni kwamba, waandishi wa vitabu teule walifaulu kuzua taswira mbalimbali za masuala ya kiafya kimantiki na kwa njia inayonasa makini ya hadhira.

### 5.6 Majazi

Kulingana na Wamitila (keshatajwa), majazi ni mbinu ya kuwapa wahusika majina kulingana na tabia zao na humsaidia msomaji kuelewa tabia na wasifu wa wahusika kwa urahisi. Isitoshe, Wangari (2019) anashadidia kwa kusema kuwa mbinu ya majazi hutokea pale ambapo hulka za wahusika huambatana na majina waliyopewa. Hivyo, kwa jinsi majina huwa na maana fulani katika jamii, suala la matumizi ya majina hufungamanishwa na ushabihikweli wa kazi husika. Aidha, matumizi ya majazi katika fasihi humsaidia msomaji kuelewa tabia na wasifu wa wahusika kwa njia rahisi. Udhaifu tu uliopo katika matumizi ya mtindo huu ni kuwa, unamnyima msomaji nafasi ya kuhusika katika kuamua wasifu wa mhusika na kulazimika kukubali maoni ya mwandishi. Hata hivyo, kwa mujibu wa Leech (1969) ufanisi wa upashaji na uelewekaji wa ujumbe unafanikiwa tu ikiwa mbinu mwafaka za kisanaa za uwazilishaji ujumbe huo zitazingatiwa. Bright (1992) anafafanua mbinu hizo kama vile matumizi bora ya lugha na muktadha wa matumizi ya lugha hiyo. Kwa kuzingatia mawazo haya mtafiti amechunguza jinsi mbinu ya majazi imetumika kuwasilisha sitiari za kiafya katika vitabu teule vya fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Baada ya kuchanganua data, imebainika kuwa mbinu ya majazi imetumika kisitiari na kwa ufasaha kusawiri hulka za wahusika mbalimbali katika matini teule.

Katika matini teule *Madhila ya Bi. Shufaa* majina yafuatayo ya kimajazi yametumiwa na mwandishi kuwasilisha sitiari za kiafya.

### 5.6.1 Fukua

Kwa mujibu wa Mdee na wengine (2022) neno *Fukua* lina maana ya kuchimbua arthi kwa lengo la kufahamu na kutoa kilichofichwa. *Fukua* ni mhusika hasidi katika matini teule *Madhila ya Bi. Shufaa* aliyekuwa na utajiri mkubwa na pia diwani wa eneo la utawala la mji wa Mangelepa. Jina lake haswa lilikuwa Bwana Juma Majanja (uk. 9). *Fukua* ni jina la kimajazi alilopewa na wakazi wa Mangelepa kwa sababu ya tabia yake ya kufanya mapenzi kiholela na kila mwanamke aliyempata bila kujali umri wa wanawake hao wala misingi yao ya ndoa. Tazama Kielelezo 8:

> Jina lake kamili lilikuwa Bw. Majanja. Jina lake hilo la msimbo- *Fukua*, alipewa na wanakijiji kwa sifa yake ya ujasiri. Angeweza kuingia kila mahali bila uoga na hata kusema kile anachotaka kwa yeyote yule. Kwa ufupi, alikuwa njemba ya mtu….
>
> Mtu huyu alikuwa hapishi rinda. Alipenda kutembea na wasichana wadogo hasa wale wa shule za msingi na upili. Wengi walimwita *honey* na wengine *Sweetheart*. Alimuradi watu wengi walimuona kama *Sugar Daddy* (uk. 9).

Kulingana na muktadha wa matumizi katika Kielelezo 8, Fukua ni jina la kimajazi na pia sitiari ya kiafya lililotumika kurejelea tabia ya Bwana Majanja ya kunyemelea na kufanya mapenzi na wasichana wadogo wa shule na wanawake za watu, bila kujali cheo chake katika jamii, misingi ya umri wa wanawake hao, miiko na kanuni za kijamii wala maambukizi ya magonjwa ya zinaa. Tabia hiyo pia imechangia kuibuka kwa majina mengine ya kimajazi kama vile '*Honey', 'Sweetheart'* na '*Sugar Daddy'* ambayo pia ni ya kisitiari yaliyotumiwa kumrejelea mhusika Majanja. Kama ilivyoangaziwa katika dondoo, mtindo wa kimajazi umetumika kuwasilisha sitiari ya kiafya *Fukua*. Neno *Fukua* limeangaziwa katika utafiti huu kama sitiari ya kiafya inayowakilisha ukahaba. Ingawa Bwana Majanja alifahamu kuwa aliugua UKIMWI, alifanya mapenzi na wanawake mbalimbali na pia kuwaambukiza ugonjwa huo. Mwandishi anasema kuwa mhusika Fukua alifukua hata visivyofukuliwa. Tazama Kielelezo 9:

> Kwa bahati mbaya mtu huyu alipenda usherati. *Alifukua hata visivyofukuliwa*. Kwa upande mwingine, aliwanyemelea wake za wenyewe na hata mabanati Tumbitumbi (uk.12).

Maelezo katika Kielelezo 9 yanamsawiri Fukua kama mtu katili asiyejali umri, rika, wala mipaka ya ndoa alipoamua kujivinjari na wanawake, ndiposa alieneza ugonjwa wa UKIMWI kwa watu wengi.

### 5.6.2 Mama Safi

Wanakijiji wa Mangelepa walimwita Bi. Shufaa Mama Safi kutokana na tabia yake ya usafi. Alidumisha usafi wa kiwango cha juu ndiposa akapewa jina la kimajazi Mama Safi. Tazama Kielelezo 10:

> Katika kijiji cha Mangelepa, Mzee Idd alifahamika mno. Alifanikiwa kuwa na mke mwenye adabu na heshima. Watoto wake wawili, Amina na Zuhura, walikuwa kama mboni ya jicho lake. Aliwapenda si haba. Mkewe mzee Iddi aliyeitwa Bi. Shufaa, alijulikana mtaani kama *Mama Safi*. Mama huyu *alijiweka nadhifu kila wakati*. Akiongea, ungedhani anayapima maneno yake kwa uzani. *Nguo zake safi, msuko wake wa nywele wa matuta* uliomtofautisha kabisa na wanawake wengi kijijini (uk. 2).

Suala la usafi limeangaziwa kwa kina katika Kielelezo 10. Usafi ni miongoni mwa masuala mtambuko yanayoangaziwa katika jamii ili kuzuia changamoto za kiafya kama vile magonjwa (WHO, 2018). Kwa jinzi hii baada ya kuchanganua data, mtafiti amebainisha kuwa maneno *Mama Safi* ni sitiari ya kiafya iliyowasilishwa kikamilifu katika matini teule kwa kutumia mtindo wa kimajazi. Katika Kielelezo 10 Bi. Shufaa amesawiriwa kama mama nadhifu na kiwakilishi cha usafi katika kiwango cha kifamilia na kijamii. Ingawa jina lake kamili ni Bi. Shufaa, alibadikwa jina la kimajazi *Mama Safi* lililosawiri tabia yake ya usafi. Mama huyo pia ni kielelezo cha kuigwa na wtu katika jamii iliyokumbwa na magonjwa hasa UKIMWI na uozo wa kimaadili.

### 5.6.3 Bi. Shufaa

Kulingana na Mdee na wengine (2022) neno shufaa humaanisha msamaa ambao mtu aliyetenda kosa fulani hupewa baada ya kutubu. Hivyo, jina *Shufaa* ni la kimajazi na pia sitiari ya kiafya, kwa sababu limetokana na msamaha ambao *Mama Safi* alimwomba bwanake kwa kushiriki katika mapenzi kisiri na Bwana Fukua aliyemwambukiza UKIMWI. Tazama kilio cha Bi. Shufaa katika Kielelezo 11:

> “Waa…aa..nangu, mimi ni..ta..ku.fa…leo, lakini.. dumi..sh..e..ni uami..nifu maishani…mwe..nu,)” Bi. Shufaa alijaribu kuongea maneno yakawa yanakataa kutoka. Alipokuwa kasimama Mzee Iddi, machozi yakamtiririka kama mtoto mdogo. Mum..e wan.. g…u, ubaki sa…lama… Mimi na…ondo…ka. Watu nze…hao we…ne…tu na wa..pe..leke shule …mp..aka chuo..kikuu. Mi..mi Kina.choni.ua ni u..go.njwa wa U..ki..m..wi. kan..iamb..ukiza Bw. Fu..fff..kua, yul..e di..wa..ni,” kisha *Bi. Shufaa* akaangusha macho chini (uk. 24).

Mazungumzo katika Kielelezo 11 yanaangazia toba ya Bi. Shufaa kwa bwanake kabla ya kuaga dunia. Ingawa alificha siri kuhusu mapenzi yake na Fukua, mwishowe alikiri kwa kinywa chake kwamba Fukua ndiye aliyemwambukiza UKIMWI. Jina *Shufaa* limeainishwa kama sitiari ya kiafya kwa sababu limetokana na toba ya Bi. Shufaa kuhusu tendo la uzinzi alilofanya na lililomwambukiza ugonjwa wa UKIMWI.

### 5.6.4 Zuhura

Zuhura ni bintiye Bi. Shufaa na Bwana Iddi. Jina *Zuhura* ni la kiamajazi linalorejelea aina ya sayari inayong’aa na inayozunguka jua. Baada ya kifo cha Bi. Shufaa wanae *Zuhura* na Amani walijiunga na kampeni dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI. Walikuwa katika mstari wa kuhamasisha watu kuhusu athari za UKIMWI ulimwenguni. Tazama Kielelezo 12:

> Amina na *Zuhura* wakawa ni wasichana wa kupaa na kutua; leo Marekani kesho Uingereza. Walizunguka ulimwengu na kupigia debe athari za UKIMWI wa wasichana wa shule na wanawake kwa jumla; bidii yao ya mchwa ikawajengea sifa si haba! Hatimaye walijulikana kama ‘role models’- yaani vielelezo kutoka Afrika. Waliweza kuibua mbinu mwafaka za kuwasaidia mayatima, wale wanaoishi na wale walioathirika na virusi vya UKIMWI (uk.26).

Tathmini ya maelezo ya mwandishi katika Kielelezo 12 kuhusu tabia ya Amina na Zuhura ni kwamba, *Zuhura* ni jina la kimajazi na pia sitiari ya kiafya inayowakilisha vita dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI. Jinsi sayari inayojulikana kama Zuhura inavyotoa nuru, ndivyo Amani na Zuhura walivyozunguka kote ulimwenguni wakifunza watu kuhusu changamoto za UKIMWI na jinsi ya kukabiliano nazo. Hivyo, mafunzo ya Zuhura yakawa nguzo kuu katika vita dhidi ya UKIMWI. Kwa msingi huu *Zuhura* ni sitiari ya kiafya iliyowasilishwa kimajazi kuwakilisha vita dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI.

### 5.6.5 Sikitu

*Sikitu* ni jina la kimajazi linalomaanisha utupu. Ingawa jina hilo ni la kimajazi, pia limetumika kisitiari kusawiri umaskini uliokithiri katika familia ya *Sikitu*. Umaskini ni mojawapo ya visababishi vya changamoto za kiafya kama vile magonjwa ya utapia mlo na unyafuzi. Magonjwa hayo yanasababishwa na ukosefu wa madini na vyakula vya kutosha mwilini (WHO, 2003). Umaskini katika familia ya *Sikitu* ulisababisha Lena kutoroka nyumbani na kujiunga na ukahaba mjini Mombasa. Vilevile, Jose ambaye ni kakake *Sikitu,* alijiunga na matumizi ya mihadarati na kuanza kuiba vifaa vya nyumbani alivyouza kwa bei nafuu ili apate hela za kununua pombe. Kwa jinsi hii *Sikitu* ni jina la kisitiari lililotumika kuwakilisha umaskini na ukosefu wa lishe bora katika jamii ya *Sikitu*. Tazama Kielelezo 13:

> "Njoo shangazi njoo, njoo unisaidie, uniauni. Usiponipa ushauri haraka utakuja matanga kwetu, kwenu ulikozaliwa. Mengi yamenikumba na mbinu za kukabiliana nayo zimenitoweka. Nimekukimbilia kwa kuwa wewe ni zaidi ya shangazi, wewe ni rafiki na msiri wangu. Nimetegwa na kunaswa na maisha. Nitajaribu kukueleza hatua kwa hatua. Ukihisi nimechanganyikiwa, usinilaumu. Kwa kweli nimechanganyikiwa usiponishika mkono na kunielekeza, kunifariji, kuniinua, lolote la kunifika litanifika." (uk.1).

Maelezo katika Kielelezo 13, yanamsawiri *Sikitu* kama mhusika aliyekufa moyo na kukumbwa na utupu katika maisha. Anajihisi mnyonge na mtu aliyeathiriwa mno na matatizo mbalimbali kama vile yanayotisha kuangamiza uhai wake na hivyo kuomba usaidizi kutoka kwa shangazi yake. Tathmini ya mawazo haya ni kwamba, *Sikitu* ameumia kimawazo na kuathirika kiafya kiasi kwamba anajihisi si kitu. Utupu huu umetawala mawazo na mwili wake.

## 5.7 Tashtiti

Kwa mujibu wa Mbatiah (2001) tashtiti ni mbinu ya utunzi ambayo inatumiwa kushambulia maovu yaliyoko katika jamii na kasoro za kitabia kama vile uzandiki kwa kubeza na utani. Wamitila (2008) anashadidia kwa kusema kuwa, tashtiti ni mbinu ya kisanaa inayotumiwa katika kazi ya kifasihi kuangazia uozo au maovu katika jamii kwa lengo la kuchochea kero, hasira, chuki na hisia zingine hasi kuhusu jambo linalozungumziwa. Hata hivyo, Wamitila (keshatajwa) anasema kuwa tashtiti ina misingi ya kimaadili ambapo kinachoshambuliwa huchukuliwa kuwa kimezikiuka.

Ingawa tashtiti hudhamiria kufichua ouzo na ila za kitabia za binadamu, baadhi ya wahakiki pia hudahili kuwa inalenga kurekebisha maovu na tabia hasi za binadamu katika jamii. Marekebisho hayo hutekelezwa ipasavyo kupitia matumizi bora ya lugha na mbinu za mawasiliano kama vile sitiari, usimulizi miongoni mwa zingine. Pia, mtindo wa mawasiliano hufanikisha ujumbe unaopashwa na tashtiti iliyotumika. Kwa mujibu wa Leech (keshatajwa), mtindo unaotumiwa katika kazi ya fasihi ndio nyenzo kuu ambayo inatumiwa na mwanafasihi kupitisha habari kwa hadhira. Kwa msingi huu utafiti huu umebaini kuwa wandishi wa matini teule za Fasihi wa Watoto ya Kiswahili wametumia tashtiti kama mtindo wa kuwasilisha sitiari za kiafya. Miongoni wa sitiari zilizotumika ni:

### 5.7.1 Muhuri wa Mauti

Nadharia ya Umitindo inasisitiza haja ya vipengele mbalimbali vya kugha kufanya kazi kwa pamoja, ili kuwasilisha kikamilifu masuala yanaoangaziwa katika kazi ya kifasihi. Hivyo, ingawa *mhuri wa mauti* ni msemo, pia ni sitiari ya kiafya iliyowasilishwa kwa mtindo wa kitashtiti katika matini teule *Sitaki Iwe Siri* kuangazia hisia hasi za wanajamii kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Tazama Kielelezo 14:

> Ugumu wa kulijibu swali lenyewe ulitokana na msimamo wa jamii kuhusu maradhi yaliyowauwa wazazi wa wajukuu zake. *Maradhi yenyewe yalichukuliwa kuwa laana kubwa kwa jamii*. Kila aliyeugua maradhi haya alianza kuepukwa kama mgonjwa wa ukoma. Akaogopwa jinsi yanavyoogopwa mauti. Akabaguliwa na jamii. *Maradhi yenyewe yakachukuliwa kuwa ni muhuri wa mauti kwa kila aliyekumbwa na mkosi wa kuambukizwa* (uk.12).

Tathmini ya mazungumzo katika Kielelezo 14 ni kwamba, ugonjwa wa UKIMWI umeangaziwa kama laana na yeyote aliyeambukizwa alitengwa na wanajamii. Kinyume na imani hii, UKIMWI ni ugonjwa kama magonjwa mengine na waathiriwa wa ugonjwa huo wana haki ya kutangamana na kuishi na wanajamii wengine bila kubaguliwa. Kuendeleza ubagusi dhidi yao ni ukiukaji wa haki za binadamu jambo ambalo ni kinyume cha sheria. Vilevile, Ingawa UKIMWI hauna dawa kuathiriwa na ugonjwa huo sio *muhuri wa mauti* kwani lishe bora na matumizi ya dawa kulingana na ushauri wa daktari unapunguza makali na waathiriwa kuishi maisha ya kawaida.

Katika matini teule *Pendo katika Shari* mtindo wa kitashtiti pia umetumika kuwasilisha sitiari za kiafya zifuatazo:

### 5.7.2 Ngamia

Ngamia ni mnyama anayevumilia maisha magumu na anatumiwa katika safari za jangwani. Mnyama huyo ana uwezo wa kusafiri kwa muda mrefu bila kunywa maji. Katika kufahamu maana inayowasilishwa na maneno yaliyotumika katika kazi za fasihi, Mlaga (2017) anasema kuwa mwanaelimumitindo ana nafasi ya kuchunguza maana mbalimbali zinazowasilishwa na neno au sentensi moja. Kwa msingi huu sitiari ya *ngamia* imetumika katika matini teule kulinganisha masaibu ya Pendo mikononi mwa Sulubu na matatizo ambayo ngamia hupata jangwani. Kulingana na muktadha wa matumizi, *ngamia* ni sitiari ya kiafya iliyowasilishwa kitashtiti kuangazia maumivu ya kimawazo, kiafya na maovu mbalimbali ambayo Pendo alipitia mikononi mwa Sulubu. Maovu haya ni pamoja na kubezwa, kunyimwa mapenzi na kuteswa na Sulubu kwa sababu ya kuendelea kujifungua watoto wa kike pekee. Tazama Kielelezo 15:

> Pendo aliketi, machozi yakamtiririka kama *ngamia*. Alipenda makamasi, akamchukua mwanawe mchanga mikononi na kumtazama usoni. Mtoto alifungua macho na kumtazama. Pendo aliacha kulia ghafla kwani alihisi kama kitoto hicho kilikuwa kinamsihi asilie kwa kuwa huo haukuwa mwisho wa maisha yake. Siku hiyo Sulubu alirejea nyumbani saa tatu usiku. Alitarajia kumkuta mkewe kutokana na simu aliyopiga Pendo afisini mwake na kuacha ujumbe afike hospitalini kumchukua. Sulubu alipuuza ujumbe huo na kumpitia rafikiye Makelele kuenda kunywa pombe (uk.12).

Tathmini ya usemi katika Kielelezo 15 ni kwamba, sitiari ya *ngamia* imetumika kusawiri uvumilivu wa Pendo na mapenzi yake katika kudumisha amani na utulivu katika ndoa. Hata hivyo, Sulubu aliendelea kumnyanyasa Pendo kila wakati na ndoa yao ikakumbwa na matatizo chungu nzima. Pendo alishindwa kuvumilia matatizo hayo na ndoa kati yake na Sulubu ikasambaratika.

### 5.7.3 Jongoo asiyeweza kupanda Mtungi

Usemi huu ni sitiari ya kiafya kwa sababu ulitumiwa na Makelele kurejelea shughuli za ukahaba ambazo baadaye zilimwambukiza Sulubu UKIMWI. Pia, ni tashtiti ya ucheshi iliyotumiwa na Makelele kumkejeli mhusika Matano kwa lengo la kumshawishi kujiunga nao madanguroni. Tazama Kielelezo 16:

> Matano aliwashauri rafikize Sulubu na Makelele na kuwatahadharisha dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI uliokuwa ukiua watu kila uchao. Lakini hawa walimpuuza na kumwona kama *jongoo asiyeweza kupanda mtungi*. Walimsuta na kumwambia hajui maisha ni nini. "Wewe wajitia ushamba bwana. Unajifanya mshago. Hujui maisha ni mafupi na lazima ule raha kwani karaha yaja? *Vunja mifupa ikiwa bado meno ipo*," rafikiye mmoja alimwambia akiwa amezidiwa na nishai zake za ulevi (uk.13).

Matamshi katika Kielelezo 16 ni ya kitashtiti yanayoangazia maovu kama vile unywaji wa pombe, usherati na maisha ya anasa yaliyokuwa yakiendelea katika jamii. Ingawa Makelele na Sulubu walimsuta Matano kwa msimamo wake dhidi ya maovu hayo, Matano alisimama kidete na kushikilia msimamo wake jambo ambalo ni funzo kwa vigeugeu wanaofuata ovyo mawaidha ya marafiki zao. Kwa mujibu wa Highet (1962), wanatashtiti hutumia lugha wazi kuelezea ukweli unaochukiza ili waathiriwa wachukue hatua mahsusi kuepuka maovu yanayowakabili. Kwa kushikilia kauli hii, Matano anajitokeza kama kiwakilishi cha wanajamii wanaofahamu madhara ya maisha ya anasa na kuwakanya wenzake kujiepusha na tabia kama hizo. Tashtiti hii imetumika kuwasilisha sitiari za kiafya kama vile *jongoo asiyeweza kupanda mtungi* na *vunja mifupa ikiwa bado meno iko* kwa njia fasaha na inayosawiri maovu yanayoathiri jamii.

### 5.7.4 Pendo katika Shari

Hii ni sitiari kuu ya kiafya inayotawala kitabu kiteule *Pendo katika Shari*. Kitabu hiki pia ni cha kitashtiti kinachosawiri maovu yanayotokea katika ndoa nyingi katika jamii. Kulingana na Highet (1962) wanatashtiti hulenga kuelezea ukweli unaochukiza ili ukweli utambulike na kuchochea watu au wahusika kupinga na kuepuka maovu yanayoangaziwa. Kwa mujibu wa Leech (1969) uelewekaji wa ujumbe utafanikiwa tu ikiwa mwasilishaji ametumia lugha na mbinu mwafaka kupasha ujumbe wake, jambo ambalo limetumika kwa ufasaha katika matini teule *Pendo katika Shari*.

Baadhi ya maovu yaliyoangaziwa katika matini teule na yanayosababisha mizozo katika jamii ni taasubi za kiume, dhuluma za kijinsia, matumizi ya pombe na kutowajibika katika ndoa. Masuala haya yameangaziwa kwa mtindo ulio wazi ili kurahisisha uelewekaji wa ujumbe unaowasilishwa. Mhusika mkuu Sulubu anakiuka majukumu yake nyumbani na kujiunga na ulevi na virukanjia mitaani kwa kizingizio kuwa mkewe hajifungui mtoto wa kiume. Hiki ni kinaya kwa kuwa Pendo hakuwa na

uwezo wa kujiamulia jinsia ya mtoto ambaye angezaliwa. Sulubu alitumia suala hilo kama kizingizio cha kutowajibika kama mume nyumbani na kujiunga na ulevi na hatimaye kumuoa Rehema ambaye pia alijifungua mtoto wa kike. Hili lilikuwa funzo kwa jamii kuwa, mwanamke hakuwa na uwezo wa kuamua jinsia ya mtoto ambaye angezaliwa. Aidha, matini hii inapiga msasa mila na desturi za kijamii zinazokuza ubabedume na kumsawiri mwanamke kama chombo cha kutawaliwa na mwanaume jinsi anavyopenda. Kilele cha masaibu hayo ni Sulubu na Upendo kuambukizwa UKIMWI na kusambaratika kwa ndoa yao. Tazama Kielelezo17:

> Pendo alianza kuyahakiki maisha yake na Sulubu kwa uangalifu, na *kuyaona kama ndoto asiyopenda kuiota tena*. Hii ni kwa sababu ya uovu aliomfanyia yeye na wanawe. Upendo wake kwa dhati kwa Sulubu uligeuka na kuwa *shari isiyostahimilika*. Hapo awali alidhani mapenzi yaliashiria raha pekee. Lakini sasa alielewa kwamba mapenzi ya dhati hayapeperushwi na dhiki au mateso ya dunia. Huzidi kunawiri pale yanapokumbwa na dhoruba za maisha... Aidha, alifahamu kuwa pendo lake kwa mumewe hal ikuwa na masharti kwa sababu hata baada ya kumpa maradhi ya moyo na ya mwili pia kamwe hakuacha kumthamini. Alielewa fika kwamba mapenzi ya dhati kama yale hayawezi kuyeyuka dhidi ya shari za dunia (uk.65).

Ingawa Sulubu alimtesa Pendo na kumwambukiza maradhi ya UKIMWI, maelezo katika Kielelezo 17 yanadhihirisha upendo wa kweli wa Pendo. Pia, maelezo hayo yanaangazia mafunzo muhimu kwa njia ya kitashtiti kuwa matatizo ya kindoa yana madhara chungu nzima kama vile kuathirika kiafya, vifo na migongano katika jamii ambayo yanapaswa kuepukwa. Isitoshe, madhila ya Pendo ni funzo kuwa kulikuwa na haja ya kudumisha mapenzi ya kweli, uaminifu na uwajibikaji kati ya bibi na bwana. Vilevile, ni funzo kwa wapenzi kuwa mapenzi pia hunawiri palipo na dhiki na ni jukumu la kila mhusika katika ndoa kuwajibika ipasavyo.

### 5.7.5 Siku ya UKIMWI

Katika matini teule *Siku ya Ukimwi*, mtafiti amebaini kuwa *Siku ya UKIMWI* ni miongoni mwa sitiari za kiafya zilizowasilishwa kwa kutumia mtindo wa kitashtiti kuangazia janga la UKIMWI. Mwandishi amewasilisha suala la UKIMWI kitashtiti na kwa kutumia lugha ya kisitiari ili aweze kupasha ujumbe kuhusu ugonjwa wa UKIMWI kwa njia inayokubalika katika jamii. Hii ni kwa sababu baadhi ya wanajamii huona haya kuhusishwa na UKIMWI. Kobia (2008) anadhihirisha haya anaposema kuwa, ni

mwiko katika baadhi ya jamii kuhusishwa na UKIMWI na ni muhimu kutumia mtindo mbadala na unaokubalika kama vile lugha ya kisitiari kuangazia suala hilo.

Kabla ya kuangazia maovu yanayohusishwa na janga la UKIMWI, mwandishi ameanza kwa kuelezea siku murua ya maadhimisho ya UKIMWI iliyokuwa imepambwa kwa mbwembwe na nyimbo za kila aina. Madhari hayo yanaangazia taswira ya furaha, na ya kupendeza. Vilevile, mwandishi amechagua wahusika kama vile Kadogo kwa makini ili kunasa makini ya hadhira na kuondoa mielekeo hasi kuhusu UKIMWI kabla ya kuzungumzia ugonjwa huo. Baadaye mhusika mkuu alijitokeza na kuzunguzia changamoto za UKIMWI na umuhimu wa kukabiliana nazo. Kilele cha maadhimisho hayo yalikuwa ni mafunzo kuhusu njia za kuepuka na kukabiliana na maradhi ya UKIMWI. Kama anavyosema Highet (1962) kuwa tashtiti hulenga kuangazia maouvu kwa lengo la kurekebisha, mwandishi wa matini teule ametumia wahusika kama vile Kadogo na Daktari kueleza visababishi vya UKIMWI pamoja na njia mbalimbali za kukabiliana na matatizo hayo (uk.7-19). Baadhi ya sitiari zingine za kiafya zilizowasilishwa kwa mtindo wa kitashtiti ni *shamba* (uk.8), *mahindi mabichi* (uk. 8) na *sumu* (uk.8).  Tathmini ya uwasilishaji wa sitiari za kiafya katika kitabu kieule kwa kutumia mtindo wa kitashtiti ni kwamba, mwandishi amefaulu kutumia mtindo huo kuangazia matatizo yanayotokana na UKIMWI na jinsi ya kukabiliana nayo.

### 5.8 Taswira

Kwa mujibu wa Wamitila (keshatajwa) taswira ni dhana inayotumiwa kuelezea neno au maelezo yanayounda picha fulani akilini mwa msomaji. Taswira hizi zinaweza kuwa za ki- ishara au kimaelezo. Arege na Chacha (2023) wanaafikiana na ufafanuzi huu na kuongezea kuwa, picha ambazo zinajengwa akilini mwa msomaji hutokana na maelezo ya lugha ya kitamathali ambayo mwandishi ametumia katika kazi ya kifasihi. Baada ya kuchanganua data, mtafiti amegundua kuwa waandishi wa matini teule wametumia taswira mbalimbali kama mtindo wa kuwasilisha sitiari za kiafya.

#### 5.8.1 Taswira za Magonjwa

Kwa mujibu wa Wamitila (2008) uchambuzi wa taswira unapaswa uchunguze mtindo wa picha za kiakili katika kujenga hali fulani. Kwa msingi huu mtafiti amegundua kuwa sitiari za kiafya mbalimbali za magonjwa zimewasilishwa kitaswira katika matini teule

*Kosa la Marehemu*. Mshindo anasimulia jinsi wazazi wake walivyoathirika kiakili na kiafya kwa sababu ya kugonjeka kwa mtoto wao. Maelezo hayo yanaangazia taswira ya magonjwa ya kimwili na kiakili yaliyodhoofisha afya ya wazazi wake. Tazama Kielelezo 18:

> Pia, alisimulia namna wazazi wake walivyozungumza kichinichini na *kukosa nyuso za furaha.* Kila siku zinavyozidi kwenda ndivyo furaha inazidi kupotea na wanaendelea kusononeka (uk. 3).

Kielelezo 18 kinaangazia taswira ya afya duni na huzuni iliyowakumba wazazi wa Daudi baada ya kugundua kuwa afya ya mwanao Daudi ilikuwa ikidorora kila siku. Taswira hiyo pia inadhihirisha kauli kuwa ingawa mtu hajaambukizwa na UKIMWI basi pia ameathirika kutokana na maambukizi ya wapendwa wao.

Vilevile, sitiari ya kiafya *macho yaliyokuwa makavu* imewasilishwa kitaswira na mwandishi ili kuwakilisha afya duni ya wagonjwa wa UKIMWI. Tazama Kielelezo 19:

> Mara yule mgonjwa akafumbua macho na kuwatazama. Mshindo na Janga walisimama wasijue la kufanya. Mili yao ilikuwa kama imekufa ngazi. *Yule mgonjwa aliwaangalia bila kupepesa macho. Jinsi alivyokonda na macho yake yaliyokuwa makavu alionekana kama mfu* (uk.28).

Taswira ya mtu aliyekonda kiasi kwamba alionekana mfu imesawiriwa katika Kielelezo 19. Kupitia picha hiyo sitiari ya kiafya *macho yaliyokuwa makavu* imewasilishwa kuwakilisha ugonjwa wa UKIMWI.

Vilevile, mtindo wa kitaswira pia umetumika kuwasilisha sitiari ya kiafya *mzee*. Katika muktadha wa matumizi sitiari *mzee* imetumika kuwakilisha athari za magonjwa. Athari hizo ni kudhoofika kiafya na kuvunjika moyo. Tazama Kielelezo 20:

> Sura ya baba yake ilikuwa imekunjamana na alionekana mchovu sana. Macho yalionekana mekundu na Mshindo alihisi kama baba yake amekuwa *mzee* zaidi muda ule. (uk.45).

Magonjwa husababisha madhara mbalimbali katika mwili wa binadamu. Baadhi ya athari hiz kama vile uchovu na macho mekundu yameangaziwa katika Kielelezo 20.

Katika matini teule *Madhila ya Bi. Shufaa* taswira ya mpanzi imetumika kuwasilisha sitiari ya *mbegu chafu* inayowakilisha ugonjwa wa UKIMWI. Mwandishi ameangazia taswira ya mpanzi ambaye anapanda mbegu za aina mbalimbali katika shamba kwa lengo la kuvuna. Hata hivyo, mpanzi aliyesawiri katika kitabu kiteule ni hasidi anayesambaza ugonjwa wa UKIMWI kiholela. Haya yamesawiriwa katika Kielelezo 21:

> Hodi hodi hazikuisha. Bw. Fukua alikuwa na kiu cha wanawake. Kinywa kilikuwa na makali kama ya nyembe. Pale mtaani tayari alikuwa na jamii kama sio jamaa. Kila nyumba alipanda mbegu, tena mbegu chafu. (uk. 11).

Maelezo katika kielelezo 21 yanaangazia taswira ya aina ya mtu mwenye tamaa ya wanawake kiasi kwamba hangelinganishwa na mtu wa kawaida. Alikuwa na sifa zilizokiuka zile za binadamu wa kawaida kama vile ukali katika kunyemelea wanawake, kufanya ngono za kiholela na wanawake mbalimbali na kusambaza UKIMWI. Baadhi ya sitiari za kiafya zilizowasilishwa kwa kutumia taswira hii ni: *Fukua*, *kiu* na *mbegu chafu*.

Vilevile, hali ya kiafya ya Bi. Shufaa imesawiriwa kitaswira kwa kuelezea umbo lake la nje ambalo lilitisha na kuogofya. Mwandishi anaangazia picha ya mwanamke aliyekonda na aliyelinganishwa na *ng'onda*. Tazama Kielelezo 22:

> Mama akapewa kila aina ya tiba na wala hakuna dawa iliyokubali mwili………. Akawa wa kuingizwa na kutolewa. Ikafika wakati ambapo Bi. Shufaa Anakuangalia hakuoni! Amekonda na kukondeana. Si sindano si ng'onda, si mtu si kifyefye. Kivuli cha mtu lingekuwa jina bora zaidi. (uk.23).

Taswira ya mtu mnyonge, aliyekonda sana kiasi kwamba asingetambulika kama mtu wa kawaida imeangaziwa katika Kielelezo 22. Kutokana na kukonda kwake alilinganishwa na *ng'onda*. Kwa jinsi matini teule inahusu Fasihi ya Watoto, taswira hii inaafikiana na kauli ya Wamitila (2008) kwamba, fasihi yoyote inayomlenga mtoto inapaswa kuwa na uwezo wa kuibua taswira fulani kama vile uoni, harufu, mwendo au mguso. Katika utafiti huu taswira iliyoangaziwa hapo awali imetumika kuwasilisha sitiari ya kiafya *ng'onda* mbayo ni ya uoni.

Katika kitabu kiteule *Sitaki Iwe Siri* taswira ya ugonjwa wa UKIMWI kama Zimwi linaloangamiza maisha ya binadamu imeangaziwa katika uk.45. Yuri ambaye ni mhusika mnyonge na aliyeathirika kiafya kutokana na magonjwa, ameambukizwa UKIMWI ambao unadhamiria kuangamiza maisha yake.Tazama Kielelezo 23:

> Ingawa wahenga walisema kuwa *Zimwi* likujualo halikuli ukakwisha, hili lililompata Yuri wakati wa pitapita zake kwenye majumba ya starehe liliapa kumumaliza mara moja. Lilihakikisha kuwa Yuri alipitisha siku zake katika sayari hii itwayo dunia kwa kasi ambayo hakuitarajia (uk.45).

Mazungumzo katika Kielelezo 23 yamesawiri ugonjwa wa UKIMWI kama *Zimwi* ambalo limeamua kuangamiza maisha ya Yuri. Taswira hii imetumika kuwasilisha sitiari ya kiafya *Zimwi* inayowakilisha ugonjwa wa UKIMWI. Kulingana na muktadha wa matumizi UKIMWI umelinganishwa na *Zimwi* kwa jinsi ugonjwa huo hauna tiba na hatima yake ni kifo. Kama inavyodaiwa na UNAIDS (2023) ugonjwa wa UKIMWI ndio huathiri binadamu zaidi na kuna haja ya kuhamasisha watu dhidi ya madhara ya ugonjwa huu.

Taswira ya kombora imetumiwa kuwakilisha ugonjwa wa UKIMWI katika matini teule *Pendo katika Shari* (uk.50). Kulingana na TUKI (2004) *kombora* ni aina ya zana za kivita zinazorushwa na kulipuliwa kwa kutumia mizinga. Zana hii ina uwezo wa kuangamiza na kusababisha maafa katika eneo kubwa. Katika muktadha wa matumizi *kombora* ni sitiari ya kiafya inayowakilisha ugonjwa wa UKIMWI. Ulinganifu huu unaashiria ya kwamba, UKIMWI ni ugonjwa hatari sana na una uwezo wa kuangamiza kizazi kizima ikiwa hatua za dharura hazitachukuliwa kuuzuia. Ulinganifu huu pia unatoa tahadhari kwa wanajamii dhidi ya kujiunga na mienendo inayoambukiza UKIMWI.

### 5.8.2 Taswira za Kifo

Kwa mujibu wa Nyandiwa (2015) fani za lugha kama vile sitiari huchangia katika kuibua maana katika kazi ya kifasihi. Hata hivyo, ni muhimu kutumia fani za lugha kikamilifu ili kuibua maana kamili. Haya yamesisitizwa na Leech (1969) aliposema kwamba, matumizi bora ya mbinu za kisanaa hufanikisha uwasilishaji na uelewekaji wa ujumbe unaopashwa kwa hadhira. Katika utafiti huu, mtafiti amechunguza na kubainisha sitiari mbalimbali za kiafya ambazo zimewasilishwa kitaswira na zinazoangazia suala la kifo. Katika kitabu kiteule *Madhila ya Bi. Shufaa* sitiari ya kiafya

*mito ya machozi* imewasilishwa kwa mtindo huu kuangazia kifo cha Bi. Shufaa. Amina na Zuhura walipofahamu kuwa mama yao alikuwa anaaga dunia, waliangua kilio kiliowaadhiri kiafya hadi wakawa na matatizo ya kuongea. Tazama Kielelezo 24:

> "Mmmm…hhhhhh…mama…eeeh. Mama usituache…mama usife mamam. .aa. Mmmhhh…Mama,mama..mamaa..ngu." Amina na Zuhura walilia sana hata ikawa hawawezi kuongea tena. Sauti zikawakauka. Wakalala sakafuni. Kisha Amina akauparaga ukuta huku akilia kwa nguvu. Ilikuwa balaa bin beluwa. *Mito ya machozi* ikaanza kutiririka. *Ikakusanya kidimbwi kikubwa Cha maji, karibu kuunda ziwa* (uk.24).

Kielelezo 24 kinaangazia taswira ya watoto wanaolia, wanyonge na waliovunjika moyo kutokana na kifo cha mama mzazi imeangaziwa. Pia, kifo kinaangaziwa kama suala tata lililopita uwezo na fahamu za binadamu. Sitiari ya kiafya *mito ya machozi* iliyowasilishwa kitaswira inawakilisha unyonge na kushindwa kwa binadamu katika kuzuia kifo. Aidha, *kidimbwi cha maji* ni sitiari ya kiafya inayoangazia kifo kama fumbo ambalo ni vigumu kwa binadamu kulielewa wala kulifumbua. Ingawa Amina na Zuhura waliathiriwa na kifo cha mama yao, hawakuwa na la kufanya ila kukubali na kuendelea na maisha. Jambo muhimu linalojitokeza ni kwamba matatizo ya kijamii kama vile vifo vya wazazi huathiri watoto zaidi kiafya na kitabia. Hivyo, masuala yanayotatiza maendeleo ya kijamii kama vile mapenzi ya kiholela yanayosababisha magonjwa yanapaswa kuepukwa.

Mlaga (2017), anaelezea umuhimu wa nadharia ya Umitindo katika kuchanganua kazi ya kifasihi kwa kusema kuwa, inamsaidia mhakiki kutathmini mtindo uliotumika katika kazi fulani na kutoa kauli ikiwa mtindo huo unafaa au la. Hivyo, baada ya kuchanganua mtindo wa uwasilishaji wa sitiari za kiafya katika matini teule *Sitaki Iwe Siri,* imebainika kuwa baadhi ya sitiari hizo zimewasilishwa kitaswira na kwa njia inayofaa. Katika uk.12 mwandishi ameangazia taswira ya mgonjwa wa UKIMWI aliyetengwa na jamii na kuchukuliwa kama mfu asiyepaswa kuhusishwa na binadamu walio hai. Taswira hiyo imetumika kuwasilisha sitiari ya kiafya *muhuri wa mauti* iliyotumika kuwakilisha dhana ya kifo. Tazama Kielelezo 25:

> Maradhi yenyewe yalichukuliwa kuwa ni laana kubwa kwa jamii. Kila aliyeugua maradhi haya alianza kuepukwa kama mgonjwa wa ukoma. Akaogopwa jinsi yaogopwayo mauti. Akabaguliwa na jamii. Maradhi

> yenyewe yakachukuliwa kuwa ni *muhuri wa mauti* kwa kila aliyekumbwa na mkosi wa kuambukizwa (uk.12).

Taswira ya athari za ugonjwa wa UKIMWI imeangaziwa katika Kielelezo 25. Maradhi hayo yamesawiriwa kama kiwakilishi cha mauti. Yeyote aliyeambukizwa UKIMWI alichukuliwa kama mfu.

### 5.8.3 Taswira za Uzinzi

Uchanganuzi wa data katika utafiti huu umedhihirisha kuwa taswira za uzinzi kadhaa zimetumika kuwasilisha sitiari za kiafya katika baadhi ya vitabu teule.

Katika matini teule *Siku ya Ukimwi* mhusika mkuu Kadogo ametumia sitiari ya kiafya *alifanya aliyofanya nami* kurejelea tendo la ngono alilofanya alipokunywa pombe. Hali hii inadhihirika kupitia usimulizi wake unaoangazia taswira ya msichana mlevi chakari na aliyepoteza fahamu. Tazama Kielelezo 26:

> " Baada ya kunywa pombe iliyokuwa kali sana, nililewa chakari. Tulipiga maji hadi usiku wa manane. Mimi nilikuwa bendera ya kufuata upepo. Nilipolewa nililala fofofo. Nikajisahau. Sikujua nilikuwa wapi. Nikaingia Katika chumba kimoja. Mmoja wa wavulana aliingia chumbani humo. *Alifanya aliyofanya nami*. Haikuwa hiari yangu. Niligundua haya baadaye usiku. Nilipoteza ubikira wangu." (uk.13).

Kielelezo 26 kinaangazia taswira ya msichana mlevi asiyekuwa na uwezo wa kujiamulia. Anajilinganisha na bendera inayofuata upepo tabia ambayo ilimtumbukiza katika maambukizi ya UKIMWI. Kadogo ametumia sitiari ya kiafya *alifanya aliyofanya nami* ili kuepuka lugha kali ya kawaida kurejelea tendo la ngono. Kama anavyosema Kobia (2008), lugha ya kisitiari hutumika kurejelea masuala yaliyochukuliwa kuwa mwiko katika jamii ili kupunguza makali yanayotokana na lugha ya kawaida. Ni muhali kutaja tendo la ngono hadharani hivyo uamuzi wa mwandishi wa kutumia lugha ya kisitiari. Simala (2000) anaafikiana na kauli hii na kusema kuwa, lugha ya kisitiari inapaswa kutumiwa kwa makini ili kukidhi majukumu ya lugha katika mawasiliano. Kwa jinsi hii taswira ya Kadogo kama msichana mlevi imetumika vyema kuwasilisha sitiari za kiafya *bendera* na *alifanya aliyofanya nami*.

Kitabu kiteule *Pendo katika Shari* pia kimesheheni taswira mbalimbali za uzinzi zilizotumika kuwasilisha baadhi ya sitiari za kiafya za uzinzi. Mifano ya sitiari za kiafya zilizowasilishwa kwa kutumia mtindo huu ni "*danger*" na *jongoo*. Gari la Sulubu lilipachikwa jina "*danger*" kutokana na tabia yake ya kulitumia kubeba wasichana mitaani kwa lengo la kufanya mapenzi. Tazama Kielelezo 27:

> Mara nyingi baada ya kazi, gari jekundu la Sulubu lilionekana likitambaa mitaani na kuondoka na wasichana mbalimbali. Kwenye mitaa hiyo, watu walizoea kuona gari lile, walilipachika jina na kuliita "*danger*" kwani walijua mwenye gari hilo alikuwa hatari kwa kuwateka bakunja wasichana mitaani humo (uk.13).

Gari la Sulubu limesawiriwa kama mnyama anayetambaa mfano wa nyoka katika Kielelezo 27. Hali hii inaangazia taswira ya wingine, ambayo Wamitila (2003) analielezea kama aina ya picha inayotumiwa kama msingi wa kulitenga au kulibagua kundi fulani la watu katika jamii. Kwa jinsi hii Sulubu amesawiriwa kama kahaba anayetumia kila mbinu kuwarai wasichana kufanya ngono naye bila kujali hali yao ya kiafya. Hatua hiyo inasababisha watu kurejelea gari lake kama "*danger*". Katika muktadha wa matumizi "*danger*" ni sitiari inayorejelea hatari. Hatari hiyo inatokana na mapenzi ya kiholelela yanayoweza kusababisha kuambukizwa na ugonjwa wa UKIMWI. Ni muhimu kwa kila mtu kuwa mwaminifu ili kuepuka maambukizi ya UKIMWI. Tabia ya Sulubu ya kubeba wasichana wa mitaani kwa gari lake kwa lengo la kufanya mapenzi ni hatari kwake na kwa wasichana hao kwa sababu ya kuambukizwa UKIMWI.

Mtindo wa kitaswira pia umetumiwa katika matini teule kuwasilisha sitiari ya kiafya *jongoo* (uk.13). Sulubu na Makele wanamlinganisha Matano na *jongoo* ambaye ni mnyama asiyekuwa na mifupa, mwenye umbo nyororo ulio na vijisehemu vyenye jozi ya miguu kila kimoja na asiyekuwa na mifupa. Katika muktadha wa matumizi neno *jongoo* limetumika kurejelea kuishiwa na nguvu za kufanya ngono.

Kulingana na nadharia ya Umitindo ni lazima vipengele vya kimtindo vifanye kazi kwa pamoja ili kazi ya kifasihi iweze kuchanganuliwa kikamilifu. Kauli hii imedhihirishwa katika matini teule *Madhila ya Bi. Shufaa* ambapo mwandishi ametumia mbinu ya majazi kisitiari kuzua taswira mbalimbali. Katika kitabu kiteule, mwandishi anamlinganisha mhusika mkuu Majanja na mnyama anayefukua ardhi ili apate kitu

fulani. Kutokana na tabia hiyo anamwita Bwana Majanja jina la kimajazi *Fukua*. Mwandishi anaangazia taswira ya mnyama kama vile chindi anayefukua mbegu iliyopandwa shambani. Kupitia taswira hii mwandishi amefaulu kuwasilisha sitiari ya kiafya *Fukua,* ambalo pia ni jina la kimajazi lililotumiwa kurejelea tabia ya Majanja ya ukahaba. Tazama Kielelezo 28:

> Kwa bahati mbaya, mtu huyu alipenda usherati. *Alifukua hata Visivyofukuliwa*. Kwa upande mwingine, aliwanyemelea wake za wenyewe na hata mabanati tumbitumbi. Kwa Bi. Shufaa alianza kujenga hema. "Hallo my *honey* Maria, mambo vipi?"Bw. *Fukua* alimtolea Maria salamu (uk.12).

Bi. Shufaa pia aliitwa Maria. Mifano ya sitiari za kiafya katika Kielelezo28 inadhibitisha jinsi mwandishi alivyofaulu kuwasilisha sitiari za kiafya *Fukua* na "*honey"* kwa ufasaha kwa njia ya kitaswira. "*Honey"* pia ni sitiari ya kiafya iliyotumia katika usemi huo kurejelea tendo la ngono.

Taswira ya msichana katili na kahaba imeangaziwa katika matini teule *Kosa la Maehemu*. Kupitia taswira hiyo, sitiari za kiafya *buzi* na *alikuwa mguu hatui akapumzika* zimetumika kusawiri tabia ya Lena ya kufanya ngono na wanaume wa kila aina bila kujali kabila wala afya yao. Tazama Kielelezo 29:

> Inadaiwa Lena alijishindia "*buzi*" jingine la kigeni aliloandamana nalo ng'ambo. *Alikuwa mguu hautui akapumzika*. Aliporejea nchini baada ya miezi miwili, alikuwa amebadilika kwa hali na mali (uk.6).

Mwandishi katika Kielelezo 29 ametumia jina 'buzi' kurejelea mwanaume aliyekuwa na Lena. Kwa mujibu wa Mdee na wengine (2022) mbuzi ni mnyama wa kufugwa. Hivyo buzi ni ndume mkubwa na hupiga kelele anapomwona mbuzi jike. Mwandishi ametumia jina hilo kuangazia taswira ya mwanaume aliyepatana na Lena. Katika muktadha wa matumizi, sitiari ya kiafya *buzi* imetumika kusawiri mwanaume mnene na kahaba. Vilevile, Lena amerejelewa pia kama mwanamke asiyetulia na aliyekuwa katika harakati za kutafuta wanaume madanguroni. Kwa ujumla dondoo hili linasawiri mazingira ya uzinzi na ya kuogofya, ambapo wanaume na wanawake wamejitumbukiza katika lindi la anasa na ukahaba bila kujali umri, kabila wala maambukizi ya magonjwa ya zinaa.

### 5.9 Chuku

Wamitila (2003) anaelezea chuku kama mbinu ya kifasihi inayotumiwa katika hali ya kuikuza sifa ya kitu au jambo fulani kuliko kawaida. Anaelezea kuwa lengo kuu la kutumia chuku katika mawasiliano, ni kusisitiza sifa fulani ili kuchimua masuala fulani katika kazi husika. Arege na Chacha (2023) wanashadidia kwa kusema kuwa chuku hutumiwa katika kutilia chumvi, ambapo jambo dogo linaweza kuelezewa hivi kwamba linaonekana kuwa kubwa sana au kubwa kuonekana kuwa dogo.

Mbinu ya chuku imetumika kuwasilisha sitiari kuu ya kiafya *Sitaki Iwe Siri* katika matini teule *Sitaki Iwe Siri*. Mtindo huo umetumika kufichua siri ambayo Mwalonga alificha wajukuu wake kwa muda mrefu. Kiini cha kufichua siri hiyo kilitokana na hatua ya Musa ya kuangazia suala la UKIMWI katika barua yake *Sitaki Iwe Siri*. Kisadfa barua hiyo ililenga kuhamasisha jamii kuhusu haja ya kuweka wazi suala la UKIMWI, ingawa hakujua siri waliyofichwa na Mwalonga ilihusu ugonjwa wa UKIMWI uliowauwa wazazi wao. Tazama Kielelezo 30:

> Nyanya aliposikia neno UKIMWI likitajwa, moyo wake ulianza kwenda kazi. Akamkazia Musa macho yaliyojaa imani huku machozi yakimlengalenga. Alikumbuka jinsi maradhi hayo yalivyowaua wazazi wa wajukuu zake. Alikuwa ameweka *siri* sababu ya vifo vya wazazi wa akina Musa. Lakini Siri hufichuliwa na muda. Miaka kumi baadaye, Musa alikuwa anafichua ukweli huo kwa kuandika insha yenye mada, *Sitaki Iwe Siri* ingawa kwa hakika hakujua ukweli huo (uk.50).

Mbinu ya chuku imetumika katika Kielelezo 30 kiustadi kuwasilisha sitiari ya kiafya *Sitaki Iwe Siri* hivi kwamba, msomaji anafahamu hisia za uchungu zilizomwathiri Mwalonga.

Mwandishi wa kitabu kiteule *Siku ya Ukimwi* pia ametumia mbinu ya chuku kunasa makini ya hadhira na baadaye kufaulu kuwasilisha sitiari mbalimbali za kiafya zinazoangazia janga la UKIMWI. Tazama Kielelezo 31:

> Kadogo alipoalikwa kuhutubia watu, alichomoka kutoka kwa umati wa watu. Alitembea kwa mwendo wa taratibu na kwa ukakamavu wa hali ya juu. atu walimpigia makofi na vigelegele vya kumshangilia. Akapanda jukuani huku ameivaa tabasamu usoni. Kadogo alikuwa msichana mrembo kweli kweli. Alikuwa na kiuno cha *nyigu*. Mwili wake kwa ujumla uliandika *Nambari 8*. Alikuwa nadhifu. *Mtoto wa*

> *watu* alikuwa ameumbwa akaumbika. Haungeamini alikuwa na virusi vinavyosababisha ugonjwa wa UKIMWI (uk.6).

Usemi katika Kielelezo 31 umetumika kuangazia urembo wa Kadogo. Kadogo amesawiriwa kama msichana mrembo kiasi kwamba ilikuwa vigumu kuhusishwa na UKIMWI. Watu wanasema, "Hata huyu mrembo hivi, kweli anaugua UKIMWI?" (uk.6).

Hii ilikuwa onyo kwamba umbo la nje pekee halingetumika kuthibitisha maambukizi ya UKIMWI. Kulingana na (WHO, 2018) njia pekee ya kudhibitisha maambukizi ya UKIMWI ni kukaguliwa na maafisa wa kiafya hospitalini. Miongoni mwa sitiari za kiafya zilizowasilishwa kwa kutumia mbinu ya chuku ni *nyigu*, *nambari 8* na *mtoto wa watu*.

Chuku pia imetumika kuwasilisha sitiari za kiafya katika matini teule *Pendo katika Shari* kwa lengo la kusisitiza jambo linalozungumziwa. Katika uk.7 mbinu hii imetumika kuonyesha namna mapenzi kati ya Sulubu na Pendo yalivyofifia kiasi kwamba kila mmoja alidhamiria kuishi kiviake. Tazama Kielelezo 32:

> Maisha kati ya Sulubu na Pendo yalizidi kuwa na tafrani nyingi, mapenzi kati yao yakaanza kutoweka mithili ya umande kwenye jua. Kwa Pendo Sulubu alibakia *mume jina tu* (uk.7).

Mtindo wa chuku pia umetumiwa katika Kielelezo 32 kusisitiza kutowajibika kwa Sulubu kama mume katika jamii. Alikiuka kutekeleza majukumu yake yote na kubakia *mume jina tu* kutokana na kudorora kwa mapenzi kati yao. Sitiari ya kiafya *mume jina* imewasilishwa kiustadi katika muktadha huo.

Hatua ya Sulubu ya kukiuka majukumu yake na kujiunga na ukahaba inamtumbukiza katika janga la UKIMWI. Ingawa alijigamba kuwa hangeweza kuambukizwa na ugonjwa huo mwishowe alijipata hospitalini akitafuta matibabu. Tazama Kielelezo 33:

> Huku akiwa na hadhari kubwa, Sulubu alimfahamisha Daktari taabu yake na kusudio lake la kutaka afanyiwe uchunguzi. Alipokuwa akimweleza hayo, Daktari Hamisi alimtazama kwa macho ambayo Sulubu *alihisi yaliangaza hadi moyoni mwake, mpaka kwa damu yake na kuona Umati wa virusi vya UKIMWI ukishambulia chembechembe za damu Iliyositiri uhai wake* (uk.50).

Mbinu ya chuku imetumika katika Kielelezo 33 kuangazia athari ya virusi vya UKIMWI ambavyo Sulubu alihisi kuwa vilinuia kumuua. Virusi hivi vimesawiriwa kama aina ya mnyama mkali anayeshambulia adui bila huruma. Kupitia matumizi ya chuku, sitiari ya kiafya *umati wa virusi vya UKIMWI ukishambulia chembechembe za damu* imewasilishwa kikamilifu kuwakilisha athari za ugonjwa wa UKIMWI.

Mwandishi pia ametumia chuku kuangazia suala la kifo katika kitabu kiteule *Pendo katika Shari*. Analinganisha maafa mengi yanayotokana na maradhi ya UKIMWI na jinsi ambayo nyota hupotea machoni mwa watu kwa sababu ya wingi wa mwangaza wa jua. Ingawa nyota huonekana usiku ni nadra kuzionya mchana kwa sababu ya nuru ya jua. Sitiari za kiafya zilizowasilishwa kwa kutumia mbinu ya chuku ni *kitanzi* na *watu wanavyopotea* zinazowakilisha dhana ya kifo. Tazama Kielelezo 34:

> Wewe una wapenzi chungu nzima na wengine huwajui hata majina yao. Kwa hivyo, huwezi kujua ni yupi atakayekuambukuza maradhi baadaye. eo una Amina, kesho kwa cheupe, kesho kutwa kwa Rosa. Huoni unajitia *kitanzi*? Unajua UKIMWI unaua maelfu ulimwenguni lakini unafikiri wewe huwezi kuwa mmoja wa hao maelfu. Tazama humu nchini, kwa mfano jinsi *watu wanavyotoweka* mithili ya nyota katika nuru ya jua (uk.30).

Mwandishi ametumia chuku katika Kielelezo 34 kuonyesha matendo maovu ya Sulubu. Amesawiriwa kama kahaba asiyejali maambukizi ya magonjwa ya zinaa, ingawa anafahamu kuwa watu wanaaga dunia kutokana na magonjwa hayo.

Mbinu ya chuku imetumika katika matini teule *Nimefufuka* kusawiri maisha kama safari ambayo ina matatizo chungu nzima. Safari hiyo inastahili msafiri awe na uvumilivu na kujitolea ili aweze kuikamilisha. Tazama Kielelezo 35:

> Mpwa wangu umeshuhudia mwenyewe, maisha ni *safari* ndefu, safari ya kupanda na kushuka, iliyojaa shari na shwari, asali na shubiri. Usione waja wanacheka ukadhani daima dawamu wana raha. Kitanda usichokilalia hujui kunguni wake (uk.17).

Sitiari ya *safari* imetumika katika Kielelezo 35 kusawiri mchakato wa maisha. Usemi huu ni aina ya chuku inayoangazia makali yaliyomo katika maisha kama vile magonjwa, mateso na hata vifo.

### 5.10 Methali

Njogu na Chimerah (1999) wanafafanua methali kama tamko ambalo linaelezea wazo la busara la binadamu kwa ufupi. Wanaelezea sifa za methali kama vile ufupi, kuwa na vina na mizani na mara nyingine kuwepo na takriri. Tathmini ya maelezo haya ni kwamba methali ni ushairi uliofupishwa. Wamitila (2008) anapiga hatua zaidi na kuhusisha methali na utamaduni wa jamii fulani. Anasema kuwa methali ni semi zilizo na muundo maalumu na zinazofahamika, kukubalika na hupokezanwa katika jamii. Pia, anadai kuwa methali nyingi huwa na umbo la kisitiari, jambo linaloshughulikiwa katika kazi hii. Fafanuzi hizi zote zinaoanishwa na ufafanuzi wa Arege na Chacha (2023) wanaoelezea methali kama utungo mdogo wa fasihi simulizi, unaotumiwa kuelezea ukweli fulani ulio na maana pana na unaoweza kufasiriwa kwa namna tofautitofauti kulingana na muktadha. Methali mbalimbali zimetuka kuwasilisha sitiari za kiafya katika baadhi ya vitabu teule vya fasihi ya Kiswahili ya Watoto.

Katika matini teule *Nimefufuka* Sikitu analinganisha udhaifu wake wa kiafya na nyumba ya udongo ambayo haiwezi kustahili kitu kizito au mtetemo. Anatumia methali ya kiafya, "*Mie nyumba ya udongo sihimili vishindo*," (uk.3) ambayo ni ya kisitiari inayolinganisha maisha na nyumba ya udongo ambayo inaweza kubomoka wakati wowote. Methali hii ni sitiari ya kiafya inayoangazia umuhimu wa mtu kutunza afya yake na kuepukana na mienendo na mambo yanayoweza kudhuru afya yake.

Kadogo ambaye ni mhusika mkuu katika matini teule *Siku ya UKIMWI* anazungumzia madhara yaliyompata baada ya kukaidi mawaidha ya wazazi na kujiunga na vijana watdu. Anatumia methali ya kisitiari kama kisengere nyuma kuonya vijana dhidi ya tabia ya mapenzi ya kiholela ambayo matunda yake ni kilio na majuto. Tazama Kielelezo 36:

> Nina majuto makuu. Lakini *majuto ni mjukuu huja baadaye*. Ninawausia vijana, usifanye mapenzi hadi uolewe (uk.13).

Katika dondoo la Kielelezo 36 methali "*majuto ni mjukuu huja baadaye*" ni ya kisitiari na imetumika kulinganisha tabia mbaya na majonzi ambayo hufuata baadaye. Katika muktadha wa mazungumzo, Kadogo analinganisha hamu ya kutenda maovu na majuto ambayo humpata mhusika baadaye.

Mwandishi wa matini teule *Madhila ya Bi. Shufaa* ametumia methali kisitiari "*mchezea chuma huchuma, kama hakuchuma tumbo hunguruma"* (uk.13), kama kisengere mbele kuangazia masaibu yaliyomngoja Bi. Shufaa kutokana na matendo yake maovu. Kwa mujibu wa King'ei na Ndalu (2011), maana ya ndani ya methali hii ni kwamba, kila kazi huwa na mafao la sivyo humletea anayeifanya dhiki. Baada ya kuchanganua data mtafiti amebaini kuwa, methali hiyo ni ya kiafya iliyotumika kuangazia athari za ugonjwa wa UKIMWI zilizompata Bi. Shufaa baada ya kushirika ngono na Fukua.

### 5.11 Hitimisho

Kwa ujumla, mtafiti ameshugulikia lengo la pili la utafiti lililolenga kuchunguza mtindo uliotumika kuwasilisha sitiari za kiafya katika matini teule za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Baada ya uchanganuzi wa data imebainika kuwa mitindo mbalimbali imetumika kuwasilisha sitiari za kiafya. Baadhi ya mitindo hiyo ni mshikamano wa kisimulizi, nyimbo, ushairi, barua, tashtiti, majazi, chuku na methali. Ingawa mitindo mbalimbali ilitumika, hii tu ndiyo ilishughulikiwa katika utafiti huu kwa sababu ya muda mfupi wa utafiti. Tathmini ya mtafiti ni kwamba, mitindo hiyo ilitumika kwa ufasaha kuwasilisha masuala ya kiafya yaliyoangaziwa katika matini teule. Hata hivyo, kila mwandishi alitumia mitindo iliyomfaa kulingana na muktadha na masuala aliyolenga kuwasilisha.

# SURA YA SITA

# MASUALA MTAMBUKO YALIYOWASILISHWA NA SITIARI ZA KIAFYA KATIKA VITABU TEULE

## 6.1 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti aliongozwa na nadharia ya sitiari ya dhana katika kushughulikia lengo la tatu la utafiti lililohusu ufafanuzi wa masuala mtambuko yaliyowasilishwa na sitiari za kiafya katika vitabu teule. Mihimili ya nadharia hiyo iliyoongoza uchanganuzi huu ni: Sitiari hurahisisha uelewa wa dhana fulani kupitia matumizi ya taswira zinazoleta ukaribu wa kihalisia na ukweli unaokubalika kuhusu suala linalozungumziwa. Mihimili kuwa matumizi ya lugha ya kisitiari yanarahisisha uelewa wa masuala changamano na yanayochukuliwa kuwa mwiko katika jamii, pamoja na kuwa mawasiliano ya kisitiari yalikuwa na nguvu ya kuvuta na kunasa makini ya hadhira na kuathiri misimamo yao kuhusu suala fulani ilifaa mno utafiti huu. Mtafiti alifafanua aina za masuala mtambuko kama vile UKIMWI, dhuluma za kijinsia na dawa za kulevya kama yalivyosawiriwa katika matini zilizoteuliwa. Mengine yaliyochunguzwa ni visababishi vya UKIMWI na jinsi ya kukabiliana na ugonjwa huo, dhuluma za kijinsia na namna ya kuzitatua, aina za dawa za kulevya na athari zake na namna ya kukabiliana nazo.

Kwa mujibu wa Mdee na wengine (2022) dhana ‘mtambuko’ hutumika kurejelea suala fungamano au jambo fulani linalohusisha jamii. Ufafanuzi huu unaafikiana na wa Arege na Chacha (2023) ambao wanaelezea suala mtambuko kama suala la kijamii, ambalo linaweza kuwa jipya au la zamani na lililo na nafasi muhimu katika maisha ya wanajamii. Kisawe cha suala mtambuko ni ‘suala ibuka.’ Njogu (2007) ana maelezo sawa na hayo kwa jinsi anavyofafanua dhana ya masuala ibuka kama masuala mtambuko. Anasema kuwa suala ibuka ni dhana inayorejelea masuala yaliyozuka na yanayoathiri jamii kama vile UKIMWI, ukiukaji wa haki za watoto, dhuluma za kijinsia, mazingira na matumizi ya mihadarati miongoni mwa mengine. Tathmini ya ufafanuzi huu ni kwamba, kuna ukuruba katika maana ya suala mtambuko na suala ibuka. Hata hivyo, dhana ‘mtambuko’ imetumiwa katika utafiti huu kurejelea masuala yanayoiathiri jamii na yaliyoangaziwa katika matini teule kama vile UKIMWI, dhuluma za kijinsia na dawa za kulevya.

Kulingana na Lloyd (2010), msukumo wa kushughulikia masuala yanayoathiri watoto ulitokana na mkutano ulioandaliwa mjini Monrovia (1989) na Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika, uliotia waandishi motisha ya kuandika kuhusu masuala ya watoto. Hivyo kwa mujibu wa Ngugi (2016), Wizara ya Elimu nchini Kenya ilipendekeza kufundishwa kwa masuala mtambuko katika shule za msingi na sekondari katika mwaka wa 2002. Ngugi (keshatajwa) anahimiza dhima ya kushughulikia masuala mtambuko kwa kusema kuwa, ulimwengu wa sasa umekumbwa na masuala mapya kama vile mazingira, afya na siasa yanayoathiri maisha ya binadamu kama vile mazingira na afya na hayangeweza kuachwa bila kushughulikiwa katika uandishi wa fasihi. Kwa msingi huu, masuala mtambuko yaliyobainishwa na kuchanganuliwa katika vitabu teule vya fasihi ya Kiswahili ya Watoto ni ugonjwa wa UKIMWI, dhuluma za jinsia na dawa za kulevya.

## 6.2 UKIMWI

Kama ilivyoangaziwa katika sura ya nne ya utafiti huu, sitiari mbalimbali za kiafya kama vile *kombora* na *moto* zimetumiwa kurejelea UKIMWI, kwa minajili ya kuonyesha hatari inayoambatanishwa na ugonjwa huo. Katika kufanikisha haya, nadharia changanuzi ya sitiari ya dhana imetumika kufafanua maana mbalimbali inayowasilishwa na sitiari hizo. Kwa mujibu wa nadharia hiyo, matumizi ya sitiari hurahisisha uelewa wa masuala changamano kama vile UKIMWI kwa njia ya kiulinganishi. Kwa msingi huu, sitiari ya kiafya *kombora* imetumika kulinganisha UKIMWI na zana ya kivita inayotekeleza hasara na maafa inapolipuka. Mlipuko wa zana hiyo pia husababisha moto. Moto ni hatari kwa jinsi unavyochoma kila kitu. Sitiari hizi zinachora taswira ya UKIMWI kama ugonjwa hatari ulio na uweza wa kusababisha maafa kwa binadamu kwa sababu hauna tiba. Katika mtini teule, Ugonjwa wa UKIMWI umesawiriwa kama janga la kimataifa linaloathiri afya ya wanajamii na kutatiza kuafikiwa kwa maendeleo endelevu ulimwenguni. Hii imedhihirishwa na ripoti ya UNAIDS (2023) inayosema kuwa, jumla ya watu milioni thelathini na nane na mia nne elfu wameambukizwa ugonjwa huo. Aidha, Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO, 2018) linasema kuwa, ingawa mashirika ya kiafya ulimwenguni na mataifa yaliyoendelea kama vile Marekani yanatia bidii kukabiliana na changamoto za UKIMWI, janga hilo limeendelea kusambaa na kuathiri maisha ya binadamu ndiposa linalinganishwa na kombora na moto. Vilevile, juhudi za kuafikiwa kwa maendeleo

endelevu pia zimetatizwa kutokana na afya duni ya wafanyikazi walioambukizwa UKIMWI.

### 6.2.1 Visababishi vya Ugonjwa wa UKIMWI

Uchanganuzi wa data katika matini teule umebainisha njia zifuatazo zinazosababisha ugonjwa wa UKIMWI:

#### 6.2.1.1 Mila na Desturi za Jamii

Kwa mujibu wa Kobia (2008), ni mwiko kuhusishwa na UKIMWI katika baadhi ya jamii. Hali hiyo imedhihirishwa katika matini teule *Sitaki Iwe Siri*, ambapo Bi. Mwalonga alikataa kuwafahamisha wajukuu wake kuhusu ugonjwa wa UKIMWI uliowaua wazazi wao, licha ya kuwa na hamu ya kuujua kwa sababu ya tamaduni hasi za jamii zilizohusisha UKIMWI na laana.

Tazama Kielelezo 1:

> Nyanya Mwalonga alipata taabu sana kulijibu swali hilo. Ugumu wa kulijibu swali lenyewe *ulitokana na msimamo wa jamii kuhusu maradhi yaliyowaua wazazi wa wajukuu zake. Maradhi yenyewe yalichukuliwa kuwa laana kubwa kwa jamii*. Kila aliyeugua maradhi haya alianza kuepukwa kama mgonjwa wa ukoma (uk.12).

Taswira ya mwelekeo hasi wa jamii dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI imeangaziwa katika Kielelezo 1, ambapo mtindo wa kitaswira umetumika kuonyesha hatari iliyoambatanishwa na UKIMWI. Ili kufasiri kwa kina athari za ugonjwa wa UKIMWI, nadharia changanuzi ya sitiari ya dhana imetumika kuchanganua matini teule kwa sababu inafaa zaidi kuangazia masuala changamano kama vile UKIMWI yanayochukuliwa kuwa mwiko katika jamii. Kwa jinsi hii, tathmini ya uchanganuzi wa data katika kitabu kiteule umedhihirisha ya kwamba, UKIMWI ulichukuliwa kama laana kwa yeyote aliyeathiriwa na ugonjwa huo. Walioathiriwa walitengwa na kunyimwa haki za kimsingi kama vile uhuru wa kutangamana na wengine, hali inayoathiri mshikamano wa kitaifa.

Katika matini teule *Pendo katika Shari*, ukaidi wa Sulubu kwa familia yake kunadhibitisha mitazamo hasi ya wanajamii kuhusu visababishi vya ugonjwa wa UKIMWI. Ingawa Sububu alikuwa ameelimika, alishikilia mwelekeo hasi wa kijamii kuwa UKIMWI ulikuwa ugonjwa wa wanawake. Tazama Kielelezo 2:

> Sulubu aliuliza Daktari, “Umeniita kuniambia juu ya magonjwa ya wanawake?” (uk.23).

Tathmini ya usemi katika Kielelezo 2 ni kuwa mila na desturi za kijamii ziliathiri pia wasomi. Watu waliokuwa na elimu na wasiokuwa nayo walishikilia msimamo kuwa, UKIMWI ulikuwa ugonjwa wa wanawake na wanaume hawangeathiriwa na ugonjwa huo. Hivyo, mielekeo hasi iliyotiwa nguvu na mila na desturi za jamii pia zilichangia katika maambukizi na kusambaa kwa ugonjwa wa UKIMWI.

#### 6.2.1.2 Tamaa ya Pesa na udanganyifu katika Ndoa

Vilevile, uchanganuzi wa data katika matini teule ya *Madhila ya Bi. Shufaa* umedhibitisha ya kwamba, tamaa ya pesa na ukosefu wa uaminifu katika ndoa pia huchangia katika maambukizi na maenezi ya ugonjwa wa UKIMWI. Bi. Shufaa aliyejulikana pia kama ‘Mama Safi,’ anadhihirisha haya kwa jinsi alivyobadilisha tabia yake kwa sababu ya tamaa ya pesa. *Mama Safi* ni jina la kimajazi na pia sitiari ya kiafya alilopewa Bi. Shufaa kwa sababu ya mtindo wa kuwa safi na tabia nzuri. Sitiari *Mama Safi* inawakilisha taswira ya afya nzuri. Bi. Shufaa alijiweka nadhifu pamoja na familia yake. Hata hivyo, mhusika Fukua aliweza kutumia pesa kumshawishi abadili tabia nzuri na mama huyo akasaliti uaminifu wake katika ndoa. Katika muktadha huu Fukua ni kiwakilishi cha afya duni. Kuanguka kwa Bi. Shufaa katika mtego wa Bwana Fukua wa kumuhusisha katika mapenzi nje ya ndoa ulikuwa pigo kubwa katika familia ya Iddi. Ingawa mama huyo alipata mapenzi na chochote alichokitamani kutoka kwa bwanake, tamaa ya pesa ilimtumbukiza katika janga la UKIMWI. Aliambukizwa UKIMWI na Bwana Fukua aliyekuwa diwani wa Mangelepa. Ilikuwa tabia ya Fukua kutumia pesa kuwarai wanawake kufanya mapenzi nao.

Tazama Kielelezo 3:

> *Baada ya kugundua kwamba njama zake zimeanza kugonga mwamba, basi aliamua kutumia pesa*. Mzee Iddi humwachia mke wake shilingi mia mbili kwa siku kwa ajili ya matumizi ya nyumbani (uk.12).
>
> Bw. Fukua huja na kumwachia Bi. Shufaa magora ya khanga zenye maandishi yanayovutia. *Magora hayo ya leso yakawa ndio asali ya moyo wa “Mama Safi.”*Ama kwa kweli mchezea chuma huchuma, kama hakuchuma tumbo hunguruma (uk.13).

Mazungumzo katika Kielelezo 3 yanasawiri uwezo wa pesa katika kubadilisha tabia ya mtu. Baada ya Fukua kushindwa kumshawishi Bi. Shufaa kuingiliana naye kimapenzi, aliamua kutumia pesa na rasilimali alizokuwa nazo. Alianza kutumia lugha ya kiushawishi na kumnunulia Bi. Shufaa magora ya leso na huo ukawa mtego uliomnasa mama huyo. Matumizi ya lugha ya kiushawishi yanaafikiana na nadharia changanuzi ya sitiari ya dhana kwamba, mawasiliano ya kisitiari yana uwezo wa kuathiri msimamo wa mtu kuhusu suala fulani. Kwa jinsi hii, Bwana Fukua alitumia lugha ya kimapenzi iliyokuwa na uwezo wa kumvuta Bi. Shufaa na akaghairi msimamo wake dhidi ya kufanya mapenzi nje ya ndoa. Katika matini teule msemo *asali ya moyo* umetumika kisitiari kuonyesha kushindwa kwa Bi. Shufaa kujitenga kimapenzi na Bwana Fukua. Inachora taswira ya mwanamke aliyeathiriwa na mapenzi kiasi cha kusaliti Bwana yake kwa sababu ya tamaa ya pesa. Tunaarifiwa kuwa magora ya leso yalikuwa kama *asali* katika moyo wa Bi. Shufaa. Ingawa bwanake alijitahidi kukimu mahitaji ya nyumbani kwa kumwachia Bi. Shufaa shilingi mia mbili kila siku, tamaa ya pesa ilimshawishi kuhusika kimapenzi na Bwana Fukua bila kujali maambukizi ya magonjwa ya zinaa wala kuvunjika kwa ndoa yake. Tazama Kielelezo 4:

> Matukio hayo yote yalitokea *baada ya tamaa ya pesa kuingia hadi katika mishipa yake ya damu. Bi. Shufaa akawa hatulii tena mpaka ampate Fukua*. Tabia ya Juma Majanja ilipiku fikra nzuri na mafunzo mema aliyokuwa nayo Bi. Shufaa. Kile ambacho hakufahamu ni kwamba Bwana Fukua alikuwa mgonjwa wa UKIMWI. *Nduli huyo alitumia pesa na magora ya khanga kumshawishi Bi. Shufaa ili kufanya naye mapenzi kinyume na kanuni za ndoa*. (uk.15)

Kulingana na maelezo katika Kielelezo 4, hapo awali Bi. Shufaa hakuwa na tamaa ya mali wala kuhusika katika mapenzi nje ya ndoa. Alikuwa mama aliyetosheka na hali ya maisha aliyokuwa akiishi. Pia, Bi. Shufaa alikuwa mwanamke aliyeheshimika katika kijiji cha Mangelepa kwa sababu ya mienendo na tabia nzuri, lakini alianguka katika mtego wa uzinzi kwa sababu ya tamaa ya pesa. Hii ni tahadhari kwa watu walio katika ndoa ya kwamba, ushawishi wa pesa una uwezo wa kuathiri na kuvunja taasisi ya ndoa. Tathmini ya uchanganuzi wa data katika utafiti huu ni kwamba, kulikuwa na haja ya Bibi na Bwana kuwa waminifu katika ndoa na kujadiliana kwa uwazi masuala yanayowaathiri ili mapenzi kati yao yaweze kudumu. Hatua ya Bi. Shufaa ya kumficha bwanake mahusiano ya kimapenzi na Fukua yalichangia katika kuendelea kwa mapenzi kati yake na Fukua. Ingawa Bwana Fukua aliambukiza wanawake ugonjwa wa

UKIMWI, hakuonyesha dalili zozote za kuwa na ugonjwa huo. Alikuwa mbebaji. Tazama Kielelezo 5:

> Haini mwanzilishi wa maafa haya Bwana Juma Majanja hakuwahi kuonekana hata mazishini. Mtu huyu, Fukua, aliishi na virusi lakini *hakuugua UKIMWI*. Diwani huyu *alikuwa mbebaji tu, yaani alikuwa 'carrier.*' *Watu wa sampuli hii ndio hufanya maisha ya wengine kuwa adha tupu. Hawana dalili za ugonjwa wowote lakini huwa pana uwezekano wa kuwa ni wagonjwa au hata pengine wana virusi* (uk.25)

Mojawapo ya athari za UKIMWI kama ilivyoangaziwa katika Kielelezo 5 ni kwamba, baadhi ya waathiriwa wa UKIMWI ni wabebaji na hawaugui. Hii ni hatari kubwa katika jamii kwa sababu mtu mmoja ambaye ni 'mbebaji' anaweza kuambukiza kizazi kizima kwani afya yake huonekana nzuri.

**6.2.1.3 Ukahaba**

Katika vitabu teule, suala la ukahaba limebainishwa kwa njia ya kimaelezo na inayotumia sitiari mbalimbali kusawiri hulka za wahusika tofautitofauti. Matumizi ya nadharia changanuzi ya sitiari ya dhana humwezesha mtu kuelewa masuala changamano kama vile ukahaba ambao watu hawapendi kuhusishwa nao kwa jinsi unavyochukuliwa kuwa aibu katika jamii. Ukahaba ni mojawapo ya njia za usambazaji wa ugonjwa wa UKIMWI zilizoangaziwa katika vitabu teule. Katika matini teule *Madhila ya Bi. Shufaa*, Bwana Fukua ni mfano wa watu waliokuwa na tabia ya kufanya mapenzi ovyo na wasichana wa shule, viruka njia mitaani na wake za watu. Aidha, kulingana na muktadha wa matumizi *Fukua* ni jina la kimajazi na la kisitiari linalowakilisha taswira ya ukahaba. Alikuwa mgonjwa wa UKIMWI na amesawiriwa kama mzee kahaba ambaye hakuchagua mwanamke au msichana alipofikiria kufanya mapenzi. Tazama Kielelezo 6:

> Mtu huyu *alikuwa hapishi rinda. Alipenda kutembea na wasichana wadogo wadogo hasa wale wa shule za msingi na upili*. Wengi walimuita '*honey'* na wengine *sweetheart*. Alimuradi watu wengi walimuona kama '*Sugar Dady*.'(uk.9).

Dondoo la Kielelezo 6 ni taswira ya mtu hasidi, mbinafsi asiyekuwa na utu. Ingawa Bwana Fukua alikuwa diwani na kiongozi aliyepaswa kulinda haki za watoto, alikuwa katika mstari wa mbele kuvunja haki hizo kwa kufanya mapenzi na watoto kinyume na sheria. Hakuna yeyote aliyedhubutu kumshtaki au kumuonya dhidi ya maovu

aliyotenda kwa sababu alikuwa kiongozi na tajiri mkubwa katika mji wa Mangelepa. Matendo ya Fukua ya ukahaba yaliyoangaziwa katika Kielelezo 6, yanasawiri uozo uliopo katika jamii ambapo viongozi wanaotarajiwa kulinda sheria na haki za wanyonge ndio wanaozikiuka na kuendeleza ukahaba na maovu mbalimbali katika jamii. Hii ni tahadhari kwa mashirika ya kijamii yanayotetea haki za wanyonge kuwa makini na kutafuta mbinu mwafaka za kukabiliana na maovu, kwa sababu wanaotarajiwa kulinda haki za watu ndio wanaendeleza maovu hayo. Kutokana na tabia ya ukahaba, Fukua aliambukiza watu wengi ugonjwa wa UKIMWI.

Fukua pia alinyemelea wasichana wa shule na wake za watu. Alitumia cheo chake cha udiwani kutembelea mboma za watu kwa kizingizio cha kuwajulia hali kama diwani wao. Alitumia mbinu hiyo kumtembelea Bi.Shufaa nyumbani na hatimaye akamwambukiza ugonjwa wa UKIMWI. Alinyemelea kila mwanamke kijijini. Tazama Kielelezo 7:

> Bwana Fukua alikuwa na *kiu cha wanawake. Kinywa chake kilikuwa na makali kama nyembe.* Pale mtaani tayari alikuwa na jamii kama sio jamaa. *Kila nyumba alipanda mbegu chafu*. Wasichana wengi walimpenda kwa sababu ya pesa zake. Licha ya hivyo, alikuwa na gari kubwa, tena la kifahari Mercedes Benz 240, si mchezo! (uk.11- 12).

Kielelezo 7 kimeangazia sitiari za kiafya *nyembe, mbegu* na *chafu* zinachora taswira mtu muovu na asiyelinganishwa na binadamu wa kawaida.

Bwana Fukua pia amesawiriwa kama mtu mwenye maadili potovu, mpenda anasa na mwenye tamaa kubwa ya wanawake. Tabia ya Fukua imewasilishwa kitaswira: Tazama Kielelezo cha 8.

> Kwa bahati mbaya, mtu huyu alipenda usherati. *Alifukua hata visivyofukuliwa.* Kwa upande mwingine, *aliwanyemelea wake za wenyewe na hata mabanati tumbitumbi!* Kwa Bi. Shufaa alianza *kujenga hema* (UK.12).

Tathmini ya ujumbe unaoangaziwa katika Kielelezo 8 ni kwamba, kuna hatari dhidi ya vita vya UKIMWI kwa sababu ya viongozi wanaoendelea kutumia mamlaka na mali yao kuendeleza ukahaba, hasa katika jamii iliyokumbwa na umaskini. Hivyo, kuna haja ya serikali kuwa na sheria inayolinda wanyonge na wasichana wa shule dhidi ya waathiriwa wanaosambaza ugonjwa wa UKIMWI kwa hiari.

Tabia ya Sulubu ya usherati imesawiriwa na sitiari ya kiafya '*danger*' neno la msimbo la Kingereza lililopewa gari ya Sulubu kuwakilisha tabia ya ukahaba. Sulubu alitumia gari hilo kubeba virukanjia mitaani na kuenda kujivinjari nao: Tazama Kielelezo 9:

> Kwenye mitaa hiyo, watu waliozoea kuona gari lile, walilipachika jina na kuliita '*danger*.' kwani walijua *mwenye gari hilo alikuwa hatari kwa kuwateka bakunja wasichana mitaani humo* (uk.13).

Kwa mujibu wa nadharia changanuzi ya sitiari ya dhana, sitiari hutumika katika mawasiliano ili kurahisisha uelewa kwa njia ya kiulinganishi na kubadili msimamo wa mhusika. Kwa msingi huu, neno '*danger'* ni la kisitiari na limetumika kuonyesha hatari inayosababishwa na ugonjwa wa UKIMWI ili watu wajikinge. Ingawa gari la Sulubu lilipachikwa jina '*danger'* kama ilivyoelezwa katika Kielelezo 9, ukweli ni kwamba neno hilo lilitumiwa kurejelea tabia ya ukahaba ya Sulubu. Tabia hiyo ilimhuzunisha Matano na kumuomba aikomeshe kwa sababu ya hatari ya kuambukizwa UKIMWI. Sulubu hakutilia maanani ushauri huo na badala yake akamkemea Matano kwa kujishughulisha na suala ambalo halikumhusu. Tazama Kielelezo 10:

> Matano aliwashauri rafikize Sulubu na Makelele na kuwatahadharisha dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI uliokuwa ukiua watu kila uchao. Lakini walimpuuza na kumuona kama *jongoo asiyeweza kupanda mtungi* (uk.12).

Sitiari ya kiafya; *jongoo asiyeweza kupanda mtungi imetumiwa* katika Kielelezo 10 imetumika kitaswira kulinganisha Matano mwanaume hoi asiyekuwa na uwezo wa kufanya mapenzi na mwanamke. Sulubu na Makelele walitumia sitiari hiyo kama njia ya kumfedhehesha Matano ili ajiunge nao katika tabia ya uzinzi. Hali hii inadhihirisha uwezo wa wanarika katika kuathiri hulka za wenzao. Hivyo, kuna haja ya wanarika kuwa na msimamo katika maisha ili waepukane na maovu yanayoweza kuwaathiri. Matano aliepuka janga la UKIMWI kwa sababu ya kuwa na msimamo katika maisha yake. Ukaidi na tabia ya ukahaba ya Sulubu ilimtumbukiza katika janga la UKIMWI. Tazama Kielelezo 11:

> "Nisikilize Sulubu," Daktari Hamisi alishauri, "*kwamba una virusi vinavyoleta ugonjwa wa UKIMWI*, haimaanishi kuwa unaugua na maisha yako yamo hatarini (uk.51).

Tathmini ya mazungumzo katika Kielelezo 11 ni kuwa, Sulubu anajihurumia kwa kuambukizwa ugonjwa wa UKIMWI. Hii ni tahadhari kwa watu waliojitumbukiza katika anasa kwamba UKIMWI upo na unaweza kumpata mtu yeyote. Ingawa Sulubu alikuwa amesoma na kuajiriwa kazi nzuri ya ukarani, aliambukizwa UKIMWI, akafuta kazi na mwishowe akaaga dunia. Hivyo, inabidi kila mtu mkubwa au mdogo, tajiri au maskini kujihadhari na ugonjwa wa UKIMWI.

Katika matini teule *Pendo katika Shari*, Sulubu amesawiriwa kama mwanaume aliyepotoka kimaadili na kahaba aliyekuwa na mazoea ya kutumia pesa na rasilimali kuwarai wasichana wa mitaani kufanya mapenzi nao. Alizoea kutembelea wasichana mitaani na mara nyingi hakulala kwake nyumbani. Tazama Kielelezo 12:

> 'Eh! Saa kumi asubuhi! Alikuwa wapi usiku wote huu?' Alijiuliza huku *akienda mwayo na kufikisha macho yake ambayo sasa yalimwasha*. Alikuwa amepoteza muda mwingi akikesha kumsubiri mumewe Sulubu, ambaye wakati huu alikuwa na mazoea ya kulala nje hadi asubuhi (uk.1).

Sitiari ya kiafya "*akienda mwayo na kufikisha macho yake ambayo sasa yalimwasha,"* iliyoangaziwa katika Kielelezo 13 inawakilisha usumbufu na maumivu ya kiakili yaliyomsumbua Pendo kwa sababu ya tabia ya Sulubu ya kuwasili nyumbani usiku. Aidha, mwandishi wa *Pendo katika Shari* anadai kwamba Pendo aliathirika kiafya na akaanza kukonda kwa sababu ya kukesha kila usiku akimngoja Sulubu. Tathmini ya ujumbe katika dondoo la kielelezo ni kwamba, kudidimia kwa mapenzi kati ya watu wanaopendana pia huathiri afya ya mtu. Pendo aliathirika kiakili na kimwili kwa sabababu ya tabia mbaya ya Sulubu. Pia, alikosa usingizi mambo yaliyochangia kudhoofika kwa afya yake.

#### 6.2.1.4 Kutowajibika

Mtindo wa watu kutojali pia umechangia katika kusababisha na kusambaza virusi vya UKIMWI. Matokeo ya uchanganuzi wa data yamedhihirisha kuwa matumizi ya kiholela ya vifaa kama vile sindano, nyembe na kupokezana damu bila kuchunguzwa na daktari kumechangia katika kusababisha ugonjwa wa UKIMWI.

Katika matini teule *Kosa la Marehemu* na *Siku ya UKIMWI*, matumizi ovyo ya vifaa vya kudunga mwili kama vile wembe na sindano huchangia katika kueneza virusi vya UKIMWI. Vifaa hivyo vinapomkata mgonjwa, hubeba virusi vya UKIMWI vilivyomo katika damu ya mwathiriwa hadi kwa mtu mwingine. Kwa mujibu wa waandishi, vifaa vya kukata au kudunga vinapaswa kutupiliwa mbali baada ya kutumiwa. Vilevile, sindano iliyotumiwa kudunga mgonjwa inapaswa kutupiliwa mbali. Hii ni tahadhari kwa wahudumu wa kiafya kuwa wanahitajika kuwa waangalifu wanapowatibu wagonjwa.

Isitoshe, uchanganuzi wa data katika matini teule umedhihirisha kuwa daktari wanapaswa kuwa makini wanapowasaidia kina mama wajawazito kujifungua. Hii ni kwa sababu damu ya mtoto anayezaliwa ikichanganyika na ya mama aliyeugua ugonjwa wa UKIMWI itasambaza virusi vya UKIMWI kwa mtoto. Vilevile, damu inayotiwa kwa wagonjwa pia inastahili kuchunguzwa na daktari kwa makini kabla ya kuongozewa kwa mgonjwa. Kuongeza damu kwa mgonjwa bila kuichunguza hutatiza juhudi za kuzuia usambazaji wa ugonjwa wa UKIMWI. Daktari wanahitaji kutumia damu ilyochunguzwa virusi vya UKIMWI ili kuzuia maambukizi zaidi kwani hakuna chanjo wala dawa ya kutibu UKIMWI. Hivyo, ni heri kuzuia kuliko kutibu.

### 6.2.2 Athari za Ugonjwa wa UKIMWI

Uchanganuzi wa data katika vitabu viteule vya fasihi ya Kiswahili ya Watoto umedhihirisha ya kwamba, janga la UKIMWI limekuwa tisho kubwa katika maendeleo ya jamii kama ilivyoangaziwa katika utafiti huu. Hivyo, ugonjwa wa UKIMWI umesawiriwa kama mojawapo ya masuala mtambuko katika matini teule na husababisha madhara yafuatayo:

#### 6.2.2.1 Vifo vya Watu

Katika matini teule *Siku ya UKIMWI*, ugonjwa wa UKIMWI umesawiriwa kama janga la kimataifa linaloangamiza watoto na watu wazima kwa pamoja. Kauli hii inathibitishwa na utafiti wa WHO (2003) uliobaini kuwa, ugonjwa huo umesababisha vifo vingi vya watoto na watu wazima hasa walio na umri wa kati ya miaka 15 na 59 ulimwenguni na ukawa ndio chanzo kuu cha maafa mengi ya watu. Zaidi ya hayo, WHO (keshatajwa) wanasema kuwa jumla ya watoto elfu moja huaga dunia barani

Afrika kila siku kutokana na UKIMWI. Hii ni dhibitisho kuwa ugonjwa wa UKIMWI hautambui kabila, jinsia, umri wala hadhi. Katika kitabu kiteule, UKIMWI umesawiriwa kama *sumu* inayoua kila aina ya mnyama aliyeikula. Tazama Kielelezo 14:

> Mkulima hakufurahia kuona shamba lake la mahindi likiharibiwa na *mbwa*.Siku moja, alitia *sumu* kwenye mahindi. Kila mbwa aliyekula mahindi yaliyotiwa *sumu* alifariki. Kila *mbwa* alikufa kifo kichungu (uk.8).

Mazungumzo katika Kielelezo 14 yanaangazia taswira ya mbwa na sumu. Katika muktadha wa matumizi sitiari ya mbwa inawakilisha uzinzi inayowakilisha wanaume wanaofanya ngono kiholela. *Sumu* ni sitiari ya kiafya iliyotumiwa kurejelea ugonjwa wa UKIMWI. Leech (1969) anasema kuwa sitiari hutumiwa kunaza makini ya hadhira. Hivyo, mwandishi wa matini teule ametumia taswira ya *sumu* na *mbwa* kunasa makini ya hadhira ili aweze kusawiri hatari inayohusishwa na UKIMWI. Kwa kulinganisha UKIMWI na sumu, mwandishi anaangazia madhara yanayotokana na UKIMWI kama vile kifo.

Katika matini teule *Siku ya UKIMWI*, mhusika mkuu Kadogo anazungumzia hatari inayotokana na ugonjwa wa UKIMWI na kuwaomba wanafunzi wajichunge ili wasiambukizwe na ugonjwa huo. Tazama Kielelezo 15:

> "Ukimwi ni hatari. Msifikirie ni ugonjwa wa watu wazima pekee. Ugonjwa wa UKIMWI unaweza kumshika hata mwanafunzi. Jihadharini. Jikingeni." (uk.9).

Matamshi yaliyotolewa na Kadogo katika Kielelezo 15 yanaafikiana na kauli ya WHO (2003) kuwa, ugonjwa wa UKIMWI umeangamiza watoto na watu wazima kwa pamoja. Hivyo, kuna haja ya kuzuia vifo vya watoto vinavyosababishwa na UKIMWI kwa kuepuka matumizi mabaya ya vyombo vya kudunga mwili kama vile sindano, nyembe na mapenzi nje ya ndoa.

#### 6.2.2.2 Kuambukizwa na Magonjwa Nyemelezi

Kwa mujibu Lakoff na Johnson (1980), matumizi ya sitiari katika mawasiliano yana uwezo wa kunasa makini ya hadhira na kuathiri mwonoulimwengu wao kuhusu suala

fulani. Kauli hii imedhihirishwa na matokeo ya uchanganuzi wa data katika kitabu kiteule *Pendo katika Shari*, ambapo mwandishi ametumia sitiari mbalimbali kuangazia taswira za athari za ugonjwa wa UKIMWI. Miongoni mwa athari hizo ni kuambukizwa na magonjwa nyemelezi, kuugua kila wakati, watoto kuachwa mayatima na vifo. Aidha, Mhusika Pendo anazungumzia masaibu hayo anapowaelezea watoto wake jinsi walivyotambuliwa kuwa na virusi vya UKIMWI. Tazama Kielelezo 16:

> "Sikilizeni wanangu. *Mimi na Zuhura tuna virusi vinavyosababisha hali ya UKIMWI. Hii ndiyo maana Zuhura sasa ni mgonjwa*. Pendo alianza kueleza lakini alipowatazama wanawe, hakuona dalili yoyote ya kushtuka. "Mama, tumefundishwa mambo mengi kuhusu UKIMWI shuleni. Hata tumefundishwa kwamba mtu akiambukizwa UKIMWI anaweza kuishi maisha marefu na kama kawaida tu (uk.26). Maneno ya watoto hao yalikuwa kama *matone ya maji baridi kwenye moyo uliokuwa ukiwaka* kutokana na mshtuko alioupata Pendo siku hiyo (uk.28).

Mazungumzo baina ya Pendo na watoto wake katika Kielelezo 16 yanaelezea athari zinazotokana na maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI, kama vile magonjwa na maumivu ya kiakili kama ilivyoangaziwa na sitiari za kiafya katika matini teule. Pia, imebainika kuwa mwanamke mjamzito aliyeathiriwa na UKIMWI anaweza kumwambukiza mtoto virusi vya ugonjwa huo anapozaliwa. Ujumbe huu ni tahadhari kwa wahudumu wa afya na kina mama wajawazito kwamba, UKIMWI huwapata watoto wakati wa kuzaliwa iwapo njia kabambe za kuwasaidia wakati wa kujifungua hazitazingatiwa. Ukweli kwamba vifo vingi vinatokana na UKIMWI unathibitishwa pia na ripoti ya WHO (2003) inayosema kuwa, UKIMWI umechangia katika kuchipuka kwa magonjwa nyemelezi kama vile kifua kikuu na kuendesha yanayochangia katika kuongezeka kwa vifo. Baadhi ya madhara ya UKIMWI kama ilivyoangaziwa katika kitabu kiteule ni vifo. Tazama Kielelezo 17:

> "Unajua UKIMWI unaua maelfu ulimwenguni lakini unafikiri wewe huwezi kuwa mmoja wa hao maelfu. Tazama humu nchini, kwa mfano, *jinsi watu wanavyotoweka mithili ya nyota katika nuru ya jua* (uk.30).

Taswira ya vifo vingi vinavyotokana na ugonjwa wa UKIMWI imezungumziwa katika Kielelezo 17. Usemi: *Jinsi watu wanavyotoweka mithili ya nyota katika nuru ya jua* ni wa kitaswira unaochora picha ya mahame yaliyosababishwa na ugonjwa wa UKIMWI. Vifo hivyo vinalinganishwa na kutoweka kwa nyota kwa sababu ya mwangaza mwingi

wa jua. Pia, ulinganishi huo ni wa kisitiari na unawakilisha vita kati ya virusi vya UKIMWI na chembechembe nyeupe za damu zinazolinda mwili wa mtu dhidi ya vijidudu vinavyoambukiza magonjwa. Kushindwa kwa chembechembe za damu na virusi vya UKIMWI kunasawiri kutoweka kwa nyota wakati wa mchana kwa sababu ya mwangaza wa jua. Kifo cha Zuhura kinadhibitisha mawazo haya. Tazama Kielelezo 18:

> *Zuhura alifariki baada ya kuzidiwa na maradhi*. Sulubu hakunyanyua mguu kwenda kwa mkewe wala kutuma ujumbe wowote. Alijua mtoto hangeishi na *mkewe alikuwa njiani kuelekea kuko huko alikoenda mwanawe* (uk.32).

Sitiari ya kiafya '*Mkewe alikuwa njiani kuelekea kuko huko alikoenda mwanawe'* katika Kielelezo 18 inaangazia taswira ya madhara yanayosababishwa na UKIMWI kama vile kuangamiza wazazi, watoto na familia yote kwa ujumla. Hivyo, UKIMWI usipodhibitiwa unaweza kuua kizazi kizima.

#### 6.2.2.3 Kusambaratika kwa Ndoa

Miongoni mwa athari zingine zinazotokana na maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI ni kusambaratika kwa ndoa. Haya yameangaziwa katika kitabu kiteule *Pendo katika Shari*. Pendo aliamua kurudi kwa wazazi wake baada ya Sulubu kutupa nje nguo na mali yake yote. Huo ulikuwa mwanzo wa kusambaratika kwa ndoa yao. Tazama Kielelezo 19:

> Sasa alikuwa anahisi uchovu mwingi mwilini. Kwa hivyo hakutaka kusema mengi. Alivitazama vyombo vyake vilivyotupwa nje na kutikisa kichwa. Alijua yangemfika haya yote. Ni wakati tu aliokuwa akisubiri. Madamu wakati ulifika, *hakuwa na jingine ila kutafuta gari la kumpeleka kwao na wanawe* (uk.28).

Kulingana na maelezo katika Kielelezo 19, kuvunjika kwa ndoa kati ya Sulubu na Pendo kuliathiri familia nzima ya Sulubu. Uchanganuzi wa data umedhihirisha kuwa, kuvunjika kwa ndoa hiyo pia kuliathiri watoto ambao hawakuwa na hatia kwa jinsi walivyokosa upendo wa wazazi wote na malezi bora. Matukio hayo yalidhihirisha athari za ugonjwa wa UKIMWI kwa taasisi ya familia ambapo jamii nzima husambaratika. Vilevile, kuvunjika kwa familia kunaathiri elimu ya watoto, mshikamano wa kijamii na kuafikiwa kwa maendeleo endelevu katika jamii kwa

sababu ya matumizi ya rasilimali katika kutafuta matibabu na makazi mapya ya familia. Matokeo ya utafiti huu pia yamebaini ya kwamba, madhara yanayotokana na UKIMWI huathiri marafiki wa mwathiriwa na kutatiza kuafikiwa kwa maendeleo endelevu katika jamii.

#### 6.2.2.4 Kuongezeka kwa Watoto Yatima

Utafiti huu pia umetambua namna ugonjwa wa UKIMWI unavyosababisha kuongezeka kwa watoto mayatima katika jamii kwa sababu ya vifo vya wazazi. Ripoti ya WHO (2003) inashadidia kwa kusema kuwa, watoto hasa katika bara la Afrika ndio wameathiriwa zaidi na UKIMWI kwa sababu ya umaskini unaokithiri katika nchi za Afrika. Yumkini, kuongezeka kwa vifo hivyo kumechangiwa na kuchipuka kwa magonjwa nyemelezi yanayotokana na maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI. Ili kudhibiti athari za ugonjwa huo, nchi zinazoendelea kama vile Marekani zimeanza kupanga mikakati ya kuimarisha afya na maisha ya watoto.

Athari za vifo vya wazazi vinavyosababishwa na UKIMWI zinashuhudiwa katika matini teule *Madhila ya Bi. Shufaa*, ambapo Amina na Zuhura wanalia kwa uchungu kwa sababu ya kifo cha mama yao. Tazama Kielelezo 20:

> Nyumba hii, ilijawa na majonzi, kilio na adha kubwa ya kimaisha baada ya kumpoteza mtu waliyemtegemea kama nuru ya jamii. *Waliopatwa na baa kuu zaidi walikuwa Amina na Zuhura, mabinti wa pekee wa Bi. Shufaa.* Kilikuwa kifo bila simile (uk.25).

Maelezo katika Kielelezo 20 ni ya kitaswira  na yanaonyesha jinsi Zuhura na Amina walivyoathiriwa na kifo cha mama yao. Mwandishi anasema kuwa *walipatwa na baa kuu zaidi*. Ingawa baba yao Iddi aliwajibika kuwatunza, hawakutosheka kwa kukosa upendo wa mama. Familia hiyo ilijawa na majozi na huzuni kwa kifo cha mama mzazi.

Katika matini teule *Sitaki Iwe Siri*, Musa, Ukwa na Haki waliachwa mayatima baada ya vifo vya wazazi wao. Watoto hao waliachwa katika utunzi wa nyanya Mwalonga. Nyanya huyo alikuwa mwanamke mkongwe asiyekuwa na uwezo wa kuwakimu kimaisha kwa sababu ya umaskini.

#### 6.2.2.5 Kuathirika kwa Jmaa na Marafiki

Athari za ugonjwa wa UKIMWI zilipiku mipaka na kuathiri jamaa na watu waliokuwa na uhusiano wa karibu na waathiriwa. Katika matini teule *Nimefufuka* Sikitu alijichunga asiambukizwe ugonjwa wa UKIMWI lakini kifo cha Lena kilikuwa mzigo kwake. Sikitu alijitwikwa jukumu la kulea mtoto aliyeachwa na Lena. Baada ya Lena kuugua UKIMWI na kuaga dunia, aliacha mtoto mdogo ambaye Sikitu alichukua jukumu la kumlea. Mtoto huyo pia alikuwa na virusi vya UKIMWI na alianza kuugua mara tu mamake alipoaga dunia. Tazama Kielelezo 21:

> Mama alishikwa na ugonjwa wa kiarusi, akawa sawa na kitoto kilichoachwa ambacho asili yake haijabainika kufikia leo. Kitoto kimalaika, chema chenye utulivu wa nafsi. *Kikembe chalialia tu lakini hakina kimliliaye. Mama hayupo Na hajulikani alipo baba. Hivi majuzi, kitoto kimeshikwa na maradhi mbalimbali* (uk.11).

Usemi *'Kikembe chalialia tu lakini hakina kimliliaye. Mama hayupo Na hajulikani alipo baba'* katika Kielelezo 21 ni wa kitaswira. Unaangazia masaibu yaliyomkumba Sikitu baada ya kifo cha Lena. Ingawa analea mtoto wa Lena, babake mtoto hakujulikana. Vilevile, mtoto huyo aliugua mara kwa mara na Sikitu alitatizika kwa kumpeleka hospitali kila wakati. Sikitu aliathiriwa mno na jukumu la kumlea mtoto ambaye hakumzaa. Tazama Kielelezo 22:

> Hivi majuzi, kitoto kimeshikwa na maradhi mbalimbali. *Hakiishi kulia. Si usiku si mchana ni Ng'wee! Ng'wee! Ng,wee! Hakipewi chakula kikakoma kutapika na kuhara. Harufu ya kinyesi chumbani mwangu haiishi. Mkojo nao kila siku ni kama mfereji usiofunguka. Nimefua matambara nimechoka*. Ndimi za waja zimeanza kusema kitoto hicho kisicho na asili wala fasili kinaugua UKIMWI kama mama yacho (uk.11).

Matamshi ya Sikitu katika Kielelezo 22 ni ya kitaswira yanayochora picha ya mtu aliyesumbuka na kuteseka kwa sababu ya mzigo ambao haukuwa wake wala kuutarajia. kilichomhuzunisha Sikitu zaidi ni kuwa hakujua kabila wala baba ya mtoto aliyekuwa akimlea. Hali hii pia inatokea katika jamii ambapo watoto wameachwa mayatima baada ya vifo vya wazazi wao vilivyosababishwa na UKIMWI. Ripoti ya WHO (2003) inadhihirisha kuwepo kwa vifo kama hivyo kwa kusema kuwa, UKIMWI umeua watu wengi ulimwenguni na kuacha watoto wengi bila wazazi. Watoto hao hukosa malezi bora, makazi na elimu. Matatizo haya yamesabisha baadhi ya watoto wengine kujiunga

na watoto mitaani. Ongezeko la watoto mitaani limesababisha kuongezeka kwa wizi, vita, unajisi wa watoto wa mitaani na magonjwa yanayotokana na uchafu. Kwa jinsi hii, kuna haja ya serikali kuimarisha na kuongeza idadi ya vituo vya kushughulikia watoto wa mitaani ili kupunguza visa vya uhalifu katika miji.

Katika matini teule *Kosa la Marehemu,* Daudi anaugua UKIMWI na kuathiri afya na shughuli za kila siku za wazazi na ndugu yake Mshindo. Wazazi wa Daudi wanaumia kutokana na safari za kila mara za kumtembelea hospitalini. Mshindo anatatizika kimawazo na kushindwa kuvumilia shuleni kwa kugonjeka kwa nduguye. Haya yamedhihirishwa katika kitabu kiteule kupitia mazungumzo kati ya Mshindo na wazazi wake walipotoka hospitalini. Tazama Kielelezo 23:

> Alipoingia ndani, aliwakuta wazazi wake wamesharudi……..Baba yake alikuwa sebuleni. Alimsalimia na kumuuliza hali ya kaka yake. Baba yake alisita kumjibu. Alionyesha kama alikuwa akitafuta la kumjibu. Mshindo alimuuliza tena huku amemkazia macho. *Sura ya baba yake ilikuwa imekunjamana na alionekana mchovu sana. Macho yalionekana mekundu na Mshindo alihisi kama baba yake amekuwa mzee zaidi Muda ule* (45).

Mazungumzo kati ya Mshindo na baba yake katika Kielelezo 23, yanaonyesha namna ugonjwa wa UKIMWI unavyoathiri jamaa wa karibu wa mwathiriwa. Ingawa Mshindo alikuwa mtoto aliathiriwa na kugonjeka kwa nduguye kiasi kwamba, ilibidi achunguze zaidi kuhusu ugonjwa wa UKIMWI ili amsaidie nduguye. Alihusisha marafiki zake kama vile Njanga ingawa juhudi zao ziliambulia patupu kwani mwishowe Daudi aliaga dunia.

Wengine walioathiriwa na janga la UKIMWI ni nyanya Mwalonga. Katika matini teule *Sitaki Iwe Siri* Mwalonga aliachiwa jukumu la kuwatunza wajukuu wake Musa, Haki na Ukwa baada ya kifo cha wazazi wao. Ingawa mama huyo alikuwa mzee, alitia juhudi kuwakimu wajukuu wake kimavazi na malezi, majukumu ambayo yalimtatiza kwa ukosefu wa mapato. Hali hii inaangazia namna UKIMWI unavyoadhiri jamii kwa ujumla wakiwemo wazee, watoto na vijana. Musa, Ukwa na Haki waliathirika kiafya, kimavazi na kimalezi. Mara nyingine Musa alisahau kuchana nywele na kuonekana kama mwendawazimu. Tazama Kielelezo 24:

> “Musa, tayari?” Haki aliuliza. “Tayari.” “ *hujachana nywele aisee. Zinaonekana kama za mwendawazimu*,” Ukwa akasema na wote wakaangua kicheko (uk.5).

Sitiari ya *mwendawazimu* katika Kielelezo 24 ni taswira ya mateso wanayoyapata watoto mayatima. Mazungumzo baina ya Ukwa, Musa na Haki yanaonyesha jinsi watoto waliokosa mapenzi na malezi ya wazazi walivyoteseka kwa kukosa ushauri na utunzi mwema. Ukosefu wa utunzi huo ndio uliathiri tabia ya Musa na kusahau kujinadhifisha kabla ya kwenda shule. Aidha, Kielelezo 24 kinasawiri jinsi wazazi walivyokuwa na majukumu muhimu ya kuwalea watoto kitabia na kiafya. Musa alisahau kuchana nywele kwa sababu ya kukosa mwelekezi. Wazazi pia ni waelekezi na huchangia pakubwa katika kurekebisha na kuimarisha tabia ya watoto. Hili ni funzo kwa wazazi wanaokiuka majukumu ya kuwalea watoto kwamba, wana wajibu wa kutekeleza katika kuimarisha tabia ya watoto wao.

**6.2.2.6 Ufukara**

Maambukizi ya maradhi ya UKIMWI husababisha ufukara katika jamii na kutatiza juhudi za kuafikiwa kwa maendeleo endelevu. Wagonjwa wa UKIMWI hutumia pesa nyingi na rasilimali za familia katika kutafuta huduma za kiafya na lishe bora. Katika matini teule *Sitaki Iwe Siri* vifo vya wazazi wa Musa, Ukwa na Haki vilisababisha umaskini uliokithiri katika familia hiyo. Nyanya Mwalonga hakuweza kutimiza mahitaji yote ya wajukuu wake kwa sababu ya umaskini. Zaidi ya hayo, Musa analia kwa kukosa furaha katika maisha kwa sababu ya uhaba wa usingizi uliosababishwa na ukosefu wa vifaa mwafaka nyumbani vya kulalia na kutumia. Tazama Kielelezo 25:

> Laiti wazazi wangu wangalikuwa hai, nami *ningalipata fursa ya kulala na kufurahia usingizi jinsi wanavyofurahia watoto wengine wenye wazazi. Maskini siwezi kufanya hivyo* kwa sababu wadogo wangu na nyanya wananitegemea mimi (uk.1).

Usemi *‘nami ningalipata fursa ya kulala na kufurahia usingizi jinsi wanavyofurahia watoto wengine wenye wazazi. Maskini siwezi kufanya hivyo’* katika Kielelezo 25 ni wa kitaswira unaoangazia taswira ya mateso ambayo watoto mayatima hupata. Musa anajutia hali waliyomo ya umaskini iliyotokana na kifo cha wazazi wake. Zaidi ya hayo, dada zake na nyanya Mwalonga wanamtegemea maishani mwao. Hiki ni kinaya kwa

sababu Musa pia ni mtoto asiyekuwa na mapato na pia aliyepaswa kuwa chini ya utunzi wa wazazi.

Kwa ujumla, ugonjwa wa UKIMWI hauathiri tu watu waliougua ugonjwa huo bali pia huathiri jamaa na marafiki wa karibu. Vilevile, UKIMWI huathiri utendakazi wa wafanyikazi na hatimaye kutatiza kuafikiwa kwa maendeleo endelevu, kwani afya bora ni mojawapo ya nguzo kuu katika kuafikiwa kwa maendeleo katika taifa lolote lile.

### 6.2.3 Njia za kukabiliana na UKIMWI

Kwa mujibu wa Lakoff na Johnson (1980), ufasiri wa maana ya sitiari mbalimbali katika kazi za kifasihi humwezesha msomaji kuchukua hatua inayofaa baada ya kusoma kazi fulani ya kifasihi. Vilevile, nadharia hii hulenga kumshawishi msomaji kuchukua hatua fulani kutokana na athari inayotokana na kazi ya kifasihi aliyosoma. Kwa msingi huu, wasomaji wa matini teule wanapaswa kubaini njia mbalimbali za kukabiliana na athari za ugonjwa wa UKIMWI baada ya kusoma kazi hizo.

Kwa mujibu wa Garret (2007) suala la afya limekuwa changamoto kote ulimwenguni kwa sababu ya uhaba wa rasilimali za kukabiliana na matatizo ya kiafya. Miongoni mwa changamoto za kiafya zinazoathiri binadamu ni magonjwa kama vile UKIMWI, kifua kikuu na malaria miongoni mwa mengine. Magonjwa hayo yameathiri zaidi watu katika nchi zinazoendelea hasa barani Afrika na kwa hivyo mataifa mengi yanatia bidii kutafuta fedha za kuzuia kuenea zaidi kwa magonjwa. Hata hivyo, miongoni mwa magonjwa yanayoathiri watu zaidi kama ilivyoangaziwa na Garret (keshatajwa) ni janga la UKIMWI. Katika matini teule, janga la UKIMWI limeangaziwa kwa kina huku madhara yake na njia za kukabiliana na ugonjwa huo zikibainishwa wazi. Ingawa vitabu teule ni vya kifasihi, vimetumika kwa ufanisi kuangazia suala la UKIMWI. Kulingana na Senkoro (1982), fasihi kama zao la jamii ina nafasi ya kumulika masuala yanayoathiri jamii kwa lengo la kuyarekebisha. Matumizi ya nadharia changanuzi ya sitiari ya dhana katika kazi hii, imesaidia kuchanganua masuala hayo changamano kwa njia ya kiulinganishi na iliyorahisisha uelewa wake katika hali halisi. Kwa mujibu wa Lakoff na Johnson (1980) na Lakoff (1992) nadharia hiyo pia huwasilisha mawasiliano kwa njia ya kisitiari na iliyo na uwezo kuathiri msimamo wa mtu kuhusu suala fulani. Hivyo, kwa sababu suala la UKIMWI limechukuliwa kama mwiko katika baadhi ya

jamii, matumizi ya nadharia hii yamesaidia kuwasilisha janga la UKIMWI kwa njia inayokubalika katika jamii. Utafiti huu umebainisha njia zifuatazo za kukabiliana na janga la UKIMWI:

#### 6.2.3.1 Kupuuza Tamaduni hasi kuhusu UKIMWI

Uchanganuzi wa data katika matini teule umebainisha kuwa, mojawapo ya njia za kuzuia maambukizi na kuenea kwa ugonjwa wa UKIMWI ni kupuuza na kuachana na tamaduni zinazoshikilia kuwa, ugonjwa huo unatokana na laana za kijamii. Katika matini teule *Siku ya UKIMWI* mhusika mkuu Kadogo anawatahadharisha vijana dhidi ya kuchukulia ugonjwa wa UKIMWI kwa utani na kuwaonya ya kwamba, ugonjwa huo upo na wanapaswa kujichunga. Imani kwamba UKIMWI haupo inatokana na tamaduni hasi zinazochukulia ugonjwa huo kuwa mwiko. Mawazo hayo pia yanaangaziwa katika matini teule *Sitaki Iwe Siri* ambapo nyanya Mwalonga anaficha kama siri ugonjwa wa UKIMWI uliowaua wazazi wa wajukuu wake, kwa jinsi ugonjwa huo ulivyochukuliwa kama laana katika jamii. Tazama Kielelezo 26:

> UKIMWI ni miongoni mwa masuala ibuka katika jamii zetu za ulimwengu wa sasa. *Suala la UKIMWI halijazungumziwa na kuwekwa wazi katika jamii kwa sababu ya ugonjwa huo kuchukuliwa kuwa ni mwiko* (uk.23).

Kulingana na maelezo katika Kielelezo 26, suala la UKIMWI halizungumziwi hadharani katika jamii. Kobia (2008) anaangazia kauli hii anaposema kuwa, jamii nyingi huchukulia UKIMWI kama laana na hali hiyo hutatiza juhudi za kukabiliana na ugonjwa huo. Hata hivyo, mhusika Kadogo anajitokeza kufafanua kuwa UKIMWI upo na unaua. Tazama Kielelezo 27:

> “ Nyinyi vijana mnaohuzunika, mjihadhari. UKIMWI upo. UKIMWI si Mchezo kamwe. UKIMWI si utani. UKIMWI si mzaha (uk.14).

Usemi katika Kielelezo 27 unaonyesha namna vijana wanavyochukulia suala la UKIMWI kimsaha. Kadogo amejitokeza kama mshauri kwa vijana dhidi ya janga la UKIMWI. Anawahimiza wajichunge ili wasiambukizwe UKIMWI na kuwatahadharisha dhidi ya imani potovu kwamba ugonjwa wa UKIMWI haupo. Tahadhari hii pia ni kwa jamii ambazo haziamini kuwa ugonjwa wa UKIMWI upo.

#### 6.2.3.2 Uaminifu na kuepuka Ngono za kiholela

Njia nyingine ya kuzuia maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI ni kuepukana na ngono za kiholela. Kauli hii imedhihirishwa katika matini teule *Madhila ya Bi. Shufaa* ambapo Bi.Shufaa anawashauri vijana watunze ubikira wao ili waepukane na janga la UKIMWI (uk.6). Pia, mwalimu wa shule ya msingi ya Kipimo anawashauri vijana kuepukana na mapenzi kabla ya ndoa ili wajinusuru katika maambukizi ya UKIMWI. Zuhura anazungumzia suala hili katika mazungumzo yake na baba. Tazama Kielelezo 28:

> "Mwalimu mkuu anasema ni vizuri watu kwenda katika 'VCT' kupimwa UKIMWI. Hata alisema vijana wanafaa *ku-chill*," Amina aliongezea. "Hiyo Ku-chill ndio nini?" Baba alihoji. "*Ku-chill"* ni "*abstain*." Amina alimchanganya baba zaidi (uk.7).

Njia za kujikinga na UKIMWI zimezungumziwa katika Kielelezo 28 ambapo mwalimu anawashauri vijana kuepukana na ngono za kiholela. Ametumia sitiari ya kiafya *Ku-chill* ambalo ni neno la kimsimbo la Sheng' linalomaanisha kuachana kabisa na ngono kabla ya ndoa. Aidha, Zuhura ametumia neno la Kiingereza '*abstain'* kulieleza. Ingawa Mwalimu mkuu na Bi.Shufaa wanawashauri vijana kuepukana na mapenzi kabla ya ndoa, kinaya ni kwamba Bi. Shufaa aliambukizwa UKIMWI na Bwana Fukua baada ya kuhusika naye kingono nje ya ndoa. Hata hivyo, Zuhura na marafiki zake walizingatia ushauri wa mwalimu na mama yao na wakaepukana na janga la UKIMWI. Msisitizo wa kujihadhari na mapenzi ovyo ovyo pia umejitokeza katika matini teule *Siku ya UKIMWI* ambapo mhusika mkuu Kadogo anawatahadharisha watu dhidi ya usambazaji wa ugonjwa wa UKIMWI. Tazama Kielelezo 29:

> "Hata kama uliambukizwa, usiambukize wengine. Usilipize kisasi. *Kwa watu wasioambukizwa, jikingeni msiambukizwe*. Msiwabague walio na UKIMWI. Wao ni binadamu kama nyinyi. Msiwatenge katika jamii." (uk.16).

Mawaidha ya Kadogo katika Kielelezo 29, yanamsawiri kama mtetezi na mhusika mkuu katika vita dhidi ya usambazaji wa ugonjwa wa UKIMWI. Hili ni funzo kwa waathiriwa wa UKIMWI kwamba, wasijifiche na wajitwike jukumu muhimu la kupiga vita maenezi ya UKIMWI kwa kuhamasisha jamii kuhusu jinsi ya kujikinga na kuishi na ugonjwa huo. Aidha, Kadogo anawashauri waathiriwa kuwa wasisambaze UKIMWI ingawa waliambukizwa kwa njia yoyote ile.

#### 6.2.3.3 Kuzingatia huduma bora za Kiafya

Kuna haja ya kila mtu kutembelea vituo vya afya ili kuchunguzwa hali ya kiafya. Ikiwa kuna maambukizi ya UKIMWI, maafisa ya kiafya hupeana ushairi kuhusu namna ya kukabiliana na ugonjwa huo. Waathiriwa wanapaswa kutembelea vituo vya afya ili kupata matibabu na dawa za kupunguza makali (ARVS). Ushauri huu umeangaziwa katika kitabu kiteule *Madhila ya Bi. Shufaa,* ambapo Zuhura na Amina wanamshauri mama yao kutembelea kituo cha afya ili apate ushauri wa daktari.

Tazama Kielelezo 30:

> "Mama, kule shuleni mwalimu Sainura alisema ni vyema *tukupeleke kwa daktari au kwa kituo cha VCT ili ujue kinachokuuma*. *Kama kwa bahati mbaya ni UKIMWI basi, uweze kupewa tembe za kuzuia makali ya ugonjwa* huo," Amina aliongeza……. Alisema zinaitwa *ARVS*; yaani *Anti-Ritrovirals*. (uk.16).

Mazungumzo katika Kielelezo 30 yanadhihirisha jukumu la taasisi ya elimu katika kuhamasisha jamii kuhusu janga la UKIMWI. Ingawa Bi. Shufaa alikuwa mtu mzima, hakuwa na ufahamu wa maenezi ya ugonjwa wa UKIMWI. Watoto wake ndio walikuwa na habari zaidi kuhusu UKIMWI na jinsi "*ARVS"* zilivyoweza kupunguza makali ya ugonjwa huo. Aidha, ujumbe wao kuhusu namna "*ARVS"* zilivyofanya kazi ulidhirishwa na wanasayansi waliokongamana katika mji wa Vancouver nchini Canada katika mwaka wa 1996. Kwa mujibu wa Garret (2007), wanasayansi hao walishuhudia kuwa, dawa za kupunga makali ya UKIMWI (ARVS) zilikuwa na uwezo wa kupunguza kuenea kwa UKIMWI na kuwawezesha waathiriwa kuishi kwa muda mrefu. Hata hivyo, watu wengi walikosa huduma hiyo kwa sababu ya gharama kubwa ya matibabu. Hali hiyo ilichochea aliyekuwa raisi wa Afrika Kusini Nelson Mandela kulalamika katika mkutano wa madaktari mjini Durban katika mwaka wa 2000 kuwa, waafrika wengi walishindwa kugharamia matibabu yao. Kulingana na Garret (keshatajwa) ukweli kuhusu malalamiko ya Mandela ulidhihirishwa katika mwaka wa 2001 na kundi la Wahathiri katika Chuo Kikuu cha Havard walioongozwa na Jeffrey Sachs. Walisema kuwa, jumla ya waafrika 40,000 pekee walikuwa wakitumia "*ARVS"* na kulikuwa na haja ya kutafuta mbinu za kuongezea idadi hiyo.

Ili kuimarisha huduma kwa wagonjwa wa UKIMWI, Garret (2007) anasema kuwa mashirika na watu mbalimbali walijitokeza kufadhili kwa njia zifuatazo: Kati ya miaka

ya 1995 na 2005 shirika la hisni la Amerika lilianza kufadhili matibabu kwa wagonjwa wa UKIMWI. Benki Kuu ya Dunia pia ilitoa mamilioni ya pesa kugharamia matibabu ya wagonjwa wa UKIMWI na kifua kikuu. Isitoshe, Shirika la Fedha Ulimwengunu (IMF) liliondolea mataifa yaliyoathiriwa na janga la UKIMWI madeni yaliyokuwa ikiwadai na kuyafadhili zaidi ili kukabiliana na changamoto za UKIMWI. Katika mwaka wa 2006, Bill Gates na Melinda Gates walitoa jumla ya dola bilioni 6.6 kufadhili matibabu ya UKIMWI na kifua kikuu. Juhudi hizo zinachangia kuimarisha viwango vya afya ulimwenguni na kuwapa wagonjwa matumaini ya kuishi.

#### 6.2.3.4 Lishe bora

Utafiti huu umetambua lishe bora kama baadhi ya njia za kukabiliana na UKIMWI, kwa sababu inaimarisha uwezo wa mwili katika kupambana na vijidudu vinavyosababisha magonjwa. Katika kitabu kiteule *Madhila ya Bi. Shufaa*, daktari anamshauri Iddi kumhudumia mkewe kwa kumpa lishe bora ili asiathiriwe zaidi na magonjwa. Tazama Kielelezo 31:

> "Unachohitaji kufanya utakapofika nyumbani ni *kumpa chakula cha kujenga mwili: yaani chenye protein, chakula cha kumpa mtu nguvu na pia matunda kama; mafenesi, tikitimaji, papai, mapera, kisamvu, na karoti* kadri ya uwezo wako. Ukifanya hivyo utamwongezea muda wa kuishi." (uk.21-22).

Kulingana na mawaidha ya daktari yaliyoangaziwa katika Kielelezo 31, ni wazi kuwa lishe bora huzipa dawa nguvu ya kufanya kazi mwilini. Kadhalika, ni muhimu kufahamu kuwa lishe bora hujumuisha chakula kilicho na madini yote kama vile proteni, kabohidrati, vitamini na kunyua maji.

Vilevile, lishe bora kwa wagonjwa wa UKIMWI imesisitizwa katika matini teule za *Sitaki Iwe Siri* na *Pendo katika Shari*. Katika *Sitaki Iwe Siri*, Daktari Ataya anahimiza ulaji wa chakula bora kwa wanaougua UKIMWI ili wasidhurike zaidi. Tazama mawaidha ya Daktari Ataya katika Kielelezo 32:

> " Hadi sasa, hakuna tiba yoyote kwa maradhi ya UKIMWI, ingawa kuna dawa ambazo wagonjwa wanaougua UKIMWI hutumia ili kupunguza athari za ugonjwa huo. *Isitoshe, lishe bora pia huwafaa wagonjwa wa UKIMWI* (uk.42).

Ushauri katika Kielelezo 32 ni tahadhari kwa kila mwanajamii kwamba ukosefu wa lishe bora kungesababisha athari zilizotokana na UKIMWI. Hii ni kwa sababu ugonjwa wa UKIMWI haukuwa na tiba.

Umuhimu wa kula vyakula vinavyotia mwili nguvu kwa wagonjwa wa UKIMWI pia umesisitizwa katika matini teule *Pendo katika Shari.* Almasi anamhimiza mamake ale chakula kizuri ili aishi maisha mema. Tazama Kielelezo 33:

> " Tunajua unaugua UKIMWI," aliongeza Almasi, " lakini sisi tunaamini kuwa ukiishi maisha mazuri na *ukila vizuri, hutateseka*." (uk.59).

Ingawa matini teule zimesisitiza umuhimu wa lishe bora katika kukabiliana na UKIMWI, gharama ya kununua aina mbalimbali za vyakula hivyo ni changamoto kuu. Garrett (2007) anafafanua changamoto za kugharamia matibabu kwa kusema kuwa, ukosefu wa rasilimali za kutosha zinatatiza juhudi za kuimarisha viwango vya afya ulimwenguni. Hii imesababishwa na umaskini unaokithiri katika jamii mbalimbali ambapo wagonjwa wanakosa namna ya kujishughulikia. Pia, ufisadi umekuwa kikwazo katika vita dhidi ya UKIMWI. Kulingana na Garret (keshatajwa) uchunguzi uliofanywa na Benki Kuu ya Dunia katika mwaka wa 2006, pia umedhibitisha madai kwamba fedha zilizofadhiliwa kuendeleza miradi ya kiafya ziliibiwa na hakufaidi waathiriwa. Tatizo hili linapaswa kukomeshwa na serikali ili wafadhili waendelee kufadhili sekta ya kiafya katika mataifa yanayoendelea.

#### 6.2.3.5 Uwajibikaji

Njia mbalimbali za kuepukana na maambukizi ya UKIMWI zimefafanuliwa katika matini teule. Katika matini teule *Kosa la Marehemu* wanajamii wanashauriwa waepukane na matumizi ya vifaa vyenye ncha kali vilivyotumiwa na mtu mwingine, wauguzi wawe makini wanaposaidia kina mama kujifungua ili damu ya mama na mtoto isiungane na kuepuka kuongezwa damu ya mtu aliyeambukizwa UKIMWI.

Katika kitabu kiteule *Madhila ya Bi. Shufaa* daktari amefafanua njia zinazosambaza ugonjwa wa UKIMWI. Tazama Kielelezo 34:

> Kuna mambo mengi yanayoweza kusababisha UKIMWI. Unaweza Kuambukizwa kwa *utumiaji wa sindano zilizotumika na mtu mwenye*

> *ugonjwa huo. Pia unaweza kutokana na kufanya mapenzi na mtu aliyeambukizwa. Mtoto anapozaliwa na mama mwenyevirusi* (uk.18).

Njia zingine zinazosababisha UKIMWI zimeangaziwa katika Kielelezo 34. Ingawa daktari amefafanua njia hizo, uchanganuzi wa vitabu teule umedhihirisha ya kwamba njia hizo zinaweza kuepukwa.

### 6.2.3.6 Kuhamasisha Jamii

Uchanganuzi wa data katika utafiti huu umedhihirisha kuwa kulikuwa na haja ya kuhamasisha jamii kuhusu visababishi na madhara yanayosababishwa na ugonjwa wa UKIMWI, ili kila mtu achukue hatua zifaazo za kuuzuia. Katika matini teule *Sitaki Iwe Siri* Musa alichukua hatua hiyo kwa kuandika insha iliyohusu UKIMWI. *Sitaki Iwe Siri* ni sitari ya kiafya iliyowakilisha uhamasishaji wa jamii kuhusu UKIMWI. Aidha, barua aliyoiandika iliwakilisha taswira ya mwangaza. Aliandika insha ya kufana kuhusu haja ya kuweka wazi suala la UKIMWI, kwa kupuuza mielekeo hasi ya kijamii iliyochukulia ugonjwa huo kama laana. Huu ulikuwa mwamko mpya uliolenga kusawiri UKIMWI kama magonjwa mengine na kuondoa uhasama kwa wagonjwa wa UKIMWI. Mawazo ya Musa yanaafikiana na ya WHO (2003) kuwa kado na UKIMWI, kuna magonjwa mengine hatari kama vile malaria na kifua kikuu yanayoua watu kwa wingi na yote yanapaswa kushughulikiwa kwa pamoja. Tathmini ya kauli hizi ni kwamba, UKIMWI sio zao la laana yoyote ile na wagonjwa wa UKIMWI hawapaswi kubaguliwa bali kuchukuliwa kama vile wagonjwa wengine wanavyochukuliwa katika jamii. Wanapaswa kupendwa, kuhudumiwa na kuhusishwa katika shughuli zote za kijamii kama vile kualikwa katika sherehe na kadhalika. Musa alifaulu kufanya hayo kwa kuandika insha ya kitaifa *Sitaki iwe Siri*, iliyofaulu kuhamasisha jamii kuhusu visababishi na hatua za kuzuia maambukizi ya UKIMWI na kuondoa kasumba ya kuhusisha UKIMWI na laana.

Tathmini ya njia za kuzuia magonjwa zilizoangaziwa katika matini teuleni ni kwamba, mtu binafsi ana nafasi ya kwanza katika kujikinga na UKIMWI. Ingawa ushauri wa madaktari ni muhimu ugonjwa huo hauna tiba na ni mtu binafsi aliyekuwa na uwezo wa kujikinga asiambukizwe. Hata hivyo, mwathiriwa anashauriwa asife moyo bali atembelee vituo vya afya ili apate mawaidha, kwa sababu ana nafasi ya kuishi maisha bora akizingatia kwa makini ushauri wa daktari. Aidha, wagonjwa wa UKIMWI

hawapaswi kutengwa wala kudhulumiwa katika jamii kwa sababu UKIMWI ni ugonjwa kama magonjwa mengine.

### 6.3 Dhuluma za Kijinsia

Uchanganuzi wa data katika vitabu teule umedhihirisha namna jinsia ya kike inavyokandamizwa na kudhulumiwa kupitia tamaduni hasi za kijamii zinazoegemea kuumeni na kuathiri afya yao. Hali hiyo pia inaathiri uzalizaji mali na kuafikiwa kwa maendeleo endelevu kwa sababu wanawake pia wanahusika katika majukumu yanayoimarisha uchumi katika jamii. Hynes (1989) anashadidia kwa kusema kuwa, tendo la kunyang'anya wanawake uwezo wa kujiendeleza kumeathiri uwezo wao wa kushiriki katika maendeleo ya kijamii kama anavyoshiriki mwanaume. Katika utafiti huu udhalilishwaji wa jinsia ya kike umeangaziwa katika matini teule *Madhila ya Bi. Shufaa, Pendo katika Shari* na *Nimefufuka.*

#### 6.3.1 Visababishi vya dhuluma za kijinsia

Utafiti huu umebainisha njia zifuatazo zinazosababisha unyanyasaji wa jinsia ya kike kama ilivyoangaziwa katika matini teule *Madhila ya Bi. Shufaa, Pendo katika Shari* na *Nimefufuka.*

##### 6.3.1.1 Utamaduni

Katika matini teule *Pendo katika Shari,* Sulubu anatumia tamaduni hasi za kijamii zinazoegemea upande wa kuumeni kumdhalilisha mkewe kwa kumtukana na kumtesa bila kumpa nafasi ya kujiamulia. Maelezo ya mwandishi katika kitabu teule yamechora picha ya mwanaume katili na mkiukaji wa haki za binadamu. Taswira hii imemsawiri Sulubu kama mlevi na mtu hohehae. Alikuwa na tabia ya kufika nyumbani usiku akiwa mlevi na mara nyingine alilala nje. Kwa upande mwingine Pendo amesawiriwa kama mwanamke aliyefungwa na minyororo ya utamaduni. Pendo hakumkosoa bwanake na aliendelea kunyamaza kwa kuogopa tamaduni za kijamii zilizomkadamiza mwanamke na kumzuia kumuuliza mwanaume maswali. Tazama Kielelezo 35:

> Lakini kwa vile *utamaduni wake ulimfunza kutomdadisi mume anapochelewa kurejea nyumbani, hakutaka kwenda kinyume na ada hii*. Isitoshe, alifunzwa kutomtia ghadhabu mumewe, na kila wakati kujaribu kudumisha amani katika nyumba yake (uk.2).

Taswira ya nguvu za utamaduni na miiko ya jamii imeangaziwa katika Kielelezo 35. Mwandishi ameonyesha jinsi utamaduni ulivyomdhibiti mwanamke kiasi kwamba asingedhubutu kubishana au kumshauri mumewe kwa kuogopa kuenda kinyume na mila na desturi za kijamii. Hali hii iliendeleza udhalilishwaji wa jinsia ya kike ambayo pia iliathiri hali yao ya kiafya.

Vilevile, desturi na mila za kijamii zilihusisha ukosefu wa kupata mtoto na shida za uzazi na mwanamke. Sitiari ya kiafya *safi safina* ilitumiwa na Sikitu kurejelea hali hiyo. Jamii haikuamini kuwa shida ya kupata mtoto ingeweza pia kutokea kwa mwanaume. Kwa msingi huu, Sikitu alidhulumiwa na kutukanwa kwa kuitwa tasa ilhali alifahamu kuwa alikuwa na uwezo wa kupata mtoto. Hata hivyo, Sikitu alimshuku bwanake kwa kutokuwa na nguvu za kuzaa na akapendekeza atembelee vituo vya afya kukaguliwa uwezo wake wa uzazi. Tazama Kielelezo 36:

> Wataalamu wa kunga na tiba walionikagua walisema sehemu zangu za uzazi hazina kasoro. ‘Ukituliza akili, utapata mtoto,’ walinipa moyo. Mume alikataa katakata himizo la kwenda hospitalini. Alisema *ukosefu wa uwezo wa kupata mtoto ni shida ya mwanamke. ‘Wanaume ni safi safina na ikiwa tatoka kasoro, hiyo ni kasoro ya mwanamke*,’ nayakumbuka maneno haya kwa uchungu usio na mfano (uk.9).

Sitiari ya kiafya *safi safina* katika Kielelezo 36 ni taswira ya ubabedume. Sikitu ametumia sitiari hiyo kuonyesha namna wanaume walivyochukuliwa kama malaika asiyekuwa na makosa katika jamii. Wanawake walihusishwa na maovu mbalimbali yaliyotokea katika jamii ilhali wanaume walisawiriwa kama viumbe ambavyo havingeweza kuathiriwa na chochote. Mfumo wa ubabedume uliotawala katika jamii ulichangia katika kuendeleza itikadi na tamaduni hasi za kijamii.

Katika matini teule *Nimefufuka,* Mhusika Upendo anashtumu tamaduni za kijamii zinazomdhalilisha mwanamke kwa tuhuma kwamba, mwanamke alichangia katika kuamua jinsia ya mtoto ambaye angezaliwa. Tazama Kielelezo 37:

> Ingawa tuko katika karne ya ishirini na moja, *inakera kuwa baadhi ya jamii bado zinashikilia tamaduni finyu, tamaduni zilizopitwa na wakati. Tamaduni zinazowabagua wasio na nguvu za kupigania haki zao.* Iweje wakwe zako wakuamulie utasa na kukutesa bila shemeji kwenda

> kuchunguzwa na madaktari? Kwa nini iwe mke kalaumiwa ikiwa dhahiri shahiri kwamba dosari iko upande wa mume? (uk.20).

Taswira ya ukandamizwaji wa jinsia ya kike pia imeangaziwa katika Kielelezo 37. Upendo analaumu tamaduni ambazo zinaendeleza ubabedume ilhali jamii inapaswa kubadilika jinsi ulimwengu unavyobadilika kisiasa, kiuchumi, kielimu na kiteknolojia. Hata hivyo, mizizi ya utamaduni inaonekana kuzama hivi kwamba ni vigumu kwa jamii kubadilika.

Isitoshe, unyanyasaji wa kijinsia umejitokeza katika matini teule *Nimefufuka,* pale ambapo wanawake wananyimwa nyadhifa za uongozi katika jamii kwa sababu ya mila na desturi zilizodunisha jinsia ya kike. Mhusika Chaurembo anazungumzia udhalilishwaji wa wanawake katika barua aliyomwandikia dadake, huku akimpongeza kwa kushinda kiti cha udiwani katika eneo la utawala la Matumaini.
Tazama Kielelezo 38:

> Kwanza, pongezi kwa kushinda kiti cha udiwani cha kata ya Matumaini. Nawavulia kofia watu wa Matumaini, ulikoolewa, kwa kukuchagua. *Watu wa kwetu wa Mjibalaa bado wanaadamwa na balaa ya kuyazingatia mambo ya zamani. Wanasumbuliwa na taasubi za kiume. Wanaamini nafasi ya mwanamke ni nyumbani, kutunza familia na kulea watoto* (uk.24).

Mazungumzo baina ya Chaurembo na Upendo katika Kielelezo 38 yanaonyesha taswira ya nguvu za tamaduni na miiko ya kijamii inamnyima mwanamke nafasi ya kushindana na wanaume katika nyadhifa za kikazi na uongozi. Hivyo, Chaurembo anadunisha mila zinazomfungia mwanamke nyumbani na kumtenganisha na jamii pana. Mazungumzo kati ya Chaurembo na Upendo yanaonyesha mwamko mpya wa wanawake wa kutambua hali waliyomo na umuhimu wa kupigania haki zao. Aidha, wanatoa kauli kwamba kulikuwa na haja ya jamii kuachana na tamaduni ambazo zilimnyima mwanamke nafasi ya kuongoza, kujieleza na uhuru wa kushirikiana na kutangamana na jinsia ya kiume katika ujenzi wa kitaifa. Uchanganuzi wa data katika matini teule umedhihirishwa kuwa, ili jamii iweze kukua na kuendelea, ushirikiano wa wanajamii wote wakiwemo wanaume, wanawake na watoto ulihitajika kwani kila mmoja alikuwa na wajibu wa kutekeleza. Hivyo, kudhibitiwa kwa jinsia ya kike na mila za kijamii zinakuamisha maendeleo na juhudi za kuafikiwa kwa maendeleo endelevu.

Utafiti huu pia umegundua kuwa majina yanayopewa watoto hasa wa kike yanachangia katika kueneza dhuluma dhidi za kijinsia. Hii imedhihirishwa na Upendo aliposhtumu tamaduni za kijamii zinazowapa watoto wa kike majina ya udhalilishwaji kama vile Sikitu. Mhusika Upendo amethibitisha madai yake kwa kusema kuwa kulikuwa na haja ya kuwapa watoto wa kike majina ya kutia moyo na yanayosawiri kufaulu katika maisha.

Tazama Kielelezo 39:

> Mpwa wangu yanayotokea katika boma letu ni *vielelezo vya uozo katika jamii nzima*. Kwanza naelekeza hasira zangu kwa kaka na shemeji. *Walikosa kwa kukuita Sikitu. Jina ambalo linakudhalilisha na kukufanya kuhisi eti wewe si kitu. Jina ambalo linawapofusha na kuwapotosha watu wasione thamani yako, utu wako, urembo wako, afya yako, mlahaka wako.* Nimeamua kuanzia leo nitakuita Chaurembo (uk.18).

Upendo katika Kielelezo 39 analalamikia mtindo hasi wa  kuwapa watoto wa kike majina. Alionyesha uwezo wa majina katika kuathiri utu na tabia ya mtu. Anamendeza kuwa watoto wapewe majina ya kuwatia moyo kama vile Chaurembo. Hii ni kuonyesha kuwa majina ambayo wazazi huwapa watoto huathiri tabia zao. Watoto wanapaswa kuitwa majina yanayotokana na mambo na hulka nzuri kama vile Amani, Rehema, Mwema miongoni mwa mengine.

**6.3.1.2 Ndoa**

Katika kitabu kiteule *Pendo katika Shari* ndoa imesawiriwa kama pingu ya kumfunga mwanamke nyumbani. Mhusika Pendo aliwajibika kwa kuwatunza watoto peke yake wakati ambapo Sulubu alistareheka na wanawake mjini, huku akiponda raha na mali bila kuitunza familia yake. Sulubu alipofika nyumbani alimshambulia na kumtusi Pendo bila huruma.  Pendo alivumilia mateso hayo yote na kujitahidi kudumisha ndoa yake na kumpenda bwanake kwa dhati. Tazama Kielelezo 40:

> Pendo *alitia masikio pamba kwa matusi yote aliyokuwa akitukanwa* na Sulubu kwani alimpenda kwa dhati na hakutaka kutengana naye. Kwa hivyo *alivumilia vitimbi vya mumewe kwa unyenyekevu* uliowashangaza marafiki na majirani zake. Aidha, alijinunulia gari jekundu aina ya *Prado* ambalo sasa *alilitumia kuivinjari mitaa ya mji akijifurahisha na marafiki zake* (uk.2-3).

Kielelezo 40 kinaangazia tabia ya Pendo na Sulubu. Kupitia tabia ya Pendo, mwanamke amesawiriwa kama mtu mvumilivu, mwenye upendo, mnyenyekevu na mtiifu, sifa ambazo zinapiku binadamu wa kawaida. Kwa upande mwingine, Sulubu amesawiriwa kama mwanaume katili, mpenda anasa, mnyanyasaji na mtu asiyekuwa na utu. Utukutu wa Sulubu unawashangaza marafiki na watu kijijini, ilhali utu wa Pendo unakuwa kielelezo cha kutiliwa mfano na wanajamii wenzake. Tathmini ya hulka za Pendo na Sulubu ni kwamba, mapenzi kati yao yalikuwa katika njia panda na ndoa yao ingeweza kusambaratika wakati wowote. Ingawa Pendo alijaribu kujenga ndoa yao kwa uvumilivu na upendo, Sulubu alikuwa akiibomoa kwa bughudha na kutowajibika kama baba nyumbani.

Kutokana na mchango wa ndoa katika kuendeleza unyanyasaji wa kijinsia, Greer (1971) anawaihimiza wanawake kususia kuolewa kwa sababu kunawatumbukiza katika kumilikiwa na wanaume na kunyimwa haki na uhuru wao. Hata hivyo, kauli ya Greer (keshatajwa) ikizingatiwa na kila mwanajamii, itaathiri asasi ya ndoa na kuangamiza vizazi vijavyo. Ni muhimu kutambua kuwa si kila ndoa imeathiriwa na vita vya kijamaa kwani baadhi ya ndoa kama vile ya Bwana Iddi na Bi. Shufaa katika matini teule *Madhila ya Bi. Shufaa,* zilidhibitiwa kwa upendo na amani na kuchangia katika maendeleo ya jamii. Tazama Kielelezo 41:

> Katika kijiji cha Mangelepa, *mzee Iddi alifahamika mno. Alifanikiwa kuwa na mke mwenye adabu na hekima. Watoto wake wawili, Amina na Zuhura, walikuwa kama mboni ya jicho lake*. Aliwapenda si haba.

Taswira ya ndoa bora imesawiriwa katika Kielelezo 41. Mkewe mzee Iddi aliyeitwa Bi. Shufaa, alijulikana kama ‘ Mama Safi.’ (uk.2). Ndoa ya mzee Iddi na Bi. Shufaa ni mfano wa ndoa iliyokuwa na utulivu na uwajibikaji wa wazazi, kinyume na ndoa ya Sulubu na Pendo iliyotawaliwa na ubabedume. Sulubu alitumia mila kama silaha ya kujificha na kukiuka majukumu yake nyumbani kwa kisingizio kwamba, mwanamke hakuwa na mamlaka ya kumwelekeza au kumshauri. Taasubi za kiume za Sulubu zilisababisha kusambaratika kwa ndoa yake.

#### 6.3.1.3 Imani Potovu

Imani kwamba wanawake ni jinsia duni imechangia katika kuendeleza unyanyasaji wa wanawake katika nyanja za kiuchumi, kisiasa, na kikazi. Vilevile, imani kwamba

wanawake ndio huamua jinsia ya mtoto atakayezaliwa ilichangia katika kutenganisha Bibi na Bwana ikiwa watoto wa jinsia moja wangezaliwa. Sulubu anatumia suala hilo kumtesa Pendo kwa tuhuma kuwa, anamzalia wasichana pekee ilhali alihitaji pia vijana. Ukosefu wa mtoto wa kiume unakuwa mwanzo wa mateso ya Pendo.
Tazama Kielelezo 42:

> " Jambwe! *Mke gani wewe unayenizalia majana jike tu hapa nyumbani*." Mimi nitatiwa kundi vipi na wenzangu ikiwa sina mtoto wa kiume atakayeniridhi."? (uk.6).

Mazungumzo ya Sulubu katika Kielelezo 42 yanaonyesha namna imani potovu ilivyochangia katika kuendeleza udhalilishwaji wa wanawake pia na watu walioelimika kama vile Sulubu. Ingawa Sulubu alisoma na kuajiriwa, imani kuwa suala la uzazi ni la wanawake pekee lilimtawala. Malalamiko kuwa Upendo alimzalia wasichana pekee bila kuchanganya na jinsia ya kiume yalimuumiza Pendo kimawazo na kimwili.

### 6.3.2 Kusuluhisha dhuluma za kijinsia

Utafiti huu umebainisha haja ya kukabiliana na dhuluma za kijinsia kwa kuzingatia haki za binadamu ili kuimarisha umoja na ushirikiano katika jamii. Baadhi ya njia za kukabiliana na dhuluma hizo ni:

#### 6.3.2.1 Kusomesha Vijana wa Kike

Elimu ni kama kurunzi inayotoa nuru gizani na kumulika chochote kilichofichika. Jamii inapoelimisha wasichana, inawafungua macho na kupiga vita vizingiti vya kimila vinavyowadunisha na kuwazuia kushiriki katika kiwango sawa na wanaume. Wahusika Haki na Ukwa katika matini teule *Sitaki Iwe Siri* walipata elimu ya juu na wakawa mifano bora ya wanawake waliojitolea kukabiliana na matatizo yaliyoathiri jamii. Walisafiri hadi ughaibuni kuhamasisha jamii kuhusu athari za UKIMWI ingawa tamaduni mbalimbali zilichukulia ugonjwa huo kama laana. Hii ilikuwa hatua kubwa ya kupiga vita tamaduni hasi zilizomzuia mwanamke kuchukua nyadhifa za uongozi katika jamii. Katika kitabu kiteule *Nimefufuka* Upendo alipigania kiti cha udiwani na na akafaulu licha ya kuwa mwanamke. Hata hivyo, analalamikia tamaduni hasi zilizoegemea upande wa kuumeni zilizodunisha uwezo wa mwanamke katika

kutekeleza majukumu yaliyotekelezwa na mwanaume. Utafiti huu umependekeza kuwa jamii itupilie mbali tamaduni zinazomkandamiza mwanake na jinsia zote zipewe nafasi sawa

#### 6.3.2.2 Sera ya Serikali

Kuna haja ya serikali kubuni sera inayowapa wanawake nyadhifa nyingi za uongozi. Katika sera hiyo wanawake watengewe asilimia hamsini ya fursa za ajira ili waepuke mashindano na wanaume na waweze kujipigania wao wenyewe kwa kuonyesha umahiri wao katika utendaji wa kazi. Katika matini teule *Nimefufuka* Upendo alidhihirisha uwezo wa utenda kazi wa wanawake alipoteuliwa na wananchi na kupewa kazi ya udiwani. Alijitokeza kama mwanamke jasiri na aliyetenda kazi yake kwa bidii na ufanisi mkubwa licha ya kupingwa na baadhi ya wanaume. Vilevile, Upendo alitumia fursa hiyo kutetea haki za wanawake ingawa alikumbana na pingamizi chungu nzima kutoka kwa wanaume waliotawaliwa na taasubi za kiume. Kupitia mhusika Upendo, utafiti huu umedhihirisha kwamba mwanamke ana uwezo sawa na mwanaume na anapaswa kupewa nafasi katika nyadhifa zote za uongozi.

## 6.4 Dawa za Kulevya

Kwa mujibu wa Kandel na Chen (1995), vijana huanzia kutumia dawa za kulevya mapema kwa sababu ya matatizo ya kiuchumi, mazoea ya kitamaduni na shinikizo za rika. Aidha, vijana wanapojiunga na ulevi jamii huelekea kuangamia kwa sababu vijana ndio jamii ya baadaye. Gathumbi (2003) anashadidia kwa kusema kuwa kuongezeka kwa matumizi ya mihadarati kumeathiri zaidi vijana. Ili kukabiliana na ongezeko la dawa za kulevya, taaluma ya fasihi ya Kiswahili pia imechangia katika kuangazia suala hilo kwa lengo la kutahadharisha jamii dhidi ya madhara yake. Kulingana na Wamitila (2008), fasihi ina wajibu muhimu wa kutekeleza majukumu mbalimbali katika jamii kama vile kuelimisha, kuburudisha, kudumisha uhusiano, kukuza uadilifu na kuonya jamii dhidi ya masuala yanayoiathiri. Hii ndio sababu waandishi wa matini teule wameangazia masuala mtambuko kama vile dawa za kulevya. Baadhi ya dawa za kulevya zinazotumiwa na zinazoathiri afya ya watu ni bangi, heroini na pombe za kienyeji kama vile chang’aa na busaa. Dawa zingine za kulevya zinazotumiwa lakini zimeruhusiwa kisheria nchini Kenya ni miraa, muguka, tumbaku, sigara na pombe. Athari inayotokana na matumizi ya dawa za kulevya ni kwamba, zinaleta msisimko na

kuathiri ubongo na mawazo ya mtumizi. Ni muhimu kuzuia kupanuka kwa matumizi ya dawa za kulevya kwa kuhamasisha jamii kuhusu athari zinazotokana na matumizi mabaya ya dawa hizo. Kuongezeka kwa matumizi ya dawa za kulevya kunaathiri afya ya watumizi na kutatiza juhudi za kuimarisha viwango vya afya ulimwenguni. Jose, Utingo, Makelele na Sulubu ni baadhi ya wahusika walioathiriwa na dawa za kulevya katika matini teule.

### 6.4.1 Kukabiliana na Dawa za kulevya

Kwa mujibu wa Kaguthi (2004) nchi ya Kenya na mataifa yanayoendelea yameathiriwa na ongezeko la dawa za kulevya hivi kwamba, matumizi yake yamesambaa hadi kwa wanafunzi kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu. Utafiti huo pia ulibaini kuwa, watoto wachanga wa miaka kumi wametumia dawa za kulevya kama vile Miraa, Tumbaku, Bangi, Pombe na Gundi. Ripoti ya NACADA (2007) inashadidia kwa kusema kuwa, matumizi ya dawa za kulevya yameenea na kuathiri watoto na watu wazima. Miongoni mwa dawa za kulevya zinazotumiwa ni miraa, bangi, pombe, sigara, tumbaku, kokeni, muguka na dawa za kuvuta kama vile petroli na gundi. Kuna haja ya kukabiliana na janga la dawa za kulevya, ili kuimarisha afya ya binadamu na kuafikiwa kwa maendeleo endelevu katika mataifa mbalimbali ulimwenguni. Ili kufaulu katika vita dhidi mihadarati, juhudi kabambe zinapaswa kuhimizwa katika taasisi za kielimu, kiwango cha jamii na kitaifa.

#### 6.4.1.1 Taasisi za Kielimu

Kaguthi (2004) anaeleza kuwa dawa za kulevya zimeenea hadi taasisi za kielimu na zimeathiri masomo na kusababisha wanafunzi kuacha shule na wengine kuathiriwa kiafya. Taasisi hizi zinajumuisha shule za msingi, sekondari, vyuo vya kiufundi na vya elimu ya juu. Ili kuzuia athari na maenezi ya dawa za kulevya katika taasisi za elimu, njia zifuatazo zinapaswa kuzingatiwa:

Walimu walio na taaluma ya ushauri na ya kufunza wanafunzi walio na akili punguani wanapaswa kupewa vipindi maalum katika viwango mbalimbali vya elimu ili, kuwaelimisha wanafunzi dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya. Katika shule za msingi walimu wanaweza kutumia nyimbo, ushairi na maigizo katika kuwaelekeza na kuhamasisha wanafunzi kuhusu athari za dawa za kulevya. Katika shule za sekondari

na taasisi za juu za elimu, walimu wanaweza kukabiliana na matumizi ya dawa za kulevya kwa kuwa na siku maalum za kukagua wanafunzi ikiwa wanatumia dawa hizo. Vilevile, walimu wanaweza kupanga vipindi maalum vya kuwashauri wanafunzi kuhusu madhara yanayosababishwa na dawa za kulevya. Pia, walimu wanapaswa kushughulikia wanafunzi walioathiriwa na dawa za kulevya kwa kuwahusisha wahudumu wa kiafya. Hata hivyo, ni muhimu kuzingatia mawazo ya Fetsch na Yang (1990) kuwa, waathiriwa wa dawa za kulevya wanapaswa kushughulikiwa kwa makini. Hii ni kwa sababu ikiwa wamezitumia kwa muda mrefu, kuwazuilia kuzitumia mara moja kutawaathiri zaidi. Hivyo, watu walioathiriwa na dawa za kulevya wanapaswa kufunzwa kuacha kuzitumia polepole.

#### 6.4.1.2 Kiwango cha Jamii

Wanajamii pia wana nafasi muhimu katika kuzuia matumizi na kuenea kwa dawa za kulevya kwa sababu wanaouza na kusambaza mihadarati wanaishi katika jamii. Hivyo, jamii inahitajika kuwa katika mstari wa mbele katika kuzuia matumizi ya dawa za kulevya. Ili kunasa wanaosambaza mihadarati, wanajamii wanapaswa kuunda vikundi maalumu vya kuchunguza na kunasa wauzaji wa dawa za kulevya na kuwapeleka katika vituo vya polisi. Pia, vikundi hivi vinahitaji kuwa na kanuni zinazozingatiwa na jamii katika matumizi ya pombe zilizokubaliwa ili watoto na wanafunzi wasizitumie. Hii ni kwa sababu matumizi ya mapema ya pombe kwa watoto huathiri tabia yao hata wanapokua. Kwa mujibu wa Purns na Mach (2009), asilimia 40 ya watu waliotumia pombe kabla ya umri wa miaka 14 hukumbwa na matatizo ya kushindwa kuiacha. Utafiti huu pia umebaini kuwa ni nadra kwa watu walioanza kutumia pombe wakiwa katika umri wa miaka 20 kuendelea kuitumia. Kati ya watu hao ni asilimia 10 pekee wanaoweza kuendelea kutumia dawa za kulevya. Hivyo, ni muhimu kuzuia watoto kuanza kutumia dawa za kuleya mapema ili kuzuia mazoea ya kuendelea kuzitumia.

#### 6.4.1.3 Kiwango cha Kitaifa

Serikali inapaswa kuwa na sera maalumu ya kuzuia matumizi na kuenea kwa dawa za kulevya. Sera hiyo inahitaji kuharamisha matumizi ya dawa za kulevya katika taifa na kutenga fedha za kugharamia utekelezaji wa mikakati ya kupambana na dawa za kulevya. Vilevile, maafisa wa utawala wanapaswa kushtaki maharamia wa dawa za

kulevya bila kuchukua hongo na kutumia mabaraza kuhamasisha jamii dhidi ya matumizi ya dawa hizo.

Vilevile, shirika la NACADA linapaswa kupewa uwezo zaidi wa kushtaki na kupambana na biashara ya dawa za kulevya. Kadhalika, shirika hilo linahitaji kupeperusha vipindi katika vyombo vya habara kila mara, kuhamasisha jamii kuhusu madhara yanayosababishwa na dawa za kulevya. Zaidi ya hayo linapaswa kuhakikisha kuwa, vileo vilivyokubaliwa pekee ndivyo vinapewa leseni na wauzaji wakikiuka sheria zilizowekwa vinyang'anywe leseni . Kwa ujumla vita dhidi ya dawa za kulevya ni jukumu la kila mtu. Ili kushinda vita dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya ni muhimu kuwe na ushirikiano baina ya mtu binafsi, serikali na mashirika ya kijamii.

### 6.4.2 Athari za dawa za Kulevya

Kwa mujibu wa Mdee na wengine (2022), athari ni matokeo mazuri au mabaya ambayo yanampata mtu baada ya kupitia hatua fulani. Utafiti huu ulichunguza athari zinazotokana na matumizi ya dawa za kulevya na watu mbalimbali katika jamii kwa mujibu wa matini teule *Nimefufuka* na *Pendo katika Shari*. Baadhi ya athari zilizoangaziwa ni kuongezeka kwa uhalifu, athari za kiafya, athari za kiuchumi na mizozo ya kifamilia.

#### 6.4.2.1 Kuongezeka kwa Uhalifu

McCabe na wengine (2009) wanadai kuwa matumizi mabaya ya dawa za kulevya yamekuwa janga la kimataifa. Dawa za kulevya zimeathiri tabia ya vijana kote ulimwenguni na kusababisha kuongezeka kwa uhalifu nyumbani na katika miji mbalimbali. Kulingana na uchunguzi wa Gathumbi (2003), asilimia 20 ya vijana waliokuwa katika umri wa kati ya miaka 12 na 22 wanavuta sigara, asilimia 9 wanavuta bangi na asilimia 23 wanakunywa pombe. Kwa sababu ya kuongezeka kwa vijana wanaotumia aina mbalimbali za dawa za kulevya kama ilivyoangaziwa na Gathumbi (keshatajwa), wizi na uhalifu wa aina mbalimbali umeendelea kuongezeka katika jamii.

Katika matini teule *Nimefufuka*, suala la matumizi ya dawa za kulevya limepewa kipaumbele kwa jinsi ambavyo dawa hizo zilivyoathiri vijana katika Mjibalaa. Mhusika Sikitu analilia kuokolewa kwa vijana waliopotoka kinidhamu katika Mjibalaa na

kuomba usaidizi wa kutoja nje ili, kuwanusuru vijana waliotekwa na dawa za kulevya na ufasiki. Matumizi ya dawa hizo yameathiri vijana kiasi kwamba wengine wamepagawa na kuwa tatizo katika jamii. Kilio cha Sikitu kuhusu athari ya mihadarati, kinazidishwa na tabia ya Jose aliyebadilika kwa sababu ya kuingilia mihadarati kinyume na matarajio yao. Tazama Kielelezo 43:

> Hakuna kileo ambacho Jose hajakitumia: *sigara kubwa*, *sindano*, *miraa*, *muratina, chang'aa,kumikumi, chibuku*- vyote amevitumia. Ameingilia uhalifu wa kila aina: *uporaji*, *ulaghai*, *ukahaba*, ilmuradi apate fedha za kununua vileo na kupumbaza akili zake (uk.14).

Maovu yanayosababishwa na matumizi ya dawa za kulevya yamezungumziwa katika Kielelezo 43. Jose ambaye ni kijana wa makamo ametumia mihadarati kiasi kwamba imeharibu tabia yake. Amesawiriwa kama mlevi sugu aliyetumia kila aina ya dawa za kulevya kiasi kwamba, hajali maisha yake ya baadaye. Somo linaloangaziwa kupitia tabia ya Jose ni kwamba wazazi, serikali na washikadau wanapaswa kushughulikia mahitaji ya watoto na kuwarekebisha kitabia wakiwa wachanga, kwani ni vigumu kubadili mienendo yao wanapokua. Wazazi wanapaswa kuwajibika na kuwa na watoto kwa muda mwingi ili waweze kutambua mapema mabadiliko yao ya kitabia. Hii ni kwa sababu ni rahisi kurekebisha tabia ya mtoto akiwa mchanga kuliko kumrekebisha akiwa mtu mzima. Pia, wanajamii wana jukumu la kuzingatia mienendo miema ili wawe vielelezo vya kupigiwa mfano na vijana. Isitoshe, katika mji wa Mjibalaa matumizi ya dawa za kulevya yalisababisha watoto kuacha shule. Jose anawakilisha vijana ambao walitupa shule kwa sababu ya kutumia mihadarati. Hata siku hizi matumizi ya dawa za kulevya yamechangia katika kusababisha upotovu wa nidhamu miongoni mwa wanafunzi. Jambo hili limeshuhudiwa pia katika jamii ya sasa ambapo vijana wanaotumia dawa za kulevya wamechoma shule na wengine kujitoa uhai. Hivyo, kuna haja ya wazazi kufunza watoto maadili mema tangu utotoni ili waweze kujikinga na janga la mihadarati wanapokuwa watu wazima. Vilevile, serikali inapaswa kutilia maanani somo la dini na kujumuishwa kwa somo linalohusu matumizi ya dawa za kulevya katika mitaala ya elimu, ili kufahamisha vijana mapema kuhusu athari za mihadarati. Jose alijiunga na uraibu wa mihadarati kwa sababu wazazi wake pia walikuwa walevi na hawakuwa na muda wa kumkosoa.

#### 6.4.2.2 Mizozo katika Familia

Umoja na ushirikiano katika familia ni nguzo muhimu katika kuafikiwa kwa maendeleo endelevu katika jamii. Hata hivyo, baada ya kuchanganua data katika matini teule, imebainika kuwa matumizi ya dawa za kulevya yametenganisha wazazi na pia watoto kwa sababu ya kuwepo kwa mizozo ya kila mara. Katika matini teule *Pendo katika Shari,* mhusika Sulubu ameingilia unywaji wa pombe na kubadilika kitabia hivi kwamba majirani wanafadhaika. Upendo anatumia sitiari *mume jina* kama taswira kuonyesha kutowajibika kwa Sulubu. Sulubu alianza kufika nyumbani akiwa mlevi na mara nyingi alilala nje, jambo lililoathiri uhusiano wake na mkewe Upendo aliyekesha akimngoja. Licha ya hayo, Sulubu alisusia wajibu wake kama baba wa watoto na akamwachia Upendo shughuli zote za kifamilia. Upendo aliteseka kwa ukosefu wa amani, upendo, malazi na afya bora. Tazama Kielelezo 44:

> Pendo alikuwa *mja mzito*. *Kule kukesha siku nyingi akimsubiri mumewe kuliudhoofisha mwili wake na aghalabu alihisi kisunzi*. Wanawe watatu Chema, Almasi na Tatu walikuwa wanamsumbua na kumuuliza maswali ambayo hakuwa na majibu yake. *Walishangaa kwa nini baba yao hafiki nyunbani kama ilivyokuwa desturi yake* na kula chakula cha jioni pamoja nao (uk.1).

Jambo linalodhihirika katika Kielelezo 44 ni kwamba, tabia ya Sulubu haikuathiri Upendo pekee, bali pia iliathiri watoto ambao walikuwa na mazoea ya kujumuika pamoja na baba yao jioni. Hivyo, watoto hao walilia kwa upweke wa kumkosa baba mzazi. Hawakutosheka kuwa na mama peke yake kwani pia walihitaji upendo wa baba. Katika jamii ya sasa, unywaji wa pombe umekithiri katika jamii na umesababisha vita katika baadhi ya familia. Baadhi ya wanaume wanalala nje ya boma kwa kuzidiwa na ulevi. Kina mama wameachiwa jukumu la kuwalea watoto peke yao. Katika vyombo vya habari, kuna matangazo kadhaa yanayotolewa kuhusu ongezeko la unywaji wa pombe haramu ambayo imeathiri umoja na maendeleo katika jamii. Kuna haja ya wanajamii kuachana na unywaji wa pombe na washirikiane ili waweze kuwapa watoto masomo na malezi bora.

Matumizi ya dawa za kulevya pia yalisababisha uharibifu wa rasilimali za familia. Sulubu alitumia pesa kwa pombe huku familia yake ikilala njaa. Ingawa mhusika

Matano alijaribu kumshawishi kuachana na unywaji wa pombe na ukahaba Sulubu ailimsuta kwa kumwambia kuwa hakuelewa maisha ni nini. Tazama Kielelezo 45:

> "Wewe wajitia ushamba bwana. Unajifanya *mshago*. *Hujui maisha ni mafupi na ni lazima ule raha kwani karaha yaja*? *Vunja mifupa ikiwa bado meno ipo*." …………..Baada ya kulewa chopi, Sulubu alifululiza hadi chumbani mwake. (uk.13-14).

Usemi katika Kielelezo 45 unaonyesha jinsi Sulubu alivyochukulia maisha kiholela na kuendelea kuponda raha bila kujali hali ya familia yake. Usemi "*Vunja mifupa ikiwa bado meno ipo*" ni wa kisitiari na unaangazia taswira ya mtu mpenda anasa na asiyejali kuhifadhi akiba ya maisha ya baadaye. Hii ni tahadhari kwa watu walio katika ndoa kuwa, maisha ya anasa hutenganisha familia na ni muhimu kwa kila mtu kuwajibika katika kuitunza familia yake. Vilevile, utafiti huu umegundua kuwa rasilimali za kijamii kama vile pesa zinapaswa kutumiwa kwa mpango unaokubalika na ulio na manufaa kwa familia ili kuleta ushirikiano na kujenga uaminifu.

Katika matini teule *Nimefufuka* mhusika Jose amesawiriwa kama mwizi na mharibifu wa rasilimali za familia. Aidha, Jose alikuwa na mazoea ya kuiba na kuuza mali ya familia kwa bei nafuu bora tu apate fedha za kununua vileo. Tabia ya Jose ya kuharibu mali ya familia inamuudhi Sikitu na anamwandikia dadake kwa machozi na uchungu mwingi. Tazama Kielelezo 46:

> Ameingilia uharibifu wa kila aina; uporaji, ulaghai, ukahaba, ilmuradi apate fedha za kununua vileo na kupumbaza akili zake. *Vitu vya maana nyumbani vimeuzwa. Ameuza ile radio kubwa aina ya Sony. Ameuza runinga ya LG iliyokuwa ikituletea malimwengu ulimwenguni. Ameuza saraka na mitoto ya meza na kisha meza nzima. Zulia ilipata bei tulipokuwa kodeni tunaisaka tija. Kondoo walioletwa na mjomba wametoweka. Idadi ya kuku, sufuria, sahani, bakuli, vijiko, ni simulizi tupu* (uk.14).

Kielelezo 46 kinaangazia taswira ya mtu jambazi, mwizi na mhalifu sugu. Sikitu analia kwa uchungu kwa sababu ya uharibifu wa hali ya juu unaotekelezwa na Jose ambaye anauza chochote anachopata nyumbani. Jose ni taswira ya uharibifu na kiwakilishi cha walevi wanaotumia mali ya familia katika anasa na unywaji wa pombe. Jamii ya sasa pia imekumbwa na hali kama hiyo ambapo vijana wamejiunga na matumizi ya mihadarati na kuwa watu hohehae. Vijana hawa hawafanyi kazi na ili wajikimu kimaisha na wapate fedha za kunywa pombe huingilia kuuza mali ya familia jinsi

anavyofanya Jose. Kwa jinsi hii mtafiti anakubaliana na kauli ya McCabe na wengine (2009) kwamba, idadi ya watu wanaotumia dawa za kulevya inaongezeka kila uchao na kufanya matumizi ya dawa za kulevya kuwa janga la kimataifa.

**6.4.2.3 Kuzorota kwa Uchumi**

Matumizi ya dawa za kulevya pia yameathiri uzalishaji wa mali na uimarishaji wa uchumi katika maji. Jamii inayokua na kuendelea kiuchumi huwa na wafanyi kazi walio na afya bora na nguvu za kufanya kazi. Hata hivyo, matumizi ya dawa za kulevya yameathiri afya ya watu wanaozitumia na kusababisha utepetevu katika kufanya kazi. Vijana na watu wazima wanapotumia dawa za kulevya huwa wadhaifu na hupungukiwa na nguvu za kufanya kazi. Hali hii imedhihirishwa katika matini teule *Nimefufuka,* ambapo Mjibalaa umekumbwa na umaskini kwa sababu ya kuongezeka kwa watu ambao hawafanyi kwa sababu ya matumizi ya mihadarati. Katika matini teule *Pendo katika Shari* Sulubu anatumia pesa na mali yake katika ulevi na ukahaba. Tabia hiyo inamfanya Pendo kufungua biashara kwa sababu ya umaskini uliokithiri nyumbani.

**6.4.2.4 Kuzorota kwa Afya**

Mwili wa binadamu unahitaji kutunzwa vyema kwa kula lishe bora na kutembelea vituo vya afya ili uweze kuhimili na kuzuia maambukizi ya magonjwa mbalimbali. Hata hivyo, matumizi ya dawa za kulevya huathiri afya ya mtu na hata husababisha vifo. Haya yamedhihirishwa katika matini teule *Nimefufuka* na *Pendo katika Shari*.

Katika kitabu kiteule *Pendo katika Shari* mhusika Matano anamwonya Sulubu dhidi ya maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI. Sulubu alitia masikio nta na badala yake akaendelea kuponda mali. Hatimaye tabia ya Sulubu ilimtumbukiza katika janga la UKIMWI ambao pia alimwambukiza mkewe Pendo. Sulubu na Pendo waliathiriwa na UKIMWI ambao uliwadhoofisha kiafya na kusababisha kifo cha Sulubu. Ingawa Pendo alijuta kwa kuolewa na Sulubu, aliendelea kuitunza familia baada ya kifo cha Sulubu. Tazama Kielelezo 47:

> Pendo alianza kuyahakiki maisha yake na Sulubu kwa uangalifu na kuyaona kama *ndoto asiyopenda kuiota tena*. Hii ni kwa sababu ya uovu aliomfanyia yeye na wanawe. Upendo wake wa dhati kwa Sulubu uligeuka na kuwa shari isiyostahimilika (uk.65).

Sitiari ya kiafya *ndoto asiyopenda kuiota tena* katika Kielelezo 47 pia ya kitaswira inawakilisha mateso na maisha magumo ambayo Pendo alipitia mikononi mwa Sulubu. Mateso ambayo Pendo alipata pia yalijumuisha kuambukizwa ugonjwa wa UKIMWI uliomtaabisha kwa muda mrefu. Matatizo ambayo Pendo alipitia pia yamedhihirika katika jamii ya sasa. Unywaji wa pombe umeathiri na kusababisha kutengana kwa familia nyingi, maambukizi ya magonjwa ya UKIMWI na vifo. Hivyo, kuna haja ya serikali kuchukua hatua kuangamiza biashara ya pombe haramu ili jamii iweze kusimama. Vilevile, makanisa na vikundi vya kijamii vinapaswa kuanzisha kampeni dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya ili kuinusuru asasi ya familia katika maangamizi.

Katika kitabu kiteule *Nimefufuka* Sikitu analilia kusambaratika kwa familia yao kwa sababu ya matumizi ya dawa za kulevya. Anaeleza namna Jose alivyoathiriwa kiafya na dawa hizi kiasi kwamba hajitambui. Vilevile, wazazi wake ni walevi na hakuna anayemsaidia mwingine. Sikitu anaelezea athari za kiafya zilizomkumba Jose kwa kuangazia hatari inayotokana na unywaji wa pombe kupita kiasi. Tazama Kielelezo 48:

> Jana, nusura Jose *atupe mkono wa buriani*. Nilimwita daktari aliyenishauri nimpeleke hospitali kuu. Anasema hivyo vileo alivyobugia na kujidunga vimemkula viungo vya ndani. Jose anahitaji msaada, maaso na huruma nyingi. Naye pia aweze kujidhamini na ajue kwamba ni binadamu kama wengine (uk.15).

Sitiari ya kiafya '*atupe mkono wa buriani'* katika Kielelezo 48 inawakilisha hali mahututi ya Jose iliyosababishwa na matumizi ya mihadarati. Hali duni ya kiafya ya Jose pia imeathiri familia nzima kwa kuhitaji malezi bora na matibabu ambayo familia haikuweza kuyagharamia. Kwa hivyo, Sikitu anasema kuwa Jose amekuwa mzigo mzito kwake kwa vile wazazi pia walikuwa walevi. Jose ni mfano wa vijana walioathiriwa na matumizi ya mihadarati. Kwa hivyo, matumizi ya mihadarati yanapaswa kukomeshwa kwa sababu vijana ndio jamii ya baadaye na wanapoangamia jamii pia imeangamia.

#### 6.4.2.5 Kuathirika Kimasomo

Matumizi ya dawa za kulevya miongoni mwa wanafunzi yameathiri masomo kwa kusababisha utovu wa nidhamu shuleni. Kwa mujibu wa Gathumbi (2003) matumizi ya dawa hizo baina ya wanafunzi nchini kenya yamesababisha migomo shuleni na shule

nyingi kuchomwa. Gelinas (2006) anasema kuwa, wanafunzi wananunua dawa za kulevya kutoka kwa manamba ambao wanaziweka mahali ambapo wanafunzi wanaweza kuzifikia kwa urahisi. Wanafunzi huzitumia kwa kuzificha katika seti za hisabati. Kwa jinsi hii utovu wa nidhamu umeongezeka katika shule za sekondari na vyuo vikuu. Isitoshe, ripoti ya NACADA (2007) inasema kuwa, watumizi wengi wa mihadarati ni vijana wa shule za sekondari na vyuo vikuu na wengi wanapatikana katika miji ya Nairobi, Mombasa na Kisumu. Kuongezeka kwa matumizi ya mihadarati pia kumeongezea kuongezeka kwa maasi katika miji hiyo.

Katika kitabu kiteule *Nimefufuka*, matumizi ya dawa za kulevya yamekumba Mjibalaa kiasi kwamba vijana wanaacha shule. Mhusika Lena anaacha masomo na kukimbilia mjini Mombasa kuponda raha. Sikitu anafafanua madhara yanayotokana na matumizi ya mihadarati katika Mjibalaa kwa kusema mji huo ulihitaji ukombozi wa haraka. Tazama Kielelezo 49:

> Mjibalaa *umetembelewa na majanga, mikasa na misiba. Unahitaji tambiko la dharura. Pepo wanahitaji kupungwa hima* (uk.1).
>
> Dada yangu mdogo hakumaliza masomo ya shule ya upili. Alitorokea Mombasa eti *kuponda maisha*. *Kumbe maisha yalikuwa yakimngoja yamponde, yamfyonze*, *yasimbakishe hata chembe* (uk.2).

Maelezo katika Kielelezo 49 ni ya kisitiari yaliyowakilishwa na sitiari ya kiafya *majanga, mikasa na misiba*. Inawakilisha maovu yanayoiathiri afya ya watu. Mfano wa pili unawakilisha madhara ya kiafya yaliyompata Lena. Jambo linalodhihirika katika mazungumzo ya mhusika Sikitu ni kwamba, dawa za kulevya zimeathiri wavulana na wasichana kwa pamoja. Wanaacha masomo na kukimbilia anasa za maisha ambazo baadaye zinawaangamiza.

Wavulana pia wameathiriwa na dawa za kulevya. Sikitu analalamika kuwa Jose aliacha shule kwa sababu ya kujiunga na matumizi ya dawa za kulevya. Tazama Kielelezo 50:

> Maisha ya awali ya Jose yalikaribiana na ya Lena. Kitindamimba wetu alianza utundu mapema. Ikawa alazimishwe ndio aende shule. Amalize mazoezi, aende kanisani, afue nguo zake, ale, alale na mengine mengi. Maisha ya kufukuzana na kulazimisha yakawashinda wazazi. Wakamwacha afunzwe na dunia. *Nayo dunia imetimiza jukumu hilo* (uk.14).

Sitiari ya kiafya *nayo dunia imetimiza jukumu lake* iliyotumika katika Kielelezo 50 inawakilisha madhara ya dawa za kulevya yaliyompata Jose. Baadhi ya madhara hayo ni kuacha shule na kuathirika kiakili. Hivyo, jamii inapaswa kuwa na mikakati ya kuzuia uuzaji wa mihadarati kwa kufahamisha maafisa wa serikali maeneo yanayouzwa dawa za kulevya na wanaoziuza. Vilevile, walimu wanahitajika kuimarisha viwango vya nidhamu katika shule na kuelimisha wanafunzi kuhusu madhara yanayosababishwa na dawa za kulevya kama vile magonjwa ya kiakili.

**6.5 Hitimisho**

Masuala tambuko kama vile Suala la UKIMWI, dawa za kulevya na dhuluma za kijinsia yamejadiliwa kwa kina katika sura hii. Uchanganuzi wa data katika matini teule umedhihirisha ya kwamba, masuala haya yamekithiri katika jamii na yameathiri afya ya watu wengi. Imebainishwa kuwa ugonjwa wa UKIMWI umesababisha magonjwa na vifo katika baadhi ya wahusika kama vile Sulubu, Pendo na Rehema katika matini teule. Dawa za kulevya kama vile unywaji wa pombe haramu na Miraa pia zimechangia kudhoofisha afya ya binadamu kama vile Jose na Utingo na kutatiza juhudi za kufanya kazi. Dhuluma za kijinsia pia zimechangia katika kutenganisha familia na kusababisha athari za kiafya kama vile ukosefu wa lishe bora. Baadhi ya njia zilizopendekezwa katika kukabiliana na changamoto hizi ni kuepukana na mapenzi ya kiholela ili kuepukana na maambukizi ya UKIMWI. Ili kukabiliana na matumizi ya dawa za kulevya, imependekezwa kuwa kila mwanajamii anapaswa kuepukana na matumizi ya dawa hizo na kupiga ripoti kwa maafisa wa serikali ili wanaozitumia na kuzieneza wachukuliwe hatua ya kisheria. Isitoshe, dhuluma za kijinsia kama vile unyanyazwaji wa jinsia ya kike zinapaswa kupigwa marufuku kisheria. Haya na mengine yaliyojadiliwa katika utafiti huu ni muhimu katika kukabiliana na changamoto za kiafya katika jamii.

# SURA YA SABA

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 7.1 Muhtasari

Utafiti huu umechanganua sitiari za kiafya katika matini teule za fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Vitabu vya fasihi ya Kiswahili ya Watoto vilivyoteuliwa ni: *Pendo katika Shari* (Momanyi, 2008), *Madhila ya Bi. Shufaa* (Bakari, 2008), *Siku ya Ukimwi* (Kobia, 2008), *Sitaki Iwe Siri* (Matundura, 2008), *Kosa la Marehemu* (Panja, 2010) na *Nimefufuka* (Nandwa, 2011). Nadharia ya Umitindo iliyoasisiwa na Leech (1969) na Nadharia Changanuzi ya Sitiari ya Dhana iliyoasisiwa na Lakoff na Johnson (1980) zimetumika kama mwongozo katika uchanganuzi wa matini teule. Nadharia Changanuzi ya Sitiari ya Dhana imetumiwa kuhakiki matumizi ya sitiari katika kazi teule ilhali nadharia ya Umitindo imetumiwa kuchanganua mitindo iliotumiwa na waandishi wa vitabu teule kuwasilisha maudhui katika kazi walizoandika.

Sura ya kwanza ya utafiti huu imeshughulikia usuli wa mada, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti na upeo na mipaka ya utafiti. Pia, maelezo ya istilahi muhimu zilizotumika katika kazi hii yametolewa.

Sura ya pili imeangazia mwauo wa maandishi. Maandishi mbalimbali yaliyohusiana na fasihi ya watoto, sitiari, suala la afya, Nadharia Changanuzi ya Sitiari ya Dhana, nadharia ya Umitindo na mitindo ya uchanganuzi katika kazi za kifasihi imejadiliwa kwa kina. Pengo la utafiti lilitokana na usomaji wa kazi mbalimbali zilizoangaziwa katika sura hii.

Mbinu za utafiti zimefafanuliwa katika sura ya tatu. Mtafiti amefafanua eneo ambalo utafiti ulifanyika, mpango wa utafiti na kundi lengwa. Isitoshe, mtafiti ameelezea namna sampuli ilivyoteuliwa, jinsi data ilivyokusanywa, kuchanganuliwa na kuwasilishwa. Pia maadili ya utafiti yaliyozingatiwa wakati wa kufanya utafiti huu yameelezwa.

Sura ya nne imejadili aina mbalimbali za sitiari za kiafya zilizotumika kuangazia masuala ya kiafya katika vitabu teule kwa kuongozwa na Nadharia Changanuzi ya Sitiari ya Dhana. Sitiari zilizobainishwa ni sitiari kuu, sitiari pana na sitiari za kikaida.

Mifano mbalimbali ya sitiari za kiafya zilizobainishwa katika matini teule imefafanuliwa kwa kina katika kazi hii. Imedhihirika kuwa kuna aina mbalimbali za sitiari za kiafya na lugha ya kisitiari hutekeleza wajibu muhimu katika kuwasilisha masuala yanayochukuliwa kuwa mwiko katika jamii.

Sura ya tano imechanganua mitindo iliotumiwa kuwasilisha sitiari za kiafya katika vitabu teule kwa kuongozwa na nadharia ya Umitindo. Utafiti huu umetambua aina mbalimbali za mitindo iliyotumiwa na waandishi wa vitabu teule kuwasilisha sitiari za kiafya. Mitindo iliotumika kama vile matumizi ya nyimbo, methali, ushairi, majazi, barua, taswira, tashtiti, mshikamano wa kisimulizi na chuku imejadiliwa kwa kina. Imedhihirika kuwa mitindo iliotumika ilifaulu kuwasilisha sitiari za kiafya kwa ufasaha.

Sura ya sita imefafanua masuala mtambuko kama vile UKIMWI, dhuluma za kijinsia na dawa za kulevya yaliyoangaziwa katika vitabu teule. Uchanganuzi wa data katika matini teule umebainisha visababishi vya masuala mtambuko na njia za kutatua matatizo yaliyotokana na masuala hayo. Miongoni mwa njia hizo ni kutembelea vituo vya kiafya ili kushauriwa dhidi ya kukabiliana na magonjwa, kuheshimu haki za kibinadamu ili kuangamiza dhuluma za kijinsia na kuwa na sera maalum inayoangazia matumizi ya dawa za kulevya katika jamii. Nadharia Changanuzi ya Sitiari ya Dhana imetumika kuchanganua masuala ya kiafya.

## 7.2 Hitimisho

Sehemu hii imeshughulikia hitimisho la matokeo ya utafiti kulingana na malengo ya utafiti. Lengo la kwanza lilihusu kujadili aina za sitiari za kiafya katika vitabu teule vya fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Lengo la pili lilihusu uchunguzi wa mitindo ambayo ilitumika kuwasilisha sitiari za kiafya katika vitabu teule vya fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Nalo lengo la mwisho la utafiti lilihusu ufafanuzi wa masuala mtambuko yaliyowasilishwa na sitiari za kiafya katika vitabu teule vya fasihi ya Kiswahili ya Watoto.

Mtafiti ameshughulikia lengo la kwanza la utafiti huu kwa kuchanganua data katika matini teule. Amebainisha aina mbalimbali za sitiari zilizotumiwa kuangazia masuala

ya kiafya. Sitiari hizo ndizo zimerejelewa kama sitiari za kiafya katika utafiti huu. Aina za sitiari za kiafya zilizotambuliwa ni sitiari kuu, sitiari za kikaida na sitiari pana. Sitiari kuu za kiafya zimewakilisha dhamira kuu ya mwandishi inayotawala matini teule kuanzia mwanzo hadi mwisho wa kisa. Sitiari za kikaida zimetumika kuwasilisha maudhui mbalimbali yaliyojenga dhamira kuu katika matini teule. Sitiari pana za kiafya zimetumiwa na waandishi wa matini teule kujenga dhamira kuu ya mwandishi.

Umuhimu wa sitiari za kiafya zilizotambuliwa katika utafiti huu ni kwamba, zimeongezea msamiati wa Kiswahili na kuimarisha hadhi ya fasihi ya Kiswahili kama taaluma ya kutumiwa katika kuangazia masuala ya kiafya. Pia, utafiti huu umedhihirisha kuwa lugha ya kisitiari inaweza kutumiwa kuangazia masuala ya kiafya ambayo hayatajwi hadharani kwa sababu ya mila na desturi hasi za kijamii. Hii ni kwa sababu ujumbe unawasilishwa kwa njia inayokubalika. Utafiti huu pia umegundua kuwa, sitiari ni dhana pana na changamano na inaweza kujengwa na aina mbalimbali za semi na mbinu zingine za lugha kama vile methali na taswira. Matumizi ya mbinu mbalimbali za lugha katika mawasiliana huvutia wasomaji jambo linalowachochea kuendelea kusoma kazi husika.

Lengo la pili la utafiti huu lilihusu uchunguzi wa mitindo ya uwasilishaji wa sitiari za kiafya katika vitabu teule. Mtafiti amegundua kuwa sitiari za kiafya zinaweza kuwasilishwa kwa kutumia mitindo kama vile nyimbo, ushairi, barua, usimulizi, majazi, tashtiti, taswira, chuku na methali. Imebainishwa kuwa, nyimbo hurahisisha mawasiliano ya kisitiari kwa jinsi zinavyowasilishwa kwa kutumia mahadhi na midundo inayonasa makini ya hadhiri. Ushairi unafaa kuwasilisha sitiari za kiafya kwa sababu una uwezo wa kuangazia masuala changamano na yanayochukuliwa kuwa mwiko katika jamii, kwa njia ya mkato na lugha fiche inayovuta makini ya wasikilizaji. Aidha, mtindo wa barua ya kirafiki umetumika kuwasilisha sitiari za kiafya katika baadhi ya matini teule. Lugha ya kirafiki humwezesha mwasilishaji wa ujumbe kutumia lugha inayompa nafasi ya kujieleza moja kwa moja. Mtindo wa mshikamano wa kisimulizi umetumika kuwasilisha sitiari za kiafya kwa njia ya moja kwa moja. Isitoshe, utafiti huu umebaini kuwa, mbinu ya kitashtiti imefaulu kuwasilisha sitiari za kiafya kwa sababu inatumia lugha ya utani na kubeza kwa lengo la kurekebisha na kuimarisha maadili katika jamii. Mtindo wa kitaswira unafaa kwa sababu unawasilisha picha ya

kinachozungumziwa moja kwa moja na kurahisisha uelewa wake kwa kuzua hali halisi ya matukio akilini mwa msikilizaji. Isitoshe, chuku imetumiwa vyema na waandishi wa matini teule kusisitiza athari za kiafya zinazotokana na ugonjwa wa UKIMWI.

Utafiti huu umegundua kuwa kuna baadhi ya matini teule zilizotumia mtindo mmoja. Mtindo wa barua pekee umetumiwa katika matini teule *Nimefufuka*. Kuna haja ya kuumia aina mbambali za mitindo ya uwasilishaji katika kazi za fasihi ya Kiswahili ya Watoto ili kuvutia wasomaji na kuwa na hamu ya kuendelea kusoma zaidi. Usomaji ni njia moja ya kuwasiliana na kupata maarifa zaidi.

Sitiari za kiafya zilizotumika katika matini teule zimewasilisha masuala mtambuko yaliyoangaziwa katika matini teule kama vile UKIMWI, dhuluma za kijinsia na dawa za kulevya. Baadhi ya athari za UKIMWI zilizotambuliwa ni maambukizi ya magonjwa nyemelezi, kuishiwa na nguvu za kufanya kazi, vifo, miongoni mwa zingine. Njia zilizopendekezwa ili kukabiliana na changamoto za UKIMWI ni: Kula lishe bora, kutembelea vituo vya afya kutibiwa na kupewa mawaidha, kuwa mwaminifu kwa mpenzi mmoja, kuepuka matumizi ya vyombo vyenye ncha vinavyotumiwa na watu wengi, uwajibikaji, kuhamasisha jamii na kutumia dawa za kupunguza makali ya UKIMWI (ARVs).

Mtafiti pia amebainisha dhuluma za kijinsia kama mojawapo ya masuala mtambuko yanayoathiri kuafikiwa kwa maendeleo endelevu katika jamii. Uchanganuzi wa data katika matini teule umebainisha kuwa mwanamke amesawiriwa kama mali yaliyomilikiwa na mwanaume. Pia, utafiti huu umebaini kuwa mila na desturi za jamii, ndoa na imani potovu zinachangia katika kuendeleza unyanyasaji wa wanawake kwa kuwanyima nyadhifa za uongozi, kuwatengea kazi duni kama vile kulisha watoto na kazi za nyumbani na kumpa mwanaume uwezo wa kumuamulia mwanamke kila jambo. Ili kuimarisha hadhi ya mwanamke katika jamii, utafiti huu umependekeza haja ya kutupilia mbali tamaduni hasi zinazomdhalilisha mwanamke, kusomesha vijana wa kike, serikali kuwapa wanawake nyadhifa za uongozi, kupiga marufuku na kuchukua hatua kali za kisheria kwa wanaoendeleza tohara za wanawake na dhuluma za kijinsia. Isitoshe, imegunduliwa kuwa, dawa za kulevya zimeathiri afya ya binadamu na kusababisha matatizo ya kiafya kama vile magonjwa, kuongezeka kwa visa vya uhalifu,

mizozo ya kifamilia, kuzorota kwa uchumi na kuathirika kimasomo. Uchanganuzi wa data katika matini teule umebainisha namna dawa za kulevya zinavyotumiwa na watu wazima na watoto. Wanafunzi wa shule za msingi, upili na taasisi za juu za kielimu wameathiriwa zaidi na dawa za kulevya na wengine wameacha shule. Baadhi ya njia zilizoangaziwa katika kukabiliana na matumizi na kuenea kwa mihadarati ni kuhusisha wanajamii katika vita dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya, wazazi kuimarisha nidhamu kwa watoto, serikali kubuni sera maalum dhidi ya matumizi ya mihadarati na mashirika ya kijamii kuhamasisha jamii kuhusu athari za dawa za kulevya. Shirika la NACADA linapaswa kupewa nguvu zaidi kisheria ili liweze kushtaki wanabiashara wa dawa za kulevya na kunyima leseni watu wanaokiuka sheria zinazoongoza matumizi ya dawa hizo humu nchini. Aidha, shirika la NACADA linapaswa kuwahusisha wataalam na wanajamii katika kuangamiza matumizi ya dawa za kulevya. Imebainika kuwa fasihi ya Kiswahili ya Watoto ina nafasi muhimu katika kuangazia masuala ya kiafya yanayoathiri jamii na kupendekeza namna ya kukabiliana na changamoto za kiafya.

Kwa ujumla ni dhahiri kuwa taaluma ya fasihi ya Kiswahili ya Watoto inaweza kutumiwa kama njia mbadala ya kuangazia masuala ya kiafya yanayoathiri jamii. Wahudumu wa kiafya wanaweza kutumia sitiari za kiafya zilizogunduliwa katika utafiti huu kuendeleza mafunzo katika jamii kwani zinaongezea msamiati katika taaluma ya afya.

### 7.3 Mapendekezo ya tafiti za baadaye

i. Matokeo ya utafiti huu yamebainisha umuhimu wa kufanya utafiti zaidi kuhusu uhakiki wa semi kama vile tashbihi, methali na taswira katika uwasilishaji wa masuala ya kiafya katika fasihi ya Kiswahili ya Watoto kwa kuongozwa na nadharia ya uhalisia. Hii ni kwa sababu matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kuwa, matumizi bora ya semi za lugha yana uwezo wa kunasa makini ya hadhira na kuwasilisha masuala changamano katika jamii kwa njia inayokubalika na kurahihisha utekelezaji wake.
ii. Vilevile, utafiti kama huu unaweza kufanywa katika tanzu zingine za fasihi ya Kiswahili kama vile riwaya, tamthilia au ushairi kwa kutumia nadharia ya

mwingiliano matini ili kubainisha misimamo ya waandishi tofauti katika athari za masuala ya kiafya katika jamii.

iii. Pia, utafiti unaweza kufanywa kuhusu mwingiliano matini katika vitabu teule vya kiafya vya fasihi ya Kiswahili ya Watoto kwa kuongozwa na nadharia ya mwingiliano matini.

iv. Utafiti wa baadaye pia unaweza kufanywa kuhusu mielekeo ya wanafunzi kuhusu masuala ya kiafya kwa kuongozwa na nadharia ya mwitikio wa msomaji. Nadharia ya mwitikio wa msomaji inampa mtafiti nafasi ya kutangamana na wahojiwa nyanjani na kupata data ya kisingi itakayompa matokeo ya kweli kuhusu masuala ya kiafya yanayowaathiri na kutambua njia bora za kutatua changamoto za kiafya.

## MAREJELEO


Adzo, F. (2022). *Kiswahili na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Huduma za Afya nchini Kenya*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Moi. (Haijachapishwa).

African Union Commission. (2015). *Agenda 2063*. *The Africa we Want*. African Union Commission.

Akivaga, S.K. na Odaga, B. (1982). *Oral Literature- A School Certificate Course*. Nairobi: Heinemann.

Anudo, C. (2018). *Conceptual Metaphors in Dholuo: A Cognitive Linguistic Approach*. PhD Thesis of Kisii University. (Unpublished).

Anudo, C. & Orwa, Q. (2016). Metaphors used to Portray Masculinity and Feminity in Dholuo Benga Music: *A Cognitive Linguistic Approach. Imperial Journal of Interdisplinary Research,* Vol 2(9). 1051-1060.

Arege, M.T na Chacha, M.L. (2023). *Kamusi ya Taaluma ya Kiswahili*. Nairobi: Access Publishers Limited.

Bakari, N. (2008). *Madhila ya Bi. Shufaa*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Bakize, L. (2013). *Changamoto Zinazoikabili Fasihi ya Watoto Tanzania Katika Kiswahili, Juz. 16*. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Kur. 61-70.

Bakize, L. (2014). *Utangulizi wa Fasihi ya Watoto*. Dar es Salaam: Monoccony Printing Press.

Bright, W. (1992). *International Encyclopedia of Linguistics*. New York: Oxford University Press.

Charteris-Black, J. (2004). *Corpus Approaches to Critical Metaphor Analysis*. Basingstoke: Palgrave Macmillan.

Fadhili, E. (2014). *Kuchunguza Dhima ya Mtindo katika Tamthiliya za Kihistoria: Utafiti Linganishi wa Tamthiliya za Morani* na *Kinjeketile*. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. (Haijachapishwa).

Fetsch, R .J. & Yang, R. K. (1990). *A ranking of critical economic and social issues facing Colorado families by three groups of Coloradans*. Unpublished raw data.

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. London: Oxford University Press.

Gaichu, N. (2016). *Uchanganuzi wa Sitiari Dhanifu katika Methali za Kiswahili: Mtazamo wa Nadharia ya Uhusiano*. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Garret, L. (2007). The Challege of Global Health*: Foreign Affairs (Council on Foreign Relations)* 86 (1): 14 – 38.

Garret, L. (2013). *Existential Challenges to Global Health*: Center on International Cooperation. New York: New York University.

Gathigia, G. (2014). *Metaphors of Love in Gikuyu: Conceptual Mappings, Vital Relations and Image Schemas*. PhD Thesis of Kenyatta University. (Unpublished).

Gathumbi, A.M. (2003). *Family and Peer Influences on substance abuse among secondary school students in Thika District* Unpublished PGDE project, Catholic University of Eastern Africa.

Gelinas, M. (2006). *How to Overcome Alcoholism*. Nairobi: Paulines Publications Africa.

Greer, G. (1971). *The Female Eunach*. New York: McGraw.

Highet, G. (1962). *The Anatomy of Sitire*. Princeton: Princeton University Press.

Hunt, P. (1999). *Understanding Children's Literature: Key Essays from the International Companion Encyclopedia of Children's Literature*. New York: Routledge.

Hynes, H. P. (1989). *Reconstructing Babylon. Essays on Women and Technology*. London: Earthsan.

Indangasi, H. (1988). *Stylistics*. Nairobi: Nairobi University Press.

Kabira, W. M. na Mutahi, K. (1988). *Gikuyu Oral Literature*.Nairobi: Heinemann.

Kaguthi, J. (2004). *Youth in Peril: Alcohol and Drug Abuse in Kenya*. Nairobi: Baseline Survey report.

Kandel, D. and Chen B. (1995). The natural history of Drug use from adolescents to mid thirties in a general population ample. *America Journal of the Public Health* 85: 41 – 47.

Kanyua, G. (2013). *Mtindo Unavyoendeleza Maudhui katika Natala*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Katutu, M. (2013). *Mtindo katika Diwani ya Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

KICD. (2017). *Education for Sustainable Development (ESD*). Nairobi: KICD.

Kitula, K. & Ndalu, A. (2011). *Kamusi ya Methali*. Nairobi: East African Education Publishers.

Kitundu, J. & Malangwa, S. (2019). Ujenzi wa Maana katika Sitiari na Tashibiha za Kiswahili *Kioo cha Lugha*, Vol. 17.

Kobia, J. (2008). *Siku ya Ukimwi*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Kobia, J. (2008). Metaphor on HIV/AIDS Discourse Among Oluluyia Speakers of Western Kenya.http://cadaad.org/ejournal Vol 2 (2): 48-66 ISSN: 1752-3079.

Kombo, D. & Tromp, D. (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction.* Nairobi: Paulines Publicatuions Africa.

Kovecses, Z. (2000). *Metaphor and Emotion.* Budapest: Cambridge University Press.

Kuzmina, S. (2013). Conceptual Metaphor in Syntax: Sentence Structure Level. *Moderna Sprak,* 2: 99- 114.

Lakoff, G. (1992). Contemporary Theory of Metaphor. In Andrew Ortony (ed.) Metaphor and Laurie, G. (2007). *The Challege of Global Health: Foreign Affairs (Council on Foreign Relations)* 86 (1): 14 – 38.

Lakoff, G. & Johnstone, M. (1980). *Metaphors We Live By*. Chicago: Chikago Universiy Press.

Leech, G. (1969). *A Linguistic Guide to Engilsh Poetry*. New York: Longman Group Ltd.

Leech, G. & Short, M. (1981). *A Style in Fiction: An Introduction to English Fictional Prose*. London: Longhorn.

Lloyd, M. (2010). *A Practical Guide to Care Planning in Health and Social Care*. Open University Press: Cc Graw.

Longhorn Publishers (2020). *ECDE & Primary Pricelist*. Nairobi: Longhorn Publishers PLC.

Matundura, B. (2008). *Sitaki iwe Siri*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Matundura, E., Kobia, J., & Mukuthuria, M. (2013). “Taswira Dunifu za Uana katika Fasihi ya Kiswahili ya Watoto,” katika *Mulika,* Na. 32, kur. 28-47. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks Graghics and Publishing.

Mbuthia, E. (2018). The role of Kiswahili Children’s Literature in Formulating their world view, volume 6 No. 2 Feb 2018.

McCabe, S.E., Boyd, C.J., & Teter, C.J. (2009) ―Subtypes of Non-medical Prescription Drug Misuse. *Drug Alcohol Dependency* 102 (1-3): 63-70.

Mdee, J.S, Njogu, & K, Shafi, A. (2022). *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (Toleo la Tatu). Nairobi: Longhorn Publishers PLC.

Ministry of Education. (2002). *Primary School Education Syllabus*. Nairobi: Kenya Institute of Education.

Mlaga, K. (2017). *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi Karne ya 21*. Dar es Salaam: Heko Publishers.

Momanyi, C. (2008). *Pendo katika Shari*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mpesha, N. (1995). *Children Literature in Tanzania: A Literary Appreciation of Its Growth and Development*. Unpublished PhD thesis: Kenyatta University.

Muriungi, K. (2006). *Emerging Trends in Kenyan Children's Fiction: A Study of Sasa Sema's Lion Books*. Unpublished PhD Theses: University of Witwatersrand. Johannesburg.

Mwakio. W. (2016). *Matumizi ya Tashbiha, Sitiari na Taashira katika Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapichwa).

Mwikali, J. & Furaha, C. (2014). Fani za Fasihi zinazoibua Fantasia katika hadithi za watoto za Nyambura Mpesha, *Nordic journal of African studies 23(4): 292-306(2014).*P.

NACADA. (2007). Report Situation Assessment of Drugs and Substance abuse in Nairobi.

Nandwa, R. (2011). *Nimefufuka*! Nairobi: Longhorn Publishers.

Nandwa, J. na Bukenya, A. (1983). *Oral Literature for Schools*. Nairobi: Longhorn.

Ngugi, P, (2014). Fasihi ya Watoto katika Kutekeleza Mahitaji ya Mtoto Kisaikolojia katika: *Kiswahili Journal of the Institute of Kiswahili Studies* vol. 77 (TATAKI). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kur. 170-180.

Ngugi, P. (2016). Usawiri wa Masuala Ibuka katika Fasihi ya Watoto: Mifano kutoka Kenya katika: *Mulika,* No 35. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kur.76- 86.

Ngugi, P. & Nabea, W. (2011). Children's Literature in Kiswahili: A Stylistic Approach katika: *East African Literature: Essays on Written and Oral Traditions*, Logos Verlag Berlin. Kur. 223- 244.

Njogu, K. (2007). *Ufundishaji wa Masuala -Ibuka* katika shule za nchini Kenya katika Kiswahili na Elimu nchini Kenya. Nairobi: Twaweza communication 11-23.

Njogu, K. & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nodelman, P. (2008). *The Hidden Adult: Defining Children's Literature*. Baltimore, Md: Johns Hopkins University Press.

Nyandiwa, H. (2015). *Uchanganuzi wa Kimtindo wa Zingua La Mzuka* na *Mbaya Wetu*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Oberstein, K. (1996). *Defining Children's Literature and Childhood*. London: Routledge.

Oladipo, R., Ikamari, L, Kiplagat, J. & Barasa, L. (2015). *General Research Methods*. Oxford University Press: Nairobi.

Odhiambo, R., & Mars, M. (2018). *Patients' understanding of telemedicine terms required for informed consent when translated into Kiswahili*. 1–3. https://doi.org/10.1186/s12889-018-5499-1

Panja, A. (2010). *Kosa la Marehemu.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Purris, G. and Mach Innis, D.M (2009). Implementation of the Community Reinforcement Approach in a Long Standing Addictions Outpatient Clinic'. *Journal of Behaviour Analysis of Sports, Health, Fitness and Behavioural Medicin*e. 2 (1) 33-44.

Republic of Kenya (2007). *Government of Kenya, Vision 2030.* Nairobi: Government Printers.

Republic of Kenya (2010). *Constitution of Kenya*. Nairobi: Government Printers.

Scott, C. Ratzan, Gary, L. Filerman, & John, W. (2000). Attaining Global Health: Challenges and Opportunities, *Population Bulletin*, vol.55, no. 1 (Washington, DC: Poppulation Reference Bureau).

Senkoro, F. (1982). *Fasihi.* Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Simala, K. (2000). *Uhakiki wa Sitiari za Uana katika Ushairi wa Kiswahili. Tasnifu ya Uzamifu.* Chuo Kikuu cha Moi. (Haijachapishwa).

Tehseem, T., & Khan, A.B (2015). Exploring the use of Metaphors in Children Literature. *A Discursive Perspective.* Vol. 2 No. 2.

Timmamy, R. (2002). *Mombasa Swahili Women's Wedding Songs: A Stylistics Analysis*. Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

UNAIDS. (2023). Global HIV and AIDS Staistics- Fact Sheet. *https//www.unaids.org.* Accessed on 25/2/ 2024.

Wangari, M. (2019). Ukumbi wa Lugha na Fasihi: Mbinu za Sanaa katika Kiswahili. Available at https://taifaleo.nation.co.ke/ukumbi-wa-lugha-na-fasihi-mbinu-za sanaa-katika-kiswahili/: Accessed on 25/01/2022.

Wanjala, A. (2015). *Usawiri wa Malezi Unavyoathiri Utambulisho wa Vijana katika Riwaya ya Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Wamitila, K. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istlahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publishers.

Wamitila, K. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Kiswahili*. Nairobi: Vide – Muwa Publishers Lt d.

World Health Organization. (2003). *Global Health: Todays Challenges*. *https//www.who.int*.chapter 1.

World Health Organization. (2018). *The State of Health in the WHO African Region. An Analysis of the Status of Health, Health Services and Health Systems in the context of the Sustainable Development Goals*. Wold Health Organization: Regional Office for Africa.

World Health Organization. (2020). *WHO EMRO |eHealth|Health topics*. http://www.emro.who.int/health-topics/ehealth/: Accessed on 25/1/2022.

# VIAMBATISHO

## Kiambatisho I: Kibali cha Utafiti

**CHUKA UNIVERSITY**

**Knowledge is Wealth *(Sapientia divitia est)* Akili ni Mali**

**CHUKA UNIVERSITY INSTITUTIONAL ETHICS REVIEW COMMITTEE**

Telephones: 020-2310512/18 P. O. Box 109-60400, Chuka
Direct Line: 0772894438 Email: info@chuka.ac.ke, Website: www.chuka.ac.ke

**27th November, 2023**

**REF: CUIERC/ NACOSTI/430**
TO: **Reuben Mwilaria**

**RE: Uchanganuzi wa Sitiari za Kiafya Katika Matini Teule za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto**

This is to inform you that *Chuka University IERC* has reviewed and approved your above research proposal. Your application approval number is *NACOSTI/NBC/AC-0812.* The approval period is 27th November, 2023 – 27th November, 2024.

This approval is subject to compliance with the following requirements;

i. Only approved documents including (informed consents, study instruments, MTA) will be used
ii. All changes including (amendments, deviations, and violations) are submitted for review and approval by *Chuka University IERC.*
iii. Death and life threatening problems and serious adverse events or unexpected adverse events whether related or unrelated to the study must be reported to *Chuka University IERC* within 72 hours of notification
iv. Any changes, anticipated or otherwise that may increase the risks or affected safety or welfare of study participants and others or affect the integrity of the research must be reported to *Chuka University IERC* within 72 hours
v. Clearance for export of biological specimens must be obtained from relevant institutions.
vi. Submission of a request for renewal of approval at least 60 days prior to expiry of the approval period. Attach a comprehensive progress report to support the renewal.
vii. Submission of an executive summary report within 90 days upon completion of the study to *Chuka University IERC.*

Prior to commencing your study, you will be expected to obtain a research license from National Commission for Science, Technology and Innovation (NACOSTI) https://oris.nacosti.go.ke and also obtain other clearances needed.

Yours sincerely

**Dr. Benjamin Kanga**
**SECRETARY**

## Kiambatisho II: Idhini Ya Utafiti

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: 246863

Date of Issue: 22/December/2023

**RESEARCH LICENSE**



**This is to Certify that Mr.. REUBEN MWILARIA MWILARIA of Chuka University, has been licensed to conduct research as per the provision of the Science, Technology and Innovation Act, 2013 (Rev.2014) in Tharaka-Nithi on the topic: UCHANGANUZI WA SITIARI ZA KIAFYA KATIKA MATINI TEULE ZA FASIHI YA KISWAHILI YA WATOTO for the period ending : 22/December/2024.**

License No: **NACOSTI/P/23/32098**

**246863**

Applicant Identification Number

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

**See overleaf for conditions**